



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



ISO 9001:2015 Certified

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23



MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU  
WA HESABU ZA SERIKALI  
MACHI 2024



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, S.L.P. 950,  
41104 Tambukareli Dodoma. Simu: +255(026)2161200, Baruapepe: ocag@nao.go.tz,  
tovuti: www.nao.go.tz

Kumb.Na.CGA.319/421/01

28 Machi 2024

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P 1102,  
1 Barabara ya Julius Nyerere,  
11400 Chamwino,  
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418.

Ripoti hii imeangazia matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua stahiki za marekebisho zinazohusiana na kuchochea uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Ninawasilisha,


Charles E. Kichere

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

## Mamlaka

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yamebainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi, Sura 418.



### Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

### Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

### Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



### Kufanya kazi kwa utaalam

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

### Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

### Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi.

---

## YALIYOMO

TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI .....	viii
SURA YA KWANZA .....	1
UTANGULIZI.....	1
SURA YA PILI.....	3
HATI ZA UKAGUZI.....	3
SURA YA TATU .....	6
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA NA MAAGIZO YA KAMATI YA HESABU YA BUNGE .....	6
SURA YA NNE .....	9
UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA.....	9
SURA YA TANO .....	20
UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA UTENDAJI KAZI .....	20
SURA YA SITA.....	35
USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA .....	35
SURA YA SABA.....	44
USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA .....	44
SURA YA NANE .....	56
USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA .....	56
SURA YA TISA.....	62
USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI.....	62
SURA YA KUMI .....	76
TATHMINI YA RASILIMALI WATU NA UTAWALA .....	76
SURA YA KUMI NA MOJA.....	86
USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA .....	86
SURA YA KUMI NA MBILI .....	95
MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI NA TAASISI ZINGINE ZA KIFEDHA .....	95
SURA YA KUMI NA TATU .....	114
MAPITIO KATIKA SEKTA YA UTALII TANZANIA.....	114
SURA YA KUMI NA NNE.....	123

---

UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI .....	123
SURA YA KUMI NA TANO.....	133
TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU.	133
SURA YA KUMI NA SITA .....	148
UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO .....	148
SURA YA KUMI NA SABA .....	156
UFANISI WA TAASISI ZA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA.....	156
SURA YA KUMI NA NANE .....	165
MAZAO NA BODI ZA MAZAO .....	165
SURA KUMI NA TISA .....	180
UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA .....	180
VIAMBATISHO.....	189

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa idadi .....	5
Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita katika mashirika ya umma.....	6
Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya kudumu ya bunge .....	7
Jedwali Na. 4: Mashirika yenye maagizo ya muda mrefu kutoka kwa kamati.....	7
Jedwali Na. 5: Mashirika yenye mitaji hasi.....	15
Jedwali Na. 6: Upungufu wa uchangiaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi.....	18
Jedwali Na. 7: Mashirika ya umma ambayo hayakulipa gawio .....	19
Jedwali Na. 8: Miradi Iliyositishwa.....	27
Jedwali Na. 9: Ufanisi mdogo wa kuhudumia mizigo bandari ya Dar es salaam na Tanga .....	28
Jedwali Na. 10: Muda wa kubadilisha meli mwaka 2022/23.....	29
Jedwali Na. 11: Muhtasari wa miradi iliyositishwa.....	32
Jedwali Na. 12: Mashirika ya umma ambayo mapato yalikusanya nje mfumo wa GEPG .....	36
Jedwali Na. 13: Mashirika ambayo hayakuhamisha fedha kwenda Benki Kuu ya Tanzania .....	40
Jedwali Na. 14: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija mwaka 2022/23 .....	45
Jedwali Na. 15: Mashirika yenye matumizi yasiyostahili kwa mwaka 2022/23 .....	49
Jedwali Na. 16: Mashirika yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu .....	51
Jedwali Na. 17: Mashirika ya umma yaliyofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti .....	59
Jedwali Na. 18: Mashirika ya umma yenye ushiriki usioridhisha katika maandalizi ya bajeti .....	60
Jedwali Na. 19: Taasisi zenyne dhamana ya bima iliyopungufu ya asilimia 15.....	63
Jedwali Na. 20: Taasisi zenyne dhamana za utekelezaji wa zabuni zilizoisha muda .....	64
Jedwali Na. 21: Orodha ya taasisi zilizochelewa kukamilisha miradi .....	66
Jedwali Na. 22: Mashirika ambayo mikataba yake haikupekuliwa na Mwanasheria Mkuu.....	68
Jedwali Na. 23: Taasisi za umma zisizokuwa na bodi za wakurugenzi .....	77
Jedwali Na. 24: Taasisi ambazo nyaraka zao hazikuidhinishwa .....	78
Jedwali Na. 25: Taasisi mbazo mali zake hazipo kwenye mfumo wa GAMIS .....	81
Jedwali Na. 26: Maafisa wanaokaimu katika nafasi zao kwa muda mrefu.....	83
Jedwali Na. 27: Mashirika ya umma yanayotoa ajira za muda mfupi bila ya mwongozo .....	84
Jedwali Na. 28: Ucheleweshaji wa kuwasilisha kodi kwa TRA.....	88
Jedwali Na. 29: Malipo bila risiti za kodi za kielektroniki.....	89
Jedwali Na. 30: Tofauti ya mapato kati ya ritani za kodi na taarifa za hesabu .....	90
Jedwali Na. 31: Tofauti ya kodi kati ya mfumo wa mamlaka na waTaasisi .....	90
Jedwali Na. 32: Maelezo ya Mwenendo wa mikopo chechefu ya Benki za Serikali.....	98
Jedwali Na. 33: Upungufu wa vitanda katika hoteli na mahema za Hifadhi za Taifa.....	119
Jedwali Na. 34: Upungufu wa uzalishaji maji katika miji ( $M^3$ kwa siku) .....	124
Jedwali Na. 35: Upotevu wa Maji .....	127
Jedwali Na. 36: Deni la mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.....	129
Jedwali Na. 37: Machapisho halisi dhidi ya lengo kwa mwaka .....	134
Jedwali Na. 38: Upungufu wa udahili wa wanafunzi .....	139
Jedwali Na. 39: Kuchelewa kuzinduliwa kwa programu zilizoidhinishwa.....	140
Jedwali Na. 40: Madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na mfuko wa bima wa afya .....	158
Jedwali Na. 41: Mwenendo wa vifaatiba na dawa zilizoisha muda wake .....	161
Jedwali Na. 42: Ubora wa mazao yaliyozalishwa .....	169
Jedwali Na. 43: Mwenendo wa sukari ndani ya nchi .....	174
Jedwali Na. 44: Mwenendo wa uwezo wa kuzalisha kwa viwanda vya CPB .....	178
Jedwali Na. 45: Mwenendo wa CPB kutumia uweza wa maghala yake kuhifadhi bidhaa.....	178
Jedwali Na. 46: Kuchelewa kuanza na Kukamilika kwa Mradi .....	186

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na bajeti kwa mwaka 2022/23 .....	189
Kiambatisho Na. II: Taasisi zilizopata hasara au nakisi kwa miaka miwili.....	196
Kiambatisho Na. III: Mashirika yaliyopata faida 2020/21 na hasara/nakisi 2022/23...	196
Kiambatisho Na. IV: Taasisi zenye uwiano wa ukwasi chini ya moja.....	197
Kiambatisho Na. V: Taasisi za umma zenye madeni zaidi ya mtaji .....	198
Kiambatisho Na. VI:Mashirika yenye madeni ya Muda mrefu wanayodai .....	199
Kiambatisho Na. VII: Mashirika ya umma yenye madeni wanayodaiwa .....	200
Kiambatisho Na. IV: Fedha za bajeti zilizotolewa kulinganisha na fedha zilizoidhinishwa .....	202
Kiambatisho Na. IX: Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani .....	203
Kiambatisho Na. X: Mashirika ya umma yenye mapungufu katika dhamana za zabuni	205
Kiambatisho Na. XI: Taasisi zilizochelewa kupokea bidhaa na huduma .....	206
Kiambatisho Na. XII: Mashirika ambayo hayakutumia Mfumo wa kutunza Taarifa na Usimamizi wa Rasilimali Watu .....	206
Kiambatisho Na. XIII: Mashirika ya umma yenye nyenzo za kufanya kazi zisizoridhisha .....	207
Kiambatisho Na. XIV: Kodi ambazo hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania..	209



## SALAMU KUTOKA KWA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2023, ambayo inajumuisha mashirika ya umma. Napenda kutambua mipango ya Serikali inayoongozwa na Mh.Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, nashukuru ushirikiano wa menejimenti za mashirika ya umma katika kutoa taarifa na ufanuzi muhimu kwa ajili ya kuandaa ripoti hii ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yamejikita katika kuangazia usimamizi wa fedha katika mashirika ya umma. Ingawa baadhi ya mashirika ya umma yameonyesha usimamizi mzuri wa fedha, mashirika mengine yamekumbana na changamoto katika udhibiti wa fedha na utendaji kazi. Ni muhimu kwa Serikali kuingilia kati na kuhakikisha mashirika haya yanafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia uchumi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ripoti hii imejumuisha sura 19, kila moja ikielezea maeneo tofauti katika ukaguzi ikiwemo, sheria za manunuzi, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti na uzingatiaji wa sheria za kazi. Ripoti hii pia, inabainisha maeneo ambayo mashirika haya yanahitajika kuboresha utendaji kazi na kusimamia mamlaka kwa ufanisi zaidi.

Katika ripoti hii nimetoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha utendaji kazi wa mashirika ya umma, ili kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuimarisha utawala bora. Ninaamini mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa Serikali na wadau mbalimbali katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mwisho, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa watumishi na kampuni binafsi za ukaguzi zilizoingia mkataba wa kufanya kazi kwa niaba yangu kwa juhudui zao za kufanya ukaguzi. Kujitoa kwao kwa bidii kumekuwa chachu muhimu katika utayarishaji wa ripoti hii na ninawashukuru sana kwa michango yao.

Charles E. Kichere

**Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Ripoti ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23 ina sura 19. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii:

## **Hati za ukaguzi**

Kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, nilikamilisha kaguzi 215 za mashirika ya umma ambapo nilitoa hati za ukaguzi. Kati ya hati za ukaguzi 215 nilizotoa, 211 zilikuwa zenye kuridhisha, na nne zilikuwa zenye shaka. Idadi ya hati zinazoridhisha imeongezeka kutoka asilimia 97 mwaka jana hadi asilimia 98 mwaka huu. Hali hii inaashiria uboreshaji endelevu katika uandaaji wa taarifa za fedha ambao unazingatia mifumo na viwango vya kimataifa vya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRS) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS).

## **Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali**

Ukaguzi wangu ulibaini, kati ya mapendekezo ya ukaguzi 6,151 niliyotoa kwa mashirika ya umma 215, mapendekezo 2,413 (asilimia 39) yalitekelezwa kabisa, mapendekezo 2,776 (asilimia 45) yalikuwa chini ya utekelezaji, mapendekezo 720 (asilimia 12) hayakutekelezwa, wakati mapendekezo 242 (asilimia 4) yalikuwa yamepitwa na wakati.

Pia, nilibaini kati ya maagizo 136 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliyotolewa hadi mwaka wa fedha 2022/23, maagizo 45 (asilimia 33) yalitekelezwa, maagizo 89 (asilimia 65) yalikuwa katika hatua za chini ya utekelezaji, na maagizo mawili (asilimia 2) hayakutekelezwa.

Kwa ujumla, kasi ya kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali inahitaji kuboreshwa ili kushughulikia vihatarishi ambavyo vilikuwa vimekusudiwa kupunguzwa au kuondolewa.

---

## **Utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma**

Nilikagua utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma 215 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Nilibaini mashirika ya umma 58 ambayo yaliripoti hasara au nakisi, ama kwa miaka miwili mfululizo 2021/22 na 2022/23 au kwa mwaka mmoja wa fedha 2022/23. Hii ni kutokana na dosari za kiutendaji zinazosababisha utendaji usioridhisha katika uwekezaji au uendeshaji wa biashara, au kupata msaada wa fedha kutoka Serikalini.

Pia, nilibaini mashirika ya umma 11 yalikuwa na mtaji hasi katika mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni 2023. Sababu kuu za mtaji hasi kwa mashirika hayo zilikuwa malimbikizo ya hasara kwa muda mrefu na madeni makubwa wanayoingia mashirika haya ili kufadhili shughuli zao.

Vilevile, nilibaini mashirika 63 yenye madeni ya muda mfupi zaidi kuliko mali za muda mfupi; ambapo 13 kati ya hayo yalikuwa mashirika ya umma ya kibiashara, huku 50 yalikuwa mashirika yasiyo ya kibiashara. Uwiano wa ukwasi ulikuwa kati ya 0.01 hadi 0.98. Hivyo basi, taasisi hizi zinaweza kushindwa kulipa mikopo na kuchelewesha malipo kwa wazabuni.

Aidha, nilibaini mashirika ya umma 28 (12 ya kibiashara na 16 yasiyo ya kibiashara) yalikuwa na uwiano mbaya wa madeni (jumla ya madeni yote dhidi ya jumla ya mtaji) kwa zaidi ya asilimia 100. Hii inaonesha mashirika haya, kwa kiasi kikubwa, yanategemea mikopo kujiendesha. Hii inasababisha kuwa na hatari kubwa ya kifedha kutokana na ghamra kubwa za kuhudumia madeni.

## **Ufanisi wa mashirika ya umma katika kuimarisha biashara**

Katika ukaguzi wangu wa ufanisi wa uendeshaji wa mashirika ya umma ya kibiashara yenye jukumu la kuweka mazingira mazuri ya biashara nilibaini:

Licha ya kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere tarehe 12 Desemba 2018, pande mbili za mkataba bado hawajasaini makubaliano ya kina ya utekelezaji wa miradi ya kijamii yenye thamani ya shilingi bilioni 262.34, ikiwa yamechelewa kwa zaidi ya miaka minne. Mkataba wa kina wa miradi ya kijamii ulipaswa kutiwa

---

saini ifikapo tarehe 13 Januari 2019. Hivyo, hakuna mradi wowote wa kijamii umetekelvezwa.

Ukaguzi wangu katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ulibaini wastani wa muda wa kuingia na kutoka kwa meli kwa sasa ni siku 6.5 kwa meli za kontena, na hadi siku 13.7 kwa meli za zinazobeba vimiminika badala ya siku tatu na tano zilizopangwa mtawalia.

### **Usimamizi wa mapato katika mashirika ya umma**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwapo kwa ukusanyaji wa mapato nje ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG) kwa shilingi bilioni 21.46 kwa mashirika ya umma saba. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 18.14 (sawa na asilimia 546) kutoka shilingi bilioni 3.32 za mwaka uliopita.

Aidha, katika Shirika la Umeme Tanzania, nilibaini wateja 6,905 waliosajiliwa katika mfumo wa kufanya maombi kwa njia ya mtandao (N-Konekt) walikuwa bado hawasajiliwa katika mfumo wa LUKU kwa siku moja hadi 438 kufikia tarehe 30 Juni 2023. Pia, nilibaini ucheleweshaji katika usajili wa wateja 12,666 katika mfumo wa LUKU kuanzia siku 7 hadi 366 toka wateja hao wajunge kwenye mfumo wa Ni - konekt. Ucheleweshaji wa usajili wa wateja unaathiri mapato ya TANESCO. Pia, nilibaini mashirika ya umma 66 yaliyорипоти madeni ya muda mrefu yanayofikia shilingi trilioni 2.92.

Vilevile, nilibaini hakukuwa na uhamishaji wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 192.44 zilizokusanywa kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Miundombinu ya Reli, ambapo fedha hizo zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zilipelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

### **Usimamizi wa matumizi katika mashirika ya umma**

Katika ukaguzi wangu kwenye usimamizi wa matumizi kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2023, nilibaini mashirika ya umma 17 yenye matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 72.36 yasiyo na tija. Hii inamaanisha kuwapo kwa ongezeko la asilimia 13 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kulikuwa na mashirika ya umma 12 yenye jumla ya shilingi bilioni 63.77. Pia, nilibaini mashirika ya umma 11 yenye matumizi yasiyostahili ya jumla ya shilingi bilioni 4.64 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 94 ikilinganishwa na shilingi bilioni 77.75 kwa mashirika ya umma 21 kwa mwaka uliopita.

---

Vilevile, kuna uwezekano wa kutopata tija kwa malipo ya shilingi bilioni 3.09 kwa ajili ya vifaa vya kukagulia magari katika Shirika la Viwango Tanzania ambapo huenda visitumike kama ilivyokusudiwa kufuatia agizo la Serikali la kusitisha ukaguzi wa magari ndani ya nchi kama ilivyokusudiwa awali.

Pia, nilibaini kutokuwapo kwa uhakika juu ya urejeshwaji wa shilingi bilioni 14.7 za kodi na tozo za uingizaji wa mafuta nchini. Fedha hizi zilizolipwa na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL kwenye shehena za mafuta zilizokuwa na zuio kwa kushindwa kulipa gharama za mafuta kwa mzabuni na baadaye kuuzwa kwa kampuni zingine za uuzaji wa mafuta; ambapo Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL haikurejeshewa kodi na tozo ilizokuwa imelipia.

#### **Usimamizi wa bajeti katika mashirika ya umma**

Nilibaini Serikali haikutoa shilingi trilioni 1.01 kwa mashirika 50 ya ya Umma kama ilivyopangwa katia mwaka wa fedha 2022/23.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma 66 hayakukusanya fedha kiasi cha shilingi bilioni 284.71 kutoka katika bajeti ya vyanzo vya ndani katika mwaka wa fedha 2022/23.

Pia, nilibaini mashirika ya umma nane yalitumia zaidi ya bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 21.14 bila idhini ya Afisa Masuuli au Bodi ya Wakurugenzi.

#### **Usimamizi wa mikataba na ununuzi**

Nilibaini kuendelea kuwapo kwa mapungufu katika mashirika ya umma 22 yaliyochelewa kupokea bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 14.84 kwa kipindi cha kuanzia siku 30 hadi 1,140 ikilinganishwa na mashirika ya umma 12 yaliyoripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2021/22.

Pia, nilibaini kutofuatwa kwa sheria ya ununuzi katika Kiwanda cha Dawa Keko kwa ununuzi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.97. Katika ununuzi huo, hapakuwa na bodi ya zabuni wala timu iliyoteuliwa kufanya tathmini ya zabuni. Hii ilisababisha michakato yote kufanywa na Mkurugenzi wa Fedha pamoja na Afisa Masuuli pekee. Aidha, nilibaini kuwa uchapishaji katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania ulifanywa nje ya Kampuni pasipo mchakato wa ununuzi wala

---

kuingia mkataba. Uchapishaji huo ulikuwa na jumla ya thamani ya shilingi bilioni 1.71.

Vilevile, nimeendelea kubaini mashirika ya umma ambayo yalitekeleza mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 31.11 bila dhamana ya utendaji kazi. Aidha, nilibaini taasisi nne hazikuwasilisha mikataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Afisa Sheria kwa ajili ya uhakiki kabla ya kusainiwa yenye thamani ya shilingi bilioni 9.89 na dola za Marekani milioni 2.95.

### **Tathmini ya rasilimali watu na utawala**

Nilibaini mashirika ya umma nane yalikuwa yanafanya kazi bila Bodi za Wakurugenzi. Hii inapunguza uwezo wa kufanya majukumu ya uongozi na usimamizi kwenye mashirika ya umma husika.

Aidha, nilibaini mashirika ya umma 40 hayakuwa na nyaraka za uendeshaji kama vile mwongozo wa hesabu uliosasishwa, sera na kanuni za kifedha pamoja na sera ya usimamizi wa vihatarishi.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma nane hayakuwata maelekezo ya Serikali yanayohitaji shirika kuhakikisha linawasilisha mpango wa motisha, mpango wa mazungumzo ya hali bora, posho, na muundo wa shirika ili kuitishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### **Usimamizi wa kodi katika mashirika ya umma**

Nilibaini kesi za rufaa ya mapato ambazo hazijaamuliwa wa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi mitano katika Bodi ya Rufani za Kodi na Baraza la Rufani za Kodi zenye jumla ya shilingi bilioni 3,681.36 na dola za Marekani milioni 4.66 mtawalia.

Pia, nilibaini mashirika ya umma 16 hayakuwasilisha makato ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 33.45 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma 12 yalichelewa kuwasilisha makato ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 29.09 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka 2022/23. Kadhalika, nilibaini malipo ya jumla ya shilingi bilioni 2.17 yaliyofanywa na mashirika ya umma tisa hayakuambatanishwa risiti za kielektroniki za kodi ya mapato.

---

## **Utendaji wa benki za Serikali na taasisi zingine za fedha**

Mapitio yangu ya mikopo chechefu nilibaini kuwa Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa na mikopo chechefu ya asilimia 21.50 kufikia tarehe 31 Desemba 2023 (2022: mikopo chechefu asilimia 20.28), wakati Benki ya Azania ilikuwa na mikopo chechefu asilimia 7.44 hadi 31 Desemba 2023 ( 2022: mikopo chechefu asilimia 18.25). Pamoja na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kutoka mwaka uliopita kwa Benki ya Azania, ni vyema kutambua kuwa benki zote mbili bado zilivuka kiwango kinachokubalika na kilichowekwa na Benki Kuu ya Tanzania cha asilimia 5.

Nilibaini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wana mikopo ya muda mrefu ambayo ilitolewa kwa taasisi za Serikali yenye thamani ya shilingi trilioni 1.73 ambayo haijalipwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi 16. Hali hii imesababisha kupunguza uwezo wa mifuko ya jamii kufanya uwekezaji zaidi.

Pia, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haikukusanya michango ipatayo shilingi bilioni 856.78 kutoka kwa wanachama; hivyo kudhoofisha uwezo wa mifuko kuhudumia wanufaika.

Vilevile, nilibaini Shirika la Bima la Taifa, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma hawakuweza kukusanya kodi ya shilingi bilioni 47.20 kutoka kwa wapangaji katika vitega uchumi vyao. Kadhalika, Shirika la Bima la Taifa lina madeni kutoka kwa wapangaji shilingi bilioni 7.95 ambapo wadaiwa wake hawajulikani walipo.

## **Tathmini ya sekta ya utalii nchini Tanzania**

Ukaguzi wangu katika sekta ya utalii ulibaini yafuatayo: Kutolewa kwa bajeti isiyotosheleza kwa ajili ya kuendesha Kituo cha Kidijitali na kutangaza utalii wa kimataifa kupitia Bodi ya Utalii. Hali hiyo inakwamisha ufikiwaji wa lengo lililokusudiwa la kutangaza utalii kwa ufanisi katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Kadhalika, nilibaini ukosefu wa huduma za kuwezesha utalii (ikiwamo uwezo mdogo wa malazi, umeme usiokuwa wa uhakika, kasi ndogo ya

---

utekelezaji wa mradi wa uwanja wa gofu). Vilevile, nilibaini hali ya kutokuendeleza na kutotangaza kreta za Empakai na Olmoti.

Aidha, niliona hatari ya kushindwa kukamilika kwa mradi wa kuwahamisha wakazi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na makadirio hafifu ya ghamama zilizotakiwa katika zoezi hilo. Hii ni kwa sababu, katika hali halisi, mkopo uliochukuliwa hauwezi kukamilisha zoezi hilo. Mradi huu unatekelezwa ili kurejesha mazingira na uoto wa asili ulioharibiwa; hivyo kuifanya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kuwa endelevu.

### **Utendaji wa mamlaka za maji**

Ukaguzi wangu ulibaini hapakuwa na uhakika wa thamani ya fedha za miradi katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Songea. Miradi hii iligharimu shilingi bilioni 17.29.

Pia, nilibaini kuwapo kwa muendelezo wa hasara ya shilingi bilioni 163.93 kutokana na upotevu wa maji (mwaka 2021/22 kulikuwa na hasara ya shilingi bilioni 162.14). Hasara hii inasababishwa na miundombinu chakavu inayovujisha maji.

Aidha, nilibaini ongezeko la madeni ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kutoka shilingi bilioni 126.23 (mwaka 2021/22) hadi shilingi bilioni 136.17 (mwaka 2022/23). Hii inatokana na utoaji wa huduma za majisafi na majitaka kwa taasisi za Serikali kuu, mashirika mengine, pamoja na wateje binafsi.

### **Tathimini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu**

Ukaguzi wangu katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ulibaini yafuatayo: kutokuwapo kwa utambulisho wa lazima, wakutegemewa na wa kipekee, kwa wanafunzi wanaopokea mikopo; kutokuwapo kwa mfumo wa kuwashirikisha wadau katika mkakati wa kuwatafuta wanufaika wanaodaiwa mikopo ya elimu.

Pia, nilibaini kuwapo kwa upungufu wa udahili wa wanafunzi ukilinganishwa na malengo; na kuwapo kwa mapungufu katika shughuli za utafiti na ushauri katika taasisi za kitaaluma.

Aidha, nilibaini: kulikuwa na programu ambazo zimepata ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania lakini bado hazijaanza kutolewa katika

---

Chuo Kikuu cha Dodoma; na programu zilizoisha muda wake hazikupatiwa ithibati mpya katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### **Ufanisi wa mamlaka za udhibiti katika kutekeleza majukumu yao**

Wakati wa ukaguzi nilibaini yafuatayo: kuwapo kwa mapungufu katika usimamizi na matumizi ya TEHAMA katika mamlaka za udhibiti ikijumuisha Soko la Bidhaa Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Bodi ya Usajili wa Makandarasi ambapo unazuia ufanisi katika utoaji wa huduma za udhibiti.

Aidha, katika Bodi ya Usajili wa Makandarasi, nilibaini kutokuwa na hatua zisizotosheleza za kusimamia wanachama waliofutiwa usajili. Hii inaweza kusababisha umma kupata huduma bila kujua kutoka kwa watu au taasisi ambazo hazijasajiliwa na hawastahiki kutoa huduma, na ambapo ubora wa kazi zao haujahakikiwa.

Pia, katika Bodi ya Usajili wa Makandarasi na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania nilibaini matumizi duni ya tafiti kama zana ya kutambua, kutathmini, na kushughulikia mapungufu ya udhibiti ndani ya nchi.

Vilevile, nilibaini kuwapo kwa mikataba ya kipekee ya usambazaji yenye vifungu vya kupinga ushindani katika ununuzi wa magari ya Serikali ambayo yanainyima nchi fursa ya kufanya ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa magari au wauzaji wakubwa, ili iweze kununua maguri kwa bei ya chini.

### **Ufanisi wa mashirika ya umma katika sekta ya afya**

Mfuko wa Bima ya Afya ulipata nakisi ya shilingi bilioni 156.77 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Pia, Mfuko unayadai mashirika ya umma jumla ya shilingi bilioni 280 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Pia, nilibaini kiwanda cha Dawa cha Keko kilipata hasara kwa miaka minne mfululizo ambapo mwaka 2019 (shilingi bilioni 3.27), mwaka 2020 (shilingi bilioni 1.35), mwaka 2021 (shilingi bilioni 1.48), na mwaka 2022 (shilingi bilioni 1.35).

Vilevile, nimekuwa nikibaini bidhaa zilizoisha muda katika Bohari Kuu ya Dawa kwa miaka mitatu mfululizo. Dawa hizo zilikuwa na thamani ya kati ya shilingi bilioni 5.92 hadi bilioni 11.75 kati ya mwaka 2020/21 na 2022/23.

---

### **Mazao na bodi za mazao**

Nilibaini mapungufu ambayo yanazuia ufanisi na tija. Mapungufu hayo yanajumuisha: Uwezo mdogo kwa bodi za mazao ili kutekeleza majukumu yao; Matumizi hafifu ya teknolojia ya kilimo na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kuboresha tija ya kilimo; Udhibiti duni wa ubora wa mazao; Usimamizi duni wa upatikanaji na usambazaji wa ubora na wingi wa mbolea; na hatua zisizofaa za kudhibiti upungufu wa sukari. Udhafifu huu unahitaji kushughulikiwa kwa kina kwa ajili ya kilimo endelevu cha mazao ya biashara na mazao ya chakula.

Pia, nilibaini hatua zisizotosheleza za kuzuia mapungufu katika programu za ruzuku ya mbolea. Vilevile, nilibaini dosari katika mchakato wa usajili wa wakulima chini ya mpango wa ruzuku ya mbolea.

### **Utendaji katika sekta ya uziduaji**

Nilibaini ukosefu wa mpango kamili na utoaji duni wa huduma za kitaalamu kwa wachimbaji wadogo nchini kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Hii inapunguza kasi ya ukuaji katika sekta ya madini.

Pia, katika Shirika la Maendeleo ya Petroli, nilibaini ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani; na kutokuwapo kwa Hifadhi ya Taifa ya Petroli ya Kimkakati ambayo itasaidia upatikanaji wa nishati ya mafuta wakati wa upungufu.



# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Muktadha

Ukaguzi ulifanyika ili kutathmini utendaji wa fedha, taratibu za usimamizi na uzingatiaji wa sheria katika mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Ukaguzi huu ni sehemu ya majukumu na wajibu wa kisheria wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418. Lengo lilikuwa kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa ufanisi, kuchangia katika uchumi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ripoti hii inaundwa na sura 19, kila sura inaelezea masuala tofauti. Masuala hayo, ni pamoja na: uzingatiaji wa sheria za ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha taslimu, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti, na uzingatiaji wa sheria za kodi. Ripoti hii pia, imebainisha mapendekezo ya kuboresha utendaji wa kazi katika mashirika ya umma, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, na kukuza utawala bora.

### 1.1 Malengo ya Ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa maoni huru kuhusu utayarishaji wa taarifa za fedha kama zilitayarishwa kwa mujibu wa mfumo unaokubalika wa utoaji taarifa za fedha, na kwa kuzingatia mambo yote muhimu. Pia, kutathmini mashirika ya umma katika kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi, pamoja na sheria ya bajeti, kanuni na miongozo. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini ufanisi wa mashirika ya umma katika kusimamia fedha za umma na kutoa huduma kwa wananchi.

### 1.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulihusisha taarifa za fedha na ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria na kanuni katika mashirika ya umma, ikijumuisha usimamizi wa mapato,

---

usimamizi wa matumizi, usimamizi wa mikataba na ununuza, usimamizi wa mishahara na rasilimali watu, utendaji kazi katika sekta ya elimu, afya, usafiri na maji, na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ukaguzi pia, ulijumuisha tathmini ya usimamizi wa viashiria vya hatari, udhibiti wa ndani, na mifumo ya utawala kwa mashirika ya umma.

### 1.3 **Methodolojia ya Ukaguzi**

Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) viliviyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA).

Methodolojia ya ukaguzi ilijumuisha njia mbali mbali, kama vile kukagua kumbukumbu na nyaraka, kufanya usaili, na kutembelea maeneo mbalimbali yaliyokaguliwa. Ukaguzi pia, ulihusisha kupima mifumo ya udhibiti wa ndani wa mashirika ya umma pamoja na kutathmini uzingatiaji wa sheria, kanuni na sera katika mashirika husika.

Aidha, ukaguzi wa kina wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ulifanyika. Ukaguzi huu ulizingatia viwango vya kimataifa kama vile ISSAI, Mwongozo wa Ukaguzi, viwango vya Wakala wa Serikali Mtandao (eGA), COBIT 5, na ISO/IEC 27001. Lengo lilikuwa kutathmini ufanisi wa mifumo, uthabiti, usalama, na hatari zinazohusiana. Lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha kama mifumo ya TEHAMA ipo salama na inafanya kazi kwa ufanisi kusaidia malengo ya Serikali.

# SURA YA PILI



## HATI ZA UKAGUZI

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea hati za ukaguzi nilizotoa kwa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23. Vilevile, inaonesha mwenendo wa maoni ya hati za ukaguzi nilizotoa juu ya taarifa za kifedha kwa miaka mitano mfululizo.

Hati za ukaguzi zilizotolewa zilitokana na tathmini ya ushahidi wa kikaguzi uliopatikana wakati wa ukaguzi, kwa kutathmini ikiwa taarifa za kifedha zinazingatia viwango husika vya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha kwa masuala yote muhimu. Viwango hivyo ni kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha (IFRSs), Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAs), na Kiwango cha Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha Tanzania Na. 1 (TFRS1). Tathmini hii inazingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

### 2.1 Aina za hati za ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi: hati inayoridhisha, hati yenze shaka, hati mbaya, na kushidwa kutoa maoni.

**Hati inayoridhisha:** Hii hutolewa wakati mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi kwa wa kuzingatia viwango na mfumo unaokubalika wa uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha.

**Hati yenze shaka:** Hii hutolewa pale taarifa za kifedha zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo baada ya kupata vielelezo na uthibitisho wa kikaguzi wa kutosha, mkaguzi anahitimisha kuwa makosa kwenye maeneo hayo likiwa moja au yakiwekwa pamoja yana athari, lakini hayaathiri maeneo yote katika taarifa za kifedha.

Pia, hati yenyе shaka hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata vielelezo na uthibitisho wa kikaguzi wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za kifedha.

**Hati mbaya:** Hii hutolewa pale mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo na uthibitisho wa kikaguzi sahihi na wa kutosha kudhihirisha kuwa kuna makosa kwenye taarifa za kifedha, na, kuwa, makosa hayo ama kwa kuyaangalia mojamoja au kwa ujumla wake ni makubwa na yenyе athari kwa taarifa zote za kifedha; hivyo, kuhitimisha kuwa taarifa hizo hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha.

**Kushindwa kutoa maoni:** Hii hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata vielelezo na uthibitisho sahihi na wa kutosha wa kikaguzi kuhusu taarifa za kifedha ili kumuwezesha kutoa hati ya ukaguzi; hivyo, mkaguzi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenyе athari kwa maeneo yote ya taarifa hiyo.

Pia, ikiwa kuna mazingira yenyе mashaka, Mkaguzi anaweza kushindwa kutoa maoni, licha ya kuwa amepata vielelezo na uthibitisho wa kikaguzi wa kutosha kuhusu kila shaka. Hii inatokana na kuwapo kwa uhusiano wa moja kwa moja na wenye athari kwenye maeneo yote ya taarifa za kifedha, hivyo kumuuwia ngumu mkaguzi kutoa maoni ya ukaguzi.

## 2.2 Hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, nimekamilisha kaguzi 215 za mashirika ya umma na kutoa hati za ukaguzi. Kati ya hati za ukaguzi 215 nilizotoa, 211 zinaridhisha, na nne ni yenyе shaka. Ongezeko la idadi ya mashirika kutoka 203 mwaka uliopita hadi 215 mwaka huu linatokana na sababu zifuatazo: kujumuishwa kwa mashirika ambayo hayakuwa na bodi ya wakurugenzi mwaka jana; kujumuishwa kwa mashirika yaliyohamishiwa divisheni ya mashirika ya umma mwaka huu; na kujumuishwa mashirika yaliyokaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka huu. Taarifa za hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu zimeoneshwa katika **Kiambatanisho Na. I.**

### 2.3 Mwenendo wa hati za ukaguzi

Jedwali Na. 1 linaonesha mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mashirika ya umma kwa miaka mitano mfululizo tangu mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23. Ongezeko la hati zinazoridhisha kutoka asilimia 97 mwaka jana hadi asilimia 98 mwaka 2022/23 ni matokeo ya uboreshaji katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa idadi**

Aina ya hati ya ukaguzi	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Inayoridhisha	147	162	185	196	211
Yenye shaka	0	3	8	5	4
Kushidwa kutoa maoni	0	0	2	2	0
Mbaya	1	0	0	0	0
<b>Jumla</b>	<b>148</b>	<b>165</b>	<b>195</b>	<b>203</b>	<b>215</b>

**Chanzo:** Uchambuzi wa taarifa za kifedha zilizokaguliwa

# SURA YA TATU

## MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA NA MAAGIZO YA PAC



### 3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji na hatua zilizochukuliwa na maafisa masuuli katika kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa menejimenti na bodi za mashirika ya umma .

Ninatambua juhudini zilizofanywa na maafisa masuuli katika kujibu na kuandaa mpango wa utekelezaji wa mapendekezo yangu na kufanya kazi maagizo yaliyotolewa na PAC kwa mashirika ya umma katika kutekeleza majukumu yao ya uangalizi na usimamizi.

### 3.1 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita katika mashirika ya umma

Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita hadi mwaka wa fedha 2021/22 imeonesha kuwa hali ya utekelezaji kwa jumla ni ya kuridhisha. Maeleo ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita kwa mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22 yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita katika mashirika ya umma**

Mwaka wa Fedha	Yame tekelezwa	Yanayo tekelezwa	Hayaku tekelezwa	Yamepitwa na muda	Jumla
2021/22	2,413 (39%)	2,776 (45%)	720(12%)	242(4%)	6,151
2020/21	2,195 (36%)	2,611 (43%)	1,064(17%)	276 (4%)	6,146

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23

Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mapendekezo yangu kunaleta uwerekano wa hatari ya kujirudia kwa dosari nilizo kwisha kuzibainisha. Hivyo, kunyaweka mashirika katika hatari ya udanganyifu, upungufu



## Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita na maagizo ya pac

wa ufanisi, na kushindwa kutekeleza majukumu yao. Ninasisitiza menejimenti za mashirika husika zitekeleze kikamilifu mapendekezo yote ambayo hayajatekelezwa ili kuboresha ufanisi wa udhibiti wa ndani.

### 3.2 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2022/23

Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 kinahitaji maafisa masuuli wa mashirika ya umma kuzingatia maagizo yanayotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali juu ya masuala ya kifedha.

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya PAC hadi mwaka wa fedha 2022/23, imeoneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

#### Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya kudumu ya bunge

Mwaka wa fedha	Yame tekelezwa	Yanayo tekelezwa	Hayaku tekelezwa	Jumla
2022/23	45(33%)	89(65%)	2(2%)	136
2021/22	70(43%)	92(56%)	1(1%)	163

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23

Pia, nilibaini kuwa, mashirika ya umma nane yalikuwa na maagizo 20 ambayo hayakutekelezwa kikamilifu kwa kipindi kinachoanzia miaka sita hadi 12, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4**.

#### Jedwali Na. 4: Mashirika yenye maagizo ya muda mrefu kutoka kwa kamati

Na.	Jina la Shirika	Yanayo tekelezwa	Hayaku tekelezwa	Jumla	Mwaka wa Maagizo	Idadi ya maagizo
1	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi	3		3	2010/11	12
2	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	3		3	2010/11	12
3	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	2		2	2011/12	11
4	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	2		2	2014/15	9
5	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi	2		2	2015/16	7
6	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	1		1	2016/17	6
7	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa	1	1	2	2016/17	6



## Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita na maagizo ya pac

Na.	Jina la Shirika	Yanayo tekelezwa	Hayaku tekelezwa	Jumla	Mwaka wa Maagizo	Idadi ya maagizo
	Mazingira Dar es Salaam					
8	Hospitali ya Taifa Muhimbili	5		5	2017/18	6
	Jumla	20				

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukgazi kwa mwaka 2022/23*

Yafuatayo ni maagizo ya PAC ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu kwa muda mrefu: -

- a) Kwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, zikiwamo Lindi, Shinyanga, Mwanza, na Dar es Salaam: kupunguza ghamra za uendeshaji ili kuendana na ukusanyaji wa mapato; kuongeza juhudhi katika kupunguza upotevu wa maji; kulinda mazingira yaliyo karibu na vyanzo vya maji ili kuzuia upungufu wa maji; na kuhakikisha ukusanyaji wa madeni unafanyika kwa wakati.

Tathmini yangu ya jumla ilibaini kuwa maagizo hayakutekelezwa kikamilifu. Hii nikutokana na upungufu wa fedha; viwango vya sasa vya malipo vinavyotozwa kwa watumiaji wa maji havikidhi ghamra za uendeshaji, hivyo kusababisha mamlaka kutegemea msaada wa Serikali. Aidha, madeni yaliyosalia, kwa kiasi kikubwa ni kutoka katika taasisi za Serikali kwa huduma za maji zinazotolewa kwa taasisi hizo.

- b) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ilitakiwa kufuta madeni ya muda mrefu inayoyadai; na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, iliagizwa kufuta maduhuli ya muda mrefu pamoja na mkopo wa wafanyakazi. Wakati huohuo, uongozi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ulielekezwa kuhakikisha kuwasilisha makato ya kodi ya mapato yatokanayo na ajira (PAYE) kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa wakati; na kuwalipa wazabuni wanao idai Hospitali kwa muda mrefu.

Vilevile, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kilielekezwa kuandaa mpango sahihi wa motisha kwa wafanyakazi wake ambao unaendana na maelekezo ya Serikali. Maagizo ya PAC hayakutekelezwa kikamilifu kutopteka na masuala kadhaa. Miiongoni mwa masuala hayo ni: mizozo, madeni ambayo hayana nyaraka za ushahidi, na kuitegemea sana Serikali katika kuwalipa wazabuni.

# SURA YA NNE

## UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA



### 4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma, ikizingatia faida, manufaa, na ukwasi. Tathmini hii inafanywa kwa aina mbili za mashirika: yanayojiendesha kibiashara na yasiyo ya kibiashara. Tathmini hii ilitumia taarifa za kifedha za mwaka wa 2022/23 kwa kulinganisha na zile za mwaka wa fedha wa 2021/22.

Mashirika ya kibiashara yanazingatia kupata faida na hayategemei ruzuku kutoka Serikalini pekee. Kwa upande mwingine, mashirika yasiyo ya kibiashara yanalenga kutoa huduma kwa umma na faida siyo lengo kuu la mashirika haya. Aidha, mashirika yasiyo ya kibiashara na hutegemea ruzuku ya Serikali, ada, tozo, na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Sura hii haijumuishi benki zinazomilikiwa na Serikali, mifuko ya hifadhi ya jamii, na taasisi zinazohusika na biashara ya dhamana zinazouzwa. Mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu ni kama yafuatayo:

### 4.1 Taasisi zilizopata hasara au nakisi

Kutokana na ukaguzi wa utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini mashirika ya umma 34 yaliripoti hasara au nakisi kwa miaka miwili mfululizo. Mashirika haya yalijumuisha mashirika yanayojiendesha kibiashara 11 na mashirika yasiyo ya kibiashara 23.

Mashirika yasiyo ya kibiashara yaliripoti nakisi kutokana na upungufu wa fedha kutoka Serikalini na vyanzo mbadala vya mapato. Mashirika yanayojiendesha kibiashara yalipata hasara kutokana na utendaji

usioridhisha katika uwekezaji uliofanywa, shughuli za biashara, na usimamizi hafifu wa matumizi na mapato. Orodha ya mashirika yenye hasara au nakisi kwa miaka miwili mfululizo imeainishwa katika **Kiambatisho Na. II.**

Pia, nilibaini kuwa mashirika ya umma 24 yaliyopata faida au ziada katika mwaka wa fedha 2021/22, yamepata hasara au nakisi katika mwaka wa ukaguzi wa 2022/23 kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. III.** Yafuatayo ni maelezo kwa ufupi juu ya utendaji wa mashirika ya kibiashara yaliyopata hasara:

**Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL)** imeendelea kupata hasara kwa miaka sita mfululizo. Mwaka wa fedha wa 2022/23 Kampuni ilipata hasara ya shilingi bilioni 56.64, hasara hii imeongezeka ikililinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 35.23 mwaka wa 2021/22, ATCL imeendelea kupata hasara licha ya kuwa inapokea ruzuku kutoka Serikalini. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2022/23, ATCL ilipokea ruzuku ya shilingi bilioni 31.55 kwa ajili ya kugharamia mishahara ya wafanyakazi, mafunzo ya majaribio, na ruzuku ya shilingi bilioni 7.45 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Sababu zinazopelekea hasara zinajumuisha kuwapo kwa gharama kubwa za uendeshaji wa shughuli za ATCL, pamoja na gharama zisizoepukika kama vile gharama za ukodishaji na bima kwa ndege ya Airbus A220 - 300 isiyofanya kazi kutokana na matatizo ya kiufundi kama vile kutu na kasoro za injini. Matatizo haya yamegunduliwa na mtengenezaji wa ndege hiyo na yameathiri idadi ya ndege za aina hi kote ulimwenguni.

Kuharibika kwa ndege ya Airbus A220 - 300 kuliathiri mwenendo wa safari za ndege, hivyo kusababisha ATCL kukosa mapato na kushindwa kufidia gharama za kudumu za ndege iliyoharibika. Aifha, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuboresha uendeshaji wa kampuni hii ikiwemo, kuundwa kwa timu ya wataalamu inayofanya tathmini ya masuala ya kiufundi ya ndege, kifedha na utendaji wa ATCL katika biashara ya usafiri wa anga.

**Kampuni ya Mawasiliano ya Tanzania (TTCL)** imepata hasara kwa miaka miwili mfululizo. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, kampuni ilipata hasara ya shilingi milioni 894 ikililinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 19.23 katika mwaka wa fedha 2021/22. Mwelekeo huu unaonesha kuwa TTCL imefanikiwa kupunguza hasara kwa asilimia 94 ikililinganishwa na mwaka uliopita.

Sababu ya kupungua kwa hasara ni ongezeko la mapato mengineyo kwa shilingi bilioni 8.05. Kwa upande mwengine, kuna kupungua kwa gharama kama vile gharama za mauzo kwa shilingi bilioni 12.58 na gharama za uendeshaji wa mtandao kwa shilingi bilioni 6.22. Haya ni matokeo ya mkakati wa kudhibiti gharama uliotumiwa na TTCL katika mwaka wa fedha wa 2022/23.

Aidha, tarehe 30 Oktoba 2022, Serikali ilitangaza nia ya kuhamisha umiliki wa Mkongo wa Taifa (NICTBB) kwenda Kampuni ya TTCL. Uamuzi huu unatarajiwa kuongeza mali za kampuni katika mwaka wa fedha 2023/24, kwa ongezeko la zaidi ya shilingi bilioni 400 kutokana na NICTBB. Vilevile, mapato ya jumla ya kampuni yanatarajiwa kuongezeka kwa zaidi ya shilingi bilioni 20 kutokana na NICTBB.

**Shirika la Masoko la Kariakoo** limepata hasara mfululizo kwa miaka miwili iliyopita. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, shirika limepata hasara ya shilingi bilioni 41.57, ambayo ni kubwa kuliko hasara ya shilingi milioni 517.97 iliyopatikana katika mwaka wa fedha uliopita 2021/22. Sababu kuu ya hasara hii ni kusitishwa kwa ukusanyaji wa mapato katika eneo la soko la Kariakoo. Hii ni baada ya tukio la moto mwaka 2020 ulioteketeza jengo la soko la Kariakoo.

Kwa matokeo hayo, shirika lilishindwa kukusanya mapato katika soko kwa ukamilifu kuanzia mwaka wa fedha 2020 hadi Juni 2023 kutokana na kusitishwa kwa shughuli za soko ili kupisha ujenzi wa majengo. Aidha, shirika lilirekodi hasara ya shilingi bilioni 41.25 kutokana na kupoteza thamani kwa jengo lililoungua ambapo ni sehemu ya matumizi yaliyorekodiwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Ukiondoa tukio la moto la mwaka 2020, ambalo lisisababisha kupungua kwa ukusanyaji wa mapato, Serikali imekuwa ikilipa gharama za uendeshaji wa kampuni, ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi na gharama zingine. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilitenga shilingi milioni 671.15 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na shilingi milioni 518.68 kwa matumizi mengineyo. Pamoja na Ruzuku kutoka Serikalini, Shirika la Masoko la Kariakoo linaendelea kupata hasara.

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)** limepata hasara mfululizo kwa miaka miwili iliyofuatana. Katika mwaka wa fedha 2022/23, shirika lilipata hasara ya shilingi bilioni 100.70, ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 190.01 katika mwaka wa fedha 2021/22. Shirika limeendelea kupata hasara licha ya kuwa linapokea ruzuku kutoka Serikalini. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilitoa jumla ya shilingi

bilioni 32.81 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengine ya kawaida kwa TRC.

Miongoni mwa sababu zilizochangia hasara hiyo ni idadi ndogo ya mabehewa ya kubeba mizigo ambayo iliathiri mwenendo wa biashara ya usafirishaji mizigo. Sababu nyingine ni ongezeko la gharama za uendeshaji wa biashara ya usafirishaji kutoka shilingi bilioni 44.30 hadi shilingi bilioni 46.83.

**Kituo cha Uwekezaji cha APC** kimepata hasara kwa miaka miwili mfululizo katika shughuli zake. Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, kituo kilipata hasara ya jumla ya shilingi bilioni 1.2, ambayo ni ndogo kutoka shilingi bilioni 1.95 iliyopatikana katika mwaka wa fedha uliopita 2021/22. Licha ya kupata hasara kwa miaka miwili, Kituo hicho kilifanikiwa kupunguza kiwango cha hasara kwa shilingi bilioni 0.75, sawa na asilimia 49. Kupungua kwa hasara, kwa kiasi, kikubwa kimechangiwa na ongezeko la mapato na kupungua kwa riba kwenye mkopo. Hasara iliyopatikana kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na ongezeko la gharama za mauzo kufikia shilingi milioni 717.49 kutoka shilingi milioni 594.10. Pia, hasara ilisababishwa na kuongezeka kwa gharama za utawala kwa asilimia 15 kwa mwaka wa fedha wa 2022/23, kutoka shilingi bilioni 1.06 zilizoripotiwa katika mwaka uliotangulia, 2021/22.

**Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL** imepata hasara ya shilingi bilioni 76.56 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 7.84 kwa mwaka wa fedha uliopita. Hii inaonesha ongezeko la shilingi bilioni 68.72 ikilinganishwa na hasara iliyopatikana mwaka wa fedha 2021/22. Sababu kuu ya hasara ya kampuni ilikuwa mafuta yaliyoagizwa kutoka nje kuzuwa kwa sababu ya TANOIL kushindwa kuwalipa wauzaji. Athari ya mafuta yaliyozuiwa ni gharama kubwa za kuhifadhi mafuta (shilingi bilioni 12.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.1 mwaka uliopita).

Sababu nyingine ilikuwa ukusanyaji duni wa mapato ambapo katika mwaka wa fedha wa 2022/23, mapato ya kampuni kutokana na mauzo ya mafuta yalipungua kwa shilingi bilioni 296 ambayo ni asilimia 49. Hii ilitokana na kupungua kwa kiwango cha mafuta kilichouzwa ambapo ni lita milioni 112 ziliuzwa katika mwaka wa 2022/23 ikilinganishwa na lita milioni 264 zilizouzwa mwaka uliotangulia.

Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ilipata hasara kwa miaka miwili mfululizo licha ya kuongezeka kwa mapato kutokana na shughuli za ubadilishaji. Mapato yaliongezeka kwa asilimia 7, kutoka shilingi milioni 162 kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 hadi shilingi milioni 173 kwa mwaka 2022/23. Ongezeko la mapato lilitokana na ongezeko la shughuli za biashara baada ya kuanzishwa kwa majukwaa ya biashara ya kakao, ufuta, na kahawa. Pia, sababu nyingine ni ruzuku ya Serikali ya shilingi bilioni 1.04 iliyotolewa na Serikali ili kufanikisha matumizi mengine ya uendeshaji wa kampuni.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, TMX ilipata hasara ya shilingi milioni 720 ikilinganishwa na hasara ya shilingi milioni 512 katika mwaka wa fedha 2021/22. Hasara hiyo, kwa kiasi kikubwa, ilitokana na TMX kuendelea kufanya kazi kwa msingi wa mnada, bila ya kutoza ada zinazoiwezesha TMX kurejesha gharama za uendeshaji.

**Kampuni ya Maendeleo ya Nishati ya Joto Ardhi Tanzania (TGDC)** ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO ilipata hasara ya shilingi bilioni 1.24 katika mwaka wa fedha wa 2022/23, ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 0.79 katika mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22. Hii ilipelekea ongezeko la hasara kwa asilimia 57. Moja ya sababu za hasara ilikuwa gharama kubwa za uendeshaji zilizosababishwa na utekelezaji wa miradi, pamoja na uwekezaji usiotosheleza wa mtaji kutoka kwa kampuni mama ya TANESCO.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, kampuni ilipata ruzuku ya shilingi milioni 201.48 kutoka Serikalini na wafadhili wengine, na fedha zilizotolewa na TANESCO kwa mwaka ziliwa shilingi bilioni 6.24.

Pamoja na ruzuku kutoka Serikalini na ufadhili kutoka kampuni mama ya TANESCO, TGDC bado inafanya kazi kwa hasara.

**Kampuni ya T-PESA** licha ya kupata faida ya shilingi milioni 55.14 katika mwaka wa fedha uliopita 2021/22, kampuni ilipata hasara ya shilingi milioni 352.74 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hasara iliyopatikana ni mara tano zaidi ya faida iliyopatikana mwaka wa 2021/22. Hii imetokana na kupungua kwa mapato kwa shilingi milioni 439.25 ambayo ni sawa na asilimia 31 ikilinganishwa na mapato yaliyopatikana mwaka wa 2021/22 ya shilingi bilioni 1.42. Uchambuzi zaidi wa uendeshaji wa T-PESA kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 ulionesha kuwa kiwango cha umiliki wa soko wa T-PESA ni asilimia 3, ikilinganishwa na makampuni

mengine katika tasnia ya pesa mtandao, ambayo kwa pamoja ilikuwa na miamala iliyofikia karibu shilingi bilioni 47.

**Shirika la Posta Tanzania** lilipata hasara ya shilingi bilioni 1.34 katika mwaka wa fedha 2022/23 wakati mwaka wa fedha uliopita 2021/22 lilipata faida ya shilingi bilioni 16.21. Faida katika mwaka wa fedha uliopita 2021/22 ilitokana na faida ya mauzo ya mali za shirika ambayo ilikuwa shilingi bilioni 22.65. Sababu ya hasara katika mwaka huu ilichangiwa na kupungua kwa huduma za EMS kutoka shilingi bilioni 18.91 hadi shilingi bilioni 14.86, huku gharama za uendeshaji zikibaki karibu sawa ikilinganishwa na mwaka uliopita (shilingi bilioni 37.46 kwa mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 37.92 kwa mwaka 2021/22).

**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora** ilipata nakisi ya shilingi bilioni 1.28 katika mwaka wa fedha 2022/23. Hii ilitokana na gharama kubwa za uendeshaji ikilinganishwa na mapato yaliyopatikana. Kinyume chake, katika mwaka uliopita wa 2021/22, mamlaka ilikuwa na ziada ya shilingi bilioni 68.94 ambayo ilitokana na ruzuku ya shilingi bilioni 71.89 kutoka Serikalini kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya maji.

Hali kama hiyo imetokea kwa mamlaka zingine za majisafi kama vile **Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu, na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga**. Nakisi katika mwaka 2022/23 ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, wakati ziada katika mwaka wa fedha 2021/22 ilitokana na ruzuku ya Serikali iliyotengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, taasisi tatu zinazojihusisha na shughuli za utalii ambazo ni TANAPA, **Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, na Bodi ya Utalii Tanzania** zilipata nakisi katika mwaka wa fedha 2022/23 ya shilingi bilioni 5.79, shilingi bilioni 19.11 na shilingi bilioni 5.47 bilioni, mtawalia. Hii ni tofauti na ziada ya shilingi bilioni 21.12, shilingi bilioni 13.87 na shilingi bilioni 7.23, mtawalia, zilitokana na upungufu wa ruzuku kutoka Serikalini kufidia matumizi ya taasisi hizo.

Ninarejea mapendekezo yangu kuwa; (a) **Mamlaka husika za umma zichagize juhudzi za Mamlaka hizo katika kuboresha ufanisi wa uendeshaji ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua**

madhubuti za kupunguza ghamama. Aidha, mamlaka hizo zinahitaji kuendeleza mikakati ya kugeuza mwelekeo kwa uwekezaji usio na ufanisi na shughuli za biashara ili kusaidia kurejesha fedha za uwekezaji na uzalishaji wa mapato; (b) Serikali ihakikishe kuwa mashirika yanaendeshwa na wafanyakazi wenyewe kiwango kinachohitajika cha ujuzi na uwezo, hivyo kuongeza ufanisi wa biashara; na (c) Serikali iimarishie uangalizi wa taasisi kwa kuteua wajumbe wa bodi wenyewe utaalamu na maarifa katika sekta na ujuzi wa biashara.

#### 4.2 Mashirika ya umma yenyе mitaji hasi

Nimekagua utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma na nilibaini mashirika 11 yalikuwa na mtaji hasi katika mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni 2023. Kati ya mashirika haya, matano ni mashirika yanayo jiendesha kibashara, wakati sita mengine ni mashirika yasiyo ya kibashara. Idadi ya mashirika yenyе mtaji hasi kwa jumla iliongezekwa kutoka mashirika 10 kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22 hadi 11 katika mwaka wa fedha wa 2022/23. Sababu kuu za mtaji hasi zilikuwa matokeo ya hasara za muda mrefu na madeni makubwa kwa mashirika hayo katika kufadhili uendeshaji wao. Mtaji hasi unanipa mashaka kuhusu uwezo wa mashirika haya katika kutoa huduma na kutimiza majukumu yao baadaye. **Jedwali Na. 5** linaonesha mashirika yenyе mtaji hasi.

**Jedwali Na. 5: Mashirika yenyе mitaji hasi**

Na.	Jina la Taasisi	Jumla ya Mali (Sh. Milioni)	Jumla ya Madeni (Sh. Milioni)	Mtaji (Sh. Milioni)
<b>Mashirika ya Kibashara (Hasara)</b>				
1	Kampuni ya Ndege ya Tanzania	339,387.93	553,738.27	(214,350.34)
2	Kampuni ya STAMIGOLD	68,006.90	74,889.74	(6,882.89)
3	Kampuni ya Gesi Tanzania	22,424.00	25,707.00	(3,283.00)
4	Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	906.8	1,487.12	(580.32)
5	Kampuni ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	1,148.04	1,420.04	(272.00)
<b>Mashirika yasiyo ya kibashara (pungufu)</b>				
6	Mamlaka ya Udhibili wa Mbolea Tanzania	6,490.47	262,533.49	(256,043.02)
7	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	148,392.21	168,274.87	(19,882.65)
8	Bodi ya Pareto Tanzania	580.07	2,019.75	(1,439.68)
9	Bodi ya Maziwa Tanzania	146.75	259.38	(112.63)
10	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	28.11	74.31	(46.19)

11	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	80.36	82.97	(2.61)
----	--	-------	-------	--------

Chanzo: *Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2022/23*

Narudia mapendekezo yangu kwa mashirika ya umma husika kuwa; (a) yafanye uchambuzi kamili wa hali zao za kifedha ili kubaini sababu za msingi za mtaji hasi. Pia, yatengeneze mkakati imara wa kukabiliana na changamoto hizi. Mkakati huu unaweza kujumuisha mipango ya kupunguza gharama, kuimarisha ufanisi, kuongeza mapato, kurekebisha madeni, au kuuza mali ambazo siyo za msingi; na (b) yatengeneze na kutekeleza mikakati ya kuwezesha uhimilivu wa muda mrefu ili kuwa na mtaji wa kutosha.

#### 4.3 **Mashirika ya umma yasiyo na uwezo wa kulipa madeni ya muda mfupi**

Ukaguzi wangu wa hali ya kifedha ya mashirika ya umma 215 uliofanywa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ulibaini uwepo wa mashirika 63 yenye madeni makubwa ya muda mfupi kuliko mali za muda mfupi. Mashirika 13 kati ya haya ni ya kibiashara na mashirika 50 si ya kibiashara. Hali hii si nzuri ikilinganishwa na mashirika 45 yenye madeni ya aina hiyo yaliyori potiwa katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22. Nilibaini pia kuwa uwiano wa mali za muda mfupi na deni la muda mfupi kwa mashirika haya ulikuwa kati ya 0.01 na 0.98, kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. IV**.

Hii inamaanisha kuwa mashirika 63 yana changamoto za uwezo wa ukwasi. Uwiano huo unaonesha usimamizi hafifu wa mzunguko wa fedha, au kutegemea sana kukopa kwa muda mfupi. Kushindwa kukidhi majukumu ya kifedha kunaweza kusababisha kutolipa mikopo, kuchelewesha malipo kwa wazabuni au wafanyakazi, kuharibu sifa ya taasisi, na kudhoofisha uwezo wake wa kufanya kazi kwa ufanisi. Hali hii inaweza kusababisha upungufu wa bajeti, kuzuia uwezo wa taasisi kutoa huduma muhimu na kutimiza majukumu yake.

Narudia mapendekezo yangu kwa mashirika ya umma husika kuwa; (a) yafanye mapitio kamili ya bajeti ya taasisi ili kutambua maeneo yenye matumizi makubwa au ufanisi duni na kurekebisha mgawo wa bajeti kwa kuweka kipaumbele kwa matumizi muhimu na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima; na (b) yaelekeze juhudhi katika kuimarisha vyanzo vya mapato na kutumia rasilimali zote zinazopatikana ili kusimamia mzunguko wa fedha kwa ufanisi.

## 4.4

**Mashirika ya umma yanayoendeshwa kwa kutumia mikopo**

Matumizi ya ufadhili wa deni ni kawaida katika mashirika ya umma, lakini huongeza hatari ya kifedha. Uwiano wa deni, unaoonesha kiwango cha deni kulinganisha na mtaji, ni kipimo muhimu cha kutegemea deni badala ya mtaji. Uwiano wa deni zaidi ya asilimia 100 unaashiria matumizi makubwa ya deni, hivyo huiweka taasisi katika hatari ya mzigzo mkubwa wa kifedha wakati wa kushuka kwa uchumi au mabadiliko ya mazingira ya biashara.

katika ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa mashirika 28 (mashirika 12 ya kibiashara na 16 yasiyo ya kibiashara) yalikuwa na uwiano usiyordhisha wa madeni (jumla ya madeni/jumla ya mtaji) kwa zaidi ya asilimia 100. Hii inaonesha kuwa mashirika haya, kwa kiasi kikubwa, yanategemea madeni kujiendesha. Mashirika hayo yanajiweka kwenye hatari zaidi ya kifedha inayotokana na gharama kubwa za madeni. Hii inaonesha ongezeko la mashirika saba ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita wa 2021/22. Hii ilichangiwa na sababu kadhaa, kama vile kutokutumika kwa ruzuku za mtaji zilizopitwa na wakati; mikopo ya ziada na ongezeko la gharama za kukopa, na kuchelewa kulipa kiasi kilichokuwa cha deni na riba. Mashirika yenye madeni zaidi ya mtaji yako kwenye **Kiambatisho Na. V.**

Narudia mapendekezo yangu kwa mashirika ya umma husika kuwa; (a) yadhibiti utendaji wa kifedha na kutathmini athari inayoweza kutokea kutokana na mabadiliko yoyote kwenye soko au uchumi kwenye uwezo wa kutimiza majukumu yao; (b) yatathmini muundo wa mtaji na ulipaji wa deni ilikuzuia ukuaji wa riba unaotokana na kuchelewa kulipa deni, na (c) Serikali itathmini uwepo wa haya mashirika na kuangalia kama Serikali inahitaji kuendelea nayo au la.

## 4.5

**Upungufu uliobainika katika uchangiaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda mfuko mkuu wa Serikali shilingi bilioni 36.33**

Kifungu Na. 2 cha Sheria ya Fedha za Umma (Uhamishaji wa mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mashirika ya umma na taasisi zingine za Serikali) ya mwaka 2019 kinayataka mashirika ya umma na mamlaka zilizoainishwa kulipa asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda mfuko mkuu wa Serikali.

Nilibaini upungufu katika uchangiaji huo ambapo Kati ya mashirika ya umma 12 yaliyotakiwa kutoa mchango, saba yalichangia chini ya kiasi

kinachohitajika. Hali hii ni ukiukaji wa agizo lililotajwa hapo juu. Mchanganuo wa mashirika hayo na kiasi yalichochangia umeoneshwa katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Upungufu wa uchangiaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi**

N a.	Jina la Taasisi	Mapato ghafi	Mchango uliotakiwa	Mchango halisi	Nakisi
			Shilingi milioni		
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	135,283.23	20,292.48	0	(20,292.48)
2.	Shirika la Viwango Tanzania	84,400.07	12,660.01	6,660.36	(5,999.65)
3.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania	23,681.69	3,552.25	206.90	(3,345.35)
4.	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii Stadi	16,925.28	2,538.79	200.00	(2,338.79)
5.	Baraza la Taifa la Uwezesajhi Wananchi Kiuchumi	13,587.60	2,038.14	300.00	(1,738.14)
6.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	14,136.18	2,120.43	0	(2,120.43)
7.	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana	3,654.51	548.18	51.38	(496.80)
Jumla		291,668.56	43,750.28	7,418.64	(36,331.64)

**Chanzo:** Uchambuzi wa taarifa za fedha 2022/23

Kushindwa kuchangia michango hii kunainyima Serikali mapato yanayohitajika kwa ajili ya utoaji wa huduma za umma.

**Ninapendekeza Serikali iboreshe mbinu za ufuutiliaji na utekelezaji wa sheria hii, ikiwa ni pamoja na kutoza adhabu kwa ukiukwaji kwa mashirika ya umma.** Pia, msajili wa hazina anapaswa kufanya ufuutiliaji ili kuhakikisha michango ya mashirika ya umma inalipwa kulingana na mahitaji ya agizo la Sheria ya Fedha za Umma la 2019.

#### 4.6 Kushuka kwa ulipaji au kutolipwa kwa gawio kwa mashirika ya umma ya kibiashara

Ukaguzi wangu wa mashirika ya umma 21 ya kibiashara ulibaini kuwa mashirika ya umma matatu yalipata faida lakini hayakutoa gawio, na mashirika ya umma 10 yaliripoti hasara kwa mwaka 2022/23; hivyo hayakuweza kulipa gawio (**Jedwali Na. 7**).

Hii inaonesha hali kuimariika ikilinganishwa na mwaka uliopita 2021/22, ambapo niliripoti mashirika tisa ya umma yenye faida ambayo hayakulipa gawio, huku mashirika nane yalipata hasara. Aidha, nilibaini kuwa Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing lililopata faida katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23, vilevile liliendelea kutolipa gawio.

**Jedwali Na. 7: Mashirika ya umma ambayo hayakulipa gawio**

Na.	Jina la shirika	Faida/(Hasara) Shilingi milioni
1.	Kampuni ya Huduma ya Meli	18,993.16
2.	Shirika la Nyumba la Taifa	58,673.91
3.	Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing	62.38
4.	Shirika la Reli Tanzania	(100,704.74)
5.	Kampuni ya Ndege ya Tanzania	(56,640.69)
6.	Benki ya Biashara Tanzania	(42,004.22)
7.	Shirika la Taifa la Maendeleo	(5,308.20)
8.	Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro	(4,236.20)
9.	Kituo cha Uwekezaji APC	(1,200.30)
10.	Shirika la Posta Tanzania	(1,343.79)
11.	Shirika la Mawasiliano Tanzania ( <i>Hesabu za Shirika pamoja na kampuni Tanzu</i> )	(1,232.00)
12.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	(1,997.00)
13.	Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania	(407.69)

**Chanzo:** *Uchambuzi wa taarifa za fedha 2022/23*

Katika Kampuni ya Huduma ya Meli, nilibaini kuwa kampuni haikulipa gawio kwa mwaka kutokana na kuwa katika mchakato wa mageuzi katika miradi yake ya maendeleo. Maoni yangu ni kuwa kutolipa gawio kunainyima Serikali fedha za kufanya shughuli zingine za maendeleo.

**Ninapendekeza mashirika ya umma ya kibiashara yaweke mikakati ya kupata faida ili kulipa gawio kwa Serikali.**



# SURA YA TANO

## UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA KUIMARISHA MAZINGIRA YA KIBIASHARA

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa uchambuzi juu ya ufanisi wa mashirika ya umma katika kuweka mazingira mazuri ya biashara. Inachambua majukumu, mikakati, sera, na mipango iliyotekelizwa na mashirika ya umma ili kuboresha hali ya biashara kwa ujumla na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi. Uchambuzi unatambua wigo wa uboreshaji wa uendeshaji katika mashirika matano ya umma kati ya mashirika 23 ya kimkakati, yaani Kampuni ya Ndege ya Tanzania, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Shirika la Nyumba la Taifa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA).

Ufanisi mdogo wa uendeshaji katika mashirika ya umma ambayo yameorodheshwa katika sura hii unajumuisha kuchelewa kukamilika kwa miradi, kutokutumia ipasavyo rasilimali zilizopo, na vizuizi vingine vilivybainishwa ambavyo vinahitaji kushughulikiwa ili kufikia utendaji bora. Mapungufu katika uendeshaji wa mashirika haya ya umma ni kama nilivyoeleza hapo chini.

#### 5.1 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Wakati wa ukaguzi wangu wa ufanisi wa uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania, nilibaini mapungufu yafuatayo.

##### 5.1.1 Kushindwa kulipa madai ya makandarasi kiasi cha shilingi bilioni 240.28

Mapitio yangu ya utekelezaji wa Miradi ya Uimarishaji wa Gridi ya Taifa na hali ya ulipaji wa madai ya makandarasi yalibaini kuwa, hadi tarehe 30 Juni 2023, kulikuwa na madai kadhaa ya makandarasi ikiwa ni pamoja na malipo ya awali na fidia yenyeye jumla ya shilingi bilioni 331.19

ambapo ni shilingi bilioni 90.91 tu ndizo zilizolipwa, huku kiasi cha shilingi bilioni 240.28 kikiwa bado hakijalipwa. Kuchelewa kulipa madeni kulichangisha na kukosekana kwa fedha kwasababu Serikali kupitia Wizara ya Nishati haikutoa fedha hizo.

Ninaamini kuwa, kutokulipa madai ya makandarasi kwa wakati kunaweza kupelekea hatari ya malipo makubwa ya riba ambayo yanaweza kuongeza gharama za mradi na kuchelewesha kukamilika kwa miradi kwa wakati unaofaa.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha itoe fedha za miradi kwa TANESCO kwa wakati ili kuepusha tozo za riba kwa ucheleweshaji wa malipo ya madai ya makandarasi.**

### **5.1.2 Mikataba iliyosainiwa kabla ya kutimiza matakwa ya kisheria ya malipo ya watu walioathirika na mradi shilingi bilioni 11.43**

Ukaguzi wangu wa utekelezaji wa miradi na ripoti za utekelezaji wa miradi ya Kuimarishe Gridi ya Taifa ulibaini kuwa baadhi ya miradi inahitaji fidia ya kulipwa kwa watu walioathirika na mradi ili kuwezesha utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, licha ya tathmini ya fidia kuidhinishwa na mamlaka husika mwezi Desemba 2022, utoaji wa fedha za malipo kwa ajili ya walioathirika wa miradi shilingi bilioni 11.43 ulikuwa bado haujakamilika hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 30 Juni 2023. Hali hii inaweza kusababisha Mkandarasi kuchelewa kukamilisha mradi kwa wakati kutohana na matatizo ya kifedha yanayosababishwa na ucheleweshaji wa malipo.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha itoe fedha za mradi kwa TANESCO na kuhakikisha watu wote ambao maeneo yao yamepitiwa na miradi wanalipwa stahiki zao ili kuwezesha utekelezaji wa miradi.**

### **5.1.3 Kuchelewa kutatua migogoro mitatu inayohusiana na tozo za Kampuni ya Songas shilingi bilioni 109.07**

Mnamo tarehe 11 Oktoba 2001, TANESCO na Kampuni ya Songas Limited walisaini Mkataba wa ununuvi wa umeme wa miaka 20, ambapo Kampuni ya Songas ilikubali kuza umeme kwa TANESCO na TANESCO ilikubali kununua umeme kutoka Songas kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa kwenye makubaliano.

Ukaguzi wangu wa utekelezaji wa mikataba na mwenendo wa malipo unaonesha kuwapo kwa mizozo endelevu ambayo haijatatuwa tangu mwaka 2022. Shirika la Umeme Tanzania lilipinga malipo hayo yanayofikia shilingi bilioni 67.94. Aidha, Kampuni ya Songas imeendelea kujumuisha gharama za kuboresha visima vya gesi (sinking cost) katika ankara za kila mwezi kuanzia mwezi Agosti 2022 hadi Juni 2023, yenye thamani ya shilingi bilioni 29.34, licha ya tangazo la kukataa tozo hizo lililotolewa na Shirika la Umeme Tanzania mwezi Desemba 2022.

Aidha, ankara iliyotolewa tarehe 4 Januari 2023, yenye thamani ya shilingi bilioni 23.94 na dola za Marekani milioni 4.02 kwa mwezi Desemba 2022, iliibua mzozo unaohusiana na deni la kodi ya ongezeko la thamani (VAT) la shilingi bilioni 11.78 ambalo halijalipwa kwa Mamlaka ya mapato (TRA) kutokana na kukosekana kwa nyaraka za kuthibitisha. Hata hivyo, hadi kufikia Desemba 2023, suala hili halikuwa limetatuliwa.

Kwa kuzingatia muda wa miaka 20 wa mikataba wa ununuzi wa umeme ambao unatarajia kuisha mwezi Oktoba 2024 na kuwapo kwa uwezekano wa kuongeza muda. Migogoro hii isiposuluhishwa inaweza kuleta utata wakati muda wa mikataba huo utakapoisha na kusababisha kuongezwa kwa muda wa mikataba huo ili kutoa njia ya kusuluhiha mizozo hiyo.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania liishirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupitia vipengele vya mikataba au makubaliano vinavyoipa Kampuni ya Songas haki ya kutoza gharama za “sinking” na kutatua migogoro kulingana na masharti ya mikataba.**

### 5.1.4 **Ubadirishwaji usio wa kawaida wa mita za umeme 108,088 katika kipindi cha muda mfupi**

Ukaguzi wangu wa ripoti ya kubadilisha mita katika mwaka wa fedha 2022/23 ulibaini kuwa jumla ya mita 108,088 kati ya mita 602,269 zilibadilishwa kabla ya kipindi cha uhai wa matumizi yake kuisha.

Upembusi zaidi ulibaini kuwa, mita 13,493 zilibadilishwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kufungwa, wakati mita 94,595 zilikuwa na muda mfupi wa matumizi kati ya mwaka mmoja hadi miaka 15 ikilinganishwa na muda unaotarajiwa wa miaka 20 ndipo zibadilishwe.

Hii imesababishwa na ubora duni wa mita zilizowekwa na pia mabadiliko ya haraka ya teknolojia ambayo yamesababisha kushindwa kufikia muda wake uliotarajiwa. Kubadilisha mita mapema husababisha gharama zaidi ambayo inaathiri utendaji wa kifedha wa shirika.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania; (a) lichunguze sababu za kubadilisha mita mapema kuliko muda unaotarajiwa wa matumizi; na (b) lihakikishe vipimo vya ubora wa mita vinafanyika ili kuongeza ufanisi wa kufikia muda wa matumizi unaotarajiwa ili kupunguza gharama zinazotokana na kubadilisha mita.**

### 5.1.5 Malipo kwa Mzabuni kwa kazi ambayo haikuthibitishwa na Mkandarasi Mshauri dola za Marekani milioni 10.16

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) lilifanya malipo ya dola za Marekani milioni 10.16 kwa mzabuni katika mkataba Na. PA/001/2018-2019/HQ/W/31 kwa ajili ya kubunifu, kusimika, kutekeleza, kutoa mafunzo na kuzindua mfumo wa usimamizi wa biashara; kusaidia miundombinu katika mfumo huo; na kutoa ushauri elekezi. Hata hivyo, nilibaini kuwa malipo hayo yalifanywa bila kuthibitishwa kwa ubora wa kazi husika na mshauri elekezi. Hii ni kinyume na Kifungu cha 4.4 cha Mwongozo wa Uendeshaji wa Kitengo cha Uwekezaji katika Shirika la Umeme Tanzania wa mwaka 2020 na Kifungu 3.3 cha Maelekezo ya Uhasibu C12 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Shirika la Umeme Tanzania wa mwaka 2022.

Hali hii imetokana na mratibu wa mradi aliyeulewa kutekeleza majukumu mawili kwa wakati mmoja, kama Meneja wa Mradi na kama mthibitishaji wa malipo ikiwa Mshauri elekezi hayupo. Kwa maoni yangu, katika hali kama hii kuna hatari ya mzabuni kulipwa kwa kazi ambazo hazijatekelezwa kama inavyotakiwa kwenye mkataba.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania; (a) limwagize mshauri elekezi anayehusika kufanya upya uthibitisho wa kazi zilizofanywa kwenye ankaa zilizokwishalipwa ili kubainisha usahihi wake na kama malipo yalifanyika kwa mujibu wa masharti ya mkataba; na (b) kwa siku zijazo, lihakikishe kuwa hakuna malipo ya zabuni yanayolipwa kwa mzabuni bila kuthibitishwa na meneja wa mradi na mshauri elekezi.**

### **5.1.6 Kulipwa kwa fedha za matazamio shilingi milioni 28.59 na dola za Marekani 30,000 bila dhamana**

Kifungu kidogo cha 14.9 cha Masharti Maalum ya Mkataba wa ujenzi wa Bwawa la umeme la Julius Nyerere kinamtaka Mkandarasi, kwa sehemu za kazi zinazokabidhiwa kwa awamu pindi zinapokamilika, kuwasilisha kwa mwajiri dhamana ya fedha ya matazamio yenye thamani sawa na nusu ya kiasi cha fedha za matazamio, ambayo inapaswa kuwa ni halali na inayotekelezeka hadi kutolewa kwa cheti cha utendaji kazi.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini vitalu nane vyenye nyumba za aina IV vilikabidhiwa na Mkandarasi kwa Shirika la Umeme Tanzania ikiwa ni sehemu ya kazi iliyokamilika. Pia, nilipitia hati ya malipo ya muda Na. 40 (IPC 40) na kubaini kutolewa kwa fedha za matazamio shilingi milioni 28.59 na dola za Marekani 30,000 zinazohusiana na vitalu hivyo, pasipo kuwasilishwa kwa dhamana ya fedha ya matazamio kinyume na Kifungu kidogo cha 14.9 cha Masharti Maalum ya Mkataba wa Bwawa la umeme la Julius Nyerere.

Hii ilitokana na usimamizi duni wa kandarasi hususani katika malipo na uthamini wa kazi zinazochukuliwa kwa awamu pindi zinapokamilika. Hali hiyo inaweza kusababisha hatari ya kutorejeshwa kwa fedha hizo endapo kutatokea kasoro zozote kwenye vitalu vilivyo chukuliwa na Mkandarasi kushindwa kurekebisha kasoro hizo.

Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe fedha za matazamio zinatolewa baada kufanya uthamini wa kina wa sehemu ya kazi zinazokamilika na kukabidhiwa; na kuhakikisha Mkandarasi anawasilisha dhamana ya fedha ya matazamio kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha 14.9 cha Masharti ya Mkataba wa ujenzi (EPC) katika Bwawa la umeme la Nyerere.

### **5.1.7 Mipango duni na ushirikishwaji mdogo wa wadau katika miradi ya uzalishaji na usambazaji umeme yenye thamani ya shilingi bilioni 301.10**

Aya 3.1 ya Sera ya Nishati ya mwaka 2015 kuhusu uimarishaji wa uhakika wa nishati na uongezaji wa mitando ya usafirishaji na usambazaji wa nishati inaeleza kuwa, Serikali itahakikisha inawekeza kwa wakati katika ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme.

Katika ukaguzi wangu juu ya mipango na mikakati iliyochukuliwa na TANESCO ili kuongeza uhakika wa umeme ulibaini kuwa, TANESCO ilianzisha mradi wa kimkakati unaojulikana kama Project Mapato wenyewe lengo la kuongeza mapato kwa kuwaunganisha wateja wa kimkakati. Mradi huu ulifadhiliwa kwa mkopo wa shilingi bilioni 303.1 kutoka benki za bishara. Hata hivyo, TANESCO haikuwashirikisha wadau katika hatua za mwanzo za uanzishwaji wa mradi huu. Licha ya TANESCO kupata idhini ya wizara ya fedha na kuchukua mkopo, mradi huu haukuweza kutekelezwa baada ya taarifa kuwa mwenendo wa sasa wa uzalishaji wa umeme hautaweza kukidhi mahitaji ya nyongeza ya wateja wanaotarajiwa.

Aidha, TANESCO ilipata kibali kutoka Wizara ya Fedha cha kubadilisha matumizi ya fedha hizo kwenda kwenye mradi mwingine uitwao “Project Mawe” uliolenga kununua mitambo ya kuzalisha umeme ya Mega Wati 150 ili kuongeza uwezo wa uzalishaji. Uendeshaji mitambo hiyo ya Project Mawe inategemea gesi kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC). Hata hivyo, tarehe 27 Juni 2023, TPDC ilithibitisha kutopatikana kwa gesi, na kusababisha TANESCO kushindwa kuendelea na mradi huo.

Ni maoni yangu kuwa kuwapo kwa mipango isoyotosheleza wakati wa uanzishaji wa miradi kumesababisha kushindwa kutekelezwa kwa miradi hiyo. Hivyo, hali hiyo imezia kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa ya kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme na kupanua wigo wa wateja.

**Ninapendekeza TANESCO iimarishe kitengo cha miradi ili kuongeza uzingatiaji wa matakwa ya miongozo ya usimamizi wa mradi. Pia, kuhakikisha katika siku zijazo kabla ya kuanza kwa mradi wadau wanashirikishwa kikamilifu ili kuepuka kukwama kwa miradi.**

### 5.1.8 Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya kijamii kwa zaidi ya miaka minne yenye thamani ya shilingi bilioni 262.34

Kifungu cha 2.1.6 cha Makubaliano ya utekelezaji wa miradi ya kijamii kinabainisha kuwa, makubaliano ya kina yatajadiliwa na kutiwa saini ndani ya mwezi mmoja baada ya kusaini mkataba wa mradi wa Bwawa la Julius Nyerere. Mkandarasi ataanza utekelezaji wa miradi ya kijamii ndani ya mwezi mmoja baada ya kusaini makubaliano ya kina huku ikizingatiwa malipo ya awali yamelipwa chini ya Mkataba wa mradi wa

Bwawa la Julius Nyerere. Miradi ya kijamii itatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 262.34 (ikiwa ni asilimia 4 ya bei ya mkataba).

Mkataba wa mradi wa Bwawa la Julius Nyerere ulitiwa saini tarehe 12 Desemba 2018 na makubaliano ya kina ya miradi ya kijamii yalipaswa kutiwa saini tarehe 13 Januari 2019. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 Mkataba wa Kina wa Utekelezaji wa miradi ya kijamii ulikuwa bado haujatiwa saini ikiwa ni ucheleweshwaji wa zaidi ya miaka minne (siku 1,610). Hii ilichangiwa na kuchelewa kuanzisha mazungumzo ya kusaini Mkataba wa Kina juu ya Miradi ya kijamii. Ninaona kuchelewa kufikia malengo yaliyokusudiwa na kuna hatari ya kushindwa kutekeleza miradi ya kijamii kwa wakati ikizingatiwa kuwa mradi uko katika hatua ya kukamilika.

Aidha, nilibaini tarehe 16 Desemba 2019 kilifanyika kikao cha majadiliano kuhusu utekelezaji wa miradi ya kijamii mbapo, pande zote zilikubaliana kutekeleza miradi hiyo, hususan ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Dodoma na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Fuga hadi Bwawa la Julius Nyerere. Hata hivyo, makubaliano haya hayakutiwa saini kutokana na Mkandarasi kueleza kuwa miradi iliyopendekezwa haiendani na vigezo vilivyoainishwa katika Mkataba wa utekelezaji wa miradi ya kijamii, kwa kuzingatia aina na utaratibu wa utekelezaji.

**Ninapendekeza kuwa TANESCO iwasiliane na Wizara ya Nishati kwa ajili ya kuhitimisha na kuchagua miradi itakayotekeliza na Mkandarasi, iwasilishwe kwa Mkandarasi ili kuwezesha utiaji saini wa Mkataba wa Kina wa utekelezaji wa Miradi ya kijamii.**

### 5.2 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Ukaguzi wangu wa shughuli za uendeshaji wa Bandari ulibaini mapungufu yafuatayo:-

#### 5.2.1 **Ukosefu wa upembuzi yakinifu wa kutosha katika miradi iliyositishwa yenye thamani ya shilingi bilioni 26.68**

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilisitisha miradi yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 26.68 ambayo iliendelezwa kutoka miaka ya nyuma na kuainishwa kama kazi inayoendelea. Uamuza wa kusitisha miradi hii ultokana na tathmini ya

Bandari juu ya uwezekano wa miradi hiyo kutekelezwa. Kutohakana na uamuzi huo, miradi hiyo ilifutwa kama hasara, ikionesha kuwa hakukuwa na thamani ya fedha kuendelea nayo. Hii ilisababishwa na usimamizi duni wa miradi uliotokana na kuwapo kwa upembuzi yakinifu usiokidhi. Miradi iliyositishwa ni kama ilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na.8.**

### **Jedwali Na. 8: Miradi Iliyositishwa**

Na.	Jina la Mradi	Mwaka ulioanza	Bei mkataba ya milioni)
1	Mfumo wa Dirisha Moja la malipo	13/04/2018	8,671.94
2	Ukarabati wa “Fendering” na kinga ya umeme kwenye banda la gati namba 2 Bandari ya Tanga	29/02/2016	5,837.46
3	Ushauri na mkandarasi kwa usambazaji, usakinishaji, mpangilio na kuzindua mradi wa Maendeleo ya POS	20/07/2020	5,197.91
4	Kiwira - Maendeleo ya bandari ya Kiwira, Kyela	09/01/2012	3,334.26
5	Ukarabati wa barabara ya kufikia lango namba 5 na eneo la maegesho ya malori katika Bandari ya Dar es Salaam.	27/09/2018	2,048.36
6	Maendeleo ya Bandari kavu kubwa Dar es Salaam (Ununuzi wa Ardhi huko Kisarawe).	17/08/2015	476.96
7	Kigoma - upembuzi yakinifu wa maendeleo ya Bandari Kavu huko Katosho	18/06/2018	421.76
8	Bandari Jamii	12/06/2019	253.12
9	Kuboresha POAS kwa kuiunganisha na TESWS	13/04/2020	157.320
10	Ujenzi wa kituo kipya cha mafuta (Awamu ya Kwanza) Mtwara.	30/03/2018	93.36
11	“Dar es salaam- One (1) No Light Duty Breakdown”	16/12/2016	85.09
12	Mtwara - Ubunifu na Ujenzi wa Mnara wa Taa 2 wa mita 35 kwa Ajili ya Uwanja Mpya wa Korosho huko Mtwara.	20/11/2017	54.65
13	Dar es Salaam - Maendeleo ya eneo la maegesho ya malori na upangaji wa logistik nje ya bandari (EX-Sukita)	12/05/2016	48.73
<b>Jumla</b>			<b>26,680.91</b>

**Chanzo:** Daftari la mali la Mamlaka 2022/23

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ifanye upembuzi yakinifu kabla ya kuanzisha miradi yake ili kupunguza hasara zinazoweza kujitokeza, na kuhakikisha miradi inatoa faida zilizokusudiwa.**

### **5.2.2 Ufanisi mdogo wa kuhudumia mizigo (Gang na Crane) katika Bandari ya Dar es salaam na Tanga**

Lengo D katika Mpango mkakati wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26 limetoa msisitizo wa kuongeza ufanisi wa bandari na kuboresha utoaji wa huduma. Lengo hili limepewaa kipaumbele katika Mpango wa utekelezaji wa 2022/23 ikionesa malengo maalum ya utendaji kwa Bandari ya Dar es Salaam. Malengo haya ni pamoja na kufikia Tani 500/Gang/Shift kwa Mizigo ya Kawaida, Tani 600/Gang/Shift kwa Mbolea kavu, Tani 1000/Gang/Shift kwa Mazao yasiyo ya vimiminika, Magari 125/Saa, na mzunguko 390/kwa siku kwa Kizimba/ kituo.

Ingawa nililielezea suala hili katika ripoti zangu kwa mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22, bado limeendelea katika mwaka wa fedha huu wa 2022/23. Ulaguzi wangu wa taarifa za utendaji wa Bandari kwa mwaka 2022/23 ulibaini tofauti kubwa katika kufikia malengo yaliyopangwa yanayohusiana kuhudumia mizigo (“gang” na “crane”), ambayo ilikuwa ni kati ya asilimia 12 na 60. Kwa mfano, Bandari ilipanga kubeba mizigo ya kawaida ya tani 500 lakini ilifanikiwa kubeba tani 306 (asililia 61) tu, wakati lengo la mizigo ya kawaida ya baharini ilikuwa tani 300 dhidi ya tani 121 (asilimia 40) zilizofikiwa (**Jedwali Na. 9**).

**Jedwali Na. 9: Ufanisi mdogo wa kuhudumia mizigo bandari ya Dar es salaam na Tanga**

Jina la Bandari	Maelezo	2022/23		kiwango cha kutofanikiwa	Asilimia ya kutofaniki wa
		Malengo	Halisi		
Dar es Salaam	Mizigo ya kawaida (Tani/Gang/Shift)	500	306	194	39
	Mbolea Kavu (Tani/Gang/Shift)	600	530	70	12
	Bidhaa kavu (Tani/Gang/Shift)	1000	777	223	22
	Magari (Idadi ya magari/kwa saa)	125	79	46	37
	Mzunguko wa kontena kwa saa 24-kituo I	390	324	66	17
Tanga	Mizigo ya kawaida - meli za 28ahari kuu (Tani/Gang/Shift)	300	121	179	60
	Mizigo ya kawaida - Meli za Pwani (Tons/Gang/Shift)	250	191	59	24

**Chanzo:** Taarifa za utendaji za Mamlaka ya Bandari Tanzania 2022/23

Mamlaka ya Bandari, iliniarifu kuwa kujirudia kwa jambo hili kunatokana na uharibifu wa mara kwa mara wa vifaa muhimu, ikiwamo “Gottwald”, “spreader”, na “reach stacker”. Aidha, kushindwa kutekeleza kwa wakati shughuli zilizopangwa kunaweza kusababisha kuchukua muda mrefu wa kushughulikia mizigo ambapo aina hii ya operesheni inaweza kuwa na athari kwa sifa ya Bandari na wateja wanaweza kuhamia bandari zingine zenyehusidani.

**Ninapendekeza TPA ianzishe mpango kamili na programu endelevu ya matengenezo ya vifaa na zana zote zinazotumika katika operesheni za bandari.** Pia, iwe na mpango wa ukaguzi wa kawaida, ratiba za matengenezo, na marekebisho ya vifaa kwa wakati ili kupunguza hatari ya uharibifu usiotarajiwa.

### 5.2.3 Kushindwa kusimamia na kudhibiti muda wa kuhudumia meli

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Bandari ya Dar es Salaam ilipanga malengo ya kufikia wastani wa siku tatu ya kuondosha mizigo kwa meli za kontena, mizigo mikavu, mizigo ya kawaida, na kupakia na kushusha magari, wakati pia ikilenga kufikia siku tano kwa meli za mizigo ya vimiminika.

Hata hivyo, katika uchambuzi wa ukaguzi wangu wa miaka iliyopita nilibaini changamoto za mara kwa mara katika kusimamia muda wa kuhudumia meli, hasa kuzidi malengo yaliyowekwa kwa meli za kontena, mizigo mikavu, mizigo ya kawaida, na meli za mizigo ya vimiminika. Katika mwaka wa fedha 2022/23, wastani wa muda wa kugeuza meli ulikuwa ni siku 6.5 kwa meli za kontena, na kiwango cha juu cha siku 13.7 kwa meli za vimiminika ikilinganishwa na malengo ya siku tatu na tano mtawalia yaliyopangwa. Maeleo zaidi yanapatikana katika **Jedwali Na. 10**.

**Jedwali Na. 10: Muda wa kubadilisha meli mwaka 2022/23**

Aina ya Meli ya Bahari Kuu	Malengo (Siku)	Siku halisi					Tofauti ya (Siku)
		Muda wa Kusubiri	Sehemu ya kubadishana (Pilotage)	Gati	Jumla		
Meli za makontena	3	3.4	0.1	3.0	6.5	3.5	
Meli za mizigo mikavu	3	3.3	0.1	6.4	9.8	6.8	
Meli za mizigo ya kawaida	3	3.6	0.1	4.5	8.1	5.1	
Meli za mizigo ya vimiminika	5	8.8	0.1	4.9	13.7	8.7	

### **Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za meli za mizigo**

Hali hii inaleta hatari ya kucheleweshwa kwa mizigo, ambayo husababisha malipo ya ucheleweshaji meli kuongezeka. Malipo haya hutozwa na mawakala wa meli kwa wateja. Matokeo yake husababisha ongezeko la gharama za bidhaa na huduma ndani ya nchi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania itumie rasilimali zilizopo kimkakati kuboresha miundombinu ya bandari na kuboresha ufanisi wa jumla wa shughuli za bandari.**

#### **5.2.4 Kutotumika kikamilifu kwa Bandari ya Ndumbi katika Ziwa Nyasa yenye thamani ya shilingi bilioni 12.28**

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilijenga Bandari ya Ndumbi kama moja ya miradi ya ujenzi wa kimkakati wa nchi iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa katika Mkoa wa Ruvuma kwa gharama ya shilingi bilioni 12.28. Ziara yangu katika Bandari ya Ndumbi ilibaini kuwa bandari imekuwa ikitumika kusafirisha abiria pekee. Hii inaifanya bandari hiyo kutotumika kikamilifu tofauti na malengo makuu ya ujenzi wa bandari hiyo ya kusafirisha makaa ya mawe kutoka Songea kwenda kiwanda cha saruji Mbeya.

Mamlaka ilinieleza kuwa sababu ya kutotumia njia ya bandari kusafirisha makaa ya mawe ilikuwa: Barabara mbovu na yenye changarawe inayounganisha migodi ya makaa ya mawe na Songea; na kiwango kidogo cha kuinadi Bandari ya Ndumbi kwa watumiaji wengine wa Ziwa Nyasa. Kutotumika kikamilifu kwa bandari kunasababisha kucheleweshwa kwa upatikanaji wa faida katika uwekezaji uliofanywa.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania ianzishe mkakati wa jinsi ya kutangazwa Bandari ya Ndumbi kwa watumiaji wengine ili kufikia matumizi bora ya bandari na kupata faida kutohana na uwekezaji uliofanywa.**

#### **5.2.5 Mapungufu ya utendaji wa bandari yamepelekea kusamehe mapato yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8**

Aya 3.2(iii) ya Sera ya Msamaha ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa tozo za Uhifadhi wa Bandari, 2019 inaeleza kuwa tozo za uhifadhi zitachukua mtazamo wa adhabu pale tu mteja amechelewesha kwa makosa yake mwenyewe na kuongeza gharama za uhifadhi mizigo

inayokaa kwa zaidi ya siku 30 tangu kuisha kwa kipindi cha msamaha, sababu ni kukataza matumizi ya Kituo cha mamlaka ya Bandari kuwa kama kituo cha kuhifadhi.

Mapitio yangu ya taarifa ya msamaha wa Bandari ya Dar es Salaam kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, yalibaini dola za Marekani 777,956 (sawa na shilingi bilioni 1.82) zilisamehewa kutokana na sababu zilizochangiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Makosa hayo yalijumuisha kutokuwepo kwa vifaa vya kutosha vya kushughulikia mizigo na kotokuzingatia katika kuwasilisha kwa wakati taarifa za mizigo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ichukue hatua za kufanikisha bandari kuwa na vifaa vya kutosha vya kushughulikia mizigo na kuwasilisha kwa wakati taarifa za kina za mizigo kwa TRA, pamoja na uhakiki wa wakati wa mizigo.**

#### **5.2.6 Utegemezi wa washauri elekezi katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa sasa haina wataalamu wa ndani wenye uwezo wa kuchukua na kuchambua taarifa kutoka kwenye kanzidata. Badala yake, imempatia jukumu hilo mshauri elekezi wa nje, hivyo kupelekea kuwa na utegemezi mkubwa kwa wataalamu wa nje.

Pia, nilibaini mikataba miwili iliyotekelezwa na mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa ripoti inayobainisha uchambuzi wa mapungufu katika mchakato wa uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za fedha mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23. Mikataba hiyo ni mkataba Na. AE/016/2022-2023/HQ/C/16 na mkataba Na. AE/016/2022-2023/HQ/C/03 yenye thamani ya shilingi milioni 407.49 na shilingi milioni 992.04 mtawalia. Kutegemea wataalamu kutoka nje ya taasisi pasipo kuwa na mkakati thabitii wa kutengeneza uwezo wa ndani kunaleta mashaka juu ya ufanisi katika gharama na ustawi endelevu wa Mamlaka.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania itengeneze mpango madhubuti wenye kujitosheleza wa kuwapatia maarifa na kurithisha madaraka kwa wafanyakazi watakao bainishwa ili wapatiwe mafunzo yatakayo wawezesha kumudu majukumu ambayo kwa sasa yanafanywa na washauri elekezi.**

### 5.3 Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

Katika ukaguzi wangu kuhusu Kwa ATCL nilibaini kasoro ifuatayo: -

#### 5.3.1 Kiwango kidogo cha ongezako la safari za ndege za kimataifa

Mpango mkakati wa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa 2022/23 hadi 2026/27 ulikuwa ni kuongeza safari za kimataifa ifikapo tarehe 30 Juni 2023. Safari hizi zilijumuisha Dzaoudzi-Mayotte, Ufaransa na Johannesburg ifikapo 30 Juni 2023. Wakati wa ukaguzi nilibaini safari za kimataifa zilizopangwa kuanzhishwa 2023 hazikutekelezwa. Hii inapelekea kutokuwa na matumizi bora ya ndege kwa ajili ya safari za nje. Hii ilichangiwa na mikakati duni ya kampuni katika kuongeza safari za kimataifa kwa ndege zilizopo.

Kushindwa kuongeza safari za ndege za kimataifa kunaweza kusababisha kampuni kupoteza mapato zaidi kutokana na matumizi yasiyotosheleza ya uwezo wa ndege.

Ninapendekeza ATCL ihakikisha matumizi bora ya ndege kwa kuhakikisha mpango wa safari za kimataifa unatekelezwa kama ulivyopangwa.

### 5.4 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Katika ukaguzi wa Shirika la Nyumba la Taifa nilibani:

#### 5.4.1 Kukwama kwa Miradi saba yenye thamani ya shilingi bilioni 55.86

Ukaguzi wangu wa miradi 13 inayoendelea, yenye thamani ya shilingi bilioni 213.12, ulionesha kuwa miradi saba, yenye jumla ya thamani ya sh. bilioni 55.86 bilioni, ilisitishwa kutoendelezwu katika mwaka wa fedha 2022/23 (**Jedwali Na. 11**). Miradi hii ilisitishwa kutokana na ukosefu wa fedha.

**Jedwali Na. 11: Muhtasari wa miradi iliyositishwa**

Na .	Jina la Mradi	Kiasi (Sh. milioni)
1	Kawe (Golden Premier Residence) Kiwanja Na. 711/2 (Awali Kiwanja 1088 Barabara ya Magore/Vijibweni Upanga High end)	29,817.54
2	Kawe (Seven Eleven) Kiwanja Na. 711/1 (Awali Kiwanja Na. 79-82 Ngano)	25,935.18
3	Viwanja vya Chato (Viwanja 5000)	50.67
4	Mradi wa Nyumba za Gharama Nafuu Luguruni	19.71

Na. .	Jina la Mradi	Kiasi (Sh. milioni)
5	Manyoni - Singida Mradi wa Makazi ya Bei Nafuu Kiwanja Na. 402 na 422 Kitalu(Block) 'MM	15.67
6	Magore/Vijibweni Alykhan Kiwanja 270, 288 & 289-Upanga	14.07
7	Mradi wa Makazi ya Bei Nafuu Ipogolo-Iringa	11.73
<b>Jumla</b>		<b>55,864.57</b>

Chanzo: Taarifa ya miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/23

Kwa maoni yangu, kuna uwezekano wa kuongezeka kwa gharama kubwa ya kuanda mahitaji ya vifaa ya miradi iliyositishwa pindi itakapo endelezwa, ambayo inaweza kuathiri faida ya miradi hiyo.

Ninapendekeza Shirika la Nyumba la Taifa; (a) lichukue hatua za kutafuta vyanzo vya fedha ili kuhakikisha miradi inayoendelea inakamilishwa na kupata mapato yanayotarajiwa kutohana na kodi au mauzo ya mali hizo; na (b) lifanye uchambuzi wa miradi inayoendelea na kuiiza kwa wawekezaji wanaotaka kununua mali hizo kwa bei ya soko ili kuepuka hasara kwa Shirika kuititia uwekezaji uliofanywa.

### 5.5 Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA)

Ukaguzi wangu katika EPZA ulibaini yafuatayo:

#### 5.5.1 Kutofanya kazi kwa mradi wa Bandari Huru ya Mtwara uliokamilika na kugharimu shilingi bilioni 2.56

EPZA ilianzisha mradi wa ujenzi wa Bandari huru ya Mtwara ambao uliokamilika tarehe 27 Oktoba 2020 na kugharimu shilingi bilioni 2.56. Katika ukaguzi wangu tarehe 2 Oktoba 2023 nilitembelea mradi huo na kubaini kuwa hakukuwa na mwekezaji aliyevutiwa kuwekeza katika Ukanda Huru wa Mtwara. Hii ilichangiwa na kupungua kwa shughuli za gesi katika mkoa wa Mtwara.

Kwa maoni yangu, kuna uwezekano wa kupoteza thamani kwa mali za mradi kutohana na uchakavu wa miundombinu iliyojengwa. Hivyo, kunaweza kusababisha hasara kwa shirika kwa muda mrefu.

Ninapendekeza EPZA ifikirie matumizi mbadala ya majengo yaliyojengwa ndani ya mradi wa kanda ya Mtwara ambayo yanaweza kuingiza mapato au kutumika kwa malengo mengine yenye manufaa. Hii inaweza kuhusisha kubadilisha miundombinu kwa shughuli

05

## Ufanisi wa mashirika ya umma katika kuimarisha mazingira ya kibiashara

zingine za kibiashara ambazo zinaendana na mahitaji ya kiuchumi ya eneo husika.



## USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

### 6.0 Utangulizi

Usimamizi wa mapato katika mashirika ya umma unahusisha mipango ya kimkakati, na ufanisi wa rasilimali za kifedha ili kuongeza uzalishaji wa mapato na kusaidia utoaji wa huduma za umma.

Sura hii inaeleza kwa ufupi kasoro za udhibiti wa ndani, kutokuwa na ufanisi katika usimamizi wa mapato katika mashirika ya umma, na mapendekezo yangu.

#### 6.1 Mapungufu katika usimamizi wa mapato

Usimamizi wa mapato unajumuisha kufuata kanuni za msingi na taratibu za ukusanyaji. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu yafuatayo katika usimamizi wa mapato:

##### 6.1.1 Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo wa GePG shilingi bilioni 21.46

Waraka wa Hazina Na. 3 wa 2017, pamoja na taratibu za Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG) toleo la 1.1 la Novemba 2019, lililotolewa na Wizara ya Fedha, linataka fedha zote za umma kukusanywa kupitia mfumo wa GePG.

Hata hivyo, mapitio yangu yalibaini mashirika saba ya umma yaliyoordheshwa katika **Jedwali Na.12** yaliyokusanya mapato ya shilingi bilioni 21.46 nje ya mfumo wa GePG kinyume na Waraka wa Hazina Na. 3 wa 2017. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 18.14 (sawa na asilimia 546) kutoka shilingi bilioni 3.32 zilizoripotiwa kwa mashirika matano mwaka uliopita. Hii inachangiwa na kutotekelizwa ipasavyo kwa Waraka wa Hazina.

**Jedwali Na. 12: Mashirika ya umma ambayo mapato yanakusanywa nje mfumo wa GEPG**

Na.	Mashirika ya umma	Kiasi kilichokusanywa sh. (milioni)
1	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	16,477.48
2	Kampuni ya Mkulazi	2,383.73
3	Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania	1,276.12
4	Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania	877.13
5	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	225.51
6	Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam	184.35
7	Taasisi ya Utafiti wa Uvvi Tanzania	33.59
<b>Jumla</b>		<b>21,457.91</b>

*Chanzo: Taarifa za makusanyo ya fedha pamoja na ripoti za GePG*

Kushindwa kukusanya mapato kuitia Mfumo wa Kielektroniki kuna madhara makubwa yakiwamo, upotevu wa mapato na ukosefu wa uwazi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yazingatie Waraka wa Hazina ili kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kuitia mfumo wa GePG ili kuimarisha uwajibikaji na uwazi.**

### 6.1.2 **Viwango vya ushuru na ada zilizotozwa kwa kutumia rasimu ya mapato bila uhakiki wa mapato ya mwisho yaliyokaguliwa shilingi bilioni 33.55**

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania na Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro wanatakiwa kuwatoza watoahuduma na wateja wengine kwa kuzingatia mapato ya muda ya uendeshaji ambayo baadaye hurekebishwa na hesabu zilizokaguliwa.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania liliripoti ushuru wa huduma wa shilingi bilioni 32.86 kulingana na taarifa za mapato ya awali zilizotolewa na washirika wa huduma za bandari na utunzaji wa mizigo bila uhakiki wa baadaye wa mapato yao yaliyokaguliwa ili kuthibitisha mapato halisi, kinyume na Sheria ya Viwango vya Ushuru na Ada za Watoa huduma ya mwaka, 2018.

Aidha, katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO), tozo ya mauzo iliyofikia shilingi milioni 691.38 ilitozwa kulingana na rasimu za taarifa za mauzo ya wateja, na KADCO haikufanya uhakiki baadaye wa mapato ya wateja yaliyokaguliwa ili kuthibitisha mapato halisi. Hii ni kinyume na vifungu vya makubaliano ya mauzo.

Kushindwa kuoanisha tozo inayotozwa kwa kuzingatia rasimu ya mapato na tozo halisi kutoka kwa taarifa zilizokaguliwa kunaweza kusababisha watoahuduma kuonesha mauzo kidogo. Kwa hivyo, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania na Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro zinaweza kukusanya mapato kidogo kuliko inavyotakiwa.

**Ninapendekeza Wakala wa Meli Tanzania na Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kuhakikisha wanafuutilia taarifa za mapato ya mwisho zilizokaguliwa ili kuhakikisha upatanisho unafanyika kwa kulinganisha rasimu ya hesabu za mauzo, na hesabu zilizokaguliwa, hii inaweza kufikiwa kwa kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kupata taarifa za kifedha zilizowasilishwa na watoa huduma ili kupunguza hatari ya uwezekano wa upotevu wa mapato.**

### 6.1.3 **Ukusanyaji wa mapato usioridhisha**

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa ukusanyaji duni wa mapato umeathiri utendaji wa kifedha na mafanikio ya malengo ya mashirika kadhaa ya umma kama yalivyoelezewa hapo chini:

**Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote:** mapato kutoka kwa machapisho, huduma za usafirishaji na utangazaji (Radio, Televisheni, King'amuzi, na Televisheni mtandao) hayakukusanya. Mfuko uliweza kutoza tozo ya huduma ya shilingi bilioni 42.14 kutoka kwa watoahuduma 47 wa mawasiliano na utangazaji. Hii ilitokana na kutozingatia matakwa ya kifungu cha 23 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, 2006.

**Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania:** Kampuni ilitegemea chanzo kimoja cha mapato yaani kamisheni iliyolipwa na kampuni ya DERM Electrics (T) Ltd kwa miaka minne mfululizo kutoka 2019/20 hadi 2022/23. Baada ya mkataba kuisha mnamo Juni 2023, mapato yalishtuka kwa asilimia 65 kutoka shilingi milioni 645 hadi shilingi milioni 225.51 kutokana na ukosefu wa mtaji wa kutekeleza lengo lake kuu la kutengeneza nguzo za zege kwa ajili ya kusambaza umeme.

**Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari:** Mfuko haukuwa na michango iliyopokelewa katika mwaka 2022/23 licha ya kuwa na jukumu la kukusanya mchango wa dola za Marekani 0.5 kwa jumla ya tani zilizobebwa na meli kwa mwaka (USD 0.5 per Gross Tonnage per vessel annually) kutoka kwa wamiliki wa meli. Hii ilisababishwa na

kutokuwapo kwa makubaliano kati ya Mfuko na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania kuhusu ukusanyaji wa mapato hayo na kutokuwapo kwa taarifa za kutosha za meli ili kutekeleza matakwa ya Kanuni za Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari za mwaka 2011.

**Ninapendekeza Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania na Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari kuimarisha udhibiti katika utekelezaji wa kanuni na sera ili kuongeza makusanyo ya mapato.**

### **6.1.4 Upotevu wa mapato kupitia punguzo lisiloidhinishwa kwa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha shilingi milioni 497.52**

Kutoka kwenye ukaguzi wangu maalumu, nilibaini kuwa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kilipata hasara ya shilingi milioni 497.52 katika mwaka wa fedha 2021/22 kutokana na kutoa punguzo kwenye bei za ukumbi na mikutano kwa wateja 70 bila idhini kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Upotevu huo unatokana na kutofuata kanuni za ndani na kutokuwapo kwa sera za usimamizi wa shughuli za kila siku za kituo.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki kwa watendaji wote waliohusika kusababisha kituo kupata hasara.**

### **6.1.5 Kuchelewa kupata mapato kutokana na ucheleweshaji wa usajili wa wateja katika mfumo wa LUKU**

Ni-konekt ni mfumo wa maombi mtandaoni unaowezesha wateja wa TANESCO kuomba huduma ya kuunganishiwa umeme. Unaowawezesha wateja kufuatilia maombi yao yaliyowasilishwa, kutoa taarifa za dharura, kufanya maombi yasiyo ya kielektroniki, kutoa malalamiko, na kuuliza maswali mbalimbali.

Ukaguzi wangu wa mchakato wa kuunganisha wateja wa TANESCO kwa mwaka ulioishia Juni 2023 ulionesha kuwa wateja 560,373 walikuwa wameunganishwa kupitia Mfumo wa Ni-konekt, ambapo kati ya hao wateja 553,468 walisajiliwa katika mfumo wa LUKU. Hata hivyo, uchambuzi wangu ulionesha kuwa wateja 6,905 (wateja wa malipo kabla) walikuwa hawajasajiliwa katika mfumo wa LUKU, kwa kipindi cha siku 1 hadi 438 mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2023, jambo ambalo linachelewesha mapato. Aidha, katika mapitio yangu nilibaini kuwa hadi

tarehe 17 Novemba 2023, ilionekana kuwa wateja hao bado walikuwa hawajasajiliwa katika mfumo wa LUKU, na hivyo kuzua wasiwasi kuhusu ufanisi wa mchakato huo.

Vilevile, nilibaini ucheleweshwaji wa kusajili wateja 12,666 katika mfumo wa LUKU, ikiwa ni kati ya siku 7 hadi 366 kuanzia tarehe ya kuunganishwa kwenye mfumo wa utumaji maombi kuitia mtandao wa Ni-konekt, kinyume na mwongozo wa uhasibu wa TANESCO wa mwaka 2022 ulioweka muda wa siku moja ya kazi kutoka mfumo wa Ni-konekt kwenda mfumo wa Luku. Hii inazua wasiwasi kuhusu ufanisi katika mchakato wa usajili.

Changamoto hii inachangiwa na kutokuwapo kwa usimamizi thabiti katika kuhakikisha usajili wa wateja kwa wakati katika mifumo ya bili na LUKU. Pia, inachangiwa na kutokusomana kati ya Mfumo wa utumaji maombi wa mtandao wa Ni-konekt na mfumo wa LUKU. Kuchelewa kusajili wateja kunasababisha uwezekano wa wizi wa umeme kwa wateja ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo wa LUKU. Pia, TANESCO inapoteza mapato kutokana na kuchelewa kutoa huduma ya umeme kwa wateja.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania;** (a) lifanye mapitio ya kina ya takwimu za wateja, kuoanisha taarifa kati ya Mfumo wa Utumaji Maombi wa Mtandao wa Ni-konekt na mfumo wa LUKU, pamoja na kutembelea wateja ili kushughulikia matatizo yatakayobainika; (b) lihakikishe mfumo wa Ni-konekt na mfumo wa LUKU unasomana, pamoja na kufanya mapitio ya ndani ya mara kwa mara ili kushughulikia matatizo yatakayobainika; na (c) lifanye ukaguzi wa mara kwa mara ili kuthibitisha uhalisia katika kuunganishiwa umeme wateja wao, pia kubaini wateja waliounganishwa bila kuidhinishwa kama wapo. Hatua hizi zitaongeza usahihi wa data na ufanisi wa mfumo.

### **6.1.6 Kutowasilishwa kwa mapato yaliyokusanya kwenda Benki Kuu ya Tanzania shilingi bilioni 21.84**

Waraka Na. 3 wa 2022/23 wa tarehe 1 Juni 2023, uliotolewa na Wizara ya Fedha unazitaka Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka na Sekretarieti za Tawala za Mikoa kupeleka Benki Kuu ya Tanzania mapato yote yasiyo ya kodi ambayo wanayokusanya kutoka Benki za Biashara kabla ya tarehe 30 Juni 2023.

Mapitio yangu yalibaini kuwa mashirika manne ya umma yalikuwa na jumla ya salio katika benki za biashara shilingi bilioni 21.84 ambazo zilikuwa hazijahamishiwa Benki Kuu ya Tanzania hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 (Jedwali Na. 13).

Kati ya mashirika hayo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuitia Bodi ya Wakurugenzi, iliidhinisha kufungwa kwa akaunti za Makusanyo katika Benki ya Biashara Tanzania (TCB) na kuhamisha fedha kwenye akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania wakati wa mukutano wake maalumu wa 112 uliofanyika tarehe 29 Aprili 2023. Hata hivyo, tarehe 31 Julai 2023, shilingi bilioni 19.04 zilihamishiwa na menejimenti kwenda kwenye Akaunti ya TPA ya matumizi ya NMB kinyume na maagizo ya bodi na Waraka. Kutumia makusanyo moja kwa moja katika akaunti za matumizi bila kuitia akaunti ya Benki Kuu kunapelekea kukosekana kwa uwajibikaji na uwazi.

**Jedwali Na. 13: Mashirika ambayo hayakuhamisha fedha kwenda Benki Kuu ya Tanzania**

Na.	Jina la shirika	Kiasi hakijahimishwa- Sh. (Milioni)	ambacho
1	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	19,044.89	
2	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini	1,927.20	
3	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara	468.18	
4	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	402.90	
	Jumla		21,843.17

**Chanzo:** Uchambuzi wa taarifa za kibenki

Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yahakikishe yanafuata waraka kwa kuhamisha fedha za mapato kutoka Benki za biashara kwenda Benki Kuu ya Tanzania.

**6.1.7 Kushindwa kuhamisha fedha zilizokusanya kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Miundombinu ya Reli shilingi bilioni 192.44**

Kifungu cha 68(3) cha Sheria ya Reli ya mwaka 2017, sura ya 170, kinabainisha kuhusu tozo ya maendeleo ya reli, ambayo ni mkondo muhimu wa mapato ya fedha za miundombinu ya reli, iliyowekwa kwa kiwango cha asilimia 1.5 ya thamani ya forodha ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Kifungu kidogo cha (7) kinampa mamlaka Kamishna Mkuu aliyeulewa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya tozo hiyo, ikielekeza kwenye Mfuko wa Miundombinu ya Reli kwa matumizi ya kipekee katika uendelezaji wa miundombinu ya reli.

Ibara ya 135 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1997 inataka mapato ambayo yameainishwa na sheria yatumike kwa madhumuni maalumu au yalipwe kwenye mfuko mwingine kwa matumizi maalumu, yaslipwe kwenye mfuko Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Hata hivyo, mapitio yangu ya malipo ya kila mwezi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, shilingi bilioni 192.44 sawa na asilimia 44 hazikuhamishiwa mfuko wa miundombinu ya Reli, ikijumuisha shilingi bilioni 4.45 kutoka makusanyo ya Julai 2022, zilizohamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali mwezi Agosti 2022 na Mamlaka ya Mapato.

Kuweka fedha za Mfuko wa Reli katika Mfuko Mkuu wa Serikali kunaweza kusababisha shirika la Reli kutotekeleza shughuli zake zilizopangwa kwa ufanisi, pamoja na kupelekea kuchelewa kwa kazi hizo.

Ninapendekeza TRA na Hazina kubuni mkakati unaoweza kutekelezeka wenye lengo la kuhakikisha kuwa fedha zote zilizokusanywa zinahamishwa kwa haraka Kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Miundombinu ya Reli chini ya TRC, hivyo kuruhusu Shirika kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kwa ufanisi.

### **6.2 Usimamizi wa madeni ya kibiashara na mengineyo**

Usimamizi wa madeni unajumuisha kufuata udhibiti wa msingi na taratibu za ukusanyaji na makubaliano na wadaiwa husika. Uguzi wangu ulibaini mapungufu yafuatayo kuhusu usimamizi wa madeni ya mashirika ya umma.

#### **6.2.1 Kuwapo madeni ya muda mrefu ambayo bado hayajalipwa shilingi trilioni 2.92**

Nilifanya mapitio ya madeni ya biashara kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2023 katika mashirika ya umma 215. Nilibaini kuwa mashirika 66 ya umma yana madeni makubwa ya zaidi ya miezi 12 yanayofikia shilingi trilioni 2.92, yanayohusiana na huduma zilizotolewa kwa wateja (**Kiambatisho Na. VI**). Niliripoti suala kama hilo katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22, ambapo mashirika 97 ya umma yalikuwa na ukusanyaji hafifu wa madeni ya biashara yenye thamani ya shilingi trilioni 3.58. Madeni ya biashara yaliendelea kuathiri mtiririko wa fedha wa mashirika na uwezo wao wa kutekeleza shughuli zilizopangwa. Maeleo zaidi

kuhusu baadhi ya mashirika yaliyokutwa na upungufu huu ni kama ifuatavyo: -

- a) Katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, nilikuta mikopo ya wanafunzi yenye jumla ya shilingi bilioni 808.11 sawa na asilimia 38 ya mikopo ilioiva ya shilingi trilioni 2.10 haijalipwa. Kuchelewa kerejeshwa kwa mikopo kumetokana na kukosekana kwa mfumo unaowaunganisha wadau wa kimkakati. Hii ni kwa sababu mkataba wa maelewano na baadhi ya wadau wa kimkakati haujakamilika ili kuwafuatilia kwa urahisi wadaiwa waliokiuka.
- b) Katika Shirika la Umeme Tanzania, nilibaini kuwa shilingi bilioni 316.67, sawa na asilimia 73 ya jumla ya salio la madeni ya biashara yasiyolipwa ya shilingi bilioni 435.44, yanahuasiana na madeni ambayo yapo chini ya mabishano na yanapendekezwa kufutwa. Miongoni mwa sababu za kutokukubaliana juu ya kiasi ni pamoja na kutokukubaliana kwenye bili zilizotolewa kwa wateja, viwango vya malipo ya umeme vinavyopingwa na Shirika la Umeme la Zanzibar kiasi cha shilingi bilioni 73.99, na Serikali kusitisha kutoa ruzuku kwenye ankara za Shirika hilo kiasi cha shilingi bilioni 175.32.
- c) Nilibaini Bohari Kuu ya Dawa inadai shilingi bilioni 366.32 kutoka kwa Serikali, kukiwa na ongezeko la asilimia 24 kutoka shilingi bilioni 295.2 iliyoripotiwa mwaka uliopita. Deni hili linaloendelea la Serikali linaweka hatari kubwa kwa mtaji wa Bohari Kuu ya Dawa na uwezo wake wa kuwa na bidhaa za kujitosheleza na kutimiza majukumu yake muhimu.
- d) Katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, nilikuta kiasi kikubwa cha deni la muda mrefu la shilingi bilioni 373.57 ambalo halijalipwa na Shirika la Umeme Tanzania kwa zaidi ya miezi 12, sawa na asilimia 78.6 ya deni lote la shilingi bilioni 475.16. Mwenendo unaonesha ongezeko la deni la Shirika la Umeme Tanzania ambalo halijalipwa kwa miaka mingi. Ninaona kuwa kushindwa kulipa ankara kwa wakati, kumesababisha Shirika la Maendeleo ya Petroli kukosa fedha za kuwekeza katika maendeleo ya mafuta na gesi.
- e) Katika Shirika la Mawasiliano Tanzania, nilibaini kuwa kwa mwaka mzima hakukuwa na ukusanyaji kutoka kwa wateja wenye jumla ya deni la shilingi bilioni 72.20. Kati ya wateja hawa, wateja 1,889 wenye jumla ya deni la shilingi bilioni 19.58 walifanya miamala ya kibiashara na Shirika katika mwaka wa fedha 2022/23. Wateja wengine 58,722 wenye jumla ya deni la shilingi bilioni 52.62 hawakufanya miamala yejote mwaka mzima.

- f) Kwenye Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, katika tathmini yangu ya ukaguzi wa madeni ya biashara yaliyokaa muda mrefu, nilibaini madeni yanayofikia shilingi bilioni 7.995 ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya siku 90 na hayajatozwa riba, jambo linalokwenda kinyume na mwongozo wa kifedha wa Kampuni hiyo. Hasara ya mapato ya riba iliyokokotolewa upya kwa deni lilopita muda ni shilingi bilioni 1.31.
- g) Katika Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL, nilibaini kukiukwa kwa vigezo vyta muda wa mkopo kuhusiana na salio la madeni lililokuwa halijalipwa kwa muda mrefu. Kampuni iliwapa wateja bidhaa za mafuta ambao walikuwa wamezidi kikomo chao cha mkopo wa siku 14. Jumla ya kiasi kinachodaiwa kutoka kwa wateja hawa mwishoni mwa mwaka ambao walizidi kikomo chao cha mkopo ilikuwa shilingi bilioni 15.8, kati ya hizi shilingi bilioni 1 zilitengwa kama madeni yasiyolipika.
- h) Katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, nilibaini kuwa shilingi bilioni 7.08 ya madeni ya wanafunzi yanajumuisha deni la shilingi bilioni 3.03 kutoka kwa watu ambao si wanafunzi tena wa chuo hicho kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwazo ni: ya kufariki dunia, kuachana na masomo, kuhitimu, kutokukamilisha usajili, kutokuwa na taarifa, na kufukuzwa, madeni hayajalipwa kwa zaidi ya siku 720.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika;** (a) kuimarisha udhibiti wa ndani wa makusanyo ya wadaiwa, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa wote kulipa madeni yao; (b) kuwasiliana na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu madeni ambayo taasisi za Serikali zinadaiwa kwa muda mrefu, na (c) kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuhakikisha Randama ya Maelewano na wadau wa kimkakati inakamilika ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mikopo.



# SURA YA SABA

## USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

### 7.0 Utangulizi

Usimamizi bora wa fedha za Serikali katika mashirika ya umma ni muhimu ili kuhakikisha ufanisi na uwajibikaji katika utumiaji wa rasilimali za umma. Fedha hizi hutumika kugharamia shughuli mbalimbali katika mashirika ya umma, ikijumuisha gharama za uendeshaji wa kila siku kama mishahara, ujira, na posho. Aidha, hutumika kununua bidhaa na huduma zinazohitajika kwa shughuli za uendeshaji na kiutawala.

Mbali na matumizi ya kawaida, fedha za Serikali pia hutumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hii inajumuisha uwekezaji katika rasilimali za muda mrefu mfano mali zisizoshikika kama vile haki miliki, na zinazoshikika kama vile samani na majengo.

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi wangu ulibaini mapungufu katika usimamizi wa matumizi. Baadhi ya mapungufu yanajirudia na niliyari poti katika ripoti yangu ya mwaka jana. Hoja hizo ni: matumizi yasiyokuwa na tija yaliyotokana na kuchelewa kwa kutimiza matakwa ya kimikataba na kisheria; na kuwapo kwa masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu pamoja na matumizi yasiyostahili.

Sura hii inaelezea mapungufu niliyoyabaini katika usimamizi wa matumizi ambayo, kwa maoni yangu yanahitaji usimamizi wa kina wa ndani na nje kutoka kwa vyombo vyenye mamlaka ya usimamizi wa mashirika husika pamoja na kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili kuongeza udhibiti wa ndani na uzingatiaji wa sera, sheria na kanuni. Kwa ujumla, nilibaini mapungufu yafuatayo:

## **7.1 Matumizi yasiyokuwa na tija ya shilingi bilioni 72.36**

Matumizi yasiyokuwa na tija hutokana na malipo ambayo shirika husika halijapata manufaa ya thamani ya fedha. Matumizi ya aina hii yanachukuliwa kuwa yanaweza kuepukika na yasiyo ya lazima, kama vile tozo za adhabu na riba zinazotokana na kutokuzingatia matakwa ya kisheria na kimikataba.

Katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, nilibaini mashirika ya umma 17 yenye matumizi yasiyokuwa na tija ya jumla ya shilingi bilioni 72.36, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo kulikuwa na mashirika 12 yenye jumla ya shilingi bilioni 63.77. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa mashirika manne yaliripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka jana na yamejirudia tena mwaka huu. Mashirika hayo ni: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza, na Shirika la Umeme Tanzania. Mashirika 13 yamebainika kwa mara ya kwanza mwaka huu.

Matumizi yasiyokuwa na tija, kwa sehemu kubwa yanatokana na tozo za adhabu na riba kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya wazabuni na makandarasi; kuchelewa kujaza na kutuma michango na makato ya watumishi yaliyoainishwa kisheria; na kununua bidhaa zilizopitwa na wakati au zisizohitajika. Hii inasababisha upotevu wa fedha za umma na kutofikiwa kwa ufanisi wa matumizi sahihi ya rasilimali fedha zilizokabidhiwa kwa mashirika husika. **Jedwali Na. 14** linaonesha orodha ya mashirika ya umma yenye matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija katika mwaka wa fedha 2022/23.

**Jedwali Na. 14: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija mwaka 2022/23**

Na	Jina la Shirika/Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh. million)
1.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (Ukaguzi maalumu kwenye miradi ya ujenzi wa miundombinu ya Bandari; na mifumo ya TEHAMA kwa mikataba iliyoteklezwa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20)	Malipo yasiyokuwa na tija yaliyobainika wakati wa ukaguzi wangu maalumu wa miradi mbalimbali ya ujenzi iliyoteklezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20 **	33,861.38
2.	Shirika la Umeme Tanzania	Riba na tozo za adhabu kwa kuchelewesa malipo ya mzabuni na michango ya pensheni; kushindwa	26,042.32

Na	Jina la Shirika/Taasisi	Maelezo	Kiasi (Sh. milion)
		kudai kodi ya ongezeko la thamani inayotokana na ununu.	
3.	Bodi ya Pamba Tanzania	Riba iliyoongezeka kutokana na kucheleweshwa kwa marejesho ya mkopo.	6,563.11
4.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	Tozo za adhabu kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya madai ya mkindarasi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Maji house.	3,583.52
5.	Shirika la Reli Tanzania	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha malipo ya kodi ya ardhi.	1,249.28
6.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Gharama za ziada zilizoongezeka zaidi ya bei ya awali ya mkataba kwa kazi ambazo hazikukamilishwa na mzabuni wa awali kutokana na kushindwa kwa mzabuni huyo kutekeleza majukumu yake hivyo kusitishwa kwa mkataba wake.	335.65
7.	Hifadhi za Taifa Tanzania	Gharama za uendeshaji zilizoongezeka kwa kuchelewa kukamilisha mradi wa uwanja wa gofu wa Serengeti	270.99
8.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha malipo ya michango ya pensheni kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	150.09
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha malipo ya michango ya pensheni kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	83.90
10.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	Riba iliyoongezeka kwa kuchelewesha malipo ya kazi ambazo zimeshathibitishwa kukamilika.	62.22
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	Riba kwa kuchelewesha malipo ya michango ya pensheni kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	39.56
12.	Tasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Riba kwa kuchelewa kulipa michango ya pensheni	30.11
13.	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	Riba na tozo za adhabu kwa kuchelewa kuwasilisha ritani za kodi	23.63
14.	Chuo Kikuu Ardhi	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha ritani na malipo ya kodi	22.32
15.	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	Gharama zilizoongezeka kwa kuchelewesha malipo ya mzungu	15.79
16.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha malipo ya kodi ya mapato, na riba iliyoongezeka kwa kuchelewesha marejesho ya mkopo.	11.78
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	Tozo za adhabu kwa kuchelewesha malipo ya michango ya pensheni kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	11.26
<b>Jumla</b>			<b>72,356.91</b>

**Chanzo:** Taarifa za fedha, vocha za malipo, na ankara

\*\*Kiasi cha shilingi bilioni 33.86 cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kilichooneshwa kwenye Jedwali Na. 14 kilibainika wakati wa ukaguzi wangu maalumu wa miradi mbalimbali inayotekelzeza na Mamlaka kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015/16 hadi 2019/20. Kiasi hicho kinajumuisha:

- (i) Malipo ya dola za Marekani milioni 0.02 (Shilingi milioni 45.76) kwa ajili ya vifaa vya TEHAMA ambavyo havikuwasilishwa na mzabuni katika mkataba Na. AE/016/2017-18/CTB/CG/15C;
- (ii) Malipo ya shilingi bilioni 9.07 kwa ajili ya vikinga-meli vya duara 47 ambavyo havikuwasilishwa, na kwa kazi ambazo hazikufanyika wakati wa ujenzi wa gati ya kupakia na kupakua mizigo kwenye gati ya RoRo katika mkataba Na. TPA/W/19-WB/2014-15;
- (iii) Malipo ya shilingi bilioni 1.48 na dola za Marekani milioni 6.94 (Shilingi bilioni 10.91) kwa makandarasi na kwa kazi ambazo hazikutekelezwa katika mkataba Na. AE/016/2011/2012/CTB/W/09-A;
- (iv) Malipo ya shilingi milioni 15.93 kwa kazi ambazo hazikutekelezwa na mkandarasi katika mkataba Na. AE/016/2017/2018/CTB/W/19/48;
- (v) Malipo ya shilingi milioni 172.84 kwa ajili ya kuweka vikinga-meli vya duara ambavyo havikutumika kama ilivyokusudiwa katika mkataba Na. AE/016/2018-2019/CG/12/LOT3;
- (vi) Malipo ya dola za Marekani milioni 0.55 (Shilingi bilioni 1.26) kwa ajili ya leseni ambazo hazikutumika zinazohusiana na mkataba Na. B1E60161 wa ugavi wa vifaa vya TEHAMA;
- (vii) Malipo ya dola za Marekani milioni 0.06 (Shilingi milioni 137.29) kwa vifaa vya TEHAMA vilivyopitwa na wakati, na leseni zaidi ya kiasi kilichohitajika katika mkataba Na. AE/016/2017-18/CTB/CG/15A;
- (viii) Hasara ya shilingi bilioni 6.57 kutokana na ukokotozi usio sahihi wa fidia ya mabadiliko ya bei za bidhaa zilizoainishwa kwenye mkataba Na. TPA/W/19-WB/2014-15;

- (ix) Marekebisho ya bei yasiyosahihi yaliyopelekea hasara ya dola za Marekani milioni 2.68 (Shilingi bilioni 4.21) kwenye mkataba Na. AE/016/2011/2012/CTB/W/09-A.

Ninapendekeza kuwa mamlaka za usimamizi wa mashirika tajwa ziboreshe na kuimarisha udhibiti na mikakati ya usimamizi wa matumizi, ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza mikakati halisi ya usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kuhakikisha ulipaji madeni kwa wakati, pamoja na kuongeza udhibiti kwenye malipo ili kuepuka matumizi yasiyokuwa na tija.

## **7.2 Matumizi yasiyostahili ya shilingi bilioni 4.64**

Matumizi yasiyostahili ni malipo ambayo hayakidhi vigezo na matakwa ya kisheria na udhibiti, makubaliano ya kimkataba, na viwango vyatuhaisib.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, nilibaini mashirika ya umma 11 yasiyokuwa na matumizi yasiyostahili yenye jumla ya shilingi bilioni 4.64 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 94 ukilinganisha na matumizi ya shilingi bilioni 77.75 katika mashirika 21 kwa mwaka jana. Uchambuzi wa ziada unaonesha kuwa mashirika ya umma matatu yamejirudia kati ya yale niliyoyaripoti mwaka jana huku mashirika ya umma nane yakiwa yametokea mwaka huu pekee. Mashirika ambayo yamejirudia ni: Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba, Chuo Kikuu cha Dodoma, Shirika la Viwango Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania.

Baadhi ya matumizi yasiyostahili yalitokana na malipo kwa makandarasi kwa kazi ambazo hazikufanyika au yaliyo kinyume na masharti ya mkataba, malipo ya posho ambayo hayakuidhinishwa, malipo yaliyolipwa kimakosa mara mbili kwa wazabuni; na malipo kwa wapokeaji wasiostahili.

Upungufu huu unaonesha uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma, na kuongeza wasiwasi wa kuwepo kwa udanganyifu na kuhatarisha ufanisi na usimamizi bora wa matumizi ya rasilimali fedha katika mashirika tajwa. **Jedwali Na. 15** linaonesha mashirika yenye matumizi yasiyostahili katika mwaka wa fedha wa 2022/23.

**Jedwali Na. 15: Mashirika yenyeye matumizi yasiyostahili kwa mwaka 2022/23**

<b>Na.</b>	<b>Jina la Shirika/Taasisi</b>	<b>Maelezo</b>	<b>Kiasi (Sh. Milion)</b>
1.	Chuo Kikuu cha Dodoma (Ukaguzi maalumu kuhusu posho za wafanyakazi)	Posho maalumu zilizolipwa kwa watumishi bila idhini ya Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.	1,018.30
2.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	Malipo ya posho ya kukaimu kwa wafanyakazi 40 bila kibali kutoka kwa Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	690.65
3.	Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (Ukaguzi maalumu 2021/22)	Malipo ya huduma za ulinzi bila miongozo sahihi, posho kwa kutumia kiwango kisichoidhinishwa, na njia zisizo sahihi za ukokotozi wa kamisheni za mawakala.	603.77
4.	Shirika la Umeme Tanzania	Malipo ya posho za kukaimu kwa wafanyakazi wasio stahili.	546.93
5.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba (Ukaguzi maalumu kwa kipindi cha kuanzia 2016/17 hadi 2018/19)	Malipo ya posho za vikao kwa wajumbe wa bodi ambao hawakuhuduria; na malipo mara mbili ya kiinua mgongo kwa Meneja wa Mfuko wa wakati huo; na dawa za viuatilifu zilizotozwa bei ya juu zaidi	508.93
6.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi	Malipo ya motisha ya kila mwezi kwa kazi ya ukusanyaji wa madeni bila idhini ya bodi	422.21
7.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	Malipo ya posho za kukaimu kwa wafanyakazi wasiostahili	252.28
8.	Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Madeni ya masurufu yaliyofutwa bila idhini ya bodi; na malipo ya posho ya wajibu bila idhini ya Msajili wa Hazina	198.53
9.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Malipo ya posho ya kukaimu kwa wafanyakazi 12 bila kibali kutoka kwa Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	175.41
10.	Shirika la Bima la Taifa	Malipo ya posho ya kukaimu, nyumba, huduma, mafuta na posho ya hatari kwa wafanyakazi wasiostahili.	170.66
11.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Malipo yaliyolipwa kimakosa mara mbili kwa watoa huduma mbali mbali.	50.22
<b>Jumla</b>			<b>4,637.89</b>

**Chanzo: Vocha za malipo**

Kiasi kilichooneshwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma kilibainika wakati wa ukaguzi maalumu. Ukaguzi huo ulikuwa ni juu ya malipo ya posho maalumu kwa watumishi mbalimbali wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi Desemba 2021. Ukaguzi huo ultibaini malipo yasiyo halali ya shilingi bilioni 1.02 kwa ajili ya posho maalumu kwa watumishi mbalimbali. Malipo hayo yalifanya kwa kutumia muongozo ambao haukuidhinishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama

ilivyoelekeza na kifungu cha 8(3)(d) na 8A (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

**Ninapendekeza mamlaka za usimamizi wa mashirika husika ziongeze usimamizi na udhibiti katika matumizi ili kuhakikisha uzingatiaji wa miongozo, sera, kanuni na sheria hasa wakati wa malipo; na kuhakikisha kiasi cha fedha kilichobainishwa kinarejeshwa.**

**7.3 Kukosekana kwa uhakika wa kurejeshewa gharama za kodi na tozo zilizolipwa kwenye shehena za mafuta ambayo yalishikiliwa shilingi bilioni 14.7**

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL ilikuwa na meli kumi za shehena ya mafuta zilizokuwa zimeshikiliwa kutokana na ukosefu wa fedha za kumlipa mzabuni kwa shehena hizo. Ukosefu wa fedha ulipelekea shehena za mafuta katika meli saba kuuzwa kwa makampuni mengine ya uuzaji wa mafuta. Hadi wakati mafuta hayo yanauzwa kwa makampuni mengine, TANOIL ilikuwa imelipia kodi na tozo za uingizaji wa mafuta za jumla ya shilingi bilioni 19.5.

Kupitia mahojiano ya ziada na Menejimenti ya TANOIL, nilibaini kuwa usuluhishi kati ya kodi na tozo zilizolipwa na TANOIL na zile zilizolipwa na Makampuni mengine yalironunua mafuta hayo ulikuwa unaendelea. Hadi kufikia mwezi Agosti 2023, TANOIL ilikuwa imerejeshewa shilingi bilioni 4.8, na kuacha shilingi bilioni 14.7 ambazo urejeshwaji wake unatia shaka. Madhumuni ya usuluhishi ni kuainisha kama TANOIL itarejeshewa kiasi kilichobakia au la kwa kulinganisha bei ya soko la mafuta wakati TANOIL ilipolipia na wakati shehena za mafuta zilipouzwa kwa makampuni mengine.

**Ninapendekeza uongozi wa Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL uhakikishe usuluhishi wa kiasi kilichobakia cha shilingi bilioni 14.7 unakamilika kwa wakati. Pia, ushirikiane na kampuni mama (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania) kuhakikisha shehena za mafuta hazizuiliwi kwa kukosa fedha za kulipia wazabuni wa mafuta.**

**7.4 Masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu ya shilingi bilioni 4.12**

Kanuni ya 96 hadi 103 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 inatoa mwongozo juu ya usimamizi wa masurufu ambayo pia umeakisiwa katika

kanuni za kifedha za mashirika ya umma. Kanuni hizo zinataka masurufu kurejeshwa ndani ya siku 14 baada ya kukamilika kwa shughuli husika; na kutotoa masurufu mengine kwa mtumishi kabla ya kurejesha vielelezo vyta uthibitisho wa matumizi ya masurufu ya awali; na ikitokea mtumishi kashindwa kurejesha vielelezo vyta uthibitisho wa matumizi akatwe moja kwa moja kwenye malipo yake ya mshahara.

Ukaguzi wangu kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulibaini mashirika ya umma 16 yaliyokuwa na masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu ya jumla ya shilingi bilioni 4.12 kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi zaidi ya mwaka. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 17 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo niliripoti mashirika ya umma 31 yaliyokuwa na jumla ya shilingi bilioni 3.51.

Uwepo wa masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kumesababishwa na watumishi waliofariki au kuacha kazi kabla ya kurejesha fedha au nyaraka za matumizi kwa fedha walizopewa. Hivyo, kunapeleka ugumu katika urejeshwaji wa fedha hizo kuitia makato ya mishahara.

Kuwapo kwa masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kunatoa mianya ambayo inaweza kutumika kufanya udanganyifu na matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia, kunaweza kusababisha kupotosha taarifa za kifedha, kwa kuwa masurufu huwekwa kama sehemu ya madeni lakini katika hali halisi matumizi yake huwa yamekwisha kamilika; hivyo kupaswa kuwa sehemu ya matumizi na siyo madeni. **Jedwali Na. 16** linaonesha mashirika ya umma yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kwa mwaka wa fedha 2022/23.

### **Jedwali Na. 16: Mashirika yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu**

Na.	Jina la shirika/Taasisi	Kiasi (Sh. milion)
1.	Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	1,272.11
2.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	916.74
3.	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi	864.76
4.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	318.15
5.	Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (Ukaguzi maalumu 2021/22)	146.22
6.	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo	88.63
7.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	81.80
8.	Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkawawa	75.82
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	73.65

10.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	67.38
11.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	62.42
12.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	44.76
13.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	39.43
14.	Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Ghalani	35.26
15.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	20.81
16.	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	10.74
<b>Jumla</b>		<b>4,118.68</b>

**Chanzo:** Rejista za masurufu

Ninapendekeza kuwa uongozi wa mashirika husika uhakikishe urejeshwaji wa haraka wa masurufu haya ikiwa ni pamoja na kukata kwenye mishahara ya watumishi husika na kuwasilisha ushahidi kwangu kwa uthibitisho.

### **7.5 Uwezekano wa kutokufikiwa kwa thamani ya fedha kwenye vifaa vya ukaguzi wa magari vilivyonunuliwa na Shirika la Viwango Tanzania shilingi bilioni 3.09**

Mnamo tarehe 9 Julai 2020, Serikali ililiagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kusitisha ukaguzi wa magari kupitia mawakala wa nje ya nchi ambao ulihusisha uhakiki wa awali wa ubora wa magari yanayoingizwa nchini kufikia Februari 2021 ambapo mikataba ya mawakala hao ilikuwa inamalizika.

Ukaguzi maalumu katika Shirika la Viwango Tanzania uliohusisha kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Desemba 2022, ulibaini kuwa, tarehe 9 Desemba 2020 Shirika la Viwango Tanzania liliaini mkataba Na. PA/044/2020-2021/HQ/G/24 kwa ajili ya ugavi, usimikaji, upimaji wa ufanisi, mafunzo na uzinduzi wa vifaa vya kukagulia magari kwa bei ya Euro milioni 1.24 sawa na shilingi bilioni 3.39. Pia, nilibaini ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mchakato wa ununuzi katika mkataba huo. Kufuatia ucheleweshwaji huo na katika jitihada za kupata vifaa vya kukagulia magari kabla ya ukomo wa mikataba na mawakala wa nje ya nchi, TBS iliingia mkataba mwengine wa ununuzi wa vifaa vya kukagulia magari vinayyohamishika tarehe 29 Januari 2021. Vifaa hivyo viliwasilishwa na mzabuni mwezi Machi 2021 kwa bei ya Euro 143,853.42 sawa na shilingi milioni 402.79.

Vilevile, nilibaini kuwa mkataba wa awali Na. PA/044/2020-2021/HQ/G/24 ulationezwa muda hadi mwezi Septemba 2022 ili kuruhusu Shirika la Viwango Tanzania kuandaa na kujenga mahali ambapo vifaa hivyo vitafungwa. Vifaa kwenye mkataba huo viliwasilishwa tarehe 12 Septemba 2022 na mzabuni alilipwa Euro milioni 1.18 sawa na shilingi bilioni 3.09 ikiwa ni asilimia 95 ya bei ya mkataba huo. Hata hivyo, hadi mwisho wa ukaguzi mwezi Novemba

2023, vifaa hivyo vilikuwa bado havijafungwa na vilikuwa kwenye ofisi za Shirika la Viwango Tanzania. Hii ilitokana na maagizo mengine ya Serikali mwezi Julai 2022 ya kusitisha ukaguzi wa magari ndani ya nchi; na Shirika la Viwango Tanzania limerudi tena kutumia mawakala wa nje ya nchi.

Vifaa nya kukagulia magari vinavyohamishika vilivyotokana na mkataba wa pili vilifungwa na vilikuwa vinatumika kukagulia magari yanayoingizwa nchini kutoka kwenye nchi ambazo Shirika la Viwango Tanzania halina mawakala kwa kuwa kiwango cha uagizaji wa magari kutoka nchi hizo ni kidogo. Maamuzi kinzani yaliyofanywa yanaweza kupelekea hasara ya shilingi bilioni 3.09 ambazo zililipwa kwenye mkataba wa awali zikiwa ni gharama za ugavi, usimikaji, upimaji wa ufanisi, mafunzo na uzinduzi wa vifaa hivyo; kwani vifaa hivyo bado havijafungwa wala kuhakikiwa ufanisi wake mpaka sasa na vinaweza visitumike tena.

**Ninapendekeza Shirika la Viwango Tanzania lishauriane na Serikali na kutafuta matumizi mbadala ya vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya ukaguzi wa magari. Zaidi ya hayo, Serikali inapaswa kuboresha mchakato na mfumo wake wa kufanya maamuzi ili kuepuka kufanya maamuzi yanayokinanza ambayo yanaweza kupelekea Serikali kupata hasara.**

#### **7.6 Ubadhilifu katika malipo uliofanyika kupitia MUSE shilingi milioni 58.94**

Wakati wa ukaguzi wangu wa malipo kupitia mfumo wa ulipaji Serikalini (MUSE) katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, nilibaini kesi tano za ubadhilifu wa jumla ya shilingi milioni 58.94 uliofanywa kupitia MUSE. Hadi mwisho wa ukaguzi wangu, suala hilo lilikuwa limeripotiwa polisi kwa taratibu zaidi za mashtaka.

Baada ya uchunguzi zaidi wa malipo hayo yaliyofanywa kupitia MUSE kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Juni 2023, nilibaini mapungufu katika matumizi ya mfumo wa malipo. Baadhi ya mapungufu hayo ni: malipo kwa baadhi ya wazabuni wa bidhaa na huduma yaliyofanywa bila kuchunguzwa na afisa mwandamizi, kuwapo kwa vocha za malipo na nyaraka ambatishi ambazo zimepitia hatua zote za malipo lakini hazikupigwa muhuri ili kuepusha kutumika tena; watumishi wenye vyeo nya chini kupewa majukumu ya kuidhinisha malipo, na kuwakabidhi watumishi wapya majukumu ya nafasi nyeti kama kutunza fedha katika ofisi ya malipo bila uchunguzi wa kina kuhusu uadilifu wao.

Ninapendekeza kuwa uongozi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, uimarishe udhibiti wa ndani kwenye malipo katika mfumo hasa juu ya uhakiki na uidhinishaji wa malipo ili kuruhusu malipo halali na yenye viambatishi toshelezi tu. Pia, kwa mujibu wa kifungu cha 2 (c) cha Sheria ya Kukusanya Madeni kutoka kwa maafisa wa Serikali ya mwaka 1970, Chuo kichukue hatua stahiki za kinidhamu na kulipwa kwa kiasi hicho kutoka kwa watumishi waliohusika katika ubadhilifu huo.

#### **7.7 Malipo ya awali ya muda mrefu ya shilingi milioni 143.58**

Chuo Kikuu Mzumbe kiliingia makubaliano na Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA) kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya jenereta ya umeme aina ya Perkins WS4501N1134459. Mnamo tarehe 23 Juni 2021, TEMESA ilihamisha jenereta husika kwenda ofisi yake ya Morogoro kwa ajili ya ukarabati. Tarehe 10 Februari 2022, TEMESA ilitoa makadirio ya ghamama za matengenezo na Chuo Kikuu Mzumbe kilifanya malipo ya awali ya shilingi milioni 21.02 kwa TEMESA mkoa wa Morogoro tarehe 18 Februari 2022.

Hata hivyo, hadi mwisho wa ukaguzi wangu mwezi Septemba 2023, ambapo ni zaidi ya miaka miwili tangu TEMESA ilipochukua jenereta hilo, bado halijarudishwa Chuo Kikuu Mzumbe. Pia, nilibaini ufuatiliaji uliofanywa na Chuo Kikuu Mzumbe hivi karibuni, tarehe 6 Mei 2022, ambao haujajibwa na TEMESA.

Pia, ukaguzi wangu ulibaini malipo ya awali ya shilingi milioni 122.56 kwa zaidi ya miaka mitatu ambayo yalifanywa na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) yenye jumla ya shilingi milioni 120.36 kwa kampuni ya Scan Tanzania; na shilingi milioni 2.19 kwa wazabuni wengine.

Malipo ya awali yaliyokaa muda mrefu bila kupata huduma na bidhaa husika yanaweza kusababisha mashirika tajwa kushindwa au kuchelewa kutoa huduma kwa wateja wake.

Ninapendekeza uongozi wa Chuo Kikuu Mzumbe na CAMARTEC kushirikiana na uongozi wa wazabuni husika ili huduma na vifaa vinavyosubiriwa viwasilishwe bila kuchelewa zaidi. Pia, waangalie namna ya kutoza riba na adhabu kama fidia kwa faida zilizopotea kutokana na ucheleweshwaji huo ikibidi hata kuapeleka mahakamani.

**7.8 Malipo ya safari za nje ya nchi ambazo hazikuidhinishwa na Katibu Mkuu Kiongozi ya jumla ya dola za Marekani 34,623**

Ukaguzi wangu kwenye gharama za safari za nje katika TANESCO nilibaini watumishi watano walilipwa dola za Marekani 34,623 na kusafiri nje ya nchi bila kupata kibali cha kusafiri ambapo ni kinyume na Aya Na.1 ya Mwongozo wa Utumiaji wa Mfumo wa Vibali vya Kusafiri toleo Na. 1 la mwaka 2016 na hali hii ilisababishwa na mapungufu ya udhibiti wa ndani unaoruhusu malipo ya posho ya kujikimu kwa safari za nje bila kibali cha kusafiri kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Napendekeza TANESCO iimarishe udhibiti wa ndani ili kuhakikisha watumishi wote wanaosafiri nje ya nchi kwa malengo binafsi au ya kikazi wanakuwa na kibali cha kusafiri kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

**7.9 Malimbikizo ya madeni ya jumla ya shilingi trilioni 3.49 wanayodaiwa mashirika ya umma**

Madeni ni madai halali ambayo bado hayajalipwa kwa bidhaa, kazi ama huduma zilizotolewa kwa mashirika ya umma.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mashirika ya umma 99 yana madeni ya jumla ya shilingi trilioni 3.49 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, sawa na upungufu wa asilimia 54 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo mashirika 99 yalikuwa na jumla ya shilingi trilioni 7.65. Taarifa za kina za madeni kwa kila shirika zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. VII.**

Madeni hayo katika mashirika ya umma yalitokana na changamoto za mtiririko wa fedha zilizochangiwa na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Serikalini, au kutokufanya vizuri kwa biashara kwa mashirika ya kibiashara.

Kuchelewa kulipa kwa wakati madeni yaliyoiva kunashusha hadhi na kuharibu taswira ya mashirika ya umma na Serikali. Pia, wazabuni wanaweza kukataa kutoa huduma au kutoa huduma kwa masharti magumu kwa mashirika husika hivyo kuathiri utendaji wa shughuli za kila siku za mashirika hayo. Aidha, ucheleweshaji wa malipo kwa muda mrefu husababisha riba na adhabu ambazo zinakuwa ni gharama za ziada na zisizokuwa na tija.

**Ninapendekeza kuwa;** (a) mashirika ya kibiashara yaboreshe na kuimarisha utendaji wake wa kibiashara ili kuwa na mtiririko wa fedha unaojitosheleza na wenyewe kuendana sawia na madeni yanayoiva; na (b) madeni yanayotegemea fedha kutoka Serikalini, Serikali ijithahidi kutoa fedha kwa wakati katika mashirika husika.

# SURA YA NANE

## USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA



### 8.0 Utangulizi

Usimamizi wa bajeti katika mashirika ya umma unazingatia miongozo na maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Fedha, pamoja na sheria ya bajeti sura ya 439 na kanuni zake.

Lengo kuu la usimamizi wa bajeti ni kusaidia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa taifa 2021/22-2025/26 na mpango mkakati wa mashirika ya umma husika.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini ukiukwaji wa miongozo ya bajeti hususani ushirikishwaji wa wadau muhimu katika kuandaa na kutekeleza bajeti, utoaji wa fedha za bajeti kutoka Serikalini, ukusanyaji pungufu wa mapato yatokanayo na vyanzo vyta ndani, na matumizi ya fedha zaidi ya bajeti.

Vilevile, nilifanya tathmini ya uandaaji na utekelezaji wa bajeti katika Mashirika ya Umma 215 na kubaini mashirika 45 yalikuwa na baadhi ya mapungufu katika kuzingatia sheria na miongozo ya bajeti (**Kiambatisho Na. I**).

Maelezo kuhusu mapungufu yaliobainika na mapendekezo ya kuboresha katika kuzingatia sheria na miongozo ya bajeti yamebainishwa hapa chini.

### 8.1 **Utoaji hafifu endelevu wa fedha za bajeti kutoka Serikalini shilingi trilioni 1.01**

Katika uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti za mashirika ya umma, nilibaini kuwa mashirika 50 kati ya mashirika yasiyo ya kibiashara 195 ambayo hupokea fedha za bajeti kutoka Serikalini, hayakupokea zaidi ya asilimia 10 ya fedha zilizopangwa kwenye bajeti. Mashirika haya yalipokea jumla ya shilingi trilioni 1.08, sawa na asilimia

52 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi trilioni 2.09. Hii inaonesha upungufu wa utoaji wa fedha za bajeti wa jumla ya Shilingi trilioni 1.01 sawa na asilimia 48 (**Kiambatisho VIII**).

Vilevile, hali hii ilionekana katika mwaka 2020/21 na 2021/22, ambapo Serikali haikutoa shilingi trilioni 1.13 (asilimia 29 ya bajeti) na shilingi bilioni 161.88 (asilimia 30 ya bajeti) mtawalia.

Utoaji hafifu wa fedha za bajeti kutoka Serikalini unaweza kusababisha mashirika husika kushindwa kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi. Hii inaweza kuzorotesha utoaji wa huduma kwa umma. Vilevile, utoaji hafifu wa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti kunaweza kusababisha kuchelewa kwa miradi au kutokamilika, hivyo kushindwa kufikia malengo ya shirika.

Ninapendekeza Serikali ihakikishe uhalisia wa makadirio ya bajeti yanayowasilishwa na mashirika ya umma ikiwa na kutoa fedha za bajeti kwa ukamilifu ili kuwzesha utekelezaji wa kazi zilizopangwa na kuwzesha kufikiwa kwa malengo ya mashirika ya umma.

## **8.2 Ukusanyaji pungufu wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani shilingi bilioni 284.71**

Mashirika ya umma hukusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani kama vile ada, mauzo, na mapato ya uwekezaji. Mapato ya vyanzo vya ndani husaidia kuongeza uwezo wa kifedha wa mashirika ya umma katika kuendesha shughuli zao za kila siku.

Nilibaini kuwa mashirika ya umma 66 kati ya 215 yalikusanya shilingi bilioni 514.39, sawa na asilimia 64 ya fedha zote za bajeti ya mapato ya vyanzo vya ndani ambayo ni shilingi bilioni 799.09. Hivyo, jumla ya shilingi bilioni 284.71, sawa na asilimia 36 ya fedha za bajeti ya mapato ya nyanzo vya ndani, hazikukusanywa (**Kiambatisho Na. IX**).

Aidha, ukilinganisha na mwaka 2020/21 na 2021/22, ukusanyaji pungufu wa mapato ya vyanzo vya ndani umekuwa unabadilika badilika, ambapo shilingi bilioni 174.63 (asilimia 32 ya bajeti) na shilingi trilioni 1.61 (asilimia 63 ya bajeti) mtawalia hazikukusanywa.

Mashirika ambayo yaliathiriwa zaidi na upungufu wa fedha kwa kushindwa kufikia malengo yake ya ukusanyaji kwa asilimia 50 na zaidi yalikuwa: Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari, Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako, Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibailojia Tanzania, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe, Kampuni ya TTCL Pesa, Mfuko wa Maendeleo ya Zao

la Pamba, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania na Bodi ya Korosho Tanzania.

Zifuatazo ni sababu za upungufu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani;

Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zinakabiliwa na changamoto za kukusanya madeni kutoka kwa wateja wao baada ya huduma kutolewa hususani mashirika ya Serikali. Hii ni kutokana na ukosefu wa mita za malipo ya kabla.

Taasisi za elimu ya juu zimeathiriwa na idadi ndogo ya wanafunzi waliodahiliwa ikilinganishwa na mpango wa udahili. Hii inatokana na umuhimu wa programu zinazotolewa na chuo kwa wanafunzi, na idadi ndogo ya wanafunzi wanaopata mikopo ya elimu ya juu kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mamlaka za udhibiti zinakumbana na changamoto ya kukosekana kwa mfumo thabiti wa kukusanya ada za kila mwaka kutoka kwa mashirika yanayosimamiwa na mamlaka hizo.

Mapato yasiyokusanywa husababisha upungufu wa fedha zilizopangwa kufanya shughuli ambazo zingesaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza tena mashirika ya umma husika yafanye tathmini kamili katika mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Tathmini hiyo inapaswa kutambua maeneo dhaifu na kutengeneza mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato.**

### **8.3 Matumizi ya fedha zaidi ya kiasi cha bajeti na uhamishaji wa fedha katika vifungu vya bajeti bila kufuata utaratibu shilingi bilioni 21.14 na shilingi bilioni 41.42 mtawalia**

Nilibaini mashirika ya umma nane yalikuwa na bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 16.29 lakini yalifanya matumizi ya shilingi bilioni 37.43. Hali hiyo ilisababisha kuwa na matumizi ya shilingi bilioni 21.14 ambayo hayakuwa katika bajeti au yalitumia zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenvye bajeti. Matumizi haya ya zaidi ya kiasi cha bajeti hayakupata idhini ya Afisa masuuli au Bodi ya wakurugenzi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.17.**

Katika Mwaka uliopita wa 2021/22, tatizo hili lilionekana pia; ambapo mashirika ya umma saba yalitumia jumla ya shilingi bilioni 118.04 ambazo hazikuwa katika bajeti bila idhini ya afisa masuuli au Bodi ya wakurugenzi. Hii inatokana na kutokuwa na Mfumo madhubuti unaosimamia na kudhibiti matumizi ya fedha zilizopangwa, makadirio

ya matumizi yasiyoridhisha wakati wa maandalizi ya bajeti, na kutofanya marejeo ya bajeti.

Matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti au zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti yanakwamisha utekelezaji kamili wa shughuli zilizopangwa kufanyika kwa mwaka husika, hatimaye kuathiri malengo ya shirika.

**Jedwali Na. 17: Mashirika ya umma yaliyofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti**

Na.	Jina la Taasisi	Aina ya matumizi	Bajeti iliyoidhini shwa	Matumizi halisi	Nakisi ya bajeti
			Shilingi milioni		
1.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Manunuzi ya mbolea	100.00	12,446.5	(12,346.50)
2.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	kuboresha miundombinu katika poli tengefu la Pololeti	0	3,877.68	(3,877.68)
3.	Shirika la Posta Tanzania	Matumizi ya kawaida	3,571.87	5,405.41	(1,833.54)
4.	Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila	Manunuza ya vifaa tiba na vifaa vingine	4,670.99	5,927.57	(1,256.58)
5.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Matumizi ya kawaida	7,343.79	8,456.38	(1,112.59)
6.	Kituo cha Uwekezaji APC	Matumizi ya kawaida	603.22	1,118.14	(514.92)
7.	Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Posho ya mujukumu	0	123	(123.00)
8.	Kampuni ya Huduma za Meli	Matumizi ya kawaida	0	77.03	(77.03)
<b>Jumla</b>		<b>16,289.87</b>	<b>37,431.71</b>	<b>(21,141.84)</b>	

**Chanzo: Taarifa za utekelezaji wa bajeti**

Kutoka kwenye jedwali la hapo juu, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ina nakisi kubwa iliyosababishwa na manunuzi ya mbolea kuzidi bajeti kwa shilingi bilioni 12.35.

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilitumia shilingi bilioni 3.88 ambazo hazikuwa katika bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika pori tengefu la Pololeti.

Pia, nilibaini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati ilihamisha fedha katika kifungu cha bajeti kwa ajili ya matumizi ya shilingi bilioni 12.69 bila idhini ya Wizara ya Fedha, kinyume na Kanuni ya 26 na 27 ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Hii inasababishwa na

kutofanyika kwa mapitio ya bajeti inayokwamisha utekelezaji wa kazi zingine.

Vilevile, nilibaini Shirika la Umeme Tanzania lilhamisha fedha katika kifungu cha bajeti kwa ajili ya matumizi ya shilingi bilioni 28.72 zilizobajetiwa lakini halikuwasilisha taarifa ya uhamisho kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya udhibiti na ufuatiliaji, kinyume na Kifungu cha 57(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Hii ni kutokana na kutotilia maanani uzingatiaji wa sheria za bajeti.

Ninapendekeza mashirika ya umma husika; (a) yahakikishe yanafanya makadirio sahihi ya bajeti na kufanya marejeo katikati ya mwaka ili kuhakikisha shughuli zote tarajiwa zimebekwa kwenye bajeti; (b) yaombe idhini kutoka kwa mamlaka husika kwa ajili ya kubadilisha matumizi ya fedha zilizo kwenye bajeti; na (c) yatumie mfumo wa udhibiti wa bajeti na kuzingatia sheria za bajetii.

#### **8.4 Ushiriki wa wadau usioridhisha katika maandalizi ya bajeti**

Mashirika ya umma yanatakiwa kuandaa mipango na makadirio ya bajeti kwa njia ya kushirikisha na kupata idhini kutoka kwa Mamlaka zao za Kisheria hususani Baraza la Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika muongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini mashirika ya umma 16 hayakushirikisha ipasavyo wadau wao katika uandaaji wa bajeti kama nilivyoainishwa katika **Jedwali Na.18**.

Mashirika hayo hayakuzingatia umuhimu wa kushirikisha wadau wote katika mchakato wa maandalizi ya bajeti. Hali hii inonesha kutokuwa na uwazi katika mchakato wa bajeti, hivyo kuibua shaka kuhusu uwajibikaji na usimamizi wa kifedha.

**Jedwali Na. 18: Mashirika ya umma yenye ushiriki usioridhisha katika maandalizi ya bajeti**

Na.	Aina ya Taasisi	Madhaifu Yaliyoonekana
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi	Kutokuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti na makadirio ya bajeti hayakuwasilishwa kwenye baraza la wafanyakazi.
2.	Chuo cha Diplomasia	Kamati ya bajeti haikufanya vikao vyta bajeti kama inavyotakiwa na kanuni ya 17(3) ya kanuni za bajeti, 2015
3.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Kamati ya bajeti ya makao makuu na ofisi za kanda hazijaundwa

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Taasisi</b>	<b>Madhaifu Yaliyoonekana</b>
4.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	Ushirikishwaji usioridhisha katika ngazi ya idara na vitengo
5.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Kamati ya bajeti haijaundwa
6.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu	Makadirio ya bajeti hayakuwasilishwa kwenye baraza la wafanyakazi
7.	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	Hakuna ushahidi unaoonesha ushirikishaji wa maandalizi ya bajeti katika ngazi ya idara,kamati ya bajeti na baraza la wafanyakazi
8.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu	Hakuna ushahidi wa ushiriki wa Kamati ya Bajeti katika mchakato wa bajeti.
9.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Kamati ya bajeti haikufanya vikao vya bajeti
10.	Hospitali ya Taifa Muhimbili Mloganzila	Hakuna ushahidi unaoonesha ushirikishaji wa maandalizi ya bajeti katika ngazi ya idara,kamati ya bajeti na baraza la wafanyakazi
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe	Kamati ya bajeti haikufanya vikao katika mwaka husika
12.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea	Kamati ya bajeti haijaundwa
13.	Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania	Hakuna ushahidi unaoonesha ushirikishaji wa maandalizi ya bajeti katika ngazi ya idara
14.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	Kamati ya bajeti haijaundwa
15.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Makadirio ya bajeti hayakuwasilishwa kwenye baraza la wafanyakazi
16.	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania	Makadirio ya bajeti hayakuwasilishwa kwenye baraza la wafanyakazi

*Chanzo: Mapitio ya taarifa mbalimbali za menejimenti*

**Ninapendekeza mashirika ya umma kutambua umuhimu wa ushiriki wa wadau wote katika maandalizi ya bajeti kwa ajili ya uwazi.**

# SURA YA TISA

## USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI



### 9.0 Utangulizi

Sheria ya Ununuzi wa Umma, [Sura 410] inafafanua mchakato wa ununuzi kuwa ni njia ya kununua, kukodisha, au upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa taasisi nunuzi na ikijumuisha shughuli zote zinazohusiana na kupata bidhaa, kazi za ujenzi au huduma yoyote, ikijumuisha maelezo ya mahitaji, uteuzi na mwaliko wa wazabuni, maandalizi ya zabuni, utoaji na usimamizi wa mikataba.

Nilifanya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba na ununuzi ili kujiridhisha iwapo sheria, sera, taratibu, haki pamoja na uwazi vilizingatiwa katika mchakato mzima wa ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi na huduma. Nilibaini kutokuzingatiwa kwa sheria za ununuzi kama vile mikataba iliyotekelizwa bila dhamana ya utekelezaji wa zabuni, usimamizi duni wa mkataba, na mikataba iliyotiwa saini bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Zaidi ya hayo, nilitoa hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake katika michakato ya ununuzi wa kazi za ujenzi, bidhaa na huduma katika mashirika ya umma 215, ambapo mashirika 85 yalikuwa na baadhi ya mapungufu katika kuzingatia sheria za ununuzi (**Kiambatisho Na. I**).

Sura hii inaonesha kasoro zilizobainika wakati wa ukaguzi wa mchakato wa ununuzi na usimamizi wa mikataba ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma katika mashirika ya umma. Hivyo nilibaini kasoro zifuatazo:-

### 9.1 Mapungufu katika usimamizi wa dhamana za utekelezaji wa mikataba iliyotolewa

#### a) Mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 31.11 iliyotekelizwa bila dhamana za utekelezaji wa mikataba

Nilibaini mashirika ya umma 14 yalitekeleza mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 31.11 bila kuwasilisha dhamana za zabuni ikilinganishwa na mashirika ya umma nane katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22. Pia, nilibaini taasisi saba zilizosaini mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 7.16, dola za Marekani milioni 3.51 na Euro milioni 0.67 kabla ya watoa huduma kuwasilisha dhamana za utekelezaji wa zabuni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 29 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na Aya ya 11.2 ya Mwongozo wa Dhamana wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma wa Februari 2022. Maeleo zaidi yametolewa katika **Kiambatisho Na. X.**

Vilevile, nilibaini uwasilishaji wa dhamana baada ya kusainiwa kwa mikataba kuwa ni sharti lililowekwa na benki zao ambazo ziliwataka kuwasilisha mkataba uliosainiwa na pande zote kwa ajili ya uthibitisho wa kuwapo kwa mkataba ambapo ni kinyume na Kanuni ya 29(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.

#### b) Dhamana za utendaji za mikataba zilizopungufu ya kiasi kinachohitajika shilingi bilioni 3.31

Aya ya 11.3 ya Mwongozo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma uliotolewa Februari 2022 inataka kiasi cha dhamana ya utekelezaji wa zabuni kuwa sawa na asilimia 10 ya kiasi cha zabuni kwa dhamana ya benki na asilimia 15 kwa dhamana ya bima.

Katika ukaguzi wangu wa mikataba iliyosainiwa katika mashirika manne nilibaini kuwa dhamana za utekelezaji wa mikataba katika mfumo wa dhamana za bima zilikuwa chini ya asilimia 15 ya thamani halisi. Wazabuni walitoa dhamana za utekelezaji wa zabuni katika mikataba kiasi sawa na asilimia 10 ya bei ya mikataba, hivyo kusababisha kuwa na mikataba yenyе dhamana iliyopungufu kwa asilimia 5 ya thamani ya dhamana ya bima kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 19**.

#### Jedwali Na. 19: Taasisi zenye dhamana ya bima iliyopungufu ya asilimia 15

Na.	Jina la Taasisi	Idadi ya Mikataba	Kiasi cha Mkataba (Sh. Milioni)
1	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi	4	1,624.17

2	Shirika la Umeme Tanzania	1	1,056.07
3	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	1	407.17
4	Shirika la Viwango Tanzania	1	226.00
<b>Jumla</b>		<b>7</b>	<b>3,313.41</b>

**Chanzo:** faili za Ununuzi

**c) Dhamana za utekelezaji wa mikataba ziliisha muda kabla ya kukamilika kwa mikataba ya shilingi bilioni 86.23**

Nilibaini kuwa Kampuni ya STAMIGOLD, Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro na Shirika la Viwango Tanzania zilipokea dhamana za zabuni kwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 31.09, shilingi bilioni 26.33 na shilingi bilioni 23.64 mtawalia ambazo hazikuwa zikidhamini muda wote wa utekelezaji wa mikataba husika.

Zaidi ya hayo, nilibaini mashirika ya umma matano ambayo muda wa dhamana za mikataba ulikuwa umekwisha kwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 5.18, na dola za Marekani milioni 6 wakati mikataba hiyo bado ikiendelea kutekelezwa kinyume na Kanuni ya 29(6) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inayotaka kuweka dhamana hadi kukamilika kwa mikataba. Taasisi husika ni kama zinavyooneshwaa katika Jedwali Na.20. Hii hutokea kutokana na kuongezwa kwa muda wa mikataba bila kuongeza muda wa dhamana za utekelezaji wa zabuni.

**Jedwali Na. 20: Taasisi zenyne dhamana za utekelezaji wa zabuni zilizoisha muda**

Na.	Jina la Taasisi	Idadi ya Mikataba	Kiasi cha Mkataba (Sh. Milioni)	Hali ya Dhamana
1	Kampuni ya Mkulazi	3	1,854.09	Kuisha muda wa dhamana
2	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	2	1,347.24	
3	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi	5	1,165.77	
4	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	1	812.14	
<b>Jumla</b>			<b>5,179.24</b>	
<b>Taasisi zenyne Kiasi cha (Dola za Marekani) "milioni"</b>				
5	Kampuni ya Huduma za Meli	4	6.00	Kuisha muda wa dhamana

**Chanzo:** Mafaili ya Ununuzi

Kutokana na kukosekana kwa dhamana za zabuni mashirika ya umma yanaweza kupata hasara au kushindwa kuwajibisha wazabuni au makandarasi iwapo watashindwa kutekeleza masharti ya mikataba wakati hakuna dhamana za utekelezaji wa zabuni.

Ninapendekeza: (a) mashirika ya umma husika yahakikishe kuwa mikataba yote ina dhamana za utekelezaji wa zabuni zinazojitosheleza ili kulinda maslahi ya mashirika husika na kuepusha upotevu wa fedha unaoweza kutokea; (b) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ichukue hatua stahiki dhidi ya taasisi husika; na (c) mashirika ya umma husika yahakikishe kuwa yanapotekeleza mchakato wa kuongeza muda wa mikataba yanaongeza pia muda wa dhamana za utekelezaji wa zabuni.

## **9.2 Mapungufu katika usimamizi wa mikataba ya utoaji wa huduma na kupokea bidhaa**

### **(a) Kuchelewa kuwasilisha bidhaa na kutoa huduma zilizonunuliwa zenye thamani ya shilingi bilioni 14.84**

Katika ukaguzi wangu wa mikataba ya ununuzi wa bidhaa na huduma katika mashirika ya umma nilibaini wazabuni katika mashirika ya umma 22 walichelewesha utoaji wa huduma na uwasilishwaji bidhaa za shilingi bilioni 14.84 kwa kipindi cha kuanzia siku 30 hadi siku 1,140. Katika ukaguzi wangu wa mwaka 2022/23 nimeendelea kubaini kuwa hali haijaimarika ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo niliripoti mashirika ya umma 12 ambayo yalicheleweshewa huduma na bidhaa zenye jumla ya shilingi bilioni 18.09 kwa muda wa siku 22 hadi 487. Mashirika ambayo yamejirudia katika udhaifu huo ni: Shirika la Mawasiliano Tanzania, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania, na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hii ina maana kuwa menejimenti za mashirika husika bado hazijachukua hatua madhubuti kusimamia na kufuatilia masharti ya mikataba katika utekelezaji wa mikataba. Ucheleweshaji huu ni kinyume na Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 na muda wa utekelezeji uliokubaliwa katika mikataba iliyosainiwa. Orodha ya mashirika husika imeoneshwa kwenye Kiambatisho XI.

### **(b) Kuchelewa kukamilika kwa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 56.11**

Nilikagua utekelezaji wa miradi katika mashirika ya umma ambapo mashirika manne yenye miradi ya jumla ya shilingi bilioni 56.11 yalikuwa na ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi kwa takribani siku 37 hadi siku 1260 ikilinganishwa na siku 90 hadi siku 515 katika

mashirika matano kwa mwaka wa fedha 2021/22, hii inaonesha mashirika ya umma bado hayajashughulikia mapungufu katika usimamizi wa miradi. Ucheleweshaji huo ultokana na kuchelewa kukabidhiwa eneo kwa Mkandarasi, kucheleweshwa kwa idhini ya utekelezaji, mvua na mabadiliko ya kazi. Maelezo ya taasisi husika yameoneshwa kwenye Jedwali Na.21.

**Jedwali Na. 21: Orodha ya taasisi zilizochelewa kukamilisha miradi**

Na.	Jina la Taasisi	Jina la Mradi	Kiasi cha Mikataba (Sh. Milioni)	Muda uliochelewa (Siku)
1	Kampuni ya Ujenzi na Matengen ezo ya Usafirisha ji na Usambaza ji wa Umeme	Ujenzi wa laini za huduma katika maeneo mbalimbali	25,896.70	37 to 611
2	Kampuni ya Mkulazi	Ujenzi wa Kambi ya Wakata Miwa	24,783.91	37 to 228
		Ujenzi wa Kilomita 56.439 za laini ya umeme wa 33kv yenye kondakta ukubwa wa 150mm <sup>2</sup> kwa ajili ya Kusambaza umeme katika Kiwanda cha Mbigiri.		
		Ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji (Bwawa la Dhahabu) lenye uwezo wa 3.5mm <sup>3</sup>		
		Kubuni, kusambaza kufungwa, kujaribiwa na kutumika ya Rasilimali za Biashara		
		Kufanya Usafi wa shamba la hekari 380		
		Kusambaza vifaa vya semina		
		Kusambaza vipuri		
3	Chuo Kikuu Mzumbe	Ujenzi wa Jengo la Utawala la Kampasi Kuu ya Maekani	4,815.69	183
		Kufungwa, kujaribiwa na kutumika kwa Vifaa vya Kuzima Moto katika Kampasi Kuu	187.99	81
4	Hifadhi za Taifa Tanzania	Ujenzi wa mradi wa umeme wa maji	511.68	1260
<b>Jumla</b>			<b>56,109.24</b>	

*Chanzo: Mafaili ya ununuzi*

Ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli husika una athari mbaya katika kufikia malengo ya mashirika ya umma na ukuaji wa Uchumi kwa nchi.

Pia nilibaini kuwa mashirika ya umma yaliyobainika hayakuchukua hatua kama vile kutoza fidia dhidi ya wazabuni wa bidhaa au watoa huduma ili kurekebisha kasoro kwa kutokuzingatia sheria na masharti ya mikataba licha ya kuwapo kwa matakwa na masharti ya mikataba.

Ninapendekeza mashirika ya umma husika yachukue hatua zitakazoimarisha utekelezaji na ukamilishaji wa miradi na kuhakikisha bidhaa na huduma zilizonunuliwa zinawasilishwa kwa wakati. Pia, yazingatie kutoza fidia kwa ucheleweshwaji wa bidhaa na huduma kulingana na masharti ya mikataba.

### **9.3 Kutokufuata sheria ya ununuzi katika Kiwanda cha Dawa Keko kwa ununuzi wa dola za Marekani milioni 4.97**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Desemba 2019 iliingia makubaliano na Kampuni ya Diocare kwa ajili ya urekebishi wa umiliki na uendeshaji wa Kiwanda cha Dawa Keko (1997) kupitia Msajili wa Hazina. Muundo wa ubia wa Kampuni ulikubali kuwa asilimia 70 itamiliwi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na asilimia 30 itamiliwi na Kampuni ya Diocare kuanzia tarehe ya makubaliano hayo.

Nilibaini Kiwanda cha Dawa Keko hakikuwa kimeanzisha bodi ya zabuni ili kuwezesha ununuzi wa bidhaa, huduma, kazi za ujenzi, na uondoaji wa mali za umma kupitia mchakato wa zabuni kinyume na matakwa ya kifungu cha 31 (1)-(2) cha Sheria ya ununuzi wa Umma Sura 410. Kutokana na hali hiyo, nilikuta ununuzi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.97 ambao mchakato wake na kuidhinishwa ulifanywa na Mkurugenzi wa Fedha pamoja na Afisa Masuuli pekee. Hii ni kinyume na Kifungu cha 33 (1)(c ) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410.

Aidha, nilibaini Afisa Masuuli hakuteua kamati ya kutathmini zabuni kama inavyotakiwa na Kanuni ya 202 za Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 iliyofanyiwa marekebiso na Kanuni ya 69 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Kama zilivyorekebishwa) za mwaka 2016. Hii ilisababisha kutokuzingatiwa kwa taratibu za tathmini katika zabuni za ununuzi.

Ni maoni yangu kuwa, kuna uwezekano wa kuwapa zabuni wazabuni wasio na uwezo kutokana na kutokufuata sheria za ununuzi, hivyo kusababisha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora na kuingia gharama kubwa kwa bidhaa ambazo haziakisi thamani ya fedha.

Ninapendekeza Kiwanda cha Dawa Keko kuzingatia udhibiti wa ununuzi uliowekwa katika sheria za ununuzi ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi, ufanisi na kupata thamani ya fedha.

#### **9.4 Mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 9.89 na dola za Marekani milioni 2.95 kutokuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Maafisa Sheria kwa uhakiki**

Ripoti yangu ya mwaka 2021/22 ilionesha mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 45.71 na dola za Marekani milioni 7.46 katika mashirika ya umma nane kutokuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hali hiyo imejirudia katika ukaguzi niliofanya mwaka huu 2022/23, Uguzi wangu ulibaini uboreshaji kidogo, ambapo kulikuwa na mikataba yenyе thamani ya shilingi bilioni 9.89 na dola za Marekani milioni 2.95 katika mashirika ya umma manne ambayo hayakufanya uhakiki wa mikataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wala Afisa Sheria wa shirika husika kabla ya kusaini mikataba hiyo, kinyume na Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama zilivyorekebishwa na kanuni ya 2 na 3 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za mwaka 2016. Orodha ya mashirika ya umma yenyе mikataba ambayo haikuhakikiwa imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 22**.

##### **Jedwali Na. 22: Mashirika ambayo mikataba yake haikupekuliwa na Mwanasheria Mkuu**

Na.	Jina la Taasisi	Idadi ya Mikataba	Kiasi cha Mikataba (Sh. Milioni)
1	Chuo Kikuu cha Dodoma	97	8,515.02
2	Bodi ya Tumbaku Tanzania	1	1,156.49
3	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	4	214.01
<b>Jumla</b>		102	9,885.52
<b>Taasisi zenye Kiasi cha (Dola za Marekeni) "milioni"</b>			
4	Kiwanda cha Dawa Keko	4	2.95

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi*

Kutokuhakikiwa kwa mikataba na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya utekelezaji kunaweza pelekea uwepo wa vifungu visivyo na tija kwa taasisi husika na kusababisha hasara wakati wa utekelezaji.

Ninapendekeza; (a) mashirika ya umma husika yahakikishe mikataba inahakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Afisa wa Sheria ili kuepusha migogoro na hasara za kisheria zinazoweza kutokea; na (b) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ichukue hatua stahiki kwa

mashirika ya umma yanayosaini mikataba yenyе thamani kubwa kabla ya kuhakikiwa.

### 9.5 Ununuzi uliofanywa kwa njia zisizosahihi na zisizothibitishwa

Nilibaini Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi walibadilisha njia ya ununuzi katika mikataba yenyе jumla ya shilingi bilioni 4.54 na shilingi milioni 128.20 mtawalia kutoka kwenye njia ya ushindani iliyoinishwa kwenye Mpango wa ununuzi wa Mwaka kwenda njia ya ununuzi ya dharura na mzabuni mmoja bila kuweka taarifa za msingi na uhalali wa mabadiliko hayo. Hii ni kinyume na Kanuni ya 149 (1) (3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 iliyorekebishwa na Kanuni ya 51 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za mwaka 2016.

Aidha, nilibaini kuwa Kiwanda cha Dawa Keko (Kinamilikiwa kwa asilimia 70 na Serikali kupitia Msajili wa Hazina) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili hawakuzingatia njia za ununuzi na kikomo kilichowekwa kwa kila njia ya ununuzi wa bidhaa zenyе thamani ya shilingi bilioni 11.21 na shilingi milioni 307.81 mtawalia, kwa kufanya ununuzi zaidi ya kiasi kilichopo kwenye njia yenyе kikomo cha shilingi milioni 120 kwa kila zabuni.

Vilevile, nilibaini Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilitoa zabuni Na. PA/001/2022-2023/HQ/W/69 ya ujenzi, ufungaji, upimaji na ukamilishaji wa Vituo Vidogo vya KV 132 katika njia za usambazaji umeme za Tabora - Katavi na Tabora -Kigoma kupitia Loti A na Loti B kwa kutumia njia ya ununuzi ya mzabuni mmoja kwa loti A na loti B kwa mkataba wa thamani ya shilingi bilioni 19.19 na shilingi bilioni 12.31 mtawalia. TANESCO ilitumia siku 83 katika mchakato wa zabuni ambazo zilitosha kutumia njia ya kitaifa ya ushindani ambayo inahitaji angalau siku 14. Nina shaka na kushindwa kwa Shirika la Umeme Tanzania kupanga mpango wa kazi za ujenzi, kusimika na kuzindua kazi kwani mikataba ya malighafi, vifaa pamoja na michoro ilisainiwa tangu tarehe

18 Septemba 2021, hivyo kupelekea kukosa uhalali wa kutumia njia ya ununuzi ya mzabuni mmoja.

Matumizi ya njia zenyet vikwazo au ununuzi kwa kutumia mzabuni mmoja hupunguza ushindani hivyo kuongeza hatari ya ununuzi kwa bei iliyozidi, hivyo kusababisha kushindwa kufikia thamani ya fedha.

Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe yanakuwa na mipango na makadirio sahihi ili ununuzi ufanyike kwa ushindani ili kufikia thamani ya fedha; na inapotokea haja ya kubadili njia ya ununuzi, uhalali wa matumizi ya njia hiyo lazima uwekwe wazi kabla ya kuidhinishwa na bodi ya zabuni.

#### **9.6 Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mikataba kulikosababisha ongezeko la gharama kiasi cha shilingi milioni 808.85 na Euro milioni 4.84**

Tarehe 10 Februari 2020, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania iliingia mkataba Na. AE/016/2019-20/HQ/G/O1C kwa ajili ya kusanifu, kuleta, kusimika na kuzindua Kreni tatu. Kreni hizo zilikusudiwa kutumika katika bandari mbili: Kreni mbili katika Bandari ya Dar es Salaam na moja katika Bandari ya Mtwara kwa bei ya mkataba wa Euro milioni 32.26 kwa miezi 16. Miogoni mwa masharti ya mkataba ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kulipa malipo ya awali ya asilimia 10 sambamba na Mkandarasi kuwasilisha dhamana ya benki ya malipo hayo ya awali.

Hata hivyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari haikuweza kufanya malipo ya awali kwa wakati na kutoa barua ya utambuzi (letter of credit) hivyo kuchelewesha kuanza kwa mkataba na kusababisha ongezeko la gharama za mkataba kwa asilimia 15 sawa na (Euro milioni 4.84) na kufanya bei mpya ya mkataba kuwa jumla ya Euro milioni 37.10.

Aidha, katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania nilibaini malipo yaliyofanywa tarehe 28 Septemba 2022 ya dola za Marekani 350,111 (Sawa na shilingi milioni 808.85) zikiwa ni gharama za ziada za uhifadhi kutokana na kuchelewa kuwasilisha chombo cha kuongoza meli kiitwacho Mwambani katika eneo la meli ya Kampuni ya Southern Engineering iliyopo Mombasa-Kenya kwa ajili ya matengenezo na kubadili injini kuu pamoja na gia.

Nina mashaka kuwa ucheleweshaji uliosababisha gharama za ziada za shilingi milioni 808.85 ilitokana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kuwa na changamoto ya ukata uliotokana na kuchelewa kupokea fedha pamoja na kupata kibali cha kusafirisha Tug - Mwambani hadi Mombasa.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ihakikishe inapanga vizuri miradi itakayofanyika kwa kuzingatia hali ya upatikanaji wa fedha; na kuweka udhibiti katika usimamizi wa mipango ya matengenezo ya vifaa ili kuepusha mabadiliko ya bei zisizokuwa za lazima kwa Mamlaka.**

#### **9.7 Wizara kuingilia mchakato wa ununuzi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na kupelekea ongezeko la gharama shilingi milioni 702.68**

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilikuwa na zabuni Na. EA/055/2020-2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka. Zabuni ilitolewa tarehe 9 Machi 2022 kwa gharama ya mkataba ya shilingi bilioni 9.80 baada ya taratibu za tathmini.

Tarehe 21 Aprili 2022 zabuni ilifutwa kwa kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu kufutwa na kutangaza upya zabuni. Baada ya hapo, zabuni ilitangazwa tena tarehe 06 Mei 2022, na mzabuni huyo huyo alipewa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 10.48 ambao ulikuwa juu zaidi kwa shilingi milioni 686.60 na gharama nyingine za mchakato wa zabuni shilingi milioni 16.08. Ni maoni yangu kuwa, hapakuwa na mantiki ya kufutwa kwa zabuni hiyo mwanzoni.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 231 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2016, iwapo kulikuwa na malalamiko yoyote kuhusu uteuzi wa mzabuni aliyeshindwa katika mchakato wa zabuni, wazabuni ambao hawakufanikiwa walitakiwa kutoa malalamiko ama kwa kuyaleta kwa Afisa Masuuli wakati wa muda wa kusubiri au kwa kukata rufaa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na si vinginevyo.

Hali hii inachangiwa na ukiukwaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kutofuatwa kwa taratibu hali iliyosababisha ongezeko la bei ya mkataba na kuchelewesha utekelezaji wa ujenzi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Wizara ya Maliasili na Utalii kuzingatia matakwa ya sheria na taratibu za ununuzi ili kuepusha gharama ambazo si za lazima na kusaidia**

ufikiwaji wa malengo ya Mamlaka. Pia, Serikali inapaswa kubaini iwapo hasara hiyo ilisababishwa na uzembe au kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo kinyume na Kifungu cha 2 (c) cha Sheria ya Kukusanya Madeni kutoka kwa Maafisa wa Serikali ya mwaka 1970 kwa ajili ya kurejesha hasara hiyo kutoka kwa maafisa husika.

#### **9.8 Ununuzi wa Magari pasipokuwa na kibali cha Waziri Mkuu yenye thamani ya shilingi bilioni 2.34**

Nilibaini Shirika la Umeme Tanzania lilinunua magari 19 kwa ajili ya mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere na mashine za kusambaza umeme (Hydraulic Digger Derrick) kwa ajili ya kazi za usambazaji umeme kwa gharama ya jumla ya shilingi bilioni 2.34 bila kupata kibali kutoka kwa Waziri Mkuu, kinyume na Waraka Na. 2 wenye kumbukumbu Na. CEA/188/292/03/2 uliotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi tarehe 20 Septemba 2021.

Maoni yangu ni kuwa, kukiukwa kwa udhibiti ulioanzishwa na Katibu Mkuu Kiongozi kuitia Waraka kuhusu usimamizi wa magari unaweza kusababisha ununuzi wa magari yasiyofaa ambayo hayakidhi vigezo na maelezo ya Serikali.

Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe linafuata miongozo na maelekezo katika kushughulikia ununuzi na usimamizi wa magari ya umma kwa kupata vibali vinavyostahili kutoka kwa Waziri Mkuu.

#### **9.9 Kutoa tuzo ya zabuni kwa mzabuni asiyekidhi vigezo yenye thamani ya shilingi bilioni 53.71**

Mnamo tarehe 2 Juni 2023 TANESCO na Kampuni ya TBEA CO LTD walitia saini mkataba wa kusanifu, kuleta, kusimika na kuzindua kituo kidogo cha Dundani cha 220/33Kv, 2x120MVA kwa bei ya mkataba ya shilingi bilioni 53.71. Ukaguzi wangu wa jalada la mkataba, ulibaini kamati ya tathmini ilipendekeza tuzo kwa Kampuni ya TBEA CO LTD Loti Na. 2 licha ya kuwa mzabuni hakukidhi baadhi ya mahitaji ya kiufundi kama ifuatavyo: - (a) Kuhusu Transfoma :- mzabuni alikuwa na uzoefu wa ugavi wa miaka 26 kinyume na mahitaji ya miaka 30; (b) Kuhusu kivunja saketi: hakuwa amefikia mahitaji ya uzoefu wa miaka 30; (c) Kuhusu Transfoma ya Mkondo na Transfoma ya Volti:- hakuwa amefikia mahitaji ya uzoefu ya miaka 30; (d) kuhusu mfumo wa KV 33 GIS:- mzabuni aliwasilisha thamani ya mkondo wa hitilafu kama KA16 badala ya

mahitaji ambayo ni KA40 na kiwango cha juu cha mzunguko mfupi wa KA16 badala ya KA25.

Licha ya kasoro zilizobainika, timu ya tathmini ilipendekeza mzabuni apewe tuze kufuatia mazungumzo kuhusu hitilafu zote za kiufundi zilizotajwa hapo juu. Bodi ya zabuni iliona kasoro zote za kiufundi zilizobainishwa kuwa ni ndogo zinazoweza kurekebishwa na mzabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya (204) (1) (2) (f), 205 na 206 (2) za Kanuni ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.

Ni maoni yangu kuwa, kasoro zote za kiufundi zilizobainishwa wakati wa tathmini ziliikuwa ni kasoro kubwa na muhimu kwa mujibu wa mwongozo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma. Hivyo, kukubaliwa kwa kasoro hizo kunaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa wigo, ubora au utendaji wa kazi zilizoainishwa kwenye mkataba. Hii inaweza kuathiri nafasi ya ushindani ya wazabuni wengine waliowasilisha zabuni zenye mwitikio mkubwa. Hii, ni sawa na kushindwa kutekeleza kanuni ya uadilifu, uwajibikaji, usawa na uwazi katika michakato ya ununuzi; hivyo thamani ya fedha inaweza kuwa vigumu kufikiwa.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lifanye tathmini ya zabuni kwa kuzingatia matakwa ya nyaraka za zabuni na kwa kuzingatia sheria na kanuni ili kuongeza haki na uwazi na thamani ya fedha na kuepuka upotevu wa fedha za umma kwa ununuzi wa bidhaa zisizokidhi viwango.**

#### **9.10 Kufanya machapisho nje ya Shirika bila mkataba na kufanya mchakato wa ununuzi shilingi bilioni 1.71**

Katika ukaguzi wangu katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania nilibaini malipo ya shilingi bilioni 1.71 yaliyolipwa kwa kampuni ya machapisho kwa ajili ya gharama za uchapishaji wa magazeti. Hata hivyo, miamala hii haikuwa na mkataba au maagizo ya ununuzi. Wakati wa ukaguzi wangu kuhusu mchakato wa ununuzi, nilielezwa kuwa hakuna mchakato rasmi wa ununuzi uliofanyika ili kupata huduma hiyo kutoka kampuni ya machapisho, badala yake Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania ilisaini hati ya makubaliano ya kufanya biashara katika maeneo mbalimbali kila inapohitajika. Hii ni kinyume na Kanuni ya 233(1) (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013, iliyorekebishwa na Kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016 na Kifungu cha 4A (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410.

Kutokana na kukosekana kwa mkataba rasmi, Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania inaweza kukabiliwa na hatari ya kupata hasara kutokana na ukosefu wa sheria na masharti ya malipo, kutowasilisha bidhaa na migogoro ambayo inaweza kutokea wakati wa utekelezaji. Pia, huongeza hatari ya kuongezeka kwa gharama, vitendo vya ulaghai, kukosekana kwa ubora pamoja na kukiuka kanuni na viwango vya misingi ya ushindani wa haki.

Ninapendekeza Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania izingatie matakwa ya sheria za ununuzi wa umma ili kuimarisha uadilifu, ushindani, uwajibikaji, uchumi, ufanisi, uwazi na kufikia thamani ya fedha. Pia, ihakikishe ununuzi wote unakuwa na mikataba rasmi katika fomu iliyowekwa na inatiwa saini na pande zote mbili.

#### **9.11 Hasara ya shilingi bilioni 1.99 katika Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya ununuzi wa vitendanishi visivyokidhi viwango**

Nilifanya ukaguzi wa uchunguzi katika Bohari Kuu ya Dawa kuhusu ununuzi wa vitendanishi vya Uviko - 19 vijulikanavyo kama (Next Generation Sequencing (NGS)). Tarehe 15 Julai 2021, nilibaini Mkurugenzi Mkuu wa Bohari Kuu ya Dawa alimwandikia barua mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa vitendanishi vyenye gharama ya shilingi bilioni 2.08 kwa mahitaji ya haraka. Ununuzi huo ulijumuisha vitendanishi vya NGS vinavyoendana na kifaa kijulikanacho kama “Ion Torrent Next Generation Sequencing Platform” vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.99 pamoja na “Nasal Pharyngeal Swabs” yenye thamani ya shilingi milioni 86.91 kwa madhumuni ya kutumika katika Maabara ya Taifa ya Afya.

Tarehe 24 Agosti 2021 Bohari Kuu ya Dawa ililipa shilingi milioni 997.82 kwa mzabuni. Tarehe 11 Desemba 2021 mzabuni aliwasilisha kifurushi kimoja. Baada ya kuchunguzwa na kuthibitishwa na mtaalamu wa Maabara ya Taifa ya Afya, ilibainika bidhaa zilizowasilishwa hazikukidhi viwango na haziendani na mahitaji ya mashine ya Maabara ya Taifa ya Afya. Licha ya taarifa ya tarehe 19 Januari 2022 ya kutokukidhi viwango na kutoendana na mashine kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Maabara ya Taifa ya Afya kwenda Bohari Kuu ya Dawa, mzabuni huyo alienedlea kuwasilisha vifurushi vinne vilivyobaki tarehe 11 Februari 2022. Pia nilibaini kuwa, tarehe 25 Februari 2022 Bohari Kuu ya Dawa ilifanya malipo ya mwisho ya shilingi milioni 997.82 kwa ajili ya bidhaa zilizowasilishwa ambazo haziendani na viwango bila kuzingatia maelezo

ya awali yaliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Maabara ya Taifa ya Afya. Hii ilisababisha hasara ya jumla ya shilingi bilioni 1.99.

Ununuzi wa vitendanishi visivyofaa ulichangiwa na kutoa zabuni kwa mzabuni asiyé mtengenezaji. Pia kamati ya tathmini ya zabuni ilikosa mjambe mwenye utaalamu wa vitendanishi vinavyotakiwa kulingana na Kifungu cha 40(4) cha Sheria ya Manunuvi ya Umma.

Ninapendekeza Serikali; (a) ichukue hatua stahiki kwa watumishi wote walioisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 1.99; (b) ibaini iwapo hasara hiyo iliyosababishwa na uzembe au kushindwa kutekeleza majukumu kwa utaratibu unaostahili kinyume na Kifungu cha 2 (c) cha Sheria ya Kukusanya Madeni kutoka kwa Maafisa wa Serikali ya mwaka 1970 kwa ajili ya kurejesha hasara hiyo kutoka kwa maafisa husika; na (c) kuhusisha vyombo vya kusimamia sheria ili kubaini dhamira ya Bohari Kuu ya Dawa katika kuendelea na ununuzi licha ya kuarifiwa na Maabara ya Taifa ya Afya kuwa vitendanishi vilivyoletwa haviendani na mashine za Maabara ya Taifa ya Afya.

# SURA YA KUMI

## TATHMINI YA RASILIMALI WATU NA UTAWALA



### 10.0 Utangulizi

Ili kuboresha utendaji kazi katika Taasisi na mashirika ya umma, Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha taasisi na mashirika hayo yanajientesha kwa ufanisi mkubwa na kukidhi malengo ya uanzishwaji wake. Mashirika ya umma yanatakiwa kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kwa kufuata misingi ya utendaji inayozingatia utawala bora, uwajibikaji na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi. Ili kufanikisha malengo haya mashirika ya umma yanategemewa kuwa na wafanyakazi wenye uwezo na usimamizi bora wa rasilimali watu.

Hata hivyo, kupitia ukaguzi wangu, nilibaini idadi kubwa ya changamoto zinazohitaji kutiliwa maanani na kuboreshwa. Changamoto hizi zinajumuisha kutokuwepo kwa bodi ya wakurugenzi katika mashirika ya umma, uwepo wa maafisa wa umma wanaokaimu kwa muda mrefu pamoja na mashirika ya umma kushindwa kufuata maelekezo ya Serikali ya liyotolewa na Msajili wa Hazina, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Wizara ya Fedha.

Sura hii, inaelezea mapungufu kwa undani na kutoa ufahamu juu ya sababu za msingi na kubainisha mapendekezo ya kuboresha. Katika ukaguzi wangu nilibaini mapungufu yafuatayo:-

### 10.1 Mashirika ya umma kutokuwa na Bodi ya Wakurugenzi

Bodi ya Wakurugenzi hutoa usimamizi wa juu wa shughuli za mashirika ya umma na inasimamia uendeshaji wa kila siku. Bodi ya Wakurugenzi inawajibika katika kufanya maamuzi yanayotoa mwelekeo wa shirika kwa maslahi ya umma. Inabeba jukumu kuu, ikiwa ni pamoja na kutambua maeneo muhimu ya hatari, kusimamia na kufuatilia maamuzi ya uwekezaji, masuala muhimu ya kifedha, na kupitia mipango ya biashara pamoja na utendaji na usimamizi wa bajeti.

Nilibaini kuwa Serikali ilichukua hatua na kuteua bodi ya wakurugenzi katika mashirika ya umma 11 kati ya mashirika 13 ambayo hayakuwa na bodi za wakurugenzi kama ilivyoripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22 ambapo Serikali ilishindwa kufanya uteuzi katika taasisi mbili ambazo ni Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Baraza la Kiswahili la Taifa. Aidha, nilibaini kuwa idadi ya mashirika ambayo hayakuwa na bodi za wakurugenzi hadi kufikia mwezi wa Februari 2024 ilikuwa ni nane. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 23.**

**Jedwali Na. 23: Mashirika ya umma yasiokuwa na bodi za wakurugenzi**

Na.	Jina la shirika	Tarehe ya mwisho kuwa na Bodii	Miezi ambayo taasisi imekaa bila kuwa na bodi hadi Februari 2024
1.	Baraza la Kiswahili la Taifa	Januari 2021	37
2.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu	Februari 2022	24
3.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Januari 2023	13
4.	Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri wa Anga	Mei 2023	9
5.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	Mei 2023	9
6.	Bodi ya Pareto Tanzania	Mei 2023	9
7.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	Juni 2023	8
8.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea	Oktoba 2023	4

**Chanzo:** Ripoti za bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma

Pia, nilibaini taasisi tatu zina wenye viti wakati uteuzi wa wajumbe wengine wa bodi bado haujafanyika ambapo uteuzi wa wajumbe hao umechelewa kwa kipindi cha miezi miwili hadi 25. Mashirika hayo ni: Taasisi ya Mifupa Muhimbili; Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori; na Bodi ya Mkonge Tanzania.

Wajumbe wa Bodi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini waliteuliwa lakini mwenyekiti bado hajateuliwa kwa miezi 13, ambayo muda wake ulikwisha tangu tarehe 31 Januari 2023.

Kutokuwepo kwa bodi ya wakurugenzi kunadhoofisha mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja; na ufanisi wa uendeshaji wa taasisi. Pia husababisha kucheleweshwa kwa maamuzi ya kimkakati na utekelezaji wa shughuli muhimu kama vile kuitisha miongozo, kanuni, bajeti, na sera.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yaliyobainishwa yashirikiane na Serikali kuhakikisha bodi za wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati.**

Aidha, Serikali, kuititia Ofisi ya Msajili wa Hazina, inapaswa kuweka mfumo wa kufuutilia tarehe za kumalizika kwa wajumbe wa bodi zote ili kuruhusu mchakato wa uteuzi mpya miezi sita kabla ya tarehe hizo za kumalizika kwa muda wao.

#### 10.2 Kushindwa kuzingatia maagizo na miongozo ya Serikali katika mashirika ya umma

Kifungu cha 8A (1) cha Sheria ya Huduma za Umma Sura 298 kinaleza kuwa bila kujali utoaji wa sheria yoyote nyingine ilioandikwa kinyume na hii katika nchi hii mishahara, marupurupu, motisha, na faida za nyongeza ndani ya Serikali na taasisi za umma lazima zipate idhini kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ukaguzi wangu ulibainisha kasoro zilizooneshwa hapa chini: -

##### a) Kutumia nyenzo za kuendesha taasisi ambazo hazijaidhinishwa na Katibu Mkuu Utumishi

Nilibaini mashirika ya umma nane hayajawasilisha nyenzo za kufanya kazi kwa ajili ya kuidhinishwa na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo ni kinyume na Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 2017. Nyenzo hizo ambazo hazikuwakilishwa ni: mpango wa motisha, mkataba wa hali bora, mpango wa malipo wa posho, muundo wa kikazi. Maelezo yanapatikana kwenye Jedwali Na. 24.

##### Jedwali Na. 24: Mashirika ya umma ambayo hayakupeleka nyaraka zao kwa ajili ya kuidhinishwa

Na.	Jina La Taasisi/Shirika	Nyenzo ambayo haikupitishwa na Katibu Mkuu Utumishi
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	Kanuni za Wafanyakazi
2.	Chuo cha Elimu ya Biashara	Mpango wa Motisha wa Chuo
3.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	Mpango wa Motisha
4.	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	Mpango wa Motisha
5.	Shirika la Nyumba la Taifa	Mpango wa Huduma za Afya wa nyongeza pamoja, Mkataba wa hali bora
6.	Kampuni ya Mkulazi	Utekelezaji wa Majukumu na Muundo wa Kampuni ya Mkulazi uliorekebishwa ulianza kutekelezwa bila idhini ya Ofisi ya Rais wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Na.	Jina La Taasisi/Shirika	Nyenko ambayo haikupitishwa na Katibu Mkuu Utumishi
		Jumla ya watumishi 95 walajiriwa na kampuni bila kupata vibali nya ajira kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi.
7.	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi	Kanuni za Wafanyakazi za mwaka, 2017 na Sera ya Mikopo kwa Wafanyakazi ya mwaka, 2017
8.	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji	Hakuna muundo rasmi wa shirika ulioidhinishwa na Katibu Mkuu (Utumishi) kwani mamlaka imekuwa ikitumia muundo wa rasimu tangu mwaka 2021

**Chanzo:** *Uchambuzi wa ukaguzi katika uzingatiaji wa nyaraka wa Serikali*

Pia, nilibaini kuwa taasisi mbili ambazo ni Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi zilichelewa kutekeleza muundo wao mpya wa taasisi ulioidhinishwa na Katibu Mkuu Utumishi. Miundo hiyo ya taasisi ilikuwa imechelewesha kwa miezi 12 na miezi 39 mtawalia.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe yanazingatia maagizo ya Serikali yaliyotolewa;** pia, **yahakikishe kuwa posho zinazolipwa na mashirika ya umma zinaendana na miongozo ya Serikali inayotolewa mara kwa mara.**

**b) Kulipa kampuni binafsi shilingi milioni 941.18 kwa ajili ya kuandaa mpango mkakati wa TANESCO**

Kifungu Na. 6 cha Waraka wa Hazina Namba 12 wenyewe kumbukumbu Na. CEA.III/372/01/15 uliotolewa tarehe 8 Desemba 2015 unaeleza kuwa, huduma za ushauri kwa mamlaka za umma na taasisi za serikali zitafanywa na wataalamu wa ndani wa taasisi husika au kutoka taasisi zingine za Serikali.

Ingawa jukumu la kuandaa mpango mkakati wa shirika lilipaswa kufanyika na wataalamu wa ndani kutoka taasisi za Serikali, Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO) liliingia mkataba na mshauri binafsi kwa ajili ya kuandaa mpango mkakati huo ambapo shirika lililipa jumla ya shilingi milioni 941.18 kinyume na muongozo tajwa wa Hazina. Ni maoni yangu kuwa mshauri binafsi angeweza kuhusika tu katika kuitia mpango mkakati mpya ulioandalialiwa na taasisi na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati uliomalizika ili kupunguza mianya ya upendeleo wa matokeo unaoweza kujitokeza.

Maoni yangu ni kuwa, haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuruhusu mshauri binafsi kufanya kazi ambayo ingeweza kufanyika kwa kutumia rasilimali za ndani za kampuni au taasisi zingine za Serikali.

Ninapendekeza TANESCO ikuze na kujenga uwezo wa ndani ili kuhakikisha kuwa katika siku zijazo, mpango mkakati wa Shirika unaandaliwa na wataalamu wa ndani badala ya kumtumia mshauri binafsi katika hatua ya maandalizi. Mshauri binafsi anaweza kutumiwa na Shirika kwa ajili ya kupitia mpango uliyokwisha tayarishwa na kufanya uchambuzi au tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati ili kupunguza upendeleo wowote unaoweza kujitekeza, hususani katika kufanya tathmini ya mafanikio, changamoto, na mipango ya mbeleni.

### **10.3 Mapungufu katika matumizi ya mifumo ya Serikali katika mashirika ya umma**

Mfumo wa kutunza rejista na usimamizi wa mali za Serikali (GAMIS) na Mfumo wa kutunza taarifa na usimamizi wa rasilimali watu (HCMIS) iliwekwa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mali za Serikali na rasilimali watu, mtawalia. Uchambuzi wa matumizi ya mifumo iliyotajwa ulibainisha mapungufu yafuatayo;

#### **10.3.1 Tathmini ya mfumo wa kutunza rejista ya mali za kudumu za Serikali**

Wizara ya Fedha ilitoa waraka unaoyotaka mashirika ya umma kuweka takwimu za mali zao kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) ifikapo tarehe 31 Agosti 2021. Matumizi sahihi ya GAMIS yataimarisha na kuongeza usahihi wa taarifa za mali za Serikali na usimamizi wake, na kufanya maamuzi sahihi kuhusu ununuvi na uuzaji wa mali hizo.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini mashirika ya umma 18 (Jedwali Na. 25) hayakuwa yanahifadhi mali zao katika mfumo wa GAMIS, kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Fedha. Hii pia iliripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka uliopita (2021/22) ambapo taasisi ambazo hazikuwa zinarekodi mali zao kwa kutumia GAMIS zilikuwa 28.

Pia, nilibaini mashirika ya umma tisa ambayo yalikuwa yaktumia sehemu ya mfumo huo kutokana na ukosefu wa namba za utambulisho wa mali pamoja na kushindwa kufanya uhakiki wa mali. Taasisi zilishindwa kutumia mfumo huo vizuri na kutii waraka huo wa Serikali kutokana na ukosefu wa uelewa na mafunzo kuhusu matumizi yake.

Mashirika yaliyotumia sehemu ndogo ya GAMIS ni: Bodi ya Korosho Tanzania, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Chuo cha Usimamizi wa

Fedha, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania, Bodi ya Nyama Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Shirika la Reli Tanzania, na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga.

#### Jedwali Na. 25: Taasisi mbazo mali zake hazipo kwenye mfumo wa GAMIS

Na.	Jina la Shirika
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha
2.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi
3.	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam
4.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam
5.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme
6.	Tume ya Ushindani
7.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita
8.	Kiwanda cha Kutengeneza dawa cha Keko
9.	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro
10.	Kampuni ya Huduma ya Meli
11.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu
12.	Shirika la Bima la Taifa
13.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega
15.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga
16.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania
17.	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania
18.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

**Chanzo:** Mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali

Hali hii ya kutotekeleza na kutokekilia kwa rekodi za mali za mashirika katika GAMIS inakwamisha juhudzi za Serikali za kufikia lengo lake la kutunza kumbukumbu za mali za mashirika yote kwa ajili ya kufanya uamuzi sahihi.

Ninapendekeza mashirika ya umma ambayo hayatumii GAMIS kutekeleza maagizo ya Serikali kwa kuanza kutumia mfumo huo ili kuhakikisha takwimu za mali za kudumu zinazoripotiwa katika taarifa za fedha zinafanana na takwimu za GAMIS. Pia, ninapendekeza kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali atoe msaada wa mafunzo ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

#### 10.3.2 Tathmini ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu

Waraka namba 1 wa Utumishi wa Umma wa mwaka 2021 uliagiza taasisi zote za Serikali kuanza kutumia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa

Rasilimali Watu (HCMIS) ambao unatumika kwa ajili ya usimamizi wa wafanyakazi wote, malipo, ajira, uhamisho, madai ya wafanyakazi na hatua zote za kibinaksi kuanzia Mei 2021.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa mashirika ya umma 56 kati ya mashirika 215 hayakutumia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu (HCMIS), jambo ambalo ni kinyume na Waraka namba 1 wa Utumishi wa Umma wa mwaka 2021 (**Kiambatisho Na. XII**).

Zaidi, nilibaini kuwa mashirika mawili ambayo ni Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania yanatekeleza mfumo huo kwa sehemu tu. Chuo Kikuu cha Elimu Dar es Salaam kina taarifa zisizo za kweli za wafanyakazi katika mfumo; na Chuo Kikuu cha Dodoma hakikuwa na taarifa sahihi za wafanyakazi katika mfumo wa HCMIS.

**Ninapendekeza uongozi wa taasisi zilizotajwa kuharakisha uendelezaji na utekelezaji wa mfumo huo wa taarifa za usimamizi wa rasilimali watu kama ilivyaoagizwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na kupitia na kusahihisha mara kwa mara kumbukumbu za wafanyakazi ndani ya mfumo.**

#### 10.4 **Mashirika ya umma yenye nyenzo za kufanya kazi zisizoridhisha**

Nilibaini mashirika ya umma 40 kati ya mashirika 215 ambayo hayakuwa na nyenzo za uendeshaji za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya kikazi. Illobainika kuwa mashirika hayo hayakuwa na nyenzo za kufanya kazi, ikiwamo taratibu za uendeshaji wa kawaida wa mashirika hayo, mpango mkakati wa muda mrefu, mpango wa kazi kila mwaka, mwongozo sahihi wa uhasibu, sera, kanuni za fedha, na sera ya usimamizi wa vihatarishi, kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. XIII**.

Hii imesababishwa na mapitio na tathmini ya muda mrefu inayofanywa na menejimenti; ucheleweshwaji unaofanywa na mamlaka zenye kuitisha nyenzo hizo; pamoja, na utegemezi uliopitiliza wa miongozo kutoka kwa kampuni mama unaofanywa na kampuni tanzu.

Kutokuwepo kwa miongozo hii ya msingi katika uendeshaji kunasababisha changamoto kubwa na kuathiri uwezo wa taasisi katika kufanya kazi kwa ufanisi, kwa uwiano na kwa mujibu wa viwango na

kanuni zilizowekwa. Pia, bila mipango mikakati, taasisi za umma zinaweza kufanya kazi bila kuwa na maono, mwelekeo, na malengo katika shughuli zao, ambayo inawafanya wawe katika hatari ya kupoteza rasilimali na kushindwa kufikia malengo muhimu.

Hii inaweza kuhatarisha ubora wa huduma zinazotolewa, usimamizi duni wa vihatarishi, kutokujibika, kupungua kwa ufanisi na uendeshaji wenye tija katika utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika kuhakikisha kuwa nyenzo zao za uendeshaji zinatayarishwa, kusahihishwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ili kuboresha utii na ufanisi wa shughuli zao.**

#### 10.5 Maafisa wanaokaimu nafasi kwa muda wa zaidi ya miezi sita

Nilibaini mashirika ya umma 11 yalikuwa na maafisa ambao walikuwa wanakaimu nafasi mbalimbali zaidi ya miezi sita, ambapo kunaongezeko la maafisa 81 kutoka idadi ya maafisa 109 iliyoripotiwa katika mwaka wa 2021/22 hadi kufikia maafisa 190 mwaka 2022/23. Wafanyakazi hao wametumikia katika nyadhifa hizo na kukaimu kwa zaidi ya miezi 17 hadi 69 (**Jedwali Na. 26**). Hii ni kinyume na Agizo D.24 (3) la kanuni za kudumu za utumishi wa umma za mwaka, 2009 ambalo linahitaji maafisa wasiwe katika nyadhifa za kukaimu kwa kipindi kinachozidi miezi sita.

Ofisi ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilieleza kuwa tatizo hili linatokana na kuchelewa katika mchakato wa uhakiki wa maafisa waliopendekezwa kwa nyadhifa hizo.

**Jedwali Na. 26: Maafisa wanaokaimu katika nafasi zao kwa muda mrefu**

Na.	Jina la Shirika	Watumishi wanaokaimu	Miezi waliyokaimu
1	Kampuni ya Huduma ya Meli	5	69
2	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	17	45
3	Chuo Kikuu Ardhi	7	42
4	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	3	42
5	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam	1	41
6	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania	10	37
7	Chuo Kikuu cha Dodoma	26	32
8	Bodi ya Nyama Tanzania	5	28
9	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi	101	24
10	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	14	11
11	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	1	17
<b>Jumla</b>		<b>190</b>	

*Chanzo:* Ripoti za risilimali watu na mafaili ya maafisa

Kushindwa kuteua na kuwafanya maafisa kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu kunaweza kuathiri hamasa ya kufanya kazi, uwezo wa kufanya maamuzi, uwajibikaji, na hatimaye utendaji wa maafisa hao kwa jumla.

Ninapendekeza mashirika ya umma husika yashirikiane na mamlaka za uteuzi na kuchukua hatua za haraka kuwathibitisha maafisa ambao wamekuwa wakikaimu nyadhifa kwa muda mrefu au kuteua maafisa wapya katika nafasi hizo endapo wataona maafisa hao wanaokaimu hawakidhi sifa za nyadhifa hizo.

#### **10.6 Kuajiri wafanyakazi wa muda kama vibarua bila kufata taratibu rasmi za ajira**

Nilibaini kuwa taasisi ziliajiri vibarua katika kufanya shughuli za kawaida ambazo ni pamoja na matengenezo na kusafisha maeneo mbalimbali, mauzo, na shughuli za uzalishaji. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza , na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam.

Hata hivyo, hakukuwa na taaarifa iliyokuwa inaonesha vigezo viliyivo wazi vyta kustahili kufanya kazi hiyo, tathmini ya mahitaji, taratibu zilizothibitishwa, mikataba na miongozo ya kuajiri, kusimamia wafanyakazi wa muda na hatua za kinidhamu endapo kibarua huyo atakiuka sheria. Hali hii inasababishwa na kutokuwepo kwa miongozo ya ndani ya kuajiri wafanyakazi wa muda. Taarifa zake zimeanishwa katika Jedwali Na. 27.

##### **Jedwali Na. 27: Mashirika ya umma yanayotoa ajira za muda mfupi bila ya mwongozo**

Na.	Jina la Taasisi	Changamoto iliyobaini
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	Jumla ya vibarua 50 walipewa ajira za muda bila kuwa na mkataba.
2.	Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	Jumla ya shilingi milioni 617 zililipwa kwa vibarua 217, wakati hifadhi hii haikuwa na taratibu na miongozo ya kuajiri na kusimamia vibarua
3.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Wafanyakazi 95 walijiriwa na mamlaka kama vibarua kwa kipindi cha mwaka mmoja mpaka 19 bila kuwa na mkataba

**Chanzo:** Taarifa za rasilimali watu

Kuajiri watumishi kama vibarua bila mikataba rasmi kunaleta hatari katika uendeshaji wa taasisi hasa ikiwa kuna utovu wa nidhamu. Pia,

kunaweza kusababisha madhara ya kisheria kwa mwajiri kutokana na mapungufu ya masharti ya kimkataba yanayoweza kutekelezwa.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yaanzishe na kutekeleza taratibu za ndani za kuajiri vibarua.**

#### **10.7 Kuajiri watumishi bila kufuata taratibu**

Wakati wa ukaguzi wangu wa taratibu za kuajiri TANESCO, nilibaini ajira za watumishi sita hazikutangazwa kwa umma na hazikufuata taratibu zilizoidhinishwa za kuajiri kwa kutafuta waombaji kazi kutoka soko la ajira ili kuhakikisha fursa sawa kwa kila mwananchi. Zaidi ya hayo, sikuweza kupata ushahidi wa namna watumishi hao walivyoajiriwa ikiwamo kutokuwapo kwa usaili wa ushindani uliofanyika ili kuwapata watumishi hao. Hii ni kinyume na Aya ya 11(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 (marejeo ya mwaka 2022). Kasoro hii inasababishwa na kutotekelawa ipasavyo kwa kanuni za utumishi.

**Ninapendekeza TANESCO ihakikishe nafasi zote zilizopo zinajazwa kwa kufanya mchakato wa ajira wenye ushindani wa wazi au kupandisha vyeo maafisa wa ndani kuziba nafasi hizo.**



# SURA YA KUMI NA MOJA

## USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA NA TAASISI ZINGINE ZA UMMA

### 11.0 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ina jukumu muhimu katika kusimamia na kutekeleza sheria za kodi. Migogoro au rufaa zinazohusiana na sheria za kodi hushughulikiwa kupitia Bodi ya Rufani za Kodi na Baraza la Rufani za Kodi.

Sura hii inawasilisha ufuataji wa sheria za kodi na usimamizi wa madai ya kodi. Hoja zinabainisha mapungufu mbalimbali yaliyoonekana katika kodi ya zuio, kutowasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya faida, kutolipa kodi ya faida, na kutokata na kuwasilisha kodi ya mapato.

Uchunguzi wangu wa matokeo haya una lengo la kutoa mwanga juu ya maeneo ya kuboresha na kupendekeza hatua za kuongeza ufuataji wa sheria za kodi na usimamizi mzuri wa masuala yanayohusiana na kodi ndani ya mashirika ya umma. Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi wangu:

### 11.1 Kodi ambazo hazijalipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 33.45

Wakati wa ukaguzi wa ulipaji kodi, nilibaini kuwa mashirika ya umma 16 (sawa na 7%) kati ya mashirika 215 yaliyokaguliwa hayakuwasilisha kodi mbalimbali zenyе thamani ya shilingi bilioni 33.45 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/23 kinyume na sheria za kodi. Tatizo hili bado linaendelea ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22 ambapo mashirika ya umma 13 (sawa na 6%) kati ya mashirika 203 yaliyopitiwa hayakuwasilisha kodi mbalimbali za jumla ya shilingi bilioni 46.83 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mchanganuo wa kodi mbalimbali ambazo hazikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambazo ni pamoja na Kodi ya ongezeko la thamani, kodi ya

zui, kodi ya mapato na kodi ya ujuzi na maendeleo, unaoneshwa katika kiambatisho Na. XIV.

Kutowasilisha kodi kulisababishwa na changamoto za mtiririko wa fedha katika mashirika ya Umma husika. Kutolipa kodi kunaweza kuongeza ghamra kwa mashirika ya umma husika kutohana na adhabu za baadaye zitakazotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam, kutokulipa kodi kulisababishwa na Serikali kuongeza wigo wa shughuli za Mamlaka hiyo kwa kuunganisha kazi za Mamlaka hiyo na DAWASCO na kuongeza eneo la huduma la Mamlaka kujumuisha maeneo ambayo awali yalikuwa yakihudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Chalinze, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkuranga na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kisarawe. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam pia ilichukua mali na madeni yanayomilikiwa na Maji Central Store. Kufuatia muungano huu, deni la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam lilikua kwa kiasi kikubwa.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe yanafuata sheria za kodi na kulipa kodi husika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

#### **11.2 Kodi zilizochelewa kulipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 29.09**

Mapitio yangu yalibaini ongezeko la kodi zilizochelewa kulipwa na mashirika ya umma kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini mashirika ya umma 12 yalichelewa kuwasilisha makato ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 29.09 kuanzia siku moja hadi 1015 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, jambo ambalo halioneshi uboreshaji kulinganisha na mwaka wa fedha 2021/22 ambapo nilibaini mashirika ya umma 18 yalichelewa kuwasilisha makato ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 5.09 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kinyume na sheria za kodi. Sheria ya Kodi ya Mapato inamtaka kila wakala wa kuzuia kulipa kwa Kamishna ndani ya siku saba baada ya mwisho wa kila mwezi wa kalenda kodi yoyote ya mapato ambayo imezuiliwa wakati wa mwezi. Kuchelewa kuwasilisha kodi kilitokana na taasisi husika kushindwa kuzingatia sheria au kuelekeza fedha zilizopangwa kwa ajili ya kodi kwenye matumizi mengine.

**Jedwali Na. 28: Ucheleweshaji wa kuwasilisha kodi kwa TRA**

N a . .	Jina la Taasisi	Makato ya Kisheria	Kiasi (Sh.) (millioni)	siku zilizochel eweshwa
1.	Shilika la Umeme Tanzania	Kodi ya zuio	2006.29	37-1015
2.	Chuo Kikuu Cha Dodoma	Kodi ya zuio	15.59	29 - 394
3.	Shirika la Posta Tanzania	kodi ya mapato	1,036.40	16-327
4.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Kodi ya mapato	21.62	2-290
5.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Kodi ya zuio	25.12	2-232
6.	Taasisi ya Elimu Tanzania	kodi ya zuio	279.92	11-206
7.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	Kodi ya zuio	13,286.29	6-187
8.	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	Kodi ya mapato	40.09	30-183
9.	Shirika la Reli Tanzania (Mradi wa SGR)	kodi ya zuio	12,095.68	27-124
10.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega	Kodi ya mapato	24.43	1-62
11.	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	Kodi ya mapato	98.27	23-57
		Kodi ya ujuzi na maendeleo	15.91	23-57
12.	Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania	Kodi ya mapato	123.51	9-32
		Kodi ya ujuzi na maendeleo	24.67	9-32
<b>Jumla</b>		<b>29,093.79</b>		

**Chanzo: Taarifa za fedha na vocha za malipo**

Kuchelewesha malipo ya kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kunayaweka mashirika ya umma katika hatari ya riba na pia kunainyima Serikali mapato yake kwa wakati kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa jamii.

**Ninapendekeza mashirika ya umma kuhakikisha yanapeleka kodi kwa wakati kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuepuka riba.**

### 11.3 Malipo bila risiti za kodi za kielektroniki shilingi bilioni 2.17

Kanuni ya 28 ya Kanuni za risiti za Kielektroniki za Kodi ya Mapato za mwaka, 2012 inamtaka kila mnunuzi kudai na kuhifadhi risiti ya fedha au ankara katika milki yake. Zaidi ya hayo, Kanuni ya 21-25 ya Kanuni hiyo inaeleza kuwa mtu ye yeyote ambaye anashindwa kudai, kuhifadhi au kutoa risiti au ankara amefanya kosa la kisheria na anawajibika baada ya hukumu kulipa malipo mara mbili ya kiasi cha kodi aliyokwepa.

Mapitio yangu yalibaini ongezeko la malipo ambayo hayakuambatishwa na risiti za kielektroniki kutoka mwaka wa fedha 2021/22, ambapo katika mwaka 2022/23 malipo yaliyofanywa na mashirika ya umma tisa kwa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 2.17 hayakuambatishwa na risiti za kielektroniki (**Jedwali 29**), wakati mwaka 2021/22, malipo yenye thamani ya shilingi milioni 556.83 yaliyofanywa na mashirika ya umma 11 hayakuambatishwa na risiti za kielektroniki za kodi.

Hii husababishwa na kutowajibika kwa mashirika ya umma katika kuwasiliana na wauzaji husika ili kutoa risiti za kielektroniki na mapungufu katika udhibiti wa ndani ili kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni.

**Jedwali Na. 29: Malipo bila risiti za kodi za kielektroniki**

Na	Jina la Taasisi	Kiasi Sh. (Milioni)
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa	1,400.00
2.	Shirika la Bima la Taifa	363.99
3.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	175.76
4.	Bodi ya Utalii Tanzania	65.60
5.	Kampuni ya Huduma ya Meli	57.78
6.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	47.58
7.	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	21.82
8.	Taasisi ya Utafiti wa Uvvi Tanzania	21.08
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi	14.54
<b>Jumla</b>		<b>2,168.15</b>

**Chanzo:** *Taarifa za vocha za malipo za mashirika husika*

Aidha, Bodi ya Nyama Tanzania ilipokea risiti za kielektroniki za kodi bandia zenye thamani ya shilingi milioni 16.30 kutoka kwa wauzaji. Hii ilisababishwa na wafanyakazi kutofahamu namna ya kutambua risiti bandia za kielektroniki za kodi.

Maoni yangu ni kuwa mashirika ya umma yanapaswa kuwa mfano katika uzingatiaji wa sheria za kodi hasa katika kutoa na kudai risiti za kielektroniki za kodi. Adhabu zinaweza kutozwa kwa mashirika ya umma husika kwa kushindwa kudai, kuhifadhi na kutoa risiti ya fedha au ankara katika milki yao. Aidha, kodi ya ongezeko la thamani kwenye ununuzi haiwezi kudaiwa bila risiti za kielektroniki za kodi hivyo, kuongeza gharama kwa mashirika ya umma husika. Vilevile, Serikali inapoteza mapato ambayo yangeweza kupokelewa kama risiti za kielektroniki za kodi zingetolewa.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yazingatie kanuni za kodi ya mapato kuhusu kudai na kuhifadhi risiti za kielektroniki za kodi.**

#### **11.4 Kutofautiana kwa taarifa za kukokotoa ritani za kodi ya ongezeko la thamani**

Kifungu cha 86 (1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014, kinasema kuwa mtu aliyesajiliwa ambaye hufanya uuzaji wa bidhaa zinazotozwa kodi, kutoa ankara ya kodi ya kweli na sahihi inayotolewa na kifaa cha kutolea risiti za kielektroniki za kodi.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini tofauti ya mapato kati ya mapato yaliyotumika kukokotoa ritani ya kodi na taarifa za fedha kwenye mashirika ya umma matatu kuanzia shilingi bilioni 0.37 hadi shilingi bilioni 9.07 (**Jedwali Na. 30**). Pia, nilibaini kuwapo kwa tofauti ya kodi iliyolipwa kwenye ununuzi kati ya taarifa zilizopo kwenye mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na taarifa za akaunti ya kodi ya mapato zilizopo kwenye mashirika mawili ya umma. Tofauti hiyo ni kuanzia shilingi bilioni 1.31 hadi shilingi bilioni 2.66 (**Jedwali 30**).

**Jedwali Na. 30: Tofauti ya mapato kati ya ritani za kodi na taarifa za hesabu**

Na.	Jina la Taasisi	Mapato ya ritani za kodi Sh.(Bilioni)	Mapato kwenye taarifa za hesabu Sh. (Bilioni)	Tofauti Sh.(Bilioni)
1	Shirika la Posta Tanzania	21.17	30.24	9.07
2	Kampuni ya MCB	2.38	6.43	4.05
3	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	6.95	6.58	0.37

**Chanzo:** Ritani za kodi ya ongezeko la thamani na taarifa za hesabu

**Jedwali Na. 31: Tofauti ya kodi kati ya mfumo wa mamlaka na waTaasisi**

Na.	Jina la Shirika	kodi kwenye mfumo wa Mamlaka ya Mapato Sh "Bilioni"	Kodi kwenye mfumo wa Taasisi Sh "Bilioni"	Tofauti Sh "Bilioni"
1	Shirika la Mawasiliano Tanzania	5.89	7.21	1.31
2	Shirika la Umeme Tanzania	183.83	181.17	2.66

**Chanzo:** Mfumo wa kielektroniki wa uwasilishaji wa ritani za kodi na akaunti ya kodi ya ongezeko la thamani

Kwa Kampuni ya MCB, tofauti ilitokana na tabia ya menejimenti kutoa risiti ya kieletroniki pale malipo yanapofanyika, yaani fedha taslimu zinapopokelewa, wakati mapato yanatambulika pale muamala wa mabadilishano unapokuwa umekamilika. Kwa Shirika la Posta Tanzania, menejimenti haikuchukua hatua ya kufanya usuluhisho wa mapato kati ya ritani za kodi na taarifa za hesabu.

Kwa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, tofauti hiyo ilisababishwa na kufutwa kwa ankara za Kodi baada ya kuwasilisha ritani za kodi na kusababisha malipo zaidi ya kodi ya ongezeko la thamani kwa shilingi milioni 63.26. Sababu kuu ya kufutwa kwa ankara ilikuwa ni kurudia ankara na makosa ambayo yalibainika wakati ankara zilikuwa tayari zimeshaingizwa kwenye mfumo.

Tofauti kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania ilisababishwa hasa na kutokuingiza ankara kwenye mfumo wa uhasibu mapema pale mzabuni anapokuwa ameiwasilisha, wakati ankara hiyo inakuwa tayari imedaiwa kwenye ritani ya kodi kuitia mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii inasababisha kutofautiana kwa muda wa kuripoti kodi iliyotozwa kwenye ununuzi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika; (a) kutoa risiti pale ambapo muamala wa mabadilishano unakamilika ili kuisaidia Serikali kutambua mapato kwa wakati; (b) kujaza ritani za kodi kwa usahihi na kulipa kiasi kinachodaiwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania; na (c) kuhakikisha yanafanya usuluhisho wa taarifa kati ya ritani za kodi na taarifa za kodi zilizopo kwenye mfumo.**

#### **11.5 Kuchelewa kukamilika kwa kesi za rufaa za mapato ya kodi kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mitano katika Baraza la Rufani za Kodi na Bodi ya Rufani za Kodi shilingi trilioni 3.68 na dola za Marekani milioni 4.66**

Aya ya 2.4 ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 wa Baraza la Rufani za Kodi inalitaka Baraza kutoa hukumu ya asilimia 80 ya rufaa za kodi zinazotokana na Bodi na asilimia 90 ya maombi ya kodi yaliyowasilishwa katika Baraza kila mwaka.

Mapitio yangu ya mafaili ya usimamizi wa kesi za Baraza la Rufani ya Kodi kwa mwaka 2022/23 yalibaini kesi 141 ambazo hazijatolewa hukumu zenye thamani ya shilingi bilioni 284.16, zikiwamo kesi 67 za rufaa zenye thamani ya shilingi bilioni 205.07 zenye mwaka mmoja mpaka mitano, ikiashiria ucheleweshaji wa kutoa hukumu.

Pia, nilipitia rejista ya maombi na rufaa za kodi katika Bodi ya Rufani za Kodi kwa mwaka wa fedha 2022/23 na kubaini kuwa rufaa 767 zenye jumla ya shilingi trilioni 6.01 na dola za Marekani milioni 5.22 zilizo katika migogoro ya kodi, zilibaki hazijaamuliwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2022/23. Kesi 441 (sawa na asilimia 58 ya rufaa

zinazosubiri) hazikuamuliwa kwa siku 184 hadi siku 1,935. Hii inatilia shaka kukamilika kwa kesi hizi kwa wakati, kinyume na malengo yaliyobainishwa katika mpango mkakati wa Bodi ya Rufani za Kodi wa kipindi cha mwaka 2021/22-2025/26 ambao unahitaji uamuzi wa haki ufanyike kwa wakati.

Hata hivyo, kwa Bodi ya Rufani za Kodi, hadi Oktoba 2023, rufaa 124 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.61 na dola za Marekani 554,761 ziliamuliwa, hivyo kubaki na rufaa 643 katika migogoro zenye thamani ya shilingi trilioni 3.40 na dola za Marekani milioni 4.66.

Hii inasababishwa na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe wa Bodi ya Rufani za Kodi, wenyeviti, na makamu mwenyekiti, pamoja na vikwazo vyatubu.

**Ninapendekeza Baraza la Rufani za Kodi na Bodi ya Rufani za Kodi kushirikiana na Waziri wa Fedha, kuhakikisha wajumbe, mwenyekiti, na makamu mwenyekiti wanateuliwa kwa wakati ili kuboresha uamuzi wa haki na wa wakati wa rufaa za kodi.**

#### **11.6 Kukosekana kwa kikomo cha muda cha kutatua rufaa Kwa njia ya maridhiano**

Kifungu cha 22 cha Sheria ya Rufaa ya Mapato ya Kodi, [Sura ya 408] kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 71 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 na kifungu cha 117 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 kinaeleza kuwa mtu anayekata rufaa anaweza kuomba kesi ikatataliwa kwa njia ya maridhiano ikiwa kesi ipo katika hatua yoyote kabla ya hukumu kutolewa na Bodi au Baraza. Zaidi ya hayo, Bodi au Baraza litahitaji pande zote zinazohusika kutoa taarifa ya matokeo ya maridhiano ndani ya muda utakapangwa na Bodi au Baraza litatoa amri ya mwisho kuhusu maridhiano hayo.

Mapitio yangu ya rejista ya maombi na rufaa za Bodi ya Rufani za Kodi kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalibaini rufaa 139 zenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni 1.38 na dola za Marekani milioni 1.73, ambapo wahusika waliomba wafanye maridhiano. Hata hivyo, katika sampuli niliyoichagua ya rufaa 39 zenye migogoro za jumla ya shilingi bilioni 398.06 kati ya rufaa zote 139, nilibaini rufaa zote 39 zilibaki bila kutatuliwa kwa zaidi ya miezi sita, na kuibua shaka juu ya utatuzi wa kesi hizo kwa wakati.

Ninapendekeza Bodi ya Rufani za Kodi iweke wazi muda maalumu wa utatuzi kwa kesi kwa njia ya maridhiano ili kuwezesha utatuzi wa haraka.

#### **11.7 Utata wa maneno "ruzuku kwa kiasi kikubwa" katika kuamua kodi ya mapato itokanayo na kipato cha ajira**

Wakati wa ukaguzi, nilibaini matumizi yasiyolingana ya Kifungu cha (7) (3) (k) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, ambayo haihusishi malipo yafuatayo katika kukokotoa kodi ya mapato; posho ya makazi, posho ya usafiri, posho ya majukumu, posho ya kufanya kazi kwa muda wa ziada, posho ya kufanya kazi za ziada, posho ya mazingira magumu au malipo ya pungezi kwa kazi nzuri yanayolipwa kwa mfanyakazi wa serikali au taasisi ambazo bajeti yake inalipwa kikamilifu au kwa kiasi kikubwa na ruzuku ya Serikali. Hata hivyo, Sheria ya Kodi ya Mapato haijafafanua wazi neno 'kwa kiasi kikubwa' linamaanisha nini.

Nilibaini kuwa, kati ya mashirika ya umma 75 yaliyopitiwa kwa sampuli, waajiriwa wa mashirika 35 (asilimia 47) walitozwa kodi, waajiriwa wa mashirika 39 (asilimia 52) hawakutozwa kodi na shirika moja la umma halikuwa na posho kwa waajiriwa.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, kati ya mashirika ya umma 35 tajwa hapo juu, waajiriwa wa mashirika nane walitozwa kodi kwenye posho zote na waajiriwa wa mashirika 27 walitozwa kodi kwenye baadhi ya posho.

Aidha, nilibaini kuwa mashirika ya umma 23 kati ya 39 yaliyotajwa hapo juu, hayakutoza kodi kwenye baadhi ya posho za wafanyakazi kwa sababu bajeti zao zinategemea ruzuku ya Serikali kwa kiasi kikubwa.

Katika mapitio yangu ya Sheria ya Mapato ya kodi nilibaini sheria hajjaweka wazi vigezo vya kujua ruzuku ya kiasi fulani kwa Taasisi ya Umma ndiyo ruzuku ya kiasi kikubwa. Pia haipo wazi kama wakati wowote kiasi cha ruzuku kutoka Serikalini kikibadilika, mashirika ya umma pia yanatakiwa kuititia upya posho zinazolipwa kwa waajiriwa ili kuziondoa au kuziweka kwenye kodi. Jambo hili linaleta utata katika kuamua posho zipi za waajiriwa zisitozwe kodi kwa mujibu kwa kifungu cha 7 (3) (k) cha Sheria ya Mapato ya Kodi.

**Ninapendekeza sheria iweke wazi kiasi au vigezo ambavyo vitatumika katika kuweka madaraja ya mashirika yanazotakiwa**

## Usimamizi wa kodi katika mashirika na taasisi zingine za umma

kutozwa kodi kwenye posho na ambayo hayatakiwi kutoza kodi kwenye posho, kutokana na ruzuku ya Serikali inayotolewa kwenye mashirika husika.



## SURA YA KUMI NA MBILI

### MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI NA TAASISI ZINGINE ZA KIFEDHA

#### 12.0 Utangulizi

Nilikagua utendaji wa benki zinazomilikiwa na Serikali, mifuko ya hifadhi ya jamii, Shirika la Bima la Taifa, na taasisi zinazohusika na usimamizi wa masoko ya mitaji na dhamana nchini Tanzania. Nilibainisha maeneo kadhaa ambayo taasisi hizi zina mapungufu ya kiutendaji na zinahitaji maboresho ili kuhakikisha utendaji wao unakuwa bora.

Kwa benki tatu zinazomilikiwa na Serikali ambazo ni, Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Azania na Benki ya Biashara Tanzania nimebaini mapungufu kadhaa kama vile kutosimamia ipasavyo kwa mikopo, na kutokidhi matakwa ya udhibiti.

Katika mifuko ya hifadhi ya jamii (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, na Shirika la Bima la Taifa nilibaini mapungufu yafuatayo: Usimamizi duni wa mikopo iliyotolewa; Kutotekelezwa ipasavyo kwa mikataba ya upangaji ili kukusanya kodi kutoka kwenye uwekezaji; na Utoaji wa huduma usioridhisha kwa wanufaika. Maeleo zaidi ya mapungufu yaliobainika ni kama ifuatwavyo:

#### 12.1 Wasiwasi juu ya ufanisi wa benki za Serikali

Nimepitia utendaji wa benki tatu za kibashara za Serikali, ambazo ni Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Azania, na Benki ya Biashara Tanzania. Nilibaini mapungufu mbalimbali katika ufanisi wa benki hizo kama ifuatavyo:

#### **12.1.1 Kutozingatiwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo kwa wateja**

- (i) **Usimamizi duni wa dhamana zilizowekwa na wakopaji wa Benki ya Biashara Tanzania na Benki ya Azania kwa mikopo iliyotolewa ya shilingi bilioni 403.62**

Benki ya Biashara Tanzania ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 6.56 kwa wateja sita ambao hawakuweka dhamana kama inavyotakiwa na vipengele vyta ya mikataba ya mikopo yao. Pia, Benki ilitoa mikopo mingine ya shilingi bilioni 5.50 kwa wateja wawili bila kuhuisha dhamana zao za awali kabla ya kupata mkopo mwengine. Vilevile, nilibaini kutokuwapo kwa ripoti za uthamini za dhamana zilizoahidiwa za wateja sita zilizohusisha shilingi bilioni 8.34 kinyume na Muongozo wa ukopeshaji.

Pia, mapitio yangu yalibaini kuwa taarifa za dhamana za Benki ya Azania zilizotumika katika kukokotoa makadilio ya matarajio ya hasara inayotokana na kutokukusanya madai, zilibaini kutokuwepo kwa nyaraka kama vile ripoti za uthamini na bima za mikopo zinazohusisha mikopo ya shilingi bilioni 383.22 iliyotolewa kwa wakopaji wapatao 60.

Hati za dhamana zisizotosheleza zinaweza kusababisha hatari ya benki kushindwa kurejesha mkopo kwa kunadi dhamana zilizowekwa endepo wakopaji watashindwa kurejesha mikopo yao.

**Ninapendekeza Benki ya Azania na Benki ya Biashara Tanzania kuhakikisha mikopo iliyotolewa ina dhaminiwa na dhamana ya kutosha na yenye ubora pamoja na kuimarisha udhibiti wa usimamizi wa mikopo iliyotolewa ikiwa ni pamoja na kufuatilia mikopo iliyotolewa ikuungwa mkono na dhamana.**

- (ii) **Mikopo iliyotolewa na Benki ya Biashara Tanzania ya shilingi bilioni 734.28 ikiwa imezidi ukomo wa mikopo na bila kupata kibali cha Bodi ya Wakurugenzi**

Aya ya 6.3 (i) ya Mwongozo wa Utoaji wa Mikopo wa Benki ya Biashara ya Tanzania wa mwaka 2022 inaeleza kuwa, ili kufikia na kudumisha amana ya mikopo yenye mfumo wa usalama wa sekta mbalimbali, menejimenti itaendelea kufuatilia utendaji wa sekta na kupendekeza mabadiliko kwenye Bodi ya Wakurugenzi kwa mapitio ya mipaka ya kiasi.

Benki ya Biashara Tanzania ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 728.07 kwa sekta tano, ambazo ni sekta binafsi, sekta ya uchukuzi na mawasiliano, hoteli, migahawa na utalii, majengo na ujenzi, pamoja na elimu. Mikopo hiyo ilikuwa juu ya ukomo ulioihinshwa katika Sera ya Benki. Pia, ilitolewa bila idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.

Vilevile, Benki ilitoa mikopo yeye jumla ya shilingi bilioni 6.21 kwa sekta ambazo ni maghala na kuhifadhi, maji, umeme, uvuvi na afya ambazo hazikuidhinshwa na Bodi ya Wakurugenzi na pia sekta hizo haziko kwenye Mwongozo wa Ukopeshaji uliopo kwa sasa. Benki ilieleza kuwa sekta zilizokuwa zimewekewa viwango ziliboreshwa katika Mwongozo wa Utoaji Mikopo wa mwaka 2023 ili kuendana na maelekezo ya Mdhibiti. Muongozo huo tayari umeidhinshwa ndani ya Benki na unsubstiri kuidhinshwa na Mdhibiti.

Aidha, Benki iliendelea kusisitiza kuwa sekta zilizojumuishwa katika muongozo ni pamoja na zile zilizobainishwa na mkaguzi.

Kuna hatari ya kuongezeka kwa hasara kutokana na kiasi kikubwa cha mikopo iliyotolewa zaidi ya kikomo na mikopo ambayo imetolewa kwenye sekta ambazo hazijaidhinshwa na Bodi ya Wakurugenzi.

**Ninapendekeza Benki ya Biashara Tanzania kuimarisha udhibiti wa usimamizi wa mikopo iliyotolewa ikiwa ni pamoja na kufuatilia mikopo iliyotolewa na kuhakikisha mikopo inatolewa baada ya kupata kibali kinachostahili cha Bodi ya Wakurugenzi na iendane na kikomo kilichoainishwa katika Sera.**

#### **12.1.2 Mikopo chechefu, na Benki zinazopata hasara**

Ukaguzi wangu ulibaini Benki ya Maendeleo ya TIB iliendelea kupata hasara kabla ya kodi, mwaka 2023 hasara ilifikia shilingi bilioni 5.92 (2022: hasara kabla ya kodi ilikuwa shilingi bilioni 131.97). Wakati Benki ya Biashara Tanzania ilipata hasara kabla ya kodi ya shilingi bilioni 41.40 (2022 faida kabla ya kodi shilingi bilioni 6.87), ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 48.27 sawa na asilimia 703. Hasara hii ilichangiwa zaidi na kufutwa kwa mikopo chechefu iliyorithiwa kutoka iliyokuwa Benki ya TIB Corporate.

Aidha, katika mapitio yangu ya mikopo chechefu nilibaini kuwa Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa na mikopo chechefu ya asilimia 21.50 kufikia tarehe 31 Desemba 2023 (2022: mikopo chechefu asilimia

20.28), wakati Benki ya Azania ilikuwa na mikopo chechefu asilimia 7.44 hadi kufikia 31 Desemba 2023 ( 2022: mikopo chechefu asilimia 18.25). Pamoja na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kutoka mwaka uliopita kwa Benki ya Azania, ni vyema kutambua kuwa benki zote mbili bado zilivuka kiwango kinachokubalika na kilichowekwa na Benki Kuu ya Tanzania cha asilimia 5. Pia, Benki ya Maendeleo ya TIB na Benki ya Azania kwa pamoja zilikuwa na mikopo chechefu ipatayo shilingi bilioni 206.04 (2022 mikopo chechefu shilingi bilioni 262.72) ikiwa imepungua kwa shilingi bilioni 56.68 huku sababu ikiwa ni kutozwa kwa mikopo chechefu (**Jedwali Na. 32**).

### Jedwali Na. 32: Maelezo ya Mwenendo wa mikopo chechefu ya Benki za Serikali

Maelezo	Banki ya Maendeleo TIB		Benki ya Azania	
	2023	2022	2023	2022
Mikopo Chechefu (Sh. bilioni) (Wateja na wafanyakazi)	80.94	75.09	125.10	187.63
Mikopo (Sh. bilioni)	376.00	370.26	1,680.70	1,027.70
Asilimia ya Mikopo Chechefu	21.50%	20.28%	7.44%	18.25%

**Chanzo:** Ripoti za Mikopo za mwaka 2023

Kuna uwezekano wa kuzorota kwa ubora wa mtaji wa mkopo kunaharibu mtaji mkuu wa Benki na unaathiri uwiano wa utoshelevu wa mtaji na utendaji wa benki hizo.

Ninapendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia masuala yanayozikabili benki hizi, ikiwa ni pamoja na kuongeza mtaji kwa Benki ya Maendeleo ya TIB, kuboresha udhibiti wa gharama na kupunguza uwiano wa mikopo chechefu hadi kufikia kiwango kinachokubalika cha asilimia 5.

### 12.1.3 Viwango vya utoshelevu wa mtaji visivyordhisha kwa Benki ya Maendeleo ya TIB

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2021 inaeleza kuwa taasisi ya fedha ya maendeleo itaanza kufanya kazi ikiwa wakati wote ina mtaji wa msingi usiopungua shilingi bilioni 200 au zaidi ya kiasi hicho.

Hata hivyo, Benki ya Maendeleo TIB hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ilikuwa na mtaji wa shilingi wa bilioni 88.12 ambao ni chini ya mahitaji ya mtaji wa shilingi bilioni 200, hivyo kuwa na upungufu wa

mtaji wa shilingi bilioni 111.88 sawa na asilimia 127. Aidha, benki hiyo ilieleza kuwa Wizara ya Fedha kupitia Msajili wa Hazina inalenga kutoa shilingi bilioni 118 kupitia bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/24 ili kuboresha mtaji ambao umeathiriwa na kuendelea kupata hasara kwa benki hiyo.

Pia, nilibaini kiasi cha shilingi bilioni 37 ambacho hakijarejeshwa tangu mwaka 2019 ambacho ni kipindi cha miaka mitano kutoka kwa Msajili wa Hazina. Mwaka 2019 Msajili wa Hazina alitakiwa kulipa shilingi bilioni 37 kwa Benki ya Maendeleo ya TIB ikiwa ni kiasi ambacho Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa ikiidai iliyokuwa Benki ya TIB Corporate ambayo ilisitisha shughuli zake na kuchukuliwa na Benki ya Biashara Tanzania. Hata hivyo, hadi nafanya ukaguzi wangu mnamo tarehe 6 Machi 2024 kiasi hicho kilikuwa bado hakijalipwa na Msajili wa Hazina. Benki ya Maendeleo ya TIB ilinieleza kuwa kiasi hicho cha shilingi bilioni 37 kuwa kitapokelewa kutoka Msajili wa Hazina baada Msajili wa Hazina kukiri kulipa kiasi hicho kupitia barua yenye Na. CAB.25/337/01 ya tarehe 5 Mei 2021 lakini hadi Machi 2024 kiasi hicho kilikuwa hakijalipwa.

Uwiano usiofaa wa utoshelevu wa mtaji unaleta hatari kwa Benki kupoteza sifa zake za kujiordesha kwa hiyo, inaweza kusababisha Benki kuwekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Nina maoni kuwa kiasi cha shilingi bilioni 37 kinachodaiwa na Benki ya Maendeleo TIB kina maana kubwa ya kuboresha mtaji wa Benki hiyo.

Ninapendekeza; (a) Serikali ichukue hatua zinazohitajika na kwa haraka ambazo ni pamoja na utoaji wa mtaji wa ziada ili kuinusuru Benki kufanya kazi kwa uwiano usiopendeza wa mtaji; na (b) Benki ya Maendeleo ya TIB kwenye mchakato wake wa kufuatilia fedha hizo ihusishe Wizara ya Fedha ili Msajili wa Hazina aweze kutimiza wajibu wake wa kurejesha shilingi bilioni 37.

### 12.1.4 Utendaji usioridhisha wa Benki ya TIB Rasilimali

Benki ya TIB Rasilimali ilianzishwa kama muendelezaji mali na baadaye kubadilishwa kuwa wakala wa masoko ya mitaji katika miaka ya 1980. Kampuni imepewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Soko la Hisa la Dar es Salaam na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kushughulikia huduma za udalali wa Dhamana, ushauri wa Uwekezaji, uthamini wa Biashara na Wakala wa Bima.

Benki ya TIB Rasilimali imeendelea kupata hasara kabla ya kodi, mwaka 2023 hasara ilifikia shilingi milioni 503 (2022: Hasara kabla ya kodi shilingi milioni 546). Pia, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023, madeni ya muda mfupi ya Benki yalizidi mali zake za muda mfupi kwa shilingi milioni 942 jambo linaloonesha kuwa Benki ya TIB Rasilimali inachangamoto ya ukwasi.

Benki ya TIB Rasilimali ilieleza kuwa inafanya jitihada za makusudi za kuongeza mapato ya kampuni kwa kushirikisha washirika wa nje katika kazi za ushauri kwa njia ya kugawana tozo, kuongeza mauzo ya biashara ndani ya mamlaka ya kampuni, kuongeza masoko na mauzo ya bidhaa za kampuni na zaidi ya hayo mbia na Kampuni imebadilisha jumla ya shilingi bilioni 1.795 kutoka kwenye mkopo na kuwa mtaji kwa njia ya hisa.

**Ninapendekeza Benki ya TIB Rasilimali; (a) iimarishe mkakati wa biashara ili kuboresha utendaji wa kampuni kupitia mseto wa kuongeza mapato; na (b) iombe mtaji wa kutosha ili kusaidia uendeshaji wa Benki.**

### 12.1.5 Kutofuta viwango vya uiano vya udhibiti vilivyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania

Kanuni za 9 (a) na (b) za Benki na Taasisi za Fedha 2014 zinataka benki au taasisi ya fedha wakati wote kudumisha mtaji wa kima cha chini usiopungua asilimia 12.5 na jumla ya mtaji usiopungua asilimia 14.5. Pia, Waraka Na. FA.130/170/01/5 wa tarehe 22 Januari 2022 uliotolewa na Banki Kuu ya Tanzania kuhusu gharama kwa mapato na mikopo isiyolipika inayohitaji benki zote na taasisi za fedha kudumisha uwiano wa gharama na mapato ya asilimia 55; na ikiwa ni zaidi ya asilimia 55, taasisi hizo zinatakiwa kuhalalisha uwiano ifikapo tarehe 31 Desemba 2022 na uwiano wa mikopo chechefu wa asilimia 5.

Mapitio yangu yalibainisha kuwa kufikia tarehe 31 Desemba 2023, mtaji mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania na jumla ya mtaji ulikuwa asilimia 13.26 na asilimia 13.26 mtawalia. Kulingana na uwiano huu, Benki ilikidhi mtaji wa msingi unaohitajika lakini inabakia chini ya kiwango cha chini kinachohitajika kwa jumla ya mtaji ambayo ni asilimia 14.5. Tathmini yangu ya utendaji wa Benki ulionesha kuwa gharama za Benki kwa mapato zilikuwa asilimia 81.82 ambayo ilizidi kiwango cha chini kinachohitajika cha asilimia 55.

Kutokufikiwa kwa uwiano wa jumla wa mtaji kunachangiwa na mikopo chechefu na kuendelea kupata hasara, hivyo kuendelea kupunguza mtaji mkuu.

Ukiukwaji wa sheria na kanuni unaweza kusababisha adhabu, vikwazo kutoka kwa mamlaka za udhibiti, na kupelekea kupata sifa mbaya kwa benki.

Ninapendekeza kuwa, Benki ya Biashara Tanzania; (a) ihakikishe inaandaa mbinu za kibiashara za muda mrefu, kwa kuchukua hatua zinazohitajika kuhakikisha kuna utoshelevu wa mtaji, na kulipwa kwa mikopo isiyolipika; na (b) ifuatilie kwa karibu gharama za uendeshaji ili kuendana na matakwa ya Waraka wa asilimia 55 ya uwiano wa gharama kwa mapato.

### 12.2 Mapungufu katika utendaji wa Mfuko wa SELF mwaka 2022

#### i) Usimamizi duni katika uwekezaji wa shilingi bilioni 19.97

Aya ya 6.3 ya Sera ya Uwekezaji ya Mfuko wa SELF ya mwaka 2018 inataka amana za benki zilizo na leseni na taasisi za fedha zilizo na ukomavu wa awali wa angalau miezi mitatu ziwe angalau na asilimia 30 na upeo wa juu wa asilimia 50 dhidi ya uwekezaji wote. Ukaguzi wangu juu ya uwekezaji wa shilingi bilioni 23.03 hadi tarehe 31 Desemba 2022, ulibaini kuwa Mfuko wa SELF umewekeza shilingi bilioni 19.77 sawa na asilimia 86 katika amana za kudumu. Hii ni zaidi ya kiwango cha juu zaidi cha asilimia 50 kilichobainishwa kwenye Aya ya 6.3 ya Sera ya Uwekezaji ya Mfuko SELF ya mwaka 2018.

Nina mashaka kuhusiana na hatari inayoweza kutokea kutokana na uwekezaji unaozidi kikomo iwapo taasisi za fedha zilizokopeshwa hazitafanya vizuri.

Ninapendekeza kuwa Mfuko wa SELF uimarishe udhibiti kwa kuhakikisha uwekezaji katika amana zisizohamishika hauzidi kiwango cha juu cha asilimia 50 ya uwekezaji wote ili kuendana na Sera yake ya Uwekezaji.

**ii) Madai ya riba za muda mrefu katika amana za kudumu zilizoiva zenye thamani ya shilingi milioni 204.15**

Aya ya 5.1 ya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 2018 inaelekeza kuwa, Mfuko utawekeza ama kwenye hati fungani iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania au Amana isiyohamishika kwenye benki za biashara.

Mapitio yangu yalibaini kuwa hadi tarehe 31 Desemba 2022 Mfuko wa SELF ulikuwa na riba ambayo ilikuwa hajjalipwa ya shilingi milioni 204.15 inayodaiwa kutoka kwenye amana za kudumu zipatazo 14 zilizoiva kwa kipindi cha kati ya miezi 29 hadi 49. Ninahusisha mapungufu haya yalitokana na mipango isiyotosheleza ya usimamizi na kufuatilia riba zilizoiva na inayodaiwa kwa benki za biashara na taasisi ndogo ndogo za fedha.

Kutolipwa kwa riba kwa muda mrefu kunazuia Mfuko kutofanya uwekezaji kwenye maeneo mengine yenye fursa.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa SELF uwasiliane na benki husika kuhusu riba ambazo hazijalipwa kwa amana za kudumu za shilingi milioni 204.15 zilizoiva.**

**iii) Usimamizi duni wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 38.89**

Kanuni 35 (1) (2) cha Kanuni ya Fedha Ndogo ya Kanuni, 2019 inahitaji taasisi ndogo za fedha kubaini utambulisho sahihi wa wakopaji na kutoa taarifa kila mwezi kwa Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo taarifa za kina kuhusu huduma zote za mikopo zinazotolewa kwa kila mkopaji; katika muundo kama benki inaweza kuagiza.

Mfuko wa SELF kufikia tarehe 30 Juni 2022 ulikuwa na mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 38.89 ambayo ilitolewa kwa wateja wapatao 4252. Hata hivyo Mfuko wa SELF haukuwasilisha taarifa za mikopo za mkopaji kwa Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo ambayo inatoa nafasi kwa wakopaji kujihusisha na huduma zingine za mikopo kutoka kwa taasisi ndogo ndogo za fedha au benki. Pia, mifumo ya Mfuko wa SELF ya Oracle na IMFAS ambayo ni mifumo iliyokusudiwa kutoa ripoti zenye taarifa za kina ili kupakiwa katika ofisi ya kumbukumbu ya mikopo lakini ilikuwa bado haijaunganishwa ipasavyo kuweza kutoa ripoti. Mfuko wa SELF ulinifahamisha kuwa mchakato wa kukamilisha mifumo hiyo iko mbioni ambayo itapelekea kupakia ripoti za mikopo na taarifa za mteja zitapatikana Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo na baada ya hapo watumishi

wa Mfuko wa SELF watapata mafunzo kutoka Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo kwa ajili ya utumiaji wa Mfumo huo.

Kuna hatari ya kuongezeka kwa mikopo chechefu kutokana na wakopaji kujihusisha na mikopo mbalimbali kutoka katika taasisi zingine za kifedha na bila kutambuliwa.

Ninapendekeza kuwa Mfuko wa SELF uhakikishe mifumo inayotumika inafanya kazi ipasavyo na yenye uwezo wa kutoa taarifa za kina na muhimu kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Kitengo cha Marejeleo ya Mikopo ili kupunguza hatari ya mikopo isiyoweza kulipika na wakopaji.

### 12.3 Mapitio ya utendaji wa Bodi ya Bima ya Amana

#### 12.3.1 Bima kutowekwa kwenye amana zilizopo kwenye benki ya maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB

Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 kinataka kila benki au taasisi ya fedha iliyopewa leseni ya kufanya biashara ya kibenki ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchangia katika Mfuko na kulipa kwenye Mfuko kiasi fulani kwa mwaka na nyakati mbalimbali, kama Bodi ya Bima ya Amana itakavyoelekeza.

Nilibaini kuwa Bodi ya Bima ya Amana inakusanya malipo moja kwa moja kutoka benki zipatazo 46 kati ya 48 za benki au taasisi za fedha zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, huku Bodi ikiwa haikusanyi michango kutoka Taasisi mbili za fedha ambazo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB.

Ukaguzi wangu ulibaini Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB zimekuwa zinapokea amana zisizohamishika kutoka kwa wateja mbalimbali ambazo hukomaa baada au zaidi ya mwaka mmoja. Hata hivyo, amana zinazowekwa na wateja wao haziwekewi dhamana, kwani Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB hazilipi bima kwa Bodi ya Bima ya Amana kwenye amana wanazopokea. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB zilieleza kuwa amana zinazopokelewa na Benki hizo hutunzwa na benki za kibiashara ambapo wanaendesha akaunti; hivyo malipo kwenye amana zao hulipwa na benki za biashara ambapo akaunti zao zipo. Hata hivyo, amana hizo katika benki za

biashara zinamiliikiwa na benki husika na si mteja binafsi mwenye amana.

Nina mashaka kuwa amana za wateja kutolipiwa bima moja kwa moja kama inavyotakiwa katika mpango wa bima kunaleta hatari ya fedha za wenyе amana kupoteza fedha zao iwapo benki itafilisika.

**Ninapendekeza Bodi ya Bima ya Amana ianzishe mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Maendeleo ya TIB huku ikihiusisha Benki Kuu ya Tanzania ili kukubaliana kuhusu njia mwafaka ya kupata amana za wateja wao.**

### 12.3.2 Amana za wateja zilizo katika mitandao ya simu kutokuwa na bima

Mpango mkakati wa Miaka Mitano wa Bodi ya Bima ya Amana wa mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027 umezingatia itifaki ya ushiriki wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia mipango iliyokubaliwa ya Kamati ya Masuala ya Fedha ya Jumuiya hiyo. Hii ikiwamo vigezo vya kufanana kwa kiwango cha bima, ukubwa wa mfuko wa lengo na utekelezaji wa utaratibu wa bima ya amana kwa miamala ya simu. Itifaki hizi zinahitaji taasisi za amana pamoja na mambo mengine kuingia mikataba ya amana na benki zinazotambua wazi uwapo kwa wanufaika mbalimbali kwenye akaunti ya udhamini; vilevile, waendeshaji wa Mitandao ya Simu kuwa na mifumo inayoweza kubainisha salio la kila mteja wakati wote.

Ukaguzi wangu wa utendaji wa Bodi ya Bima ya Amana ulibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 kulikuwa na kampuni sita zenyе leseni za uendeshaji wa mtandao wa simu. Lakini mfumo wa sasa wa bima ya amana na sheria zinazohusiana na amana, hazilindi amana zinazomilikiwa na wendeshaji wa mtandao wa simu. Kwa sasa amana zinazoendeshwa na waendeshaji wa mitandao ya simu katika akaunti za wadhamini zinalipwa chini ya sheria ya mfumo wa malipo wa kitaifa ya mwaka 2015 ambayo inatambua akaunti za amana pekee zilizo kwenye benki. Kwa mujibu wa Kanuni za Malipo za Kitaifa za mwaka 2015, amana katika akaunti za wadhamini ndani ya benki moja ya biashara hazipaswi kuzidi asilimia 25 ya jumla ya dhamana ya akaunti ya amana kama njia ya kupunguza hatari inayoweza kutokea. Maoni yangu ni kuwa dhamana hii inatakiwa kujitanua na kulinda amana binafsi kuititia Waendeshaji wa Mtandao wa Simu.

Nina mashaka kuwa chini ya utaratibu uliopo sasa amana za mtu binafsi zinakabiliwa na hatari ya kupotea endapo benki za biashara zilipowekwa amana hizo zitafilisika.

Ninapendekeza Bodi ya Bima ya Amana ishirikiane na wadau, wakiwamo Waendeshaji wa Mitando ya Simu mamlaka za usimamizi na wataalamu wa sekta hiyo kwa ajili ya kufanya utafiti na kutathmini kiwango cha malipo na dhamana za watu binafsi wanaoweka amana zao kwa Waendeshaji wa Mitando ya Simu.

### 12.4 Mapitio ya Utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya hifadhi ya jamii ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mafao ya kijamii kwa wanachama na wananchi kwa ujumla au kwa sekta fulani za kijamii. Ukaguzi wangu wa mifuko ya hifadhi ya jamii ulibaini mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kuboresha utendaji wa mifuko hiyo. Yafuatayo ni maelezo ya mapungufu hayo:

#### 12.4.1 Kiasi inachodaiwa Serikali kwa malipo ya watumishi walio kuwapo kabla ya kuanzishwa mfuko wa PSPF shilingi trilioni 2.28

Mwaka 2023 kampuni huru ilifanya tena tathmini ya hali halisi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na kutoa ripoti ilioonesha uhalisi. Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa ripoti hiyo ilionesha kuwa uthamani wa Mfuko ulikuwa na kiwango cha fedha cha asilimia 22.30 ambacho kiko chini ya kiwango kilichopendekezwa cha asilimia 40. Hivyo kusababisha upungufu wa asilimia 17.7 ya kiwango kinachohitajika. Baada ya ripoti hiyo kutolewa, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma uliitaka Serikali kulipa deni lililohusishwa na watumishi wa mfuko wa hifadhi ya jamii wa kabla ya mwaka 1999 ambalo ni shilingi trilioni 4.46 lililorithiwa kutoka mfuko wa zamani uliofutwa, ili kuweza kukabiliana na nakisi iliyobainika.

Aidha, tarehe 15 Desemba 2021 Serikali ikatoa bondi maalumu ya shilingi trilioni 2.18 na kuahidi kulipa kiasi kilichosalia cha shilingi trilioni 2.28 mara baada ya zoezi la uhakiki kukamilika ambalo linategemea kukamilika tarehe 31 Machi 2024.

kwa maoni yangu, ili kuongeza mzunguko wa fedha kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, kwa ajili ya uwekezaji na kulipa madeni yake kwa wakati, Serikali inapaswa kulipa deni hilo la

shilingi trilioni 2.28 ambazo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma unaidai.

Ninapendekeza Serikali iharakishe zoezi la uhakiki na kutoa ripoti kuhusiana na uhakiki huo; na ikamilishe malipo ya deni lililobaki la kabla ya mwaka 1999 la shilingi trilioni 2.28 la michango ya watumishi, fedha ambazo zitaboresha kiwango cha fedha cha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma hadi kufikia kiwango kilichopendekezwa cha asilimia 40.

#### **12.4.2 Usimamizi usioridhisha wa mikopo na malipo ya michango ya wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii**

##### **i) Mikopo iliyoiva inayodaiwa Serikali shilingi trilioni 1.73**

Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2021/22, nilibainisha mikopo ya muda mrefu iliyoilewa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa taasisi za Serikali na kupendekeza kuwa Wizara ya Fedha ishirikiane na taasisi hizo ili kuweka mipango mizuri ya marejesho ya mikopo husika, huku mifuko ya hifadhi ya jamii ikiimarisha mifumo ya udhibiti ya ndani kabla ya kutoa mikopo na kuendelea kufuatilia kwa karibu hivyo kuhakikisha mikopo yote iliyochelewa kulipwa inarejeshwa.

Katika mwaka huu, hadi tarehe 30 Juni 2023, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ilikuwa na mikopo ambayo haijalipwa na taasisi za Serikali na mashirika mengine shilingi trilioni 1.73. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ilikuwa na mikopo ambayo haijalipwa ya shilingi trilioni 1.50 (2021/22: shilingi trilioni 1.17) ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 330 sawa na ongezeko la asilimia 28. Wakati huohuo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulikuwa na mikopo ya shilingi bilioni 231.40 (2021/22: shilingi bilioni 231.40) ambayo ilibakia ileile. Mikopo hii haijalipwa kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi 16.

Hali ya wakopaji kushindwa kurejesha mikopo hiyo inathiri uwezo wa mifuko ya hifadhi ya jamii kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa tija na ufanisi. Pia, kuna mkopo wa muda mrefu wa shilingi bilioni 148.08 ikiwa ni asilimia 40 ya gharama zote za ujenzi wa mradi wa Daraja la Nyerere. Hata hivyo Serikali iliazimia kulipa deni hili pamoja na mikopo mingine ya Serikali kwa njia ya hati fungani isiyokuwa na fedha taslimu.

Narudia pendekazo langu la awali kuwa Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na taasisi za Serikali ambazo zimekopa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ifanye mipango ya marejesho ya mikopo hiyo huku mifuko ya hifadhi za jamii inatakiwa kuimarisha udhibiti kabla ya kutoa mikopo na kuendelea kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha mikopo iliyopitisha muda inarejeshwa.

- ii) **Walakini wa kurejeshwa kwa mikopo iliyotolewa kwa watumishi na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi pamoja na Shirika la Bima la Taifa shilingi bilioni 1.26**

**Mikopo isiyo na dhamana:** ukaguzi wangu wa mikopo ya nyumba iliyotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi yenyе thamani ya shilingi bilioni 5.05 ulibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 669.37 hakikuwa na dhamana, kinyume na Aya ya 9 ya Sera ya Mikopo ya Wafanyakazi ya mwaka 2017. Ilibainika pia kuwa Shirika la Bima la Taifa limekuwa na mikopo ya wafanyakazi yenyе thamani ya shilingi milioni 65.95 iliyotolewa kwa watumishi 34 kwa muda mrefu ambao wameshindwa kufanya marejesho kwa zaidi ya mwaka mmoja na hawajajumuishwa kwenye orodha ya malipo ya kila mwezi kwa ajili ya urahisi wa marejesho.

**Mikopo ambayo haijalipwa na watumishi walioacha kazi:** Pia, nilibaini mikopo ya watumishi yenyе thamani ya shilingi bilioni 1.43, ambapo kiasi cha shilingi milioni 472.22 kilihusisha watumishi 10 ambao walikwisha hama kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Hali kadhalika, mikopo hiyo ilikuwa haikatwi riba ya asilimia 12 ya mwaka kama inavyotakiwa na mikataba ya mikopo hiyo. Vilevile, Shirika la Bima la Taifa lilitoa mikopo ya shilingi milioni 50.21 kwa wafanyakazi 38 ambao kwa sasa hawafanyi kazi kwenye Shirika hilo. Nina mashaka na urejeshwaji wa mikopo hii kwa kuwa hakukuwa na makubaliano ya kurejesha mikopo hii baada ya wafanyakazi hao kutengana na taasisi tajwa.

Kutokuwapo kwa dhamana dhidi ya mikopo iliyotolewa kunaathiri urejeshwaji wa mikopo hiyo. Aidha, kutokuwapo kwa makubaliano ya kurejesha mikopo kwa wale wafanyakazi waliohama au walioacha kazi kunaweza kuwachochea wafanyakazi hao kutoheshimu ratiba ya kurejesha fedha walizokopa na kupelekea hasara itakayotokana na mikopo hiyo kufutwa.

Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Fidia kwa Watumishi na Shirika la Bima la Taifa wahakikishe mikopo iliyotolewa kwa watumishi inakuwa na dhamana. Pia, kwa watumishi walioacha kazi, waingie nao makubaliano ya kurejesha mikopo wanayodaiwa. Jambo hili lifanyike kwa kushirikiana na waajiri wao wa sasa ili mikopo hiyo ijumuishwe katika orodha ya malipo ya kila mwezi. Pia, wahakikishe watumishi waliohama kutoka Mfuko wa Fidia wanalipa riba ya asilimia 12 kama ilivyoelezwa katika makubaliano ya mkopo.

### iii) Mapungufu katika usimamizi wa madai ya michango ya wanachama shilingi bilioni 856.78

Ukaguzi wangu katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulibaini kutokukusanya kwa michango ya shilingi bilioni 710 ambazo zilitakiwa kukusanya. Upembusi wangu ulionesha kuwa shilingi bilioni 330 sawa na asilimia 46 ya shilingi bilioni 710, zilikuwa na muda wa zaidi ya miezi 12 kinyume na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ya mwaka 2018 inayomtaka mwajiri anayechangia kulipa michango ya Mfuko ndani ya mwezi mmoja baada ya mwezi ambao michango inadaiwa na kulipwa. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulinifahamisha juu ya juhudi zilizochukuliwa za kutekeleza ukusanyaji michango kutoka kwa waajiri walioshindwa kuwasilisha michango ya waajiriwa wao ikiwa ni pamoja na kutoa barua za madai kwa waajiri wote walioshindwa kuwasilisha michango, kufungua kesi 126 zenye michango ya thamani ya shilingi bilioni 35.89 dhidi ya waajiri walioshindwa kulipa na kuunda timu maalumu ya wajumbe kutoka taasisi tano za Serikali ili kutekeleza lengo la makusanyo.

Vilevile, ukaguzi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, umebaini kuwepo kwa michango ya shilingi bilioni 13.54 sawa na asilimia 44 ya shilingi bilioni 30.83 za michango yote ikiwa na walakini wa ukusanyaji wake ambapo shilingi bilioni 12.65 ni kutoka kwa waajiri wapatao 4,124 ambao wamesimamisha biashara zao huku shilingi milioni 891.14 ni kutoka kwa waajiri wapatao 590 ambao biashara zao zimefungwa.

Pia ukaguzi wangu wa ripoti ya wadaiwa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulibaini kutopokelewa kwa mchango wa shilingi bilioni 102.36 sawa na asilimia 77 za shilingi bilioni 133.24 ukiwa na muda wa zaidi ya siku 122 kinyume na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 2018 inayomtaka mwajiri kuchangia ndani ya mwezi mmoja baada ya mwisho wa kila mwezi.

Kuchelewa kukusanya michango kunaweza kuathiri uwezo wa kifedha na kusababisha mifuko ya hifadhi ya jamii kutotimiza majukumu yake likiwalipo kuwalipa wanufaika. Pia, kuna uwezekano mkubwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kushindwa kulipa fidia kutokana na kushindwa kukusanya michango kulingana na hali ya wadaiwa.

**Ninapendekeza Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi undelee kuwasiliana na wanachama kuwahimiza kulipa madeni wanayodaiwa.**

**iv) Waajiri waliosajiliwa ambao hawachangii Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

Nilibaini kuwa, kati ya waajiri 30,866 waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, waajiri wapatao 2,402 walikuwa wamefunga biashara, na kusalia waajiri 28,464 ambao wana biashara hai. Ugaguzi wangu ulibaini kuwa, waajiri wapatao 10,216 kati ya 28,464 hawakuchangia mfuko. Kwa maoni yangu kushindwa kukusanya michango kutoka kwa waajiri waliosajiliwa kwa asilimia 36 kunapelekea wafanyakazi wa taasisi husika kukosa fursa ya matibabu pindi watakapoumia wakiwa kazini.

**Ninapendekeza Mfuko wa Fidia kwa Watumishi uweke mikakati ya kuhakikisha kuwa kila mwajiri aliyesajiliwa anachangia katika Mfuko kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2015.**

**12.4.3 Ukusanyaji usioridhisha wa kodi ya pango unaofanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Shirika la Bima la Taifa kiasi cha shilingi bilioni 47.10**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulikuwa unadai kodi ya pango ya shilingi bilioni 22.86. Ugaguzi wangu wa ripoti ya madeni ya kodi ulibainisha kuwa shilingi bilioni 20.22 sawa na asilimia 88 ya kodi yote inayodaiwa zilikuwa na muda wa zaidi ya miezi 12, wakati shilingi bilioni 2.64 zikiwa na muda wa chini ya miezi 12.

Vilevile Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulikuwa na jumla ya mikataba 491 ya uuzaaji wa nyumba (Hire purchase agreements) zilizopo Kijichi na Kinyerezi, ambapo jumla ya makusanyo

ya kodi yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 33.38. Hata hivyo, Mfuko uliweza kukusanya shilingi bilioni 18.63 sawa na asilimia 56 huku kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 14.75 sawa na asilimia 44 hakikukusanya.

Pia, ukaguzi wangu wa ratiba ya malipo ya wapangaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulibaini wapangaji watatu kutolipa kodi kwa muda wa miaka mitatu ambayo imefikia shilingi milioni 102; isitoshe hapakuwa na ufuatiliaji wa karibu wala hatua zilizochukuliwa kuwafanya wapangaji hao kuondoka katika nyumba hizo.

Vilevile, Shirika la Bima la Taifa lina madeni ya kodi ambayo yanafikia shilingi bilioni 9.35 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa shilingi bilioni 8.05 sawa na asilimia 86 ya shilingi bilioni 9.35 za madeni yote ya kodi zilishu madeni yaliyokuwa na umri wa zaidi ya mwaka mmoja. Shirika la Bima la Taifa lilini julisha kuwa jumla ya kodi ya shilingi bilioni 9.35 iliyorekodiwa tarehe 30 Juni 2023 inajumuisha wadaiwa ambao hawajulikanivalipo ambao wanachangia asilimia 85 sawa na shilingi bilioni 7.95.

kuwapo kwa juhudhi ndogo katika ukusanyaji wa kodi ya pango kunaweza kuzuia maendeleo zaidi kwa taasisi kutokana uhaba wa fedha ambazo zilitakiwa kukusanya kutoka kwenye pango.

**Ninapendekeza taasisi zikijumuisha Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, na Shirika la Bima la Taifa zihakikishe vifungu katika mikataba ya ukodishaji vinatekelezwa ili kuruhusu ukusanywaji wa kodi kutoka kwenye vitegauchumi vyake kupitia kuanzisha mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa kodi za pango.**

#### **12.4.4 Mapungufu katika utoaji wa huduma kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

- i) **Kuchelewa kuandikisha wastaifu wapya wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma katika orodha ya malipo ya Hazina**

Ukaguzi wangu wa mchakato wa malipo ya pensheni kwa wastaifu wapya uliohusisha miezi ya Septemba 2022, Novemba 2022, na Mei 2023 ulibaini wastaifu sita walicheleweshwa kuandikishwa katika orodha ya hazina kwa kipindi cha kuanzia miezi 6 hadi 83. Kuchelewesha kwa

kusajili wafanyakazi wapya waliostaafu katika Orodha ya malipo ya Hazina kunawanyima haki zao za kupokea mafao yao ya kila mwezi.

**ii) Ucheleweshaji wa Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi kushughulikia madai kwa wanufaika hadi siku 60**

Nilikagua madai 40 kati ya madai 1836 yaliyorekodiwa mwaka 2022/23. Nilibaini Kifungu cha 75 (1) Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2015 [Sura 263] kimetoa muda usiozidi siku 30 kwa ajili ya kushughulikia na kukamilisha madai. Ila ukaguzi wangu ulibaini madai 19 kati ya 40 (sawa na asilimia 48) yалишугулікія kwa muda wa siku kuanzia 32 hadi 90. Hali hii inaashiria kuchelewa kwa siku 2 hadi 60 dhidi ya muda uliowekwa kisheria. Kuchelewa kushughulikia madai yaliyowasilishwa kuna athari katika kazi. Maoni yangu ni kuwa ucheleweshaji wa madai una mtazamo hasi kutoka kwa walengwa.

**Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi uimarishe, na kuanzisha utaratibu utakaoruhusu walengwa kuhudumiwa kwa wakati.**

**12.4.5 Changamoto za kiutendaji katika kampuni tanzu na vitega uchumi vya mifuko ya hifadhi ya jamii**

**i) Utendaji usioridhisha wa Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro**

Mwaka 2022/23 Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro kilikadiria kufanya mauzo ya shilingi bilioni 6.78; hata hivyo kilifanikiwa kufanya mauzo ya shilingi bilioni 3.48. Mauzo haya ni pungufu kwa lengo kusudiwa kwa shilingi bilioni 3.3 sawa na asilimia 49. Pia, Kampuni ilizalisha jozi za viatu 59,272 kati ya lengo la jozi za viatu 88,111; hivyo haikufikia lengo kwa jozi za viatu 28,839 sawa na asilimia 33. Vilevile, kutokana na ukosefu wa malighafi Kampuni ilishindwa kutimiza oda za jozi 14,261 za wateja ambazo zingeingiza mapato ya shilingi bilioni 1.06.

Pia, nilipitia Mpango Mkakati wa Biashara wa miaka mitano unaoanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 ikiwa ndiyo dira ya uendeshaji wa Kampuni. Tathmini yangu ya utekelezaji wa mpango ilibaini kuwa mpango huo hauendani na mipango ya uendeshaji ya mwaka ambayo ilithibitishwa kutokana na makadirio ya mauzo ya mwaka kwenye mpango mkakati ilikuwa shilingi bilioni 39.57 dhidi ya makadirio ya mauzo ya shilingi bilioni 6.78 iliyoainishwa kwenye mipango ya mwaka

mmoja mmoja na kusababisha tofauti ya shilingi bilioni 32.79 hiyo kuwa ni dalili ya kupanga malengo ya juu yasiyoweza kufikiwa.

Mwenendo wa kutofikia lengo na kutopeleka oda za wateja kuna athari mbaya kwa usitawi na ukuaji wa Kampuni kibiashara. Pia, maoni yangu ni kuwa kutounganishwa kwa Mpango mkakati wa Kampuni na mipango mingine ya uendeshaji kunasababisha mpango mkakati kutokuwa na umuhimu na malengo yaliyowekwa hayawezi kufikiwa.

**Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa kushirikiana na Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro wafanye yafuatayo; (a) waje na mkakati wa mabadiliko ili waweze kuongeza wigo wa soko ya bidhaa wanazozalisha; na (b) waanzishe mchakato wa kuitia upya mpango mkakati ili kuweza kuweka malengo yenyeh uhalisia na ambayo yatafikiwa.**

**ii) Mapungufu katika kusimamia na kuendesha Kampuni ya Mkulazi ambayo hadi sasa ina mtaji wa shilingi bilioni 312.98**

Kampuni ya Mkulazi inamiliwi kwa pamoja na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi kwa asilimia 96 na Magereza kwa asilimia 4. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Kampuni ilipata hasara kabla ya kodi ya shilingi bilioni 21.97 ikilinganishwa na hasara ya kabla ya kodi ya mwaka 2021/22 ya shilingi bilioni 10.35. Aidha, upembuzi wa ukaguzi ulibaini kuwa hasara imeongezeka kwa shilingi bilioni 11.62 sawa na asilimia 112 kutokana na kuongezeka kwa gharama za utawala, uendeshaji wa mashamba na mishahara ya wafanyakazi.

Nilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa mradi na kubaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2023 wanahisa walikuwa wamewekeza shilingi bilioni 312.98. Pamoja na kuwekeza kiasi hicho cha fedha mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2016 bado ulikuwa unasuasua kwani hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 miaka saba tangu kuanzishwa kwake kazi ilikuwa bado ikiendelea. Mpango wa awali wa uzalishaji wa sukari ulipaswa kuanza Septemba 2018 hatahivyo hadi wakati wa ukaguzi wangu mradi ulikuwa bado unafanyiwa majaribio.

Pia, nilibaini kuwa Kampuni ya Mkulazi ilikuwa na mifumo ya umwagiliaji yenyeh uwezo wa kumwagilia hekta 2,731 za mashamba ya miwa wakati mashamba ya miwa ambayo yanayolimwa ni hekta 3,133 na kusababisha hekta 402 bila kuwa na mfumo wa umwagiliaji. Kampuni iliniarifu kuwa imeishaingia makubaliano na mkandarasi kwa ajili ya kuweka mfumo wa umwagiliaji kwa mwaka wa fedha wa 2023/24 ambapo mradi utahusu hekta 500 ambapo hekta 402 ni sehemu ya hekta 500.

Kuendesha hekta 402 bila miundombinu ya umwagiliaji kunaweza kuwa na athari kubwa wakati wa msimu wa ukame na kiangazi pia kunaweza sababisha kuathirika uzalishaji wa miwa.

Maoni yangu ni kuwa Serikali haipati thamani halisi ya fedha kutokana na mradi huo kuchelewa; hivyo kusababisha malengo kusudiwa kuchelewa.

Ninapendekeza yafuatayo; (a) Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Magereza kwa Kushirikiana na Kampuni ya Mkuluzi kuhakikisha mradi unatekelezwa bila kuchelewa zaidi, na (b) Kampuni ya Mkulazi ifunge haraka mfumo wa Miundombinu ya Umwagiliaji wa Semisolid ambao utahakikisha miwa inasitawi hata wakati wa kiangazi au wakati wa ukame.

**iii) Kutokuwa na uhakika wa kulipwa kwa kodi ya pango ya shilingi bilioni 10.98 inayotokana na kitega uchumi cha Ubungo Plaza**

Ubungo Plaza inamiliikiwa kwa pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Shirika la Bima la Taifa. Upembusi wangu wa ukaguzi kutoka kwa uchanganuzi wa muda wa madeni ulibaini deni la shilingi bilioni 10.98 lilikuwa limedumu kwa zaidi ya siku 360. Aidha, nilibaini kuwa sehemu kubwa ipatayo shilingi bilioni 8.89 sawa na asilimia 79 ya madeni yote ilitokana na mdaiwa mmoja ambaye ni Hoteli ya Blue Pearl.

Katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023, nilibaini kuwa kampuni ilipata hasara kabla ya kodi ya shilingi bilioni 8.83 ikilinganishwa na faida kabla ya kodi ya shilingi milioni 605.42 iliyoripotiwa mwaka 2021/22. Hii ilisababisha nakisi ya shilingi bilioni 9.44. Sababu kuu ilikuwa ni kuhusiana na deni la Hoteli ya Blue Pearl.

Ninaona kuwa, upo uwezekano wa Ubungo Plaza kushindwa kufanya maendeleo zaidi kutokana na ufinyu wa mapato yatokanayo na uwekezaji uliopo.

Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Shirika la Bima la Taifa kwa kushirikiana na kitega uchumi cha Ubungo Plaza kuhakikisha vifungu katika mikataba ya ukodishaji vinatekelezwa ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uwekezaji, hii ni pamoja kwa kuweka mikakati sahihi na thabiti ya ukusanyaji wa kodi inayodaiwa.



# SURA YA KUMI NA TATU

## MAPATIO KATIKA SEKTA YA UTALII TANZANIA

### 13.0 Utangulizi

Utalii unachangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa; na ni asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni. Vivutio vya utalii vilivyopo nchini Tanzania ni pamoja na Hifadhi za Taifa, utalii wa uwindaji na fukwe za mwambao wa pwani<sup>1</sup>. Mionganoni mwa Taasisi muhimu za kutangaza utalii ni pamoja na Hifadhi za Taifa Tanzania inayosimamia Hifadhi za Taifa zipatazo 22, wakati Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro inasimamia maeneo mawili ambayo ni hifadhi ya eneo la Ngorongoro na Pori tengefu la Poloreti, huku Bodi ya Utalii Tanzania ikiwa na jukumu la kukuza na kutangaza masuala yote ya utalii nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, Serikali imekusudia kuongeza idadi ya watalii kutoka 1,527,230 kwa mwaka 2019/20 hadi 5,000,000 kwa mwaka 2025/26. Hii itasababisha ukusanyaji wa dola za Marekani bilioni 6 ifikapo mwaka 2025. Mnamo mwaka 2023, wageni wa kimataifa waliowasili nchini Tanzania walikuwa 1,808,205, sawa na ongezeko la watalii 353,285 sawa na asilimia 24 ikilinganishwa na watalii 1,454,920 waliowasili nchini kwa mwaka 2022 na kupelekea sekta ya utalii kuingiza dola za Marekani bilioni 3.37 kwa mwaka 2023<sup>2</sup>.

Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watalii ikilinganishwa na miaka iliyopita, ukaguzi wangu ulibaini kuwa vivutio vya utalii vinakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji hatua za makusudi kukabiliana nazo. Baadhi ya changamoto hizo ni: Uwezo mdogo wa malazi ya watalii kutokana na uhaba wa hoteli katika hifadhi za Taifa; Kuenea kwa magugu vamizi katika hifadhi za Taifa; Kukatika kwa umeme mara kwa mara ambapo kunatatiza shughuli za hifadhi; Upungufu wa fedha za

<sup>1</sup> Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26

<sup>2</sup> Taarifa za utalii zilizotolewa na Wizara ya Utalii kwa mwaka 2023

utangazaji na kukuza utalii; na pamoja na uvamizi wa maeneo ya mipaka ya hifadhi za taifa.

Sura hii inaangazia changamoto zinazoikabili sekta ya utalii na mapendekezo juu ya hatua ya kukabiliana nazo.

### **13.1 Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutangaza utalii katika Bodi ya Utalii Tanzania**

#### **13.1.1 Kutoanza kufanya kazi kwa kituo cha kidijitali**

Bodi ya Utalii Tanzania ina kituo cha kidijitali kilichokamilika mnamo mwezi Aprili 2022, kwa gharama ya jumla ya shilingi bilioni 1.06. Lengo kuu la kituo hicho ni kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa njia ya kisasa zaidi ya kidijitali kwa kuviweka vivutio hivyo katika viwango vya kimataifa ili kuzidi kujulikana kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kama vile vile Facebook na X (zamani twitter).

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini kuwa Kituo hicho hakijawahi fanya kazi ya kutangaza utalii kama lengo kusudiwa tangu kukamilika kwake (miezi 20 iliyopita). Aidha, mapitio yangu ya bajeti ya Bodi kwa mwaka 2022/23 yilibaini kuwa bajeti ya shilingi milioni 228.52 iliyotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa Kituo hicho hazikutolewa na Serikali ili kuweza kufungua kituo hicho.

Kuchelewa kufunguliwa kwa kituo hicho cha kidijitali kunachelewesha na kuinyima sekta ya utalii faida ambazo zingetokana na utangazaji utalii kupitia kituo hicho katika kutangaza vivutio vya utalii.

**Ninapendekeza Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kufuatilia kwa karibu Serikalini ili kupata fedha zinazohitajika kwa ajili ya uendeshaji wa kituo cha kidijitali ili kuweza kutimiza malengo ya kutangaza utalii.**

#### **13.1.2 Kutofanyika matukio ya kutangaza utalii wa kimataifa**

Mapitio yangu ya bajeti ya kutangaza utalii kitaifa na kimataifa ulibaini kuwa mwaka 2022/23 bajeti ya Bodi ilikuwa shilingi bilioni 4.50 kwa ajili ya kutangaza utalii kitaifa na kimataifa lakini Serikali ilitoa shilingi bilioni 3.15 huku shilingi bilioni 1.35 hazikutolewa.

Katika mwaka wa 2022/23, Bodi ya Utalii ilipanga kushiriki katika kutangaza utalii wa kimataifa kama mbinu ya kimkakati ya masoko kwa vivutio nya utalii. Miongoni mwa masoko yaliyolengwa ni pamoja na kushiriki kwenye maonesho manne ya utalii barani Ulaya, maonesho mawili ya utalii barani Asia, maonesho matatu ya utalii Amerika Kaskazini na Kusini, na kushiriki katika makongamano mbalimbali ya kimataifa, yote hayo yalitengewa bajeti ya shilingi bilioni 1.13.

Hata hivyo, tathmini yangu juu ya Bodi ya Utalii katika kutangaza shughuli za utalii Tanzania ilibaini kuwa, kongamano na hafla zilizopangwa hazikufanyika kwa sababu fedha tarajiwa za kutangaza utalii wa kimataifa hazikutolewa na Serikali.

Kutotumia hafla na kongomano ili kutangaza utalii wa kimataifa ipasavyo kuna athari katika kutangaza vivutio nya Tanzania. Aidha, kunaweza kusababisha kupungua kwa watalii wa kimataifa wanaoitembelea Tanzania.

**Ninapendekeza Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ifuatilie kwa ukaribu Wizara ya Fedha kuhusiana na utolewaji kamili wa fedha za bajeti ya utangazaji wa utalii ili kutekeleza shughuli za utangazaji utalii.**

### 13.2 **Kutochukua hatua za kulinda na kusimamia mipaka ya Hifadhi za Taifa kutokana na shughuli za kibinadamu katika Hifadhi za Manyara na Arusha**

Katika ukaguzi wangu wa mipaka ya Hifadhi za Taifa ulibaini shughuli za kibinadamu zinazoingiliana na mipaka ya Hifadhi za Taifa. Vilevile, nilibaini kuwa kilomita za mraba zipatazo 10 za Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara zimevamiwa na wanakijiji wa kijiji cha Buger. Pia, nilitembelea Hoteli ya Hatari katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha na kukuta shughuli zisizo za kitalii zikifanyika ndani ya Hifadhi ya Arusha. Niliona vibanda vidogo vilivyojengwa kwa madhumuni ya kupanda miti ndani ya hifadhi bila ridhaa ya Hifadhi ya Taifa Tanzania kinyume na mkataba wa ukodishaji. Pia, niliona bustani iliyozunguka eneo la jikoni ambalo limepandwa mimea isiyo ya kiasili kama vile ndizi, mboga mboga na viazi vitamu.

Hifadhi za Taifa Tanzania ilinifahamisha kuwa Hoteli ya Hatari iko ndani ya ekari 608 zinazomilikiwa na Hifadhi za Taifa; hata hivyo shamba ambalo Hoteli ya Hatari ipo bado halijaunganishwa na Hifadhi ya Taifa

ya Arusha. Aidha, walieleza kuwa Mkataba wa leseni iliyotolewa kwa mwekezaji ni Mkataba wa Leseni Sanifu zinzotolewa kwa wawekezaji wote wanaowekeza katika Hifadhi za Taifa. Leseni hiyo ilitolewa kwa matarajio kuwa, shamba hilo litaunganishwa kwenye hifadhi kwa haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, eneo hilo halikuunganishwa kama ilivyotarajiwa kutokana na kufunguliwa kwa kesi mahakamani na baadhi ya wanakijiji, kesi ambazo bado hawajalipwa fidia zilizobaki kwenye shamba hilo.

Kuendelea kwa shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi za taifa kunaweza kusababisha uharibifu wa uoto wa asili kwa kuwezesha kuenea kwa magugu vamizi na magonjwa kwa wanyamapori.

**Ninapendekeza Serikali kwa kushirikiana na Hifadhi za Taifa kusimamia sheria za Hifadhi za Taifa ili kulinda mipaka ya Hifadhi za Manyara na Arusha.**

### 13.3 Uvamizi wa maeneo ya Mambo Kale

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro inasimamia maeneo ya mambo kale yapatayo matano ambayo ni Kimondo cha Mbozi, Mapango ya Amboni, Magofu ya Engaruka, Nyayo za Engare-sero, na Mumba Rock Shelter. Ukaguzi wangu kupitia ripoti za robo mwaka za Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kuhusiana na usimamizi wa mambo kale ulibaini kuwa maeneo ya mambo kale yapatayo matatu kati ya matano yalikuwa yamevamiwa. Maeneo hayo ni pamoja na Nyayo za Engare-sero, Miamba ya Mumba na Magofu ya Engaruka. Ziara yangu ilishuhudia shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, uchimbaji mawe, ukusanyaji wa mchanga zikiendelea kutoka maeneo haya.

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilinifahamisha kuwa wana shauriana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu kutafsiri ya mipaka ya maeneo haya kwa sababu Tangazo la Serikali lililoweka kumbukumbu za mipaka ni la zamani na baadhi ya vipengele vya mipaka vimefutika.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii watatue haraka masuala ya mipaka kupitia Tangazo la Serikali ili kuruhusu uendelezaji wa maeneo ya mambo kale.**

### 13.4 Kusambaa na kuongezeka kwa mimea vamizi zaidi ya uwezo wa hifadhi kuyadhibiti

Nimekuwa nikitoa taarifa juu ya hali mbaya ya kuenea kwa mimea vamizi, nilipendekeza kuwa Serikali ifikirie kutangaza tatizo la mimea vamizi kuwa suala la kitaifa na kuhakikisha wadau katika ngazi zote wanahusishwa ili kuchukua hatua stahiki katika kuondoa, kudhibiti na kuzuia kuwapo kwa mimea hiyo ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, kwenye Hifadhi za Taifa, na katika maeneo mengine nchini. Nimekuwa nikiripoti juu ya suala hili katika miaka minne mfululizo ya fedha, lakini hakuna jitihada kubwa zilizochukuliwa na Serikali kulishughulikia tatizo hilo.

Ukaguzi wangu wa 2022/23 umeendelea kubaini kuendelea kwa tatizo hilo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2022/23 Hifadhi ya Taifa ilipanga kung'oa na kuondoa magugu vamizi kwenye hekta za mraba zipatazo 3,384.22 katika hifadhi za taifa 15. Hata hivyo, Mamlaka iliweza kung'oa hekta za mraba zipatazo 2,352.53 (asilimia 69.5) ya maeneo yaliyopangwa. Pia, Hifadhi ya Taifa ilifanya utafiti kwenye hifadhi zingine mbili za Kilimanjaro na Burigi-Chato na kubaini Hekta 507.01 ambazo zimeathiriwa na magugu vamizi.

Kwa hiyo, ninarudia pendelezo langu kuwa Serikali ifikirie kutangaza tatizo la mimea vamizi kuwa suala la kitaifa na kuhakikisha wadau wa ngazi zote wanahusishwa ili kuchukua hatua za kuondoa, kudhibiti na kuzuia kuwapo kwa mimea hiyo ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, katika hifadhi zingine za taifa, na katika maeneo mengine kote nchini.

### 13.5 Hatari ya kutokamilika kwa mradi wa kuwabdalishia makazi jamii ya watu wanaoishi ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kwa kushirikiana na taasisi zingine za Serikali na wadau mbalimbali, imeanza kutekeleza mradi wa kuwabdalishia makazi watu wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro tangu mwezi Juni 2022.

Katika mwaka 2022/23, nilibaini Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro imeendelea kuweka miongozo na mpango wa awamu ya pili wa kuwashamisha watu kutoka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Mamlaka

ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilikopa shilingi bilioni 266.68 na Serikali ikaongezea shilingi bilioni 20 na kufanya jumla ya fedha zilizopo kwa ajili ya uhamisho kuwa shilingi bilioni 286.68. Mamlaka iliamini kiasi hicho kingetosha kufanikisha zoezi la kuhamisha watu kutoka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Dhana ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kuwa shilingi bilioni 286.68 zingeweza kukamilisha zoezi la uhamishaji, haikutokana na makadirio ya mshauri elekezi, hivyo kusababisha tofauti kubwa kati ya makadirio ya mkandarasi (SUMA JKT) na yale ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Kwa mfano; nyumba moja kwa awamu ya pili ilikadirwa kujengwa kwa shilingi milioni 9.97 lakini makubaliano halisi na mkandarasi (SUMA JKT) yakaja kuwa shilingi milioni 19.48 kwa nyumba moja ikimaanisha kuwapo kwa ongezeko la shilingi milioni 9.51 sawa na asilimia 95. Hata hivyo kiasi kilichokopwa kinaweza kujenga nusu ya makadirio ya nyumba.

Ninarudia pendekezo langu kuwa Serikali, kwa kushirikiana na wadau wote, iandae na kutekeleza mpango wa kina wa utekelezaji wa mradi na kuhakikisha zoezi la kuhamisha watu linakamilika.

### **13.6 Upungufu wa vifaa wezeshi kutoa huduma za utalii ndani ya Hifadhi za Taifa**

#### **13.6.1 Upungufu wa sehemu za kulala kwa ajili ya watalii katika Hifadhi za Taifa**

Ukaguzi wangu wa taarifa za uwezo wa hoteli na mahema katika Hifadhi za Taifa ya mwaka 2022/23 umebaini kuwa kiwango kinachohitajika cha vitanda kwenye mahema na hoteli kwa ajili utalii ni 30,825, huku uwezo wa vitanda vilivyokuwapo kwa hifadhi zote 22 zinazoendeshwa na Hifadhi za Taifa ni 10,094 sawa na asilimia 33 ya mahitaji ya vitanda. Mchanganuo uko kwenye Jedwali Na. 33.

**Jedwali Na. 33: Upungufu wa vitanda katika hoteli na mahema za Hifadhi za Taifa**

Na	Aina ya Hoteli	Uwezo wa vitanda unaotakiwa	Uwezo wa vitanda uliopo	Upungufu wa vitanda
1	Mahema ya muda mfupi	16,203	6,515	9,688
2	Mahema ya kudumu	7,230	1,154	6,076
3	Bandas/Nyumba ndogo za wageni	2,817	1,175	1,642
4	Nyumba za kulala wageni	4,575	1,250	3,325
<b>Jumla</b>		<b>30,825</b>	<b>10,094</b>	<b>20,731</b>

**Chanzo:** Ripoti ya uwezo wa vitanda katika Hifadhi za Taifa ripoti ya 2022/23

Ili kukabiliana na uhaba wa malazi, Hifadhi ya Taifa ya Saadani ilitenga maeneo 10 kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli na mahema. Maeneo hayo ni Saadani, Sable, Kwamsuko, Igimba, Makenene, Maguruwe, Kidunda, Mlima Dumi, Mabumo, na Forodha ulaya.

Hata hivyo, nilibaini kuwa ni maeneo mawili tu kati ya 10 yaliyoyengwa hoteli na kuacha maeneo nane bila kuendelezwa. Idadi ya wageni kwa mwaka 2022/23 ilizidi makadirio kwa asilimia 22 kwani kulikuwa na ongezeko la wageni 6,496 zaidi ya 29,552 waliotarajiwa; ambayo inalazimu kuongeza uwezo wa malazi.

Nilielezwa kuwa menejimenti ya Hifadhi za Taifa imekuwa ikitangaza maeneo ya uwekezaji kuitia majukwaa mbalimbali, kama vile maonesho ya biashara, vyombo vya habari vya kielektroniki, pamoja na kuwaalika waendeshaji watalii na wawekezaji watarajiwa kutembelea maeneo ya hifadhi. Kutokana na jitihada hizo wawekezaji wanne wameanzisha mchakato wa uwekezaji katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Ni maoni yangu kuwa uhaba wa malazi unaweza kuchangia kukosa fursa ya kuwakaribisha wageni zaidi hali ambayo ingesababisha kuongezeka kwa mapato yanayotokana na ushuru kutoka kwa waendeshaji wa hoteli na mahema.

**Ninapendekeza Hifadhi za Taifa iharakishe mchakato wa kuongeza uwezo wa hoteli na mahema kwenye hifadhi kwa kuomba fedha za maendeleo kutoka Serikalini na kuvutia wawekezaji kuweza kujenga hoteli na mahema ili kukabiliana na uhaba wa malazi.**

### 13.6.2 Ukosefu wa umeme wa uhakika katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere

Lango la Mtemele ndilo linalofikika zaidi katika Hifadhi ya Nyerere. Lango hilo linahudumia takribani asilimia 90 ya wageni wote wa hifadhi hiyo. Kupitia tathmini yangu kuhusiana na uendeshaji wa hifadhi ya Nyerere nilibaini kuwa lango la Mtemele halijaunganishwa na umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania wala jenereta, badala yake lango linategemea mfumo wa sola ambao siyo wa uhakika. Kukosekana kwa chanzo cha kuaminika cha usambazaji wa umeme kunasababisha kuchelewa kushughulikia vibali vya wageni kwenye lango hilo. Hii ni kwa sababu malipo hufanywa kwa njia ya kielektroniki.

Ninapendekeza Hifadhi za Taifa kuitia mipango ya muda mfupi ifunge jenereta ambalo litapunguza tatizo la kukatika kwa umeme; na kwa ufumbuzi wa muda mrefu wawasiliane na Shirika la Umeme Tanzania ili kuhakikisha umeme unaunganishwa kwenye lango la Mtemele.

### **13.6.3 Kasi ndogo katika utekelezaji wa mradi wa uwanja wa gofu hifadhini Serengeti**

Uwanja wa Gofu wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni mionganini mwa miradi iliyoibuliwa na Bodi ya Wadhamini kwa lengo la kuongeza bidhaa mbalimbali za utalii katika hifadhi za Taifa ili kufikia lengo la Serikali la kupata watalii wa kimataifa wasiopungua milioni 5 na kuongeza mapato angalau kufikia dola za Marekani bilioni 6 ifikapo mwaka 2025. Kuanzishwa kwa uwanja wa gofu kama bidhaa mpya ya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kinalenga kuvutia wachezaji wa kimataifa wa gofu duniani kote. Hii ni sehemu ya utalii ya kutegemewa ambayo imeachwa tangu kuanzishwa kwa hifadhi hiyo mwaka 1959.

Mapitio yangu ya muundo wa mradi wa uwanja wa gofu kuitia andiko la mradi lenye nambari ya kumbukumbu Na.D.170/235/01.F la tarehe 28 Machi 2022 yalibaini kuwa mradi huo utachukuwa eneo lenye ukubwa wa ekari 450 ili kushughulikia usanidi na mpangilio wa kimkakati wa matundu 18, anuwai, uwanja wa ndege wa kipekee na idadi ya nyumba za kifahari za malazi. Tathmini yangu zaidi ilibaini kuwa mradi huo ulikadiriwa kugharimu shilingi bilioni 9.5 wakati tarehe ya kukamilika ilikuwa Desemba 2023 baada ya kuzinduliwa na Baraza la Wadhamini tarehe 29 Desemba 2022. Hadi kufikia Desemba 2023, nilifanya tathmini ya maendeleo na kubaini kuwa mradi ulikuwa umefikia asilimia 20 ya kukamilika, kutohana na kusuasua kwa utoaji fedha za maendeleo kwa ajili ya uendelezaji wa mradi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 ni shilingi bilioni 1.55 (asilimia 16) tu ndizo zilikuwa zimetolewa kati ya gharama za mradi za shilingi bilioni 9.5.

Kulingana na kasi ndogo ya utoaji wa fedha, ni vigumu kwa mradi wa uwanja wa gofu kukamilika; hivyo lengo la mradi halitafikiwa kama ilivyopangwa.

**Ninapendekeza Hifadhi za Taifa Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii iwasiliane na Wizara ya Fedha ili kutoa fedha za mradi wa uwanja wa gofu ili uweze kukamilika bila kuchelewa zaidi.**

### 13.6.4 Haja ya uboreshaji wa miundombinu ya Empakai na Olmoti Kreta ili kupanua wigo wa utalii

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ina kreta tatu ambazo ni Ngorongoro, Empakai na Olmoti. Kreta maarufu na inayotembelewa zaidi ni Kreta ya Ngorongoro huku kreta za Empakai na Omoti zikiwa ndizo zinazotembelewa kwa uchache zaidi. Nilitembelea Kreta ya Empakai na kuona changamoto kadhaa ambazo zinazuia kufika katika eneo hilo la utalii. Changamoto hizo ambazo zinahitaji utatuzi wa haraka. Utatuzi wa changamoto hizo ni pamoja na hitaji la kujengwa kwa barabara ili kurahisisha kreta kufikika, na kuwaalika wawekezaji kuweza kujenga hoteli na maeneo ya mahema kuzunguka kreta hizo.

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilinifahamisha juu ya mpango wa kufanya uchambuzi wa kina kwa ajili ya kuboresha maeneo mengine ya utalii, yakiwemo Kreta ya Empakai na Kreta ya Olmoti ili kupanua wigo wa utalii. Uboreshaji huo unalenga upanuzi wa miundombinu kama vile barabara na njia za kutembea watalii ambazo zitawawezesha watalii kujihusisha zaidi na utamaduni katika utalii.

Aidha, Mamlaka ilieleza zaidi kuwa inaweka mpangilio wa bei kwa ajili ya kuongeza mapato yake kutoka kwa watalii katika Eneo la Ngorongoro.

Uboreshaji wa miundombinu na huduma pamoja na utangazaji wa kreta za Empakai na Olmoti kutapelekea ongezeko la mapato kwa sababu ya kuongeza vivutio vya utalii.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ianzishe mpango wa kina kwa ajili ya maendeleo ya kreta za Empakai na Olmoti ili kuimarisha bidhaa za utalii.**



# SURA YA KUMI NA NNE

## UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

### 14.0 Utangulizi

Utendaji wa mamlaka ya huduma za maji na usafi wa mazingira unapimwa kuitia malengo yaliyobainishwa katika makubaliano yaliyofanyika baina ya mamlaka ya huduma ya maji na Wizara ya Maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inasimamia masuala ya kiufundi na kiuchumi ya shughuli za mamlaka za maji.

Viashiria muhimu vyta utendaji kwa mamlaka za maji ni pamoja na kulinda maslahi ya wateja, uhimilivu na uendelevu wa huduma za maji, ustawi wa miundombinu na mazingira, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na gharama za uendeshaji, kusimamia upotevu wa maji, pamoja na kuongeza vyanzo vyta maji.

Licha ya jitihada za Serikali za kuboresha upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira, kumekuwa na changamoto kadhaa zinazokwamisha hatua zinazochukuliwa. Sura hii inaangazia mapungufu katika utendaji wa mamlaka za huduma za maji na usafi wa mazingira na masuala mengine yanayohusiana na utendaji wa mamlaka za maji.

### 14.1 Mwendelezo wa upungufu wa uzalishaji maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira

Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, Sura 272 inaelekeza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kutoa huduma ya majisafi na majitaka katika miji.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 31 kati ya 36 zilizokaguliwa zilikuwa na upungufu katika uzalishaji wa maji kwa asilimia 8 mpaka asilimia 92 kila siku kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 34**. Upungufu wa uzalishaji maji unasababishwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi na usimamizi duni wa miradi kutokana na kutotolewa kwa fedha za kutosha

kutoka Wizara ya Maji. Tatizo hili bado linaendekea. Katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22 niliripoti mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 25 zenyenye upungufu au uhaba wa uzalishaji maji kuanzia asilimia 11 hadi 80 kwa mahitaji ya kila siku.

**Jedwali Na. 34: Upungufu wa uzalishaji maji katika miji (M3 kwa siku)**

N A.	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	Kiasi cha Maji Kinachohitajik a	Maji Yanayozal ishwa	Mapung ufu ya Maji	Mapunguf u ya Maji (Asilimia)
1.	Bariadi	21,292	1,633	19,659	92.33
2.	Namtumbo	4,731	625	4,106	86.79
3.	Korogwe	13,943	1901	12,042	86.00
4.	Makambako	9,125	2,122	7,003	76.75
5.	Babati	31,826	11,265	20,561	64.60
6.	Bukoba	26,200	10,500	15,700	59.92
7.	Songea	20,366	8,680	11,686	57.38
8.	Morogoro	87,335	37,509	49,826	57.05
9.	Mpanda	12,234	5,375	6,859	56.07
10.	Sumbawanga	27,890	13,450	14,440	52.00
11.	Masasi Nachingwea	14,934	7,299	7,635	51.12
12.	Karatu	8,454	4,227	4,227	50.00
13.	Mtewara	25,200	12,700	12,500	49.60
14.	Dodoma	133,400	68,400	65,000	49.00
15.	Mwanza	160,000	84,407	75,593	47.25
16.	Kyela Kasumulu	9,301	5,023	4,279	46.00
17.	Arusha	127,392	68,920	58,472	45.90
18.	Moshi	73,246	40,409	32,837	44.83
19.	Kigoma Ujiji	22,747	12,824	9,923	43.62
20.	Lindi	7,270	4,186	3,084	42.42
21.	Ngara	3,000	1,741	1,260	42.00
22.	Tabora	29,519	17,184	12,335	41.79
23.	Mbeya	90,206	53,632	36,574	40.54
24.	Nzega	5,680	3,390	2,290	40.31
25.	Singida	16,179	9,815	6,364	39.33
26.	Kahama	23,000	14,500	8,500	36.96
27.	Tanga	46,544	32,082	14,462	31.07
28.	Geita	7,256	5,220	2,036	28.06
29.	Tukuyu	15,000	10,834	4,166	27.77
30.	Shinyanga	18,833	14,300	4,533	24.07
31.	Iringa	19,000	17,451	1,549	8.15

**Chanzo:** Ripoti za utendaji za mwaka za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira

Ninarudia pendekezo langu la awali kwa Serikali kupitia Wizara ya Maji ihakikishe uwezo wa uzalishaji wa majisafi unaongezwa na usambazaji wa maji unaimarika kwa kutoa fedha zinazohitajika kwa wakati na ufuatiliaji wa karibu wa miradi inayoendelea.

#### 14.2 Kutokuwa na uhakika wa thamani ya fedha kwenye miradi ya maji ya shilingi bilioni 17.29

Katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22, nilitoa taarifa ya ucheleweshaji wa miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam

wa kuchimba visima 20 Kigamboni, hali iliyopelekea ongezeko la gharama la shilingi bilioni 7.97. Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini visima saba tu ndiyo vimekamilika na kutokuwa na uhakika kuhusu umaliziaji wa visima vingine 13 vyenye thamani ya shilingi bilioni 17.2.

Pia, nimebaini tarehe 11 Aprili 2023 Wizara ya Maji iliridhia mapendekezo ya mhandisi mshauri wa kufunga mradi wa kuchimba visima vilivyobaki Kigamboni. Ninahusisha hili na usimamizi duni wa mradi na utendaji duni wa mkandarasi.

Vilevile, nilibainia mradi wa upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa maji katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea ulisitishwa kutokana na mkandarasi kukiuka masharti ya mkataba wakati jumla ya shilingi milioni 94.39 tayari zilikuwa zimetumika kwenye fedha zilizotengwa kwenye mkataba jumla ya shilingi milioni 596.97 na kazi ambazo hazijakamilika zilikadiriwa kuwa shilingi milioni 502.58.

**Ninapendekeza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Songea kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kufanya uchambuzi wa kina wa uwezekano wa utekelezaji wa miradi uliobaki na kuhakikisha usimamizi wa mradi wa kutosha kwa ajili ya miradi ya baadaye.**

#### 14.3 Ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi ya maji

Katika utekelezaji wa miradi ya maji kwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, Wizara hutoa mwongozo na ufadhilli kupitia bajeti ya Serikali, na mamlaka za maji hutumia mapato ya ndani na fedha za wahisani kutekeleza miradi ya maendeleo ya maji. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu katika Mamlaka za Maji za Dar es Salaam, Karatu, Kahama Shinyanga, Njombe, Songea na Lindi kama inavyobainishwa katika aya zinazofuata;

Uhakiki wangu wa miradi inayoendelea katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam ulibaini ucheleweshaji katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa. Mradi wa upanuzi wa laini ya Ubungo Msakusi Kaskazini, ikijumuisha ukanda wa kitopeni na ukanda wa Mshikamano haikutekelezwa kwa asilimia 53 na 69 mtawalia. Katika ukanda wa Magomeni miradi 37 ya upanuzi iliyopangwa haikufanyika na katika miradi 36 ya kubadilisha mitambo, ni miradi mitatu tu iliweza

kukamilika. Katika eneo la Kigamboni kulikuwa na miradi mitatu ya upanuzi wa laini, ambapo miradi miwili haikutekelezwa na mmoja katika eneo la Magogoni haukuwa umeteketelezwa kwa asilimia 73. Pia katika eneo la Makongo kati ya miradi 26 iliyopangwa ni miradi nane tu ndiyo imeanza.

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu nilibaini ujenzi wa mradi wa Bwawani ulicheleweshwa na kutokutekelezwa kwa asilimia 30.

Mamlaka ya Majisafi Kahama Shinyanga nilibaini ucheleweshaji wa miezi minne kwenye kuanzisha mradi wa upanuzi wa bomba la kusambaza maji kutoka skimu ya Maji ya Ziwa Viktoria hadi miji ya Malampaka na Malya.

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Lindi, kulikuwa na mradi wa Angaza wenye thamani ya shilingi bilioni 1.14 ambapo nilibaini mkandarasi alilipwa malipo ya awali shilingi milioni 170.75. Hata hivyo ujenzi wa mradi ulisitishwa kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya shilingi milioni 287.47 kwa zaidi ya miezi mitatu, wakati mradi huo ulikuwa umefikia asilimia 35. Pia katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe nilibaini ucheleweshaji wa zaidi ya miezi nane katika kuanzisha mradi wa ujenzi wa mitambo ya majitaka katika mji wa Ngalanga wenye thamani ya shilingi bilioni 1.24.

Pia katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea nilibaini kuwa ujenzi wa mradi wa maji wa Subira ulicheleweshwa kwa zaidi ya miezi mitatu hadi kukamilika kwa thamani ya mkataba wa shilingi bilioni 1.17.

Ninahusisha upungufu huu na ucheleweshaji wa fedha kutoka Wizara ya Maji. Ucheleweshaji huo unakwamisha kufikiwa kwa lengo lilokusudiwa la kusambaza majisafi na usafi wa mazingira kwa jamii.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji iingilie kati kuhakikisha miradi yote ya maji inakamilika ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi.** Pia, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zinapaswa kuhakikisha kuwa miradi inaanzishwa kwa vyanzo vya uhakika vya fedha na uthibitisho wa dhana za mradi ili kuepusha ucheleweshaji kwa siku zijazo.

#### 14.4 Mwendelezo wa hasara kutokana na upotevu wa maji shilingi bilioni 162.25

Upotevu wa maji ni kipimo muhimu cha ufanisi na utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kwa kutathmini kiasi cha maji kinachozalishwa na kununuliwa lakini hypotea kabla ya kufikia wateja. Upotevu wa maji huwasilishwa kwa asilimia na hutathminiwa kwa kutoa kiasi cha maji kilichouzwa kwa watumiaji kutoka kwenye jumla ya kiasi kilichozalishwa au kununuliwa. Sababu zinazochangia upotevu wa maji ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ambayo ni ya zamani inayosababisha uvujaji wa maji na uunganishaji haramu unaosababisha kupotea kwa mapato. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji imeweka kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika kuwa kisizidi asilimia 20.

Kwa miaka minne mfululizo, nimekuwa nikitoa taarifa kuhusu suala hili na kupendekeza Serikali kuingilia kati na kuititia upya miundombinu ya maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, pamoja na kupanga mikakati ya kuboresha usimamizi wa miundombinu ili kupunguza upotevu wa maji. Hata hivyo, tatizo limeongezeka katika mwaka huu wa fedha. Nilibaini mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 30 (23 kwa mwaka 2021/22) zina upotevu wa maji zaidi ya kiwango cha juu cha asilimia 20 kinachoweza kuvumilika, ambapo kiwango cha upotevu kilianzia asilimia 21 mpaka asilimia 65 (**Jedwali Na. 35**). Jumla ya hasara kwa mwaka 2022/23 ilikuwa sawa na shilingi bilioni 162.25, ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 162.14 kwa mwaka 2021/22.

**Jedwali Na. 35: Upotevu wa Maji**

Na.	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	2019/20 (Asilimia)	2020/21 (Asilimia)	2021/22 (Asilimia)	2022/23 (Asilimia))
1.	Kigoma	30	30	30	65
2.	Ngara	45	40	40	48
3.	MtWARA	21	26	29	48
4.	Arusha	48	50	37	46
5.	Korogwe	42	41	38	45
6.	Karatu	40	40	40	45
7.	Dar es Salaam	41	39	39	42
8.	Kyela Kasumulu				41
9.	Njombe	29	29	39	39
10.	Bukoba	44	44	43	39
11.	Morogoro	43	44	40	39
12.	Musoma	50	43	40	38
13.	Sumbawanga	31	31	31	35
14.	Mwanza	37	37	36	34
15.	Tanga	36	33	31	34

Na.	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	2019/20 (Asilimia)	2020/21 (Asilimia)	2021/22 (Asilimia)	2022/23 (Asilimia)
16.	Lindi	33	37	35	33
17.	Makambako	44	45	44	32
18.	Singida	33	31	29	31
19.	Bariadi	28	28	28	31
20.	Geita	38	38	28	30
21.	Namtumbo				29
22.	Dodoma	26	34.7	33.6	28
23.	Mbeya	30	28	28	28
24.	Tukuyu	26	35	34	28
25.	Masasi Nachingwea	24	23	20	26
26.	Iringa	24	24	23	25
27.	Moshi	22	20	27	23
28.	Babati	32	31	25	23
29.	Songea	23	21	21	22
30.	Shinyanga	23	21	24	21

Chanzo: Ripoti za utendaji za mwaka za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira

Ninarudia pedekezo langu kwa Serikali kuingilia kati kwa kupitia upya miundombinu ya maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na kuandaa mipango ya kuboresha usimamizi wa miundombinu na kupunguza upotevu wa maji.

#### 14.5 Kutokuwapo kwa miundombinu ya majitaka

Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira wanalahimika kutoa huduma za usafi wa mazingira kwa utoaji wa vifaa na huduma zinazofaa kwa ajili ya ukusanyaji na utupaji wa majitaka.Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 12 hazijaanza kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya usafi wa mazingira.

Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zilizochelewa kujenga miundombinu ya majitaka ni Karatu, Makambako, Mtwara, Bariadi, Bukoba, Kahama, Kigoma Ujiji, Korogwe, Kyela, Lindi, Shinyanga, na Babati. Kutokuwapo kwa miundombinu ya majitaka kumesababishwa na matatizo ya kifedha, kwa sababu miradi hiyo inahitaji uwekezaji mkubwa ili kukamilishwa.

Ucheleweshaji huo unakwamisha maendeleo ya wananchi kutokana na ucheleweshaji wa matumizi yenye tija ya huduma za majitaka kwani unahatarisha afya ya jamii ambayo inaweza kusababisha magonjwa na kuhatarisha ustawi wa jamii. Aidha, kutokana na kukosekana kwa huduma za majitaka, mamlaka inakosa mapato kwa ajili ya utoaji wa huduma hizo kwa jamii.

Ninapendekeza mamlaka husika za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kuomba fedha kutoka kwa wafadhili, na/au kutafuta fedha kutoka vyanzo vyatatu ndani ili kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya majitaka unakamilka.

#### 14.6 Ongezeko la madai ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira hadi shilingi bilioni 136.17

Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zinateneleza sera ya mikopo inayotaka ankara kulipwa ndani ya mwezi mmoja na kusitisha huduma kwa wateja ambao hawajalipa ankara kwa zaidi ya siku 90. Hata hivyo, licha ya kuwapo kwa sera hii, mamlaka za maji bado zinakumbana na ongezeko la madeni yanayozidi kipindi cha ukusanyaji madeni kilichowekwa.

Ukaguzi wangu wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 27 ulibaini ongezeko la wadaiwa katika kipindi cha miaka minne kama inayobainishwa kwenye **Jedwali Na. 36**. Mwaka 2022/23 mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zilikuwa zinadai shilingi bilioni 136.17 (2021/22: Shilingi bilioni 126.23) kwa ajili ya utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Serikali kuu, mashirika mengine na wateja binafsi.

Zaidi nilibaini kuwa Mamlaka za maji za Dar es Salaam, Arusha na Mtwara zilikuwa na wateja ambao hawajakatiwa maji na walikuwa na bili ambazo hazijalipiwa za shilingi bilioni 10.87, shilingi milioni 809.2 na shilingi bilioni 1 mtawalia.

Upungufu katika urejeshaji wa deni huathiri ukwasi wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na huweza kusababisha vikwazo vyatatu kifedha katika kukidhi mahitaji mengine ya uendeshaji wa mamlaka.

**Jedwali Na. 36: Deni la mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira**

Na.	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
		Sh. (Milioni)	Sh. (Milioni)	Sh. (Milioni)	Sh. (Milioni)
1.	Dar es Salaam	58,165.64	69,643.53	62,285.22	65,225.88
2.	Kahama-Shinyanga	3,818.42	5,355.51	10,920.76	13,544.38
3.	Dodoma	6,596.58	6,757.49	6,717.27	7,434.28
4.	Mwanza	6,705.41	7,039.29	7,097.50	6,892.95
5.	Arusha	1,714.52	4,040.01	5,446.45	6,432.10
6.	Tanga	5,460.36	5,579.85	5,639.37	6,066.78
7.	Mbeya	5,863.61	6,263.26	5,565.19	5,061.02
8.	Moshi	4,572.02	5,003.53	4,232.85	4,709.95
9.	Tabora	1,971.13	1,930.08	2,058.73	3,082.34
10.	Morogoro	2,748.14	2,832.71	2,954.89	2,512.81

Na.	Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	2019/20 Sh. (Milioni)	2020/21 Sh. (Milioni)	2021/22 Sh (Milioni)	2022/23 Sh. (Milioni)
11.	Iringa	1,492.71	1,815.64	2,145.12	2,137.05
12.	Shinyanga	1,886.69	1,625.01	1,455.15	2,098.81
13.	Kahama	1,552.79	1590.47	1,592.61	1,817.08
14.	Musoma	2,167.94	2,353.91	1,430.22	1,678.85
15.	Songea	1,692.80	1,412.78	1,139.43	1,201.49
16.	Bukoba	768.41	834.27	836.37	1,070.94
17.	Mtwara	1,860.82	1,783.66	842.38	1,002.17
18.	Singida	606.65	706.49	677.31	842.63
19.	Masasi Nachingwea	672.79	587.84	725.14	841.52
20.	Lindi	786.21	776.27	797.71	565.07
21.	Babati	446.52	522.04	522.24	522.02
22.	Karatu	21.41	40.17	54.3	431.01
23.	Sumbawanga	557.84	529.12	466.88	410.05
24.	Njombe	273.8	337.71	334.7	286.45
25.	Geita	105.77	90.44	131.73	130.66
26.	Bariadi	69.97	65.18	92.32	116.47
27.	Ngara	75.03	43.08	63.37	56.11
Jumla		112,653.98	129,559.34	126,225.21	136,170.87

Chanzo: Taarifa za fedha za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira

Ninarudia pendekezo langu kuwa Serikali isaidie mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika kutekeleza hatua madhubuti zaidi za ukusanyaji wa madeni na kuzingatia uwekaji wa mita za maji ya kulipia kabla kwa wateja wenye historia ya madeni ya muda mrefu.

#### 14.7 Ucheleweshaji katika utoaji wa huduma kwa wateja

Aya ya 5.1 (iv) ya mkataba wa huduma kwa mteja inahitaji muunganisho mpya wa maji kufanya ndani ya siku 7 tangu tarehe ya maombi. Hata hivyo, bado nilibaini ucheleweshaji wa uunganishaji ya maji kwa wateja wapya katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira ya Dar es Salaam, Geita, Mwanza na Tanga.

Ucheleweshwaji wa kuunganisha wateja wapya ni kati ya siku tano hadi siku 408 kutoka mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira. Hali hii inahusishwa na uhaba wa vifaa hasa mabomba na mita mpya za maji kwa ajili ya kufanya uunganishaji mpya wa maji. Hali hii inasababisha wateja kutoridhika na kuchelewa kufikia malengo ya Serikali ya kuwapatia wananchi majisafi na salama.

Aidha, pia nilibaini kulikuwa na ucheleweshaji wa utatuzi wa malalamiko ya wateja ndani ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira. Ucheleweshaji huo ulianzia siku nane hadi siku 129 ambapo ni kinyume na mkataba wa huduma kwa wateja unaotaka uchunguzi wa

malalamiko kukamilika na suala hilo kutatuliwa ndani ya siku tano za kazi. Tatizo hili libainika katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira Dar es Salaam na Tanga. Pia katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi, nilibaini mapungufu katika daftari la malalamiko, ambapo halikuwa na usajili mzuri wa malalamiko hayo kuanzia tarehe ya kupokelewa hadi tarehe ya kutatuliwa malalamiko hayo. Hali hii ilisababisha kutokuwapo na ufanisi katika kusimamia malalamiko.

Ninapendekeza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zihakikishe kuna akiba ya kutosha ya mita na vifaa vya kuunganisha maji na hili litafanikiwa kuititia kufanya tathmini za uhakika na ubashiri wa wakati halisi wa mahitaji mapya ya maunganisho ya maji. Pia kuwe na ufuutiliaji wa mkataba wa huduma kwa wateja katika kutatua matatizo ya wateja.

#### **14.8 Kutofanya maboresho ya tozo za maji wanazolipa wateja**

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga nilibaini tozo zinazotumika kuwatoza wateja wa huduma ya majisafi na majitaka kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023 ni bei zilizopitishwa mwaka 2018 na Mamlaka ya Uhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na kuchapishwa mwaka 2021. Pamoja na kuwapo kwa ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo kama vile gharama za kemikali za maji, vitendanishi, mafuta na mabomba kwa wastani wa asilimia 69 hadi kufikia mwaka 2023, bado Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Tanga ilikuwa bado haijapewa idhini kutoka Wizara ya Maji ya kufanya mabadiliko ya tozo mpya.

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga, nilipitia maombi ya tozo mpya ambayo yaliwasilishwa Wizara ya Maji kuititia barua yenye nambari ya kumbukumbu AD.32/45/01G/75 ya tarehe 26 Julai 2021 kwa ajili ya kupata barua ya kutokuwa na pingamizi la utekelezaji wa tozo mpya. Hata hivyo hapakuwa na majibu kutoka Wizara ya Maji kwa muda wa miaka miwili tangu maombi yake yalipowasilishwa tarehe 26 Julai 2021. Kukosekana kwa idhini hiyo kunatokana na kuchelewa kutolewa kwa barua ya kutokuwa na pingamizi na Wizara ya Maji kama inavyotakiwa na kanuni za mamlaka ya udhibiti wa huduma za nishati (Maombi ya Ushuru wa maji na upangaji wa viwango ) ya mwaka 2020.

Kucheleweshwa kwa uidhinishaji wa tozo mpya kunaweza kusababisha upungufu wa kifedha na kushindwa kukidhi gharama za uendeshaji za mamlaka kutokana na mapato yanayokusanywa kuwa madogo ikilinganishwa na gharama ya uendeshaji ambazo ziko juu. Pia Changamoto ya ukwasi inaweza kusababisha kushindwa kufanya matengenezo na uboreshaji wa miundombinu. Hali hii inaweza kusababisha kuzorotesha ubora wa maji na uhakika wa usambazaji wa maji na hatimaye kuathiri uendelevu na ufanisi wa mfumo wa usambazaji wa maji.

Ninapendekeza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za Tanga na Kahama Shinyanga ziwasiliane na Wizara ya Maji kwa ajili ya utekelezaji wa tozo mpya ambazo zinaendana na gharama za uendeshaji ili kuimarisha utoaji wa huduma ya maji kwa jamii.



# SURA YA KUMI NA TANO

## TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU

### 15.0 Utangulizi

Taasisi za elimu ya juu, mafunzo, na utafiti zinajumuisha vyuo vikuu, vyuo vya elimu ya juu, vituo vya utafiti, na taasisi za mafunzo ya ufundi. Taasisi hizi ni nguzo muhimu katika taifa letu kwa; kusambaza maarifa na kukuza maendeleo ya rasilimali watu; kukuza na kuhamasisha ubunifu katika ujasiriamali; kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi; na kukuza ushindani kimataifa.

Ingawa Serikali, kuitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi unaojulikana kama mradi wa HEET ina lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia, na usimamizi wa elimu ya juu; na kusaidia huduma za taasisi hizi kuendana na mahitaji ya soko la ajira, ukaguzi wangu ulibaini mapungufu kadhaa katika utendaji na usimamizi wa taasisi na vituo hivi.

Mapungufu hayo ni: idadi ndogo ya wanafunzi waliojiandikisha; uhaba wa miradi ya utafiti, huduma za ushauri na kozi fupi; miundombini duni; na ukosefu wa nyenzo na vifaa vya kufundishia. Mapungufu hayo nimeyaelezea kwa kina katika aya zifuatazo:-

### 15.1 Upungufu uliobainika katika shughuli za utafiti na ushauri elekezi katika tasihi za kitaaluma

Taasisi ya kitaaluma ya elimu ya juu ina majukumu makuu matatu ya msingi: kufundisha, utafiti, na kutoa huduma za umma na ushauri. Ukaguzi wangu katika kazi za utafiti na ushauri elekezi katika Chuo Kikuu Mzumbe, na Dodoma, pamoja na Chuo cha Bandari nilibaini mapungufu yafuatayo:

**Chuo Kikuu Mzumbe** hakina mfumo wa usimamizi wa utafiti na uchapishaji. Hii ilisababisha kupungua kwa mapato yatokanayo na shughuli za ushauri elekezi kwa shilingi milioni 156.26 kutoka shilingi

milioni 408.85 (Lengo: shilingi milioni 400) katika mwaka 2021/22 hadi shilingi milioni 252.59 (Lengo: shilingi milioni 450) katika mwaka 2022/23. Hali hiyo inasababisha ugumu katika kutambua mwenendo, kupima maendeleo, na kutathmini ufanisi wa shughuli za utafiti na ushauri elekezi. Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa motisha isiyotosheleza inayotolewa kwa washauri kwa mchango wao mkubwa katika shughuli za ushauri elekezi zimekuwa zikichangia kuwakatisha tamaa kwenye kusajili miradi katika chuo.

**Ninapendekeza Chuo Kikuu Mzumbe kuanzisha mfumo wa usimamizi wa utafiti na ushauri elekezi na kutoa motisha toshelezi kwa wahadhiri ili kuboresha shughuli za ushauri.**

**Chuo Kikuu cha Dodoma** hakikutimiza malengo ya kila mwaka ya uchapishaji na utafiti katika ndaki, shule, na taasisi zake. Hii ilitokana na vitengo sita vya kitaaluma kushindwa kutimiza malengo ya uchapishaji ya mwaka ambapo utendaji wake ukiwa kati ya asilimia 0 hadi asilimia 65. (**Tazama Jedwali Na. 37**).

**Jedwali Na. 37: Machapisho halisi dhidi ya lengo kwa mwaka**

Na. .	Ndaki/Shule/Taasi	Malengo	Machapisho	Asilimia ya Uhalsia
1	Shule ya Sheria	20	13	65
2	Chuo cha Sayansi ya Ardhi na Uhndisi	40	18	45
3	Kurugenzi ya Huduma za Maktaba	10	4	40
4	Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo	30	8	27
5	Shule ya Tiba na Meno	70	11	16
6	Taasisi ya Confucius	10	0	0

**Chanzo:** Ripoti ya mwaka 2022/23 ya Kurugenzi ya utafiti, uchapishaji na ushauri elekezi

Pia, vitengo vitano vya taaluma vya Chuo Kikuu cha Dodoma (Shule ya Sheria, Taasisi ya Confucius, Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo, Shule ya Tiba na Meno na Kurugenzi ya Huduma za Maktaba) havikufanya utafiti wowote ikilinganishwa na lengo lao la tafiti moja kwa kila kitengo kwa mwaka 2022/23. Hii ilisababishwa na uhaba wa wahadhiri; hivyo kazi nyingi za ufundishaji kufanya na wahadhiri waandamizi ambao walikuwa na idadi kubwa ya vipindi vya ufundishaji.

Kushindwa kufikia malengo ya utafiti na uchapishaji kunaweza kuharibu sifa ya chuo, na kukifanya kisivutie wanafunzi na wanataaluma watarajiwa. Pia kutokuwa na uwezo wa kufanya utafiti kunaweza kuathiri ubora wa elimu inayotolewa.

Ninapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kitengeneze programu za ushauri na mitandao ya usaidizi ili kuwasaidia watafiti wa fani ya awali katika kuchapisha na kufanya utafiti kwa ufanisi na kutoa motisha kwa kitivo kinachofanya vizuri katika utafiti. Pia kuajiri wafanyakazi zaidi wa kitaaluma ili kupunguza wingi wa kazi za ufundishaji kwa wahadhiri waandamizi ili wawezi kujikita zaidi katika utafiti.

**Chuo cha Bandari:** Aya ya 3.6.1 ya Mwongozo wa Uthibiti Ubora ya mwaka, 2023 inataka chuo kiwe na sera ya utafiti na ushauri elekezi iliyoidhinishwa. Hata hivyo, hadi kipindi cha ukaguzi sera hizo hazikuwapo. Zaidi ya hayo, chuo kilifanikiwa kukamilisha tafiti nne kati ya tano zilizopangwa, lakini hakuna tafiti iliyochapishwa. Hii inamaanisha kuwa maarifa hayo hayajasambazwa kwa jamii. Pia, hii inaashiria kuwa shughuli za utafiti zinapewa kipaumbele cha chini. Hivyo, malengo ya mabadiliko yaliyotarajiwa kupitia kwa matokeo ya utafiti hayakufikiwa.

Ninapendekeza Chuo cha Bandari kihakikishe kuwa sera ya utafiti na ushauri elekezi inaanadaliwe na kutumika. Pia, kuhakikisha tafiti zilizofanywa zinachapishwa ili kuleta mabadiliko katika nyanja za huduma za bahari na bandari.

## 15.2 Upungufu katika zana za kufundishia na miundombinu katika vyuo vikuu na taasisi za mafunzo

### 15.2.1 Upungufu wa miundombinu shirikishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine

Katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine nilibaini kuwa, vyumba vyaa madarasa hasa nya zamani na maktaba, havitoi fursa kwa watu wenye ulemavu kwa vile hakuna njia za wao kupita, na kutokuwepo kwa vyoo nya watu wenye ulemavu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Watu wenye Mahitaji Maalumu ya mwaka 2010. Kifungu cha 35 (1) cha sheria hiyo kinamtaka Waziri husika kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya majengo, na kwa kadri inavyowezekana, kuhakikisha kuwa kila jengo la umma na majengo mengine yanayotoa huduma kwa umma yanafikiwa na watu wote wenye ulemavu. Miundombinu duni kwa wa watu wenye ulemavu husababisha ubaguzi katika elimu, kwani haitoi nafasi sawa kwa watumishi na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kihakikishe miundombinu yake ya mazingira ya chuo, kama vile madarasa, maktaba na maabara, yana vifaa zinavyoweza kutumika na watu wenye mahitaji maalumu. Hii itakuza elimu-jumuishi na kurahisisha watu wenye mahitaji maalumu kutoka sehemu moja hadi nyingine.

### 15.2.2 Uhaba wa maji kwa asilimia 49 katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma kina wastani wa jumla ya watu 38,203. Idadi hii inajumuisha watumishi na wanafunzi. Kuna upungufu wa maji wa lita 1,123,600 kwa siku, sawa na asilimia 49 ya makadirio ya mahitaji. Hii inachangiwa na ukosefu wa vyanzo vya maji katika chuo hicho. Upungufu huu unapelekea mazingira mabaya ya kuishi kwa wanafunzi, ongezeko la hatari za magonjwa kwa jamii nzima na huchangia kuzorota kwa miundombinu na mazingira ya chuo.

Pamoja na uhaba huo wa majisafi, nilibaini Chuo Kikuu cha Dodoma kililipa shilingi milioni 148.1 katika kipindi cha mwaka 2021/22 na 2022/23 kwa ajili ya ankara za umeme kwa niaba ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma kwaajili ya kuendesha mitambo ya uzalishaji na usambazaji maji kama vile pampu za kuvutia maji kutoka kwenye visima vilivypopo katika eneo la chuo bila ya kuwa na makubaliano juu ya malipo hayo.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kitafute vyanzo vingine vya majisafi kama vile visima, kuvuna maji ya mvua, na kuwasiliana na mamlaka zote zinazohusika kama vile Wizara ya Maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma ili kuimarisha upatikanaji wa maji chuoni. Pia, Chuo kiingie makubaliano rasmi au kandarasi ambayo inaeleza kwa uwazi masharti na wajibu wa pande zote mbili kuhusu gharama za uendeshaji wa kituo cha uzalishaji na usambazaji maji katika eneo la Chuo.

### 15.2.3 Upungufu wa zana za mafunzo katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti

Ukaguzi wangu ulibaini uhaba wa zana za ufundi stadi na miundombinu ya kujifunzia katika Kituo cha Huduma ya Mafunzo ya Ufundisti cha VETA Mkao wa Manyara. Baadhi ya upungufu huo ni: ukosefu wa vyumba vya madarasa na mashine za kupigia chapa kwa kozi ya uhazili; uhaba wa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wa ngazi ya 3 ya kozi ya “Agromechanics” inayoendana na mitaala ya sasa, ukosefu wa karakana

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

sahihi kwa wanafunzi wa magari, na madarasa madogo kwa maktaba ya sayansi. Pia, katika Kituo cha Huduma ya Mafunzo ya Ufundis Stadi Mkao wa Mbeya kuna uhaba wa mashine za kuchanganya saruji, kufyatua tofali, kupimia pembe mlalo na wima kwenye karakana ya uashi na ufyatuaji matofali, ukosefu wa mashine za kisasa za uchomeleaji wa gesi na ukosefu wa mashine ya kuchimba mashimo katika uchomeleaji na utengenezaji wa vyuma katika karakana za mafunzo.

Uwepo wa miundombinu, zana na vifaa vya elimu duni kumesababishwa na ufinyu wa bajeti. Iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa, upungufu huo utaathiri ubora na viwango vya elimu yetu kutokana na wanafunzi kushindwa kufanya mazoezi ya vitendo kwa kiwango na muda unaotakiwa ili kuimarisha uwezo wao wa kutenda kazi baada ya kumaliza chuo.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi ihakikishe kuna vitendea kazi vya kutosha katika karakana za mafunzo ili kuzalisha nguvukazi inayokidhi mahitaji ya ndani.**

### 15.2.4 Upungufu wa vifaa vya maktaba katika vymo vikuu na taasisi zingine za kitaaluma

Maktaba katika vymo vikuu na taasisi zinginze za kitaaluma ni muhimu zaidi ili kuwezesha usomaji, ufundishaji na utafiti. Maktaba hutoa mazingira tulivu na yanayofaa kwa kusoma, kufanya utafiti, na kupata vitendea kazi kama vile vitabu vya kiada, nyenzo za marejeleo, nakala za wasomi, na kanzidata. Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa vymo vikuu na taasisi zingine za kitaaluma nilibaini upungufu ufuatao:

**Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam** nilibaini kuwa hakuna nafasi ya kutosha ya maktaba, nafasi iliyopo inauwezo wa kutosheleza wanafunzi 100 tu kati ya takribani wanafunzi 3,000 waliopo kwa sasa. Pia, maabaraya kompyuta ni ndogo na inauwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kati ya takribani wanafunzi 3,000 waliopo. Zaidi ya hayo, chuo kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vitabu vya kitaaluma ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wa maktaba. Hii inachangiwa na uhaba wa fedha. Ukosefu wa vifaa vya maktaba unaweza kusababisha mazingira magumu ya usomaji kwa wanafunzi.

**Ninapendekeza Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam**, kiweke juhudizaidi ili kuhakikisha kuwa maktaba ya chuo ina vifaa vya kutosha ili kuongeza ufanisi wa kazi, ukusanyaji na usambazaji wa taarifa kwa

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

wanafunzi/umma na kudumisha imani kwa umma katika huduma zinazotolewa na chuo. Chuo kiongeze ukubwa wa maktaba kwa kujenga maktaba mpya. Pia, kijiandikishe kwenye maktaba ya mtandaoni kwa kutengeneza tovuti za vitabu na majarida ya kielektroniki kama vile Z-Library, na Library Genesis. Hii itasaidia wanafunzi kupata vitabu vya kitaaluma.

**Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini** niliona uhaba wa nafasi ya kusomea katika maktaba, mazingira yasiyofaa, na tatizo hili linaonekana zaidi katika vipindi vya wiki za maandalizi ya mitihani. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa kuna vitabu vichache vya kiada, muunganisho hafifu wa intaneti na kompyuta katika maabara ya kompyuta ambamo mlikuwa na kompyuta tatu tu, wakati mahitaji yalikuwa 60; hivyo kuwa na upungufu mkubwa wa kompyuta 57 (sawa na asilimia 95). Hii inasababishwa na kuchelewa kukamilika kwa jengo la maktaba pamoja na kutokuwapo kwa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Uhaba wa kompyuta na nafasi ya maktaba huathiri usomaji na ufaulu wa wanafunzi.

Ninapendekeza Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, kihakikishe kuna vifaa vya kutosha vinavyohitajika katika maktaba kama vile vitabu vya kiada, mtandao wa uhakika, kompyuta na kuongeza ukubwa wa maktaba, ili kurahisisha mafunzo ndani ya chuo.

**Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi** nilibaini upungufu mkubwa wa kiutendaji wa mfumo wa kupambana na wizi na upotevu wa vitabu katika maktaba. Baadhi ya vitabu viliyojaribiwa katika mfumo wa udhibiti vitabu “Sentry”, mfumo huo ulishindwa kupiga kengele ya tahadhari. Hii inaonesha kuwa usalama wa vitabu ni mdogo na kuwa kwenye hatari ya upotevu. Kwa kuongezea, skana ya vitabu kwa ajili ya kutambua vitabu haikuwa inafanya kazi. Hii inafanya mfumo mzima kuwa batili. Zaidi ya hayo, mapitio ya kazi za kila siku za maktaba yalibaini kutofuatwa kwa kifungu cha 6.7.1 cha Kanuni za Vitabu na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi za mwaka 2015. Faini ambayo ni shilingi 500 kwa siku kwa kila siku hazikutozwa kwa vitabu viliyochelewa. Masuala haya kwa pamoja yanaonesha usalama hafifu wa vitabu na usimamizi usioridhisha wa kifedha katika maktaba. Hali hii inahitaji mabadiliko na uangalizi mzuri wa haraka ili kuhakikisha usalama na mapato katika maktaba.

Hali hii inachangiwa na kutokuwapo kwa ufuutiliaji mzuri wa utendaji wa mifumo ya maktaba na kushughulikia upungufu unaobainika kwa

wakati. Kuna uwezekano wa kupoteza vitabu bila kugunduliwa na kuchelewa kurudishwa kwa vitabu bila kujulikana na kupoteza mapato.

**Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kihakikishe kinakuwa na mfumo mzuri wa kudhibiti upotetu wa vitabu kwenye maktaba.**

### 15.3 Kutokuwa na ufanisi katika usimamizi wa mafunzo

#### 15.3.1 Kushindwa kufikia malengo ya idadi ya udahili wa wanafunzi wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu

Nilibaini kuwa kuna upungufu wa idadi ya wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu (Jedwali Na. 38). Kutofikiwa kwa lengo la uandikishaji wanafunzi kunasababishwa na uhaba wa vitendea kazi, wakiwemo walimu, miundombinu, vifaa vya kazi, utangazaji hafifu wa kozi zinazotolewa na vyuo, pamoja na idadi ndogo ya wanafunzi wanaopata mikopo ya elimu ya juu kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Kwa mfano katika mwaka huu wa ukaguzi, nilibaini kuwa ni asilimia 83 tu ya wanafunzi wapya walipata ufadhilli wa elimu ya juu kuititia bodi ya mikopo kwa mwaka wa fedha wa 2022/23. Jumla ya wanafunzi wapya waliopangiwa mikopo walikuwa 73,315 tu kati ya wanafunzi 88,142 waliohitimu. Hali hii inaathiri mapato ya ndani na kushindwa kufikia kiwango kilichotarajiwa na umma. Kwa maoni yangu wanafunzi wanaostahiki ambao hawakupokea mikopo wanaweza kukosa kumudu elimu ya juu, hivyo kuwazuia kupata elimu na uwezekano wa kuathiri matarajio yao ya baadaye.

**Jedwali Na. 38: Upungufu wa udahili wa wanafunzi**

Na.	Taasisi	Malengo	Uhalisia	Tofauti	Tofauti katika asilimia
1	Mamlaka ya Elimu ya Ufundini na Mafunzo ya Ufundini Stadi	100,000	69,347	30,653	31
2	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	5,200	3,763	1,437	28
3	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	7,709	5,534	2,175	28
4	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	6,917	5,177	1,740	25
5	Chuo Kikuu Mzumbe	6,692	5,055	1,637	24
6	Chuo cha Ufundini Arusha	5,643	4,276	1,367	24
7	Chuo Kikuu Ardhi	8,048	6,081	1,967	24
8	Chuo Kikuu cha Dodoma	40,000	34,100	5,900	15
9	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini	16,663	14,422	2,241	13
10	Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkawawa	6,276	5,543	733	11

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

Na.	Taasisi	Malengo	Uhalisia	Tofauti	Tofauti katika asilimia
11	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	2,002	1,782	220	11
12	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	6,546	5,883	663	10

**Chanzo:** Ripoti ya Takwimu; Mpango mkakati; na Data ya Usajili wa Mwaka wa Sasa, Mkataba wa Utendaji na Hazina

Ninapendekeza taasisi za elimu ya juu zihakikishe malengo yote ya uandikishaji yaliyopangwa yanatekelezwa kwa kuboresha miundombinu, kuongeza idadi ya watumishi wa kitaaluma. Aidha, napendekeza Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo itaongeza wanufaika wa mikopo na udahili.

### 15.3.2 Kuchelewa kuzindua programu zilizoidhinishwa na kutoidhinishwa kwa programu baada ya kumalizika kwa muda wake wa awali

Nilibaini upungufu mbalimbali katika kuzindua programu zilizoidhinishwa na programu zisizoidhinishwa baada ya kumaliza kwa muda wake wa awali kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 39.

**Jedwali Na. 39: Kuchelewa kuzinduliwa kwa programu zilizoidhinishwa**

Na.	Taasisi	Idadi ya programu	Hali
1	Chuo Kikuu cha Dodoma	8	Chuo kilikuwa na programu ambazo zimepata ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania lakini bado haijaanza kutolewa kutokana na uhaba wa watumishi
2	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	64	Kutopata ithibati mpya kwa programu zilizoisha muda wake kuanzia mwaka 1 hadi miaka 8
3	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Programu zote	Kampasi ya Mafunzo ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima tawi la Mwanza haina ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi .

**Chanzo:** Ripoti za kurugenzi ya shahada ya awali na uzamili

Ucheleweshaji huo unaweza kuzuia wanafunzi wenyewe nia ya kujiunga na programu hizi, kuaathiri mwelekeo wa udahili, na kusababisha kutotambuliwa kwa wanafunzi wanaohitimu. Yote haya yanaweza kusababisha wahitimu kukosa nafasi za kazi kwa sababu ya kusoma kozi zisizoidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Pia, huweza kuathiri ubora wa utendaji wa taasisi ya elimu ya juu.

Ninapendekeza taasisi za elimu ya juu zihakikisha programu zote zinaidhinishwa na kuanzishwa kwa wakati. Pia, zinapaswa kuhakikisha kuwa programu zote zinazotolewa zimeidhinishwa kwa mujibu wa Viwango na Miongozo ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ya mwaka 2019. Zaidi ya hayo, zihakikisha zinazingatia mahitaji yote ya ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi na Mafunzo ya Ufundsi kwa mujibu wa Kanuni za Ithibati na Utambuzi wa Taasisi za Ufundsi za mwaka 2002 ili kuruhusu uthibitishwaji kamili wa vituo kama vile Kituo cha Mwanza kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

#### **15.3.3 Kuchelewa kwa mapitio ya mitaala 13 ya wahitimu wa ngazi ya I, II, na III katika Chuo cha Ufundsi Arusha**

Ukaguzi wa mitaala ya Chuo cha Ufundsi Arusha ulibaini ucheleweshaji mkubwa wa mapitio ya mitaala. Mitaala 13 haikupitiwa kwa miaka 7 hadi 10 kufikia tarehe 30 Juni 2023, kinyume na sheria ya mapitio kila baada ya miaka 5. Hii ilichangiwa na ukosefu wa usimamizi kutoka Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi. Mitaala hii iliyopitwa na wakati inaathiri ubora wa elimu kwa kushindwa kuendana na maendeleo ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira.

Ninapendekeza Chuo cha Ufundsi Arusha kihakikishe mitaala inapitiwa kwa wakati ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia kwa kulifuatilia kwa karibu Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundsi ili kuidhinishwa.

#### **15.3.4 Kazi za Uhakiki wa Ubora hazijafanyika katika shughuli za kijamii katika Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

Kitengo cha Uhakiki Ubora cha Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilianzishwa ili kutoa huduma za ushauri kuhusu masuala ya uhakiki wa ubora kwa ajili ya kuimarisha ufanisi wa shughuli zake za msingi za ufundishaji, utendaji wa utafiti, mafunzo ya utafiti, ushauri na usimamizi wa jumla katika chuo.

Ukaguzi wangu uligundua ukosefu wa uhakiki wa ubora katika huduma za kijamii na shughuli za utawala. Hii inasababishwa na kukosekana kwa mpangokazi wa uhakiki wa ubora kila mwaka. Hii inaleta wasiwasi kuhusu viwango vya ubora wa elimu inayotolewa na chuo, na huenda ikaathiri vibaya huduma zinazotolewa.

Ninapendekeza Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kiimarishe huduma za uhakiki wa ubora na tathmini ya ubora itakayofanywa kwa kazi zote za chuo.

### **15.3.5 Usimamizi duni wa mchakato wa tathmini katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

Ukaguzi wangu wa ripoti za tathmini ya matokea ya mtihani uliofanywa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yalionesha "ukosefu wa uwazi" katika karatasi nyingi za mitihani. Jambo hili lilijitokeza kama dosari kubwa iliyosababishwa na kukosekana kwa miongozo ya kusahihisha. Tathmini ya usahihi wa usahihishaji ilifanywa kwenye karatasi za matawi ya Dar es Salaam na Morogoro. Tathmini hiyo ilionesha kuwapo kwa makosa ya usahihishaji ya asilimia 6.1 (tawi la Dar es Salaam) na asilimia 26.4 (tawi la Morogoro)

Hii ilichangiwa na ufuatiliaji usiofaa wa shughuli za upimaji wa wanafunzi, ukosefu wa miongozo inayofaa ya upangaji na uwekaji alama za mitihani, pamoja na ulegevu wa utekelezaji wa kanuni za upimaji. Usimamizi usiofaa wa mchakato wa tathmini una athari hasi kwenye ubora wa kitaaluma na ubora wa mhitimu ambayo inaweza kuharibu sifa ya taasisi husika.

Ninapendekeza Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima iandae na kufuata miongozo ya kitaasisi ya kuandaa mitihani, na mwongozo wa kusahihisha mitihani, kuhamasisha wanataluma juu ya umuhimu wa ubora na uhakikisho wa ubora katika shughuli za kitaaluma katika vituo vyote. Pia, kuimarisha kitengo cha udhibiti ubora kwa kuendelea kuwajengea uwezo na kufanya kazi zake kwa ufanisi.

### **15.3.6 Kutokuwapo kwa sera ya kuendesha programu za masafa katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

Nilibaini kuwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima haina sera na miongozo ya kusimamia programu za mafunzo ya masafa. Hii ilichangiwa na uelewa duni, kutoona umuhimu wa udhibiti na ukosefu wa kipaumbele cha sera ya elimu ya masafa. Kutokuwapo kwa sera na miongozo ya jumla kwa elimu za masafa kunaweza kusababisha usimamizi usiofaa wa utekelezaji wa programu katika vituo tofauti vyta Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Hii inaweza kudhoofisha ubora wa utoaji wa programu, hivyo kuharibu taswira ya taasisi.

Ninapendekeza kuwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima iandae na kutekeleza "Sera na miongozo ya mafunzo ya masafa" ambayo inabainisha malengo ya kimkakati, kanuni na taratibu zinazohitajika katika kuendesha programu za masafa. Pia, ihakikishe kunakuwa na usimamizi thabiti wa programu ili kuendana na mkakati wa jumla wa taasisi.

**15.3.7 Uendelevu hafifu wa mfuko wa maendeleo ya ujuzi katika kutoa ruzuku kwa vijana walio katika mazingira magumu katika Mamlaka ya Elimu Tanzania**

Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitumia fedha za maendeleo ya ujuzi kutoa ruzuku kwa vijana walio katika mazingira magumu kwa mafunzo ya muda mfupi katika.

Tathmini yangu ya mpango wa mafunzo kuititia fedha za mfuko wa maendeleo ya ujuzi kwa vijana walio katika mazingira magumu kuhusu ufanisi wake wa muda mrefu ilibainisha kuna upungufu wa mbinu za kuwasaidia wanafunzi kujihusisha na shughuli za kiuchumi wanaporejea kwenye jamii zao. Hii inatokana na kutokuwa na njia njema ambayo inaweza kuwanufaisha vijana walio katika mazingira magumu baada ya kuhitimu. Ukosefu huu wa usaidizi baada ya mafunzo unazuia uwezo wao wa kutumia ujuzi wao walioupata na kukidhi mahitaji yao ya sasa na baadaye ambalo lilikuwa lengo la Serikali.

Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu Tanzania ichukue hatua za kkusanya rasilimali kutoka kwa wadau na Serikali ili kuboresha uendelevu wa ruzuku kwa vijana walio katika mazingira magumu na kutoa msaada baada ya mafunzo ili kuongeza na kutumia ujuzi wao walioupata.

**15.3.8 Uwiano usiotosheleza baina ya wahadhiri na wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma**

Mapitio yangu ya lkama na Mwongozo wa Elimu ya Chuo Kikuu cha Dodoma yaligundua kuwa kuna uwiano usiotosha wa wahadhiri ikilinganishwa na wanafunzi katika vitengo vitatu vya kitaaluma kati ya vitengo 11 vya kitaaluma ambavyo ni Ndaki ya Elimu, Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo na Shule ya Uugazi na Afya ya Umma (1.50: 1.79, 1.50:1.59, na 1.25: 1:34 mtawalia).

Ukaguzi ulibaini ubaba wa wakufunzi wa kudumu katika programu saba za Shule ya Uugazi na Afya ya Umma. Programu hizi zinategemea sana wafanyakazi wa muda, jambo ambalo linasababishwa na ubaba wa wafanyakazi na uwiano usiofaa wa wahadhiri na wanafunzi. Hali hii inaweza kuathiri vibaya ubora wa elimu kwa kupunguza muda wa wahadhiri kufanya kazi za kitaaluma kama vile utafiti na uchapishaji. Zaidi ya hayo, mzigo mkubwa wa ufundishaji kwa wahadhiri unaweza kuathiri ufanisi wao na ubora wa ufundishaji. .

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kitumie wahadhiri wa mikataba: hivyo kupunguza mzigo wa kazi kwa wahadhiri wa kudumu waliopo, hasa wahadhiri waandamizi ambao watapata muda zaidi wa kufanya kazi za utafiti na ushauri. Pia, wawasiliane na Serikali ili kupata watumishi wa kudumu.

### 15.4 Utendaji duni wa taasisi za kitaaluma

#### 15.4.1 Kutofanya vizuri kwa shamba la biashara la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine

Kifungu cha 5.1.1 cha Sera ya Maendeleo ya Mashamba ya mwaka, 2006 kinataka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kuwa na shamba la biashara ambalo litakuwa kitovu cha ubora wa kilimo, kuongeza kipato katika biashara za kilimo, na utoaji wa mafunzo kwa ajili ya ujuzi wa vitendo na utafiti na kuwa mfano mzuri kwa umma.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kuna utendaji hafifu katika shamba la biashara la mazao ya kilimo. Kutokana na kuwa na mashine na vifaa vyta zamani, shamba lilipata hasara ya jumla ya shilingi milioni 227.07 kwa miaka minne mfululizo. Utendaji duni unachangiwa na miundombinu ya kizamani na kutokuwapo kwa mikakati ya kina. Hii inadhoofisha taswira ya chuo kwa wananchi ambao wanatakiwa kujifunza kwa mfano na vitendo wakati shamba linapata hasara.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kitengeneze mikakati na sera za maendeleo ya shamba ambayo yataboresha uzalishaji na mapato katika biashara za kilimo, na kuwa na vifaa vyta mafunzo ya vitendo, utafiti na mafunzo kwa wananchi.

#### 15.4.2 Ucheleweshaji wa utoaji wa vyeti na matokeo ya Taaluma

##### i) Ucheleweshwaji katika kutoa vyeti vyta wahitimu katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti

Nilibaini Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti inatoa vyeti miezi sita baada ya kuchapishwa kwa matokeo ya mitihani na miezi mitatu baada ya tathmini au kufanya mitihani, ambayo kwa jumla huwa miezi tisa. Maoni yangu ni kuwa utoaji wa cheti miezi tisa baada ya tarehe ya tathmini ni muda mrefu sana jambo ambalo linaweza kusababisha wahitimu kukosa fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa ngazi nyingine kutokana na kukosekana cheti cha elimu ya awali. Hii inaweza kuathiri sifa za mamlaka kwa jamii. Hii ilichangiwa na uzembe wa taratibu za kiutawala ndani ya mamlaka katika utoaji wa vyeti.

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi kushughulikia ucheleweshaji huu kwa kupitia upya taratibu za kiutawala zinazohusika katika uandaaji na utoaji wa vyeti, ikiwamo kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa mwaka 2019 ili kupunguza muda wa utoaji wa vyeti.

- ii) **Kucheleweshwa kwa uidhinishaji na uwasilishaji wa matokeo ya stashahada kwenye Mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi Stadi kwa Mafunzo ya Ufundsi Stadi katika Chuo Kikuu cha Dodoma**

Nilipitia Fomu Na.3 (Muhtasari wa jumla wa matokeo) unaotumiwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Stashahada ya Teknolojia ya Habari. Nilibaini kuna ucheleweshaji wa kupakia upya matokeo ya wahitimu 20 katika mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi kwa miaka miwili tangu mwaka wa masomo 2020/21. Hii ilisababishwa na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi kuchelewa kukubali na kutoa kibali cha kuweka tena matokeo ya stashahada yaliyowasilishwa tena na Chuo Kikuu cha Dodoma nje ya muda uliobainishwa. Kwa maoni yangu wahitimu hawa wa Stashahada wanaweza kukosa fursa zaidi za masomo au nafasi za kazi kutokana na kutokuwapo kwa matokeo ya mwisho yaliyoidhinishwa kwa miaka yote miwili.

Ukaguzi wangu pia ulibaini ucheleweshaji mkubwa katika kuwasilisha matokeo ya mwisho ya mwaka wa masomo 2022/23 kwa programu ya stashahada. Matokeo yalipitishwa na Seneti ya Chuo tarehe 25 Agosti 2023, lakini hayakuwasilishwa kwenye mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (NACTVET) hadi tarehe 15 Septemba 2023, baada ya dirisha la maombi kufungwa. Hii ilisababishwa na ratiba ya masomo kwa programu ya stashahada kutoingiliana na kalenda ya NACTVET. Ucheleweshaji huu unaweza kupunguza chaguo la wanafunzi kwa vyuo vya kati na vyuo vikuu na kuwalazimisha kungoja hadi mwaka wa masomo unaofuata.

Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kitathmini uwezekano wa kurekebisha ratiba ya muhula kwa programu zisizo za digrii ili kuhakikisha matokeo ya mwisho yanatolewa na kuidhinishwa kwa wakati na seneti ya chuo. Hii itawawezesha wanafunzi kutuma maombi ya vyuo na programu za chuo kikuu kwa mujibu wa kalenda ya maombi ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Pia, ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kiendelee kufuutilia kwa karibu ili kuweza kupata kibali cha kupakia tena matokeo ya wanafunzi wasio wa

## 15 Tathmini ya utendaji wa taasisi za mafunzo, utafiti na elimu ya juu

shahada katika mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi na Mafunzo ya Ufundsi Stadi.

### 15.4.3 Mbinu duni za ukusanyaji wa mikopo katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Nilibaini Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ina deni la mikopo ya wanafunzi lililoiva la shilingi trilioni 2.10. Hadi tarehe 30 Juni 2023, HESLB imeweza kukusanya shilingi trilioni 1.29 (asilimia 62 ya mikopo yote iliyoiva) tangu mwaka 2006/07. Hii inamaanisha kuwa shilingi trilioni 0.81 (asilimia 38) ya mikopo iliyoiva bado haijakusanya. Ukosefu wa ushirikiano wa mifumo na wadau wa kimkakati unachangia kushindwa kukusanya mikopo hii. Hii inazuia HESLB kutoa mikopo kwa wanafunzi wengine wenye uhitaji. .

Ukaguzi wangu pia ulipitia utendaji wa urejeshaji mikopo. Nilibaini kuwa bodi haina utambulisho wa lazima na wa kutegemewa wa kipekee kwa wanafunzi wanaopokea mikopo na kukosa mfumo shirikishi na wadau wa kimkakati kama utaratibu wa kuwatafuta wanufaika.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inategemea nambari za mitihani ya kidato cha nne ili kubaini wapokeaji wa mikopo. Hata hivyo, mbinu hii haiwezi kufanya kazi ipasavyo baada ya kuhitim, huku wanafunzi wakijiajiri, au kuajiriwa, au kuendelea kusoma zaidi.

Kwa maoni yangu, kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wa mikopo kunahitaji zaidi kuwa na mfumo thabiti na wa jumla wa utambulisho kama Nambari ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA). Utekelezaji wa NIDA kama hitaji la lazima utaiwezesha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuwafuatilia wakopaji ipasavyo na kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa mikopo, na hatimaye kuhakikisha uendelevu wa utoaji mikopo.

**Ninapendekeza uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu uweke mwongozo unaohitaji uwasilishaji wa NIDA kuwa ni lazima kwa waombaji wote wa mikopo wenye umri wa zaidi ya miaka 18. Waombaji walio chini ya umri wa miaka 18 wanapaswa kuwasilisha watakafikisha miaka 18 kwa ajili ya kulipwa awamu za mikopo zinazofuata. Pia, iwatake wanafunzi wanaoendelea au wakopaji waliopo kutoa NIDA zao kabla ya kupohea mikopo zaidi na kuingia makubaliano na wadau wa kimkakati ili kuimarisha ujumuishaji wa mfumo huo.**

#### **15.4.4 Uhakiki hafifu katika ufuutiliaji, uzingatiaji na tathmini kwa Taasisi zilizosajiliwa za Mafunzo ya Ufundi Stadi**

Nilipotia ripoti ya ufuutiliaji na tathmini nilibaini mapungufu katika ufuutiliaji, uzingatiaji wa kanuni, na tathmini kwa taasisi zilizosajiliwa za mafunzo ya ufundi stadi, asilimia 88 (taasisi za mafunzo ya ufundi stadi 1,176 ) chini ya Teknolojia ya Sayansi Shirikishi, Utalii wa Biashara na Mipango na Sayansi Shirikishi za Afya hazikutembelewa kwa ajili ya ufuutiliaji, uzingatiaji na tathmini katika mwaka huo. Baraza liliweza kutembelea asilimia 12 tu (taasisi za mafunzo ya ufundi stadi 162) kati ya taasisi 1338.

Aidha, ukaguzi wangu wa daftari la malalamiko la Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi la 2022/23 ulibaini malalamiko kutoka kwa wanafunzi na wadau wengine kuhusu taasisi za Mafunzo ya Ufundi Stadi ambazo hazijasajiliwa. Hii inatokana na kuwa na idadi ndogo ya wafanyakazi na fedha za kuwezesha ufuutiliaji, uzingatiaji na tathmini ya shughuli.

Maoni yangu ni kuwa ufuutiliaji wa taasisi za Mafunzo ya Ufundi Stadi ni mdogo mno kiasi cha kushindwa kupata uhakikisho wa ubora wa elimu ya kiufundi inayotolewa na taasisi husika. Pia, taasisi ambazo hazijasajiliwa nchini zinaweza kuzalisha nguvukazi isiyi na sifa na ubora wa chini.

**Ninapendekeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na mafunzo ya ufundi Stadi; (a) liingie katika Mkataba wa Makubaliano na vyombo vingine vya Serikali kama Halmashauri na Manispaa, ili kusaidia kutoa taarifa za kuwapo kwa taasisi za mafunzo ya elimu ya ufundi stadi kwenye maeneo yao; (b) liombe watumishi zaidi kutoka Ofisi ya Rais, Menjimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na (c) Kupitia Baraza la Uongozi liwasiliane na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuomba fedha za kusaidia shughuli za utekelezaji kwa kuboresha mgao wa bajeti.**

# SURA YA KUMI NA SITA



## UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO

### 16.0 Utangulizi

Serikali ya Tanzania ilianzisha mamlaka za udhibiti 57 ili kusimamia shughuli zinazohusiana na utoaji wa huduma, uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa. Mamlaka hizi zina wajibu wa kubuni na kutekeleza sera, miongozo, na sheria za udhibiti ili kuweka mazingira ya usawa kwa wadau mbalimbali kufanya kazi kwa ushirikiano katika sekta wanazozisimamia. Katika taarifa zangu za ukaguzi za miaka iliyopita, nilibaini kasoro mbalimbali katika taasisi hizi. Pia, Serikali ina malengo ya kuziunganisha baadhi ya taasisi hizi ili kuongeza ufanisi.

Sura hii imeeleza kwa ufupi mapungufu ya kiudhibiti yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi hizi kwa mwaka wa fedha 2022/23, kama vile kutotosheleza kwa huduma za kiudhibiti na kutotumia mifumo ya kielektroniki kwa ukamilifu ili kuboresha ufanisi wa huduma za udhibiti.

Pia, sura hii imetua mapendekezo ya kuboresha huduma za udhibiti kwa Serikali na taasisi husika. Maeleo ya kina juu ya masuala haya ambayo yanahitaji msukumo wa Serikali ili kuboresha udhibiti yametolewa katika aya zinazofuata.

### 16.1 Kutotumia mifumo ya kielektroniki kwa ukamilifu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za udhibiti

Matumizi na usimamizi wa mifumo ya kielektroniki ni muhimu katika kuweka misingi na ufanisi wa udhibiti ambapo bila hivyo kunakuwa na changamoto za utoaji wa huduma na bidhaa kwa jamii hasa bidhaa na huduma muhimu.

Katika ukaguzi wa mwaka huu wa fedha (2022/23), nimebaini kujirudia kwa mapungufu katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa mamlaka za udhibiti katika utoaji wa huduma za udhibiti kama

ilivyoainishwa na aya ya 16.1 ya taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka 2021/22.

Hali hii inaonesha kuwa mamlaka za udhibiti hazikuchukua hatua za kutosha kurekebisha kasoro zilizobainishwa na hatua za kuboresha kuzuia kasoro hizo zisijirudie ili kuhakikisha kuwapo kwa ufanisi wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma za udhibiti

Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) halitumii mfumo wake wa biashara kutoa taarifa za kukamilika kwa biashara, taarifa za kukamilika kwa oda na taarifa za mabadiliko ya oda. TMX imekuwa ikihifadhi taarifa zake kwenye “MySQL database” ambayo haikidhi vigezo vya kuzuia kughushi. Hii inaiweka TMX katika hatari ya kuwapo kwa taarifa zilizoghushia.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) haitumii mfumo wa Taifa wa petroli na gesi (NPGIS) katika kuhakikisha ufuatwaji wa taratibu za uwasilishaji wa taarifa, hali inayoweza kusababisha ukusanyaji wa taarifa zisizo kamili au zisizo sahihi na kusababisha ufuatiliaji na usimamizi duni katika sekta ya mafuta na gesi.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) haijaweka kwa ukamilifu mifumo ya kielektroniki katika utekelezaji wa majukumu yake muhimu ya usajili wa makandarasi. Kwa mfano, fomu za maombi ya usajili zinajazwa kwa mkono na kuziwasilisha katika ofisi za CRB. Pia, CRB inatumia mfumo wa CIMIS kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya fedha wakati baadhi ya mifumo ya udhibiti wa fedha kama vile maombi ya mikopo ya watumishi na usuluhishi hufanywa nje ya mfumo huo, hali inayoongeza hatari ya kuwapo kwa makosa..

Vilevile, katika mapitio ya taarifa za kagazi zilizofanywa na CRB nilibaini mfumo wa CIMIS unaotumiwa na CRB kusajiri makandarasi, miradi ya ujenzi, na kufutilia taarifa za kagazi za makandarasi haujawezeshwa kutoa taarifa za kina za kagazi zinazofanywa, na haujaunganishwa na mifumo mingine kama vile CMVRS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRERA) kwa ajili ya uhakiki wa usajili wa magari na taarifa za umiliki, mtawalia. Hali inayoathiri ufanisi katika mchakato wa usajili.

Kasoro hizi zinaweza kuchangia kuwapo kwa taarifa zisizo sahihi ama udhaifu katika udhibiti wa taarifa; hivyo kuathiri ufanisi wa utoaji wa huduma za udhibiti.

Ninapendekeza mamlaka za udhibiti kuchukua hatua za kuhakikisha zinatumia mifumo ya kielektroniki kwa ukamilifu ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za udhibiti.

### **16.2 Mamlaka za udhibiti kutokuwa na taratibu thabiti za kudhibiti watu au makampuni yaliyofutiwa usajili**

Mamlaka za Udhibiti zina mamlaka ya kusajili na/au kufuta usajili wa makampuni au watu, katika sekta wanazosizimamia kwa kuzingatia vigezo vya kusajili ama kufuta usajili, mtawalia. Changamoto zinazozikumba Mamlaka za Udhibiti ni namna ya kudhibiti vyeti vya usajili na mienendo ya makampuni au watu waliofutiwa usajili kwa kuwa baada tu ya kufutiwa usajili, makampuni au watu hao wanakuwa hawako chini ya Mamlaka zao.

Kwa kipindi cha hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ilifuta usajili wa makandarasi 510 kutokana na sababu mbalimbali za ukiukwaji wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi ya mwaka 1997. Wakati wa ukaguzi wa taarifa na nyaraka za kumbukumbu za CRB nilibaini kuwa makandarasi waliofutiwa usajili hawakurejesha vyeti vyao vya usajili walivyopewa awali hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023. Hali inayoweza kusababisha jamii kupotoshwa au kudanganywa juu ya uhalali wa vyeti vya usajili vya makandarasi hao, na CRB haina utaratibu wa kuiwezesha kudhibiti mienendo ya makandarasi baada ya kufutiwa usajili.

Katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), nilibaini vituo 12 vya mafuta na utunzaji wa mafuta (Petroleum Retail and Storage Outlets (PRSOS)) ambavyo vimetelekezwa kwa zaidi ya mwaka mmoja bila EWURA kuchukua hatua. Hali hii inaonesha udhaifu katika kuhakikisha uzingatiwaji wa kanuni ya 25(1) (g) na 50(1) (b) ya kanuni za petroli za 2022 na kanuni za petroli (za Uchakataji wa Mafuta Yaliyotumika) za mwaka 2017.

Pia, katika mapitio ya daftari la orodha ya leseni za ujenzi zilizopitishwa na EWURA nilibaini kuwa vibali 101 (asilimia 26) vya ujenzi wa vituo vya mafuta kati ya 393 vilishakwisha muda wake na hakuna hatua zilizochukuliwa na EWURA juu ya vibali hivyo.

Hali hii inaweza kusababisha jamii kuhudumiwa na makampuni au watu ambaeo hawajathibitishwa au wasio na vigezo na ambaeo kuna mashaka juu ya ubora wa kazi zao.

Ninapendekeza mamlaka za udhibiti kuweka na kusimamia hatua za kuilinda na kuiepusha jamii kuhudumiwa na makampuni au watu ambao hawajasajiliwa wala kuthibitishwa.

**16.3 Matumizi hafifu ya tafiti kama nyenzo ya kuainisha na kutathmini mapungufu katika sekta kwa ajili ya kuchukua hatua madhubuti za kiudhibiti**

Kwa kuzingatia sheria zilizoanzisha taasisi, miundo ya taasisi na mipango mikakati ya taasisi, tafiti zimepewa umuhimu mkubwa kwa baadhi ya Mamlaka za Udhibiti katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuwa zinawezesha kupatikana kwa taarifa zenyetushahidi wa kutosha, kutoa nyenzo na ufahamu sahihi katika kuunda kanuni, kufanya tathmini ya vihatarishi, kufuatilia uzingatiwaji wa sheria, kufanya tathmini ya sera, kulinda afya ya jamii, kuwezesha na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa, na kuwezesha kuendana na ukuaji wa teknolojia.

Kinyume na sheria zilizoanzisha taasisi, miundo ya taasisi na mipango mikakati ya taasisi, wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, mamlaka za udhibiti hazifanyi tafiti mara kwa mara ili kufanya tathmini ya hali ya vihatarishi katika udhibiti kwa sasa au baadaye, na kwa ajili ya kuchukua hatua endelevu za kiudhibiti. Kutofanya tafiti kunazinyima mamlaka za udhibiti fursa za kuwa na mikakati thabiti ya kiutafiti ambayo inatattua kwa uhalsia madhaifu halisi ya usimamizi na udhibiti nchini.

Nilibaini kuwa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) haina muongozo wa tafiti wala sera ya tafiti. Pia, haijafanya tafiti zozote kubaini na kutathmini matatizo na changamoto zinazoikabili sekta ya ujenzi nchini kwa makandarasi, mashirika nunuzi na jamii kwa ujumla. Hali hii inaweza kuzuia ufanisi wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi katika kufanya maamuzi yaliyotokana na tafiti, ambayo yangethesha Serikali kuititia CRB kutatta matatizo halisi katika sekta.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inatakiwa, kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya mwaka 2003, kufanya tafiti na uchambuzi wa shughuli za sekta hiyo. Hata hivyo, ingawa jumla ya tafiti mbili zilifanywa kufikia tarehe 30 Juni 2023, athari za mapendekezo ya utafiti hazikufuatiliwa, na sera ya utafiti iliyotumika haikuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Pia, nilibaini TCRA haikuwa na agenda za tafiti, hali inayoweza kuikwamisha mamlaka hiyo katika kujiridhisha na thamani/tija ya kazi za tafiti zilizofanywa, kukosekana kwa ulingano na muongozo katika kufanya

kazi za tafiti, na uwezekano wa kufanya tafiti ambazohaziendani na kazi mama ama malengo ya mamlaka hiyo.

**Ninapendekeza mamlaka za udhibiti kufanya tafiti na kuzitumia kama nyenzo ya kuendelea kusimamia, kuanzisha mbinu mpya, na kuboresha mbinu za udhibiti za sasa.**

#### **16.4 Mapungufu katika usimamizi wa sekta ya nishati**

Sekta ya nishati Tanzania inasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliyochini ya Wizara ya Nishati. Sehemu hii imejikita katika mapungufu yaliyobainika katika kusimamia nishati ya umeme, mafuta na gesi wakati usimamizi wa masuala ya huduma za maji yamezungumziwa katika sura ya 14 ya ripoti hii.

Mfumo wa Taarifa za Leseni (LOIS) ulionesa kuwa kuna jumla ya wafanyabiashara wanne wa mafuta na gesi asilia hadi tarehe 30 Juni 2023, ambapo wawili walikuwa wakitoa huduma ya kuunganisha gesi kwa watumiaji kama vile watumiaji wa majumbani na kwa ajili ya biashara, na walikuwa wakitoza tozo za huduma za uunganishaji.

Wakati wa ukaguzi, nilipitia ripoti ya mwaka ya EWURA ya mwaka 2021/22 ili kutathmini utendaji wa mwaka uliopita ili kuhusianisha na utendaji wa mwaka unaokaguliwa. Mapitio hayo yamebaini kuwa, EWURA ilipokea ripoti iliyoonesha kuwa jumla ya bidhaa za mafuta na gesi za 72,533.56 MMscf zilizalishwa, na jumla ya shilingi bilioni 1,042 zilitozwa na watoa huduma kama tozo za uunganishaji wa gesi asilia, hususani TPDC na PAET, lakini tozo hizo hazikuidhinishwa na EWURA ikiwa ni kinyume na Kanuni ya 20 ya Kanuni za Upangaji Bei ya Petroli na Gesi Asilia za mwaka 2020. Vilevile, hakukuwa na hatua zilizochukuliwa na EWURA dhidi ya watoa huduma hao. Hali hii inaweza kuathiri haki na uwazi katika upangaji wa bei wa soko katika sekta ya gesi asilia.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) haikuwachukulia hatua wazalishaji wadogo 11 (Small Power Producers (SPPs)) kati ya 15 waliopewa leseni na haikuchukua hatua kwa wazalishaji wadogo zaidi 10 (Very Small Power Supplies (VSPPs)) waliosajiliwa, ambao hawakuwasilisha taarifa zao za mwaka kinyume na kanuni za uzalishaji wa umeme za mwaka 2020 ambazo zinawataka wazalishaji hao kuwasilisha taarifa zao za mwaka ndani ya siku 120

baada ya mwaka wa fedha kuisha. Hii inaweza kuathiri uwezo wa EWURA katika kupanga na kukadiria mahitaji ya nishati ya umeme.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) halitekelezi kwa ukamilifu hadidu za rejea za uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta zilizo kwenye makubaliano kati yake na EWURA, ambapo hadidu za rejea 4 kati ya 9 sawa na asilimia 44 hazikutekelezwa. Hali hii inaathiri juhudzi za kuzuia uingizaji wa mafuta yaliyochepushwa na kuingiza katika soko la ndani bidhaa za mafuta za magendo zinazokuwa zinasafirishwa nje ya nchi, hivyo kuzima juhudzi za Serikali za kuzuia ukwepaji wa kodi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Hakuna viwango vya ujenzi wa uuzaji wa rejareja wa mafuta kwa wafanyabiashara wenye angalau vituo vinne kwenye majiji, manispaa au miji ya wilaya kinyume na kanuni ya 7(1)(2)(3) 7(1)(2)(3) ya Kanuni za Petroli za mwaka 2022. Nilibaini kuwa, kwa sasa EWURA haifuatilii uzingatiwaji wa kanuni hii. Hii inaweza kusababisha kutokuwapo kwa usawa wa mgawanyo wa nishati ya mafuta kati ya jamii za mijini na vijijini, kuathiri sekta zingine na kuzuia usawa katika kukuza uchumi wa kikanda.

Jumla ya wauzaji wakubwa wa mafuta na gesi asilia 12 wamepewa leseni za biashara hiyo na walikuwa wakiendelea na biashara hata ilipofika tarehe 30 June 2023. Baada ya kufanya mahojiano na menejimenti ya EWURA na mapitio ya rejista ya leseni, nilibaini kuwa EWURA haivisajili wala kuvifua tilia vituo vya uuzaji rejareja wa mafuta na gesi, pia EWURA hakukagua wala kufanya udhibiti wa vituo hivyo kinyume na kanuni ya 46(1) ya kanuni za petroli za mwaka 2020. Hali hii inaweza kusababisha udhaifu katika usimamizi, utunzaji na usafirishaji wa petoli na gesi asilia na hasa kusababisha majanga kama vile kuvuja kwa mafuta na gesi, moto au milipuko na kuhatarisha usalama wa jamiii.

Aidha, hakuna mkakati ulionzishwa na kuidhishwa wa kusimamia na kuhakikisha kiwango cha chini cha bidhaa za mafuta kinahifadhiwa na wauzaji wa jumla na wauzaji wadogowadogo kinyume na kanuni ya 25(2)(b)(iii) ya Kanuni za Petroli za mwaka 2022. Hali hii inaweza kusababisha baadhi ya wauzaji wenye leseni kutohifadhi kiwango cha kutosha cha mafuta na kusababisha uwezekano wa kuwapo kwa upungufu wa mafuta na kuathili watumiaji.

Ninapendekeza EWURA kwa kushirikiana na Serikali na wadau wengine, kuchukua hatua kwa wakati kuondoa kasoro zote zilizobainishwa.

#### **16.5 Mikataba ya udalali wa ununuzi wa magari yenyenye vifungu vinavyozuia ushindani katika ununuzi wa magari ya Serikali**

Kifungu cha 9(I) cha Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, imezia mtu ye yote kuweka vifungu vyenye lengo la (a) upangaji wa bei mingoni mwa wafanyabiashara (b) wafanyabiashara washindani kuungana na kufanya mgomo wa pamoja; au (c) washitiri kuungana na kupanga namna ya kuomba zabuni.

Katika ukaguzi nilibaini madalali wakubwa watatu (Toyota Tsusho Corporation, African Automotive Trading Limited and Tata Motors Limited) walikuwa na makubaliano maalumu na wasambazaji/watengenezaji watatu wa magari kama ilivyoripotiwa katika taarifa ya uchunguzi ya Tume ya Ushindani (FCC), uchunguzi uliofanywa baada ya Wizara ya Fedha kubaini kasoro hizo na kuagiza kufanyika kwa uchunguzi huo. Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi ya FCC, mikataba hiyo ilikuwa na vipengele vinavyozuia ushindani kinyume na kifungu cha 9 (I) cha Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003. Vifungu hivyo vinazuia watengenezaji wa magari kuuza magari kwa Serikali ya Tanzania bila kuititia kwa madalali hao. Hivyo, Serikali ya Tanzania inalazimika kununua magari kutoka kwa madalali hao kwa kuva vifungu vyenye mikataba hiyo vinawazuia watengenezaji wa magari kuiuzia Serikali moja kwa moja bila wao.

Mikataba hiyo imeingiwa kwa namna ifuatayo;

Kampuni ya Toyota Tsusho Corporation na kampuni ya Hino Motors Limited zina makubaliano maalumu na Toyota Tanzania Limited; kampuni ya African Automotive Trading Limited ina makubaliano na kampuni ya CFAO Motors Limited; na kampuni ya Tata Motors Limited ina makubaliano na kampuni ya Tata African Holdings (Tanzania) limited pamoja na kampuni ya Motor-Hub East African Limited.

Hoja zilizo katika taarifa ya uchunguzi ya FCC imewezesha majadiliano na kuchukuliwa kwa hatua za kusimamisha mikataba hiyo hasa vifungu vinavyozuia ushindani, ili kuiwezesha Serikali kutumia fursa za soko huria katika ununuzi wa magari. Wakati kampuni ya Toyota Tsusho Corporation na Toyota Tanzania Limited wamekubaliana na madai hayo

na kuanza makubaliano ya kusitisha mikataba ama vifungu vya mikataba hiyo; kampuni ya African Automotive Trading Limited na CFAO Motors Tanzania Limited hawajakubaliana na hoja za ripoti ya uchunguzi ya FCC, hali inayoitaka FCC kuendelea na hatua zaidi za kutoa hoja za mwisho na kuchukua hatua.

Mikataba maalumu kama hii inainyima Serikali fursa ya kuokoa fedha kwa kutumia bei za soko huria kununua magari moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji au wasambazaji. Nina mashaka juu ya kasi ndogo ya kukamilika kwa majadiliano na upingaji wa usitishwaji wa mikataba hiyo hali inayozidi kuichelewesha Serikali kuokoa fedha kwa kununua magari kwa bei shindani kutoka katika soko huria.

Ninapendekeza Tume ya Ushindani; (a) longeze kasi katika kukamilisha mambo yaliyobaki katika majadiliano na madalali hao ili kuhakikisha vifungu vya mikataba hiyo vinavyozuia ushindani vinaondolewa ili kuiwezesha Serikali na wanunuaji wengine wa magari kununua magari moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji au wasambazaji wao; na (b) lharakishe kufanya uchunguzi zaidi kwa kampuni ya African Automotive Trading Limited na kampuni ya CFAO Motors Tanzania Limited na taarifa ya mwisho itolewe na kupelekwa kwa madalali hao kwa utekelezaji.



## SURA YA KUMI NA SABA

### UFANISI WA TAASISI ZA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA

#### 17.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia masuala yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi wa ufanisi wa mashirika ya umma katika sekta ya afya, yakijumuisha Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Bohari Kuu ya Dawa, Kiwanda cha Dawa Keko (1997), na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Masuala yaliyobainika ni pamoja na Bohari Kuu ya Dawa kutotimiza mahitaji ya wateja kwa asilimia 24 ya bidhaa 105,646,079, na kukataliwa kwa madai ya Mfuko wa Bima ya Afya yenye thamani ya shilingi bilioni 11.83 yaliyowasilishwa na hospitali za umma. Yafuatayo ni mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi.

#### 17.1 Kuchelewa utoaji wa majibu ya vipimo vyya huduma za maabara katika Hospitali ya Taifa Muhimbili

Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuitia mpango mkakati wake wa mwaka 2022-2027, inalenga kuimarisha huduma zake za kibingwa, uchunguzi na matibabu. Lengo kuu ni kuboresha huduma za kliniki, hususani kwa kupunguza muda wa kuchukua na kufanya kazi vipimo vyote vyaa maabara kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2023.

Maabara ya Patholojia ina jukumu muhimu katika kutoa matokeo ya maabara kwa wakati na usahihi, muhimu kwa wataalamu katika kufanya maamuzi sahihi kwenye shughuli za kliniki, kugundua magonjwa mapema, na kuwa na mipango ya matibabu. Kufikiwa kwa lengo hili kutachangia huduma ya haraka kwa mgonjwa, kuhakikisha utambuzi wa haraka wa magonjwa na kuwekwa kwa mikakati bora ya matibabu.

Baada ya kufanya ukaguzi wa muda uliotumika katika Maabara ya kuchukua vipimo na kutoa majibu, nilibaini ucheleweshaji mkubwa

katika baadhi ya vipimo. Nilifanya ukaguzi wa sampuli za vipimo 50 kutoka kwa vitengo mbalimbali katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023. Kati ya hivyo, vipimo 26 vilichukua muda mrefu zaidi ya uliopangwa, kuanzia saa 4 hadi saa 260, ambapo ni kinyume na muda uliobainishwa kwenye mpango mkakati wa mwaka wa 2022-2027.

Sababu kuu za kuchelewa zilikuwa kuharibika kwa mashine za vipimo bila kuwa na mashine mbadala na upungufu wa vitendanishi. Hali hii inasababisha kuchelewa kwa matokeo ya vipimo; hivyo kuathiri ufanisi wa maabara. Muda mrefu unaotumiwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili kuchukua vipimo na kutoa majibu unazorotesha huduma za afya kwa njia mbalimbali. Wagonjwa wanasubiri muda mrefu, ufanisi wa hospitali unapungua, na wateja wanakuwa katika hali ya kutoridhika.

**Ninapendekeza Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ifanye tathmini ya vifaa vyote vya vipimo vya maabara na mashine na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na mashine za akiba ambazo zinaweza kutumika wakati mashine husika zimeharibika na pale zinapohitaji ukarabati na matengenezo makubwa.**

## **17.2 Vifaatiba 406 vyenye hitilafu vilivyopo Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila**

Ukaguzi wangu wa vifaatiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila umebaini kuwa vifaatiba 406 kati ya 2565 (sawa na asilimia 16) vilibainika havifanyi kazi. Pia hakukuwa na mpango wa matengenezo ya vifaa hivyo.

Ukaguzi wangu ulionesha dosari katika kutekeleza mpango wa matengenezo ya kuzuia vifaatiba kuharibika. Vifaa 60 (asilimia 31) kati ya 192 ndivyo vilivyofanyiwa matengenezo yanayotakiwa, kutokana na ukosefu wa fedha za kufanya matengenezo. Hii inaweza kuharibu vifaa mapema na kuongeza gharama za ukarabati au uagizwaji.

Vifaatiba visivyofanya kazi vinaathiri utoaji wa huduma kwa wagonjwa kwa kuchelewa kutoa huduma, hivyo kuhatarisha afya za wagonjwa. Kuendelea kukarabati au kubadilisha vifaa visivyofanya kazi kunaweza kuwa na gharama kubwa. Vifaa vyenye kasoro vinaweza kupunguza kasi ya utendaji kazi wa kitabibu, kuongeza muda wa kusubiri kwa mgonjwa na kupunguza ufanisi wa utoaji wa huduma ya afya ndani ya hospitali.

Ninapendekeza Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha bajeti ya kutosha inatengwa kwa ajili ya marekebisho ya vifaatiba ili kuboresha huduma za matibabu, kupunguza muda wa wagonjwa kusubiri huduma, na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za afya ndani ya hospitali.

### **17.3 Madai ya hospitali yaliyokataliwa na mfuko wa bima wa afya shilingi bilioni 11.83**

Wakati wa ukaguzi wangu kwa mwaka 2022/23 nilibaini Mfuko wa Bima wa Afya ulikataa jumla ya shilingi bilioni 11.83 sawa na asilimia 15 ya madai yote ya shilingi bilioni 76.89 kutoka hospitali nne za umma kama zinavyoonekana kwenye Jedwali Na. 40. Uchambuzi wa mwenendo huu unaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la kukataliwa kwa madai ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 madai ya shilingi bilioni 3.87 (sawa na asilimia 7 ya madai) yalikataliwa na katika mwaka wa fedha 2021/22 madai ya shilingi bilioni 8.84 sawa na (asilimia 10 ya madai) yalikataliwa.

Sababu kuu za kukataliwa ni: udanganyifu katika madai na kutokuwapo kwa uhalali wa sababu za kutozingatia taratibu au kanuni zinazohusiana na malipo ya madai, kudai mara mbili, matumizi makubwa ya huduma, kutozingatia bei za Mfuko wa Bima, na huduma ambazo hazijaoneshwa katika utambuzi. Pia husababishwa na ukosefu au ubatili wa nambari za uidhinishaji, kukosa maelezo ya huduma zinazodaiwa baada ya kuthibitishwa, kutokuwapo kwa saini ya mgonjwa au saini ya mgonjwa isiyo sahihi, huduma zisizo ndani ya kifurushi cha Mfuko wa Bima, makosa ya kukokotoa, kuandika dawa nyingi kupita kiasi, na kutofuata miongozo ya kawaida ya matibabu.

#### **Jedwali Na. 40: Madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na mfuko wa bima wa afya**

Na.	Jina la Taasisi	Kipindi	Jumla ya Kiasi Kilichotozwa	Kiasi kilichokat alia	Asilimia iliyokatali wa
Shilingi "Milioni"					
1	Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila	Julai 2022-Mei 2023	13,993.65	3,055.36	22
2	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Julai 2021-Juni 2023	53,967.45	7,400.23	14
3	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	Julai 2021-Juni 2023	7,423.37	1,259.42	17
4	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	Julai 2022-Juni 2023	1,501.92	115.84	8

Jumla	76,886.39	11,830.85	15
<i>Chanzo: Uchambuzi wa Hati za madai za Mfuko wa Bima ya Afya</i>			

Ukwasi ya mashirika haya unaweza kuathiriwa sana kutokana na kukataliwa kwa madai kunakosababisha upotevu wa fedha.

Ninapendekeza Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Chuo Kikuu Cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; (a) Kuweka utaratibu wa kupitia sababu zote za kukataliwa na kutoa mrejesho kwa wakati kwa maafisa wanaohusika katika idara na sehemu zote zinazohusika na utoaji wa huduma za afya ili kuzuia au kupunguza kujirudia kwa tatizo katika siku zijazo; na (b) Kushauriana na Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya kutoa mafunzo na semina ya mara kwa mara kuhusu utoaji wa huduma za afya ambao hautaathiri mahitaji yaliyobainishwa.

#### 17.4 Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza mahitaji ya vituo vya afya kwa asilimia 24

Bohari Kuu ya Dawa ilipokea oda 105,646,079 za vifaatiba na dawa kutoka hospitali za rufaa, mikoa, na vituo vya afya katika mwaka wa fedha 2022/23. Kati ya oda hizo walitimiza oda 85,525,584 za vifaatiba sawa na asilimia 76 ya maagizo yote. Kuna ongezeko la utimizaji wa mahitaji ya wateja ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22 ambapo asilimia 33 ilitimizwa.

Mahitaji ambayo hayakutekelezwa yalisababishwa na ukosefu wa vifaatiba na dawa za kutosha ghalani ili kutoa huduma. Kutotosha huko kulitokana na kukosea kukadiria mahitaji ya wateja. Hii ni kwa sababu zilitumika takwimu zisizo na ubora kutokana na kutokuwapo kwa utaratibu madhubuti wa kusimamia vifaatiba na dawa zilizopo ghalani na makadirio ya Wizara ya Afya kwa kuzingatia matumizi; pamoja na upungufu wa mtaji unaosababishwa na malimbikizo ya madeni ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 366.32 ya uhifadhi na usambazaji wa bidhaa za afya za Programu ya magonjwa tishio (Kifua kikuu, Virusi vya ukimwi, Malaria, na Afya ya uzazi, mama na mtoto).

Hospitali za Rufaa, mikoa na vituo vingine vya afya vinaweza kupata upungufu wa vifaatiba na dawa, hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Bohari Kuu ya Dawa inakosa mapato ambayo

yangeweza kupatikana kutokana na uuzaaji wa vifaatiba na dawa kwa vituo vyta afya.

Ninapendekeza; (a) Bohari Kuu ya Dawa ihakikishe mfumo wa usimamizi wa vifaatiba unaboresha ili kutoa takwimu sahihi zinazoonesha wakati sahihi wa kuagiza vifaatiba na dawa, na kufuatilia kiasi kilichobakia ili kuwezesha makadirio sahihi, na (b) Serikali ilipe deni la shilingi bilioni 366.32 kwa Bohari Kuu ya Dawa ili kuongeza mtaji.

**17.5 Kuwapo kwa bidhaa au vifaa visivyotumika, vilivyopitwa na wakati, na vinavyotumika polepole vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.57 katika ghalaa la Bohari Kuu ya Dawa**

Mwongozo wa Usimamizi wa mali ghalani wa Bohari Kuu ya Dawa wa 2018 unaeleza kuwa vifaa visivyotumika vinahitaji kutolewa au kuuzwa na vifaa vinavyotumika polepole vinahitaji kugawiwa kwenye hospitali zingine.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini jumla ya vifaatiba na dawa katika ghalaa ya Bohari Kuu ya Dawa zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 123.67, vifaatiba na dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 6.57 kati ya hizo, zilikuwa hazitumiki, zimepitwa na wakati na vifaatiba na dawa zinazotumika polepole.

Vifaatiba na dawa ambazo hazitumiki, zilizopitwa na wakati na zinazotumika polepole ni matokeo ya mabadiliko katika teknolojia kama vile mashine za x-ray ambazo zimepitwa na wakati ambapo kwa sasa mashine ya x-ray ya kidigitali ndiyo inatumika; makadirio duni ya mahitaji ambayo hayatumiki sana; na magonjwa ambayo yanatangazwa kuwa siyo janga tena kama UVIKO-19.

Fedha zimetumika katika vifaatiba na dawa ambazo hazitumiki na zimepitwa na wakati, ambazo zingeweza kutumika katika shughuli zingine.

Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa; (a) Ifikirie kuondoa vifaatiba na dawa ambazo hazitumiki na zimepitwa na wakati kwa kugawa au kuuza; na (b) Kushirikiana na Wizara ya Afya kuchunguza njia bora zaidi ya kupunguza idadi ya vifaatiba na dawa ambazo hazitumiki, zimepitwa na wakati na zinazotumika polepole.

## 17.6 Kuwapo kwa vifaatiba na dawa za kawaida na Maalumu zilizoisha muda Katika Bohari Kuu ya Dawa- shilingi bilioni 9.70

Vifaatiba na dawa ghalani zimegawanywa katika makundi ya kawaida, maalumu, Maduka ya Dawa ya Bohari Kuu ya Dawa, na zile zinazohusiana na magonjwa ambayo ni janga kwa taifa, kama ilivyobainishwa katika Mwongozo wa usimamizi wa Vifaatiba na dawa wa Bohari Kuu ya Dawa wa mwaka 2018. Mwongozo huo unaeleza kuwa vifaatiba na dawa zilizoisha muda wake hazipaswi kuzidi asilimia 2 ya jumla ya thamani ya vifaatiba na dawa.

Tathmini yangu ya vifaatiba na dawa zilizopo ghalani kwa mahitaji ya kawaida na maalumu kwa miaka mitatu mfululizo ya 2020/21, 2021/22 na 2022/23 ilibaini mwenendo wa kubadilika kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 41**.

**Jedwali Na. 41: Mwenendo wa vifaatiba na dawa zilizoisha muda wake**

Mwaka wa Fedha	Bidhaa za kawaida	Bidhaa Maalumu	Jumla
Shilingi "Milioni"			
2020/21	11,091.75	658.23	11,749.98
2021/22	5,508.96	408.58	5,917.54
2022/23	8,826.14	872.52	9,698.66

*Chanzo: Taarifa ya bidhaa ya mwaka 2022/23*

Vifaatiba na dawa zilizoisha muda wake wa matumizi hutokana na kupokea bidhaa za afya zenye maisha yanayokaribia kumalizika; makadirio yasiyo na ufanisi, na kuzuia magonjwa ya janga ambayo hayapo tena (UVIKO 19) kwani bidhaa hizi nyingi zilipatikana katika mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22 kwa njia ya msaada au ununuzi wa dharura ikiwa ni utayari wa kupambana na UVIKO-19.

Ingawa bidhaa zilizoisha muda wake ni chini ya asilimia 2 ya jumla ya thamani ya bidhaa zilizopo ghalani, bidhaa hizi ni upotezaji wa fedha kwa sababu dawa zilizoisha muda wake hazitauzwa, hutumia nafasi ambayo inaweza kutumika kuhifadhi bidhaa zingine.

Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa ihakikishe; (a) Bidhaa za afya zipokelewe zikiwa na maisha zaidi ya asilimia 80 au miaka 2 ya maisha yote; na (b) Makadirio yafanyike kutegemea data za kuaminika za mahitaji.

### **17.7 Madeni ya michango ya wanachama ambayo hayajalipwa katika mfuko wa bima ya afya shilingi bilioni 11.56**

Kifungu cha 9 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kinawataka waajiri waliosajiliwa kuwasilisha michango inayodaiwa kwa mwezi husika ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi. Jumla ya michango iliyokuwa inadaiwa hadi kufika tarehe 30 Juni 2023 ilikuwa shilingi bilioni 42.57, kati ya hiyo, michango ambayo zinadaiwa Taasisi za Serikali ni shilingi bilioni 19.04 sawa na asilimia 45 na shilingi bilioni 23.53 sawa na asilimia 55 zinajumuisha madeni kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Katika uchambuzi zaidi nilibaini kuwa, kati ya michango yote ya wanachama inayodaiwa na Mfuko wa Bima ya Afya, michango ya shilingi bilioni 19.6 (sawa na asilimia 40) inadaiwa zaidi ya siku 30. Aidha, mfuko ulikusanya shilingi bilioni 5.34 ya madeni hadi kufikia mwishoni mwa Novemba 2023 na kuacha deni linalodaiwa la shilingi bilioni 11.56.

Sababu kuu zinazochangia madeni ya muda mrefu ya michango inayodaiwa kutoka mashirika ya umma, ni urasimu katika kuthibitisha madeni.

Hali hii inasababisha kuwa na mkusanyiko wa madeni ya muda mrefu kutoka mashirika ya umma, jambo ambalo linaathiri hali ya kifedha ya Mfuko wa Bima ya Afya.

Madeni ya muda mrefu yanababisha changamoto za ukwasi kwenye mfuko, hivyo huweza kuathiri shughuli za mfuko, ikiwa ni pamoja na kushindwa kuwalipa watoahuduma kwa wakati.

**Ninapendekeza; (a) Serikali ihakiki malimbikizo ya michango iliyobaki na kuidhinisha kwa ajili ya malipo; na (b) Mfuko wa Bima ya Afya uendelee kufuatilia madeni ambayo bado hayajalipwa na kuhakikisha kiasi chote kinakusanya.**

### **17.8 Hali ya uhimilivu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekuwa ukipata hasara kwa miaka mitano iliyopita. Mfuko umepata hasara ya shilingi bilioni 156.77 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiwa ni uimarikaji kutoka hasara iliyopatikana mwaka wa fedha 2021/22 ya shilingi bilioni 205.95.

Michango ya wanachama kwa mwaka wa fedha 2022/23 imeongezeka kwa asilimia 14.6 kutoka shilingi bilioni 552.58 mwaka 2021/22 mpaka shilingi bilioni 633.51 mwaka wa fedha 2022/23, ambayo ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na ongezeko la matumizi ya wanachama ya asilimia 10.2 kutoka shilingi bilioni 674.25 mwaka 2021/22 mpaka shilingi bilioni 743.28 mwaka wa fedha 2022/23. Hasara kutohana na kuhudumia wanachama ilipungua kutoka shilingi bilioni 121.67 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 109.77 mwaka 2022/23.

Hii inaashiria kuimariika kutoka mwaka wa fedha 2021/22 ambapo ongezeko la michango ya wanachama ilikuwa asilimia 12.9 kutoka shilingi bilioni 489.48 mwaka 2020/21 mpaka shilingi bilioni 552.58 mwaka wa fedha 2021/22, ikiwa ni kidogo kulinganisha na ongezeko la matumizi ya wanachama la asilimia 24.6 kutoka shilingi bilioni 540.55 mwaka 2020/21 mpaka shilingi bilioni 674.25 mwaka wa fedha 2021/22.

Mambo kadhaa muhimu yanayoweza kuathiri uhai wa muda mrefu wa Mfuko wa Bima ya Afya ni:

- a) Mikopo ya Serikali ambayo hajalipwa:** mikopo ambayo hajalipwa ya shilingi bilioni 208 inasababisha mzigo mkubwa wa kifedha, na hivyo kupunguza uwezo wa Mfuko kuwekeza katika huduma muhimu na miundombini. Serikali kupitia Wizara ya Fedha imepanga kulipa shilingi bilioni 180.03 (bila riba na adhabu) katika bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25.
- b) Wastaifu kunufaika bila kuchangia:** Mfuko unagharamia matibabu ya wastaifu na wenza wao ambao hawachangii mfuko, hali hii inadhoofisha mfuko kwa sababu matumizi ya wastani ya kundi hili ni shilingi bilioni 84.70 kwa mwaka.
- c) Kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza:** Kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa wanachama, kunadhoofisha mfuko kwa kiasi kikubwa, sababu matumizi ya wastani kwa kundi hili ni shilingi bilioni 137.80.
- d) Uchaguzi wa wanachama walio na wagonjwa:** Wanachama wa hiari kwa makundi fulani, hasa kutoka sekta binafsi zilizo rasmi na zisizo rasmi, inasababisha kuwa na uchaguzi wa wanachama usio na mafanikio, ambapo wanachama hujiunga na mfuko pale tu

wanapohitaji matibabu ya gharama kubwa, hali inayodhoofisha mfuko.

Hasara endelevu kutokana na kuhudumia wanachama na hasara ya mfuko kwa ujumla inaathiri uimara na uendelevu wa mfuko.

**Ninapendekeza Mfuko wa Bima ya Afya;** (a) Ufikirie upya mikakati ya namna ya kuzalisha faida kutokana na kushughulika na wanachama na faida ya jumla kwa miaka mingi kwa uendelevu wa Mfuko; na (b) Serikali ilipe mkopo inayodaiwa.

#### **17.9 Utendaji usioridhisha wa Kiwanda cha Dawa Keko**

Kiwanda cha dawa Keko kinamiliikiwa na Serikali kwa asilimia 70 kuitia Msajili wa Hazina.

Wakati wa tathmini yangu nilibaini madeni ya muda mfupi ya Kampuni yanazidi mali za muda mfupi kwa shilingi bilioni 5.23 mwaka 2019 hadi shilingi bilioni 12.17 mwaka 2022. Hali hii ni ishara ya matatizo ya ukwasi. Pia, nilibaini kwa miaka minne mfululizo Kampuni imekuwa ikipata hasara. Kampuni ilipata hasara ya shilingi bilioni 3.27 mwaka 2019; shilingi bilioni 1.35 mwaka 2020; shilingi bilioni 1.48 mwaka 2021 na shilingi bilioni 1.35 mwaka 2022.

Hasara hizi zilisababishwa na ukosefu wa ufanisi katika uzalishaji ambao ulisababisha kushindwa kuzalisha mauzo ya kutosha ili kufidia gharama za uzalishaji na menejimenti kutokuwa na uwezo wa kuchunguza soko la nje kutokana na kutegemea zaidi mteja mmoja ambaye ni Bohari Kuu ya Dawa.

Nilibaini tarehe 20 Desemba 2021 Kiwanda cha Dawa Keko kiliingia Mkataba wa Makubaliano na Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya usambazaji wa dawa za aina 10 tofauti zilizotengenezwa kiwandani hapo. Kuanzia Oktoba 2020 hadi Desemba 2022, Bohari Kuu ya Dawa iliagiza dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 18.48. Hata hivyo, Kampuni ilitoa dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 12.99 tu licha ya kiwanda kupokea malipo ya awali ya shilingi bilioni 16.29. Hii ilisababishwa na ukosefu wa mtaji wa kufanya kazi na utendaji usiofaa wa mashine za utengenezaji.

**Ninapendekeza Kiwanda Cha Dawa Keko kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha kiwanda kinakuwa na ufanisi, kuboresha mtaji, kuboresha ufanisi wa kiwanda kuitia vifaa vy'a kisasa ambavyo vitasaidia kuongeza mauzo ili kufidia gharama za uzalishaji.**



## SURA YA KUMI NA NANE

### MAZAO NA BODI ZA MAZAO

#### 18.0 Utangulizi

Sekta ya kilimo ni muhimu kwa uchumi na ustawi wa nchi kama inavyositisizwa katika sera ya kilimo ya Tanzania. Sekta hii imeundwa kwa namna ambayo kila zao la biashara limeundiwa taasisi maalum kwa ajili ya kuliendeleza na kulikuza. Pia, Serikali ilianzisha taasisi zingine maalumu kwa ajili ya kushughulikia mambo muhimu yanayoathiri kilimo. Kwa mfano; Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) husimamia uzalishaji na usambazaji wa mbolea; Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania kwa ajili ya afya ya mimea na udhibiti wa viuatilifu; Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa ajili ya kufanya tafiti za kilimo. Pia, udhibiti wa mazao ya chakula unafanywa na Wizara ya Kilimo kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) pia, iliundwa kwa ajili ya kufanya biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko ikiwa ni sehemu ya mbinu za kuwahakikishia wakulima soko la uhakika la mazao yao. Mpango huu unalenga kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya kilimo.

Sura hii inalenga kuelezea changamoto na mambo yanayokabili uzalishaji wa mazao ya biashara na mazao ya chakula kwa kuwianisha na ufanisi wa Bodi za mazao zilizoanzishwa kusimamia mazao hayo. Mazao ya biashara yanajumuisha pamba, korosho, mkonge, kahawa, chai, miwa na pareto. Pamoja na sera, juhudini na uwekezaji wa Serikali ukuaji na uendelezaji wa mazao ya kilimo unakwamishwa na kutokuwapo kwa mifumo toshelevu ya uwezeshaji wa kifedha na uratibu duni miongoni mwa wadau wa kilimo, kilimo cha kutegemea mvua, na gharama kubwa ya pembejeo za kilimo, kama nilivyoripoti katika taarifa yangu ya mwaka uliopita.

Sambamba na mambo yaliyoelezwa kwenye taarifa ya mwaka uliopita wa 2021/22, katika ukaguzi wa mwaka huu wa fedha nimebaini

yafuatayo; Bodi za mazao kushindwa kudhibiti ubora wa mazao kikamilifu; Bodi za mazao kukosa nguvu na nyenzo za kuhakikisha uendelezaji na ukuzaji wa mazao; na kukosekana kwa ufanisi katika kuhakikisha usambazaji wa mbolea za kutosha na zenye ubora; maelezo ya kina juu ya mapungufu haya ni kama inavyoiezwa katika aya zinazofuata:

#### **18.1 Bodi za mazao zinakosa uwezo na nyenzo za kutosha kutekeleza majukumu yao**

Bodi za mazao zina wajibu wa kuendeleza na kukuza kilimo cha mazao wanayoyasimamia kwa kuhakikisha watu wengi zaidi wanalima na kuzalisha mazao hayo kwenye mazingira wezeshi ambayo bodi hizo zinawajibika kuyaweka kwa niaba ya Serikali. Hii inafanywa kwa kuongeza kampeni za kilimo, kutoa elimu ya kilimo, kufanya uhamasishaji, kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa viuatilifu na mbolea ya kutosha na yenye ubora, kufanya mafunzo ya kilimo, matumizi ya teknolojia sahihi za kilimo, upatikanaji wa mbegu bora nk. Hivyo, bodi za mazao zinatakiwa kuwa na fedha za kutosha, watumishi wa kutosha na wenye weledi kwa ajili ya huduma za ugani, miundombinu ya kilimo na teknolojia sahihi.

Lakini nilibaini kuwa bodi za mazao zinakabiliwa na ukosefu wa fedha za kutosha, miundombinu ya kilimo, teknolojia na watumishi wa kutosha na wenye weledi ili kutimiza majukumu yao. Mapungufu haya yanadhoofisha uwezo wa bodi za mazao katika kuendeleza na kukuza kilimo cha mazao wanayoyasimamia kwa ufanisi. Utegemezi uliokithiri wa fedha kutoka Serikalini unaathiri sana uwezo wa bodi hizi kama nilivyoainisha katika aya ya 18.5 ya ripoti yangu ya mwaka uliopita 2021/22.

Kwa mfano, Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHTDA) haikupokea jumla ya shilingi milioni 827.95 sawa na asilimia 51 kati ya shilingi bilioni 1.63 za bajeti. Pia, ilikuwa na upungufu wa watumishi 53 wa kutoa huduma za ugani zikijumuisha upandaji mashambani.

Bodi ya Kahawa Tanzania haikupokea jumla ya shilingi bilioni 1.31 sawa na asilimia 81 kati ya shilingi bilioni 1.61 za bajeti kutoka Serikalini hali iliyofanya Bodi ya Kahawa kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu mpango mkakati wa kahawa kwa kazi zilizopangwa kufanya mwaka wa fedha 2022/23.

Bodi ya Tumbaku Tanzania haikupokea shilingi milioni 568.99 kati ya shilingi bilioni 2.19 za bajeti kama ruzuku ya Serikali kwa ajili ya mishahara na miradi ya maendeleo; wakati Bodi ya Korosho haikuweza kukusanya shilingi bilioni 1.56 kati ya shilingi bilioni 6.17 zilizopangwa kwenye bajeti.

Kukosekana kwa fedha kunazodhohofisha uwezo wa bodi za mazao kuiga mbinu bora, kuziboresha ama kununua teknolojia, mitambo na miundombinu ya kisasa ili kuongeza ufanisi katika kilimo na kuongeza uzalishaji.

**Ninapendekeza Serikali ifanye marejeo ya mfumo unaotumika sasa wa kuzipatia fedha bodi za mazao ili kuja na mfumo bora na wenye ufanisi utakaoziwezesha bodi za mazao kuwa na uwezo wakifedha.**

#### **18.2 Matumizi duni ya teknolojia ya kilimo na mifumo ya kielektroniki katika kuongeza ufanisi wa uzalishaji**

Teknolojia ya kilimo ni mionganini mwa nyenzo muhimu zinazowezesha ufanisi katika kilimo na inachochea uzalishaji kwa gharama nafuu japo inahitaji uwekezaji mkubwa wa fedha mwanzoni. Inajumuisha usimikaji wa miundombinu ya umwagiliaji, uzalishaji wa mbegu bora, matumizi ya mbolea za kutosha na zenye ubora, vifaa vya kisasa vya kilimo na mbinu za kisasa za kilimo. Kwa upande mwingine, mifumo ya kielektroniki inawezesha kuwapo kwa njia rahisi na zenye ufanisi kwa bodi za mazao kuweza kutekeleza majukumu yao kwa kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali, kuzichakata, na kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau kwa wakati.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa bodi za mazao zina uwezo duni wa teknolojia. Matumizi ya teknolojia duni au kutotumia teknolojia kabisa, imekuwa ni mionganini mwa sababu kubwa zinazokwamisha ufanisi wa uzalishaji. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023, Bodi ya Pamba Tanzania, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba iliwekeza jumla ya shilingi bilioni 96.03 kwa ajili ya kilogramu 26,398,652.63 za mbegu za pamba, viutilifu kiasi cha hekari 12,216,629 acre/hekari na vinyunyiziaji 46,203 kwa makadirio ya kuvuna tani 253,195 za pamba. Hata hivyo, mwishoni mwa msimu wa soko wa 2022/23, uzalishaji wa pamba ulikuwa tani 174,486 ikiwa ni kidogo kuliko kiasi cha mavuno kilichotarajiwa kutokana na ukame wa muda mrefu na wadudu, hali ambayo ingeweza kukabiliwa kwa kutumia teknolojia ya skimu za umwagiliaji na matumizi ya ndege zisizo na

rubani au vinyunyiziaji vyatvutifuli vyenye shinikizo kubwa ambavyo vingeboresha ufanisi katika udhibiti wa wadudu.

Kwa upande wa Bodi ya Kahawa Tanzania, katika taarifa yake ya bodi ya wakurugenzi ilieleza kuwa, kiwango cha juu cha uzalishaji ambacho ni 1Kg kwa kila mtaa mmoja wa kahawa, kingeweza kufikiwa kama kungekuwa na matumizi ya teknolojia bora sambamba na pembejeo zingine za kilimo cha kahawa. Kwa sasa kiwango cha uzalishaji ni kilogramu 0.375 kwa kila mtaa mmoja wa kahawa.

Bodi ya Tumbaku Tanzania imeripoti kuwa uzalishaji ni kilogramu 1,300 kwa hekta kwa mwaka 2022/23 amba ni chini ya malengo ya kilogramu 1,400 kwa hekta kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo kuchelewa kutumia pembejeo za kilimo kulikotokana na kuchelewa kwa usambazaji wa pembejeo hizo, uwezo mdogo wa miundombinu ya kukaushia tumbaku, mazao kuathiriwa na mgawanyo wa mvua usio sawa kwa kuwa hakuna miundombinu ya umwagiliaji, na kukosekana kwa teknolojia ya kukabiliana na athari za majanga asilia (mvua za mawe, dhoruba na radi); hali zilizosababisha kupotea kwa majani mengi ya tumbaku.

Tofauti na ilivyo kwa Bodi ya Sukari Tanzania ambayo ina mifumo kama Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Biashara za Kilimo, Programu ya ukaguzi wa sukari , Mfumo wa Usimamizi wa Sukari Viwandani, Mfumo wa Kufuatilia Uzalishaji na Usambazaji wa Sukari na Mfumo wa usajili wa wakulima. Bodi zingine za mazao kama vile Bodi ya Chai Tanzania na Bodi ya Pareto Tanzania hazina mifumo kama hiyo ambayo ingewaongezea uwezo wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi. Kwa mfano, Bodi ya Chai Tanzania haina mifumo wa kusajili wakulima, kukusanya takwimu pamoja na kufuatilia takwimu za chai kwani michakato yote hufanyika kuititia Ms Words au Excel ambayo huweza kuwa na makosa na zinatoa mianya ya udanganyifu. Pia, nilibaini vivyo hivyo kwa Bodi ya Pareto Tanzania ambapo karibu shughuli zote za mawasiliano na takwimu zinafanywa nje ya mifumo, hivyo kuzifanya ziwe na mapungufu, kutiliwa shaka kutokana na makosa, na ni rahisi kutumiwa kwa udanganyifu.

**Ninapendekeza bodi za mazao ziwekeze kwenye teknolojia ya kilimo na mifumo ya kielektroniki ili kuwezesha kuongeza uzalishaji na ufanisi wa upatikanaji, uchakataji na utoaji wa taarifa muhimu za kilimo.**

### 18.3 Kukosekana kwa uthabiti wa usimamizi na udhibiti wa ubora wa mazao

Soko la uhakika na bei nzuri ya mazao ya wakulima vinategemea sana hali ya uhitaji na upatikanaji wa bidhaa husika sokoni. Lakini, viwango vya ubora wa baadhi ya mazao kama vile kahawa, korosho, chai, pamba na tumbaku vinaathiri hali ya uhitaji wa bidhaa hizo na bei yake sokoni. Hivyo, udhibiti na usimamizi wa ubora wa mazao ni muhimu na ni miongoni mwa majukumu muhimu ya bodi za mazao.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa suala la udhibiti wa ubora ni changamoto kwa bodi za mazao. Bodи za mazao bado hazijaweza kusimamia na kuhakikisha ubora wa mazao wanayosimamia unafikia viwango vilivyowekwa, isipokuwa Bodi ya Korosho tu, ambayo ubora wa korosho zilizosalishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulizidi viwango vya ubora uliokusudiwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 42** hapa chini.

**Jedwali Na. 42: Ubora wa mazao yaliyozalishwa**

	Kahawa (Asilimia)	Pamba (Asilimia)	Korosho (Asilimia)	Pareto (Asilimia)	Tumbaku (Asilimia)
Kiwango kusudiwa/kinachotaki wa	15	75	97	1.29	94
Kiwango kilichofikiwa	6.20	37.59	98.2	1.24	88
Tofauti	8.80	37.41	-	0.05	6

**Chanzo:** ripoti za bodi za wakurugenzi wa bodi za mazao

Bodi za mazao zinapata ugumu na zinashindwa kusimamia na kudhibiti kikamilifu ubora wa mazao wanayosimamia kwa sababu bodi hizo sizo zinazolima mazao hayo moja kwa moja bali zinasimamia wakulima wa mazao hayo ambao kutokana na sababu tofauti tofauti wanawenza wasizingatie mahitaji ya kazi zinazohitajika kuhakikisha ubora. Ili kuondokana na changamoto hiyo, bodi za mazao zinahitaji kutoa huduma za ugani kwa kina na kwa upana mkubwa kuwafikia wakulima wengi wa mazao husika, hali inayohitaji fedha za kutosha, watumishi wa ugani wa kutosha, magari ya kuwezesha kuwafikia wakulima wengi zaidi, na matumizi ya mbinu na teknolojia bora za kilimo ili kuwezesha udhibiti wa ubora. Kwa sasa, hoja tajwa hapo juu, hazitekelezwi kwa ukamilifu.

Natambua juhudzi za Serikali za kuwapatia maafisa kilimo vifaa vya baiskeli, mafunzo na mahitaji mengine ili kuimarisha harakati zao za kuwahudumia wakulima wengi zaidi kwa urahisi. Lakini mazao ya

biashara yanahitaji maafisa kilimo mahususi ambao wana vifaa vyatubishwa kutosha kwa kusimamia kwa ukamilifu ubora wa mazao ya biashara. Udhibiti ubora wa mazao unajumuisha kuweka mipango ya kudhibiti ubora, kutekeleza kazi za kudhibiti ubora, ukaguzi wa mashamba, ukusanyaji, uchakataji na udhibiti wa takwimu na kazi za ubora, na mambo mengine ya kudhibiti ubora ambayo bodi za mazao zinakosa fedha, rasilimali na nyenzo za kuhakikisha kazi hizo zinafanyika kikamilifu

**Ninapendekeza bodi za mazao kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha rasilimali za kutosha zinapatikana kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kwa kina kwa wakulima kama kichocheo cha kuboresha shughuli za usimamizi wa ubora**

#### 18.4 Mapungufu katika kusimamia ubora na usambazaji wa mbolea

Mbolea ni mionganini mwa mambo muhimu ambayo haiwezekani kuacha kuzingatiwa katika kilimo cha kisasa kwani ina umuhimu mkubwa katika kuwezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao, ubora wa mazao na kuongeza rutuba ya udungo. Inatoa virutubisho muhimu kwa mimea ya mazao kuongeza ukuaji, mavuno na ubora wa mazao. Serikali imejidhatiti kuhakikisha kunakuwa na ufanisi na uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa ajili ya kudhibiti uzalishaji, uingizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi, uuzaaji, na matumizi ya mbolea nchini ikiwa ni sambamba na kulinda wakulima na jamii kwa jumla kuepukana na majanga na madhara yatokanayo na matumizi ya mbolea zisizokidhi viwango vinavyotakiwa na udanganyifu katika soko la mbolea.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kasoro mbalimbali katika uzalishaji, usambazaji, utumiaji na usimamizi wa mbolea. Kasoro hizo zinaathiri sekta ya kilimo kama ilivyoelizwa katika aya zinazofuata;

##### 18.4.1 Ucheleweshaji malipo kwa wauzaji wa mbolea ya ruzuku

Kanuni 5.5 ya kanuni za mbolea ya ruzuku inaielekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kuwalipa wauzaji wa mbolea ya ruzuku ndani ya siku 14 tangu kupokelewa kwa ankara ya muuzaji ili kuwezesha na kurahisisha uendeshaji wa mpango wa mbolea ya ruzuku.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ilishindwa kulipa madai ya wauzaji 18 wa mbolea ndani ya

muda wa siku 14 mpaka zaidi ya siku 60, kinyume na inavyotakiwa na kusababisha malimbikizo ya madeni kufikia shilingi bilioni 262 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023. Ucheleweshwaji huu umetokana na Serikali kuititia Wizara ya Kilimo kupeleka fedha zisizotosheleza ama kutopeleka kabisa fedha kwa Mamlaka, hivyo kuifanya Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kuwalipa wauzaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakati unaotakiwa. Hali hii inaweza kuwavunja moyo wauzaji wa mbolea ya ruzuku na kuhatarisha ushiriki wao kwenye mpango wa mbolea ya ruzuku na kusababisha kupungua kwa upatikanaji wa mbolea ya ruzuku wa walengwa.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha fedha za kutosha zinapatika na zinalipwa kwa wakati kwa wauzaji wa mbolea ya ruzuku kwa ajili ya uendelevu himilivu wa mpango wa mbolea ya ruzuu.**

#### **18.4.2 Hatua zisizotosheleza za kudhibiti vitendo visivyo vya kiuadilifu katika mpango wa mbolea ya ruzuku**

Serikali ilianzisha mpango wa mbolea ya ruzuku ambao unalenga kuhakikisha usambazaji wa mbolea bora ya kutosha kwa wakulima kwa bei ambayo wakulima wanaimudu. Pia, iliweka mfumo wa kielektroniki wa kusajili wakulima wenye sifa na vigezo vinavyotakiwa kwa wanufaika walengwa wa mpango wa mbolea ya ruzuku. Hata hivyo, endapo mpango huu hautasimamiwa vizuri, kuna hatari kuwa walengwa wa mpango huu kutonufaika kama ilivyokusudiwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya wafanya biashara wa pembejeo za kilimo walikuwa wakiuza mbolea na viuatilifu ambavyo havikusajiliwa ambapo asilimia 61 (2,634 kati ya 4,346) ya wafanyabiashara waliosajiliwa katika mpango wa mbolea ya ruzuku hawakuuza wala kufanya muamala wowote juu ya mpango wa mbolea ya ruzuku. Kutoshiriki kwa wafanya biashara tajwa kwenye mpango, kunaathiri usambazaji wa mbolea ya ruzuku hasa kwa maeneo ya vijijini ambako wakulima wengi wanategemea mbolea ya ruzuku. Pia, nilibaini mbolea iliyokuwa ikiuzwa haikuwa imewekewa alama ya utambuzi “QR codes” kwa kuwa alama hizo hazikuwa zikibandikwa kwenye mifuko ya kuuzia mbolea. Badala yake QR Codes zilikuwa zikichapishwa tofauti na kupigwa chapa kwenye mfumo kwa kuangalia kiwango cha mbolea ambacho muuzaji ameomba hali inayoweza kupelekea udanganyifu katika mfumo na kusababisha ubadhilifu wa madai ya mbolea ya ruzuku,

makosa katika upangaji wa bajeti, na kukosekana kwa uwazi katika usambazaji wa mbolea ya ruzuku.

Pia, nilibaini wauzaji 70 wa mbolea ya ruzuku walipewa leseni zaidi ya moja zenyenamba tofauti kwa aina moja ya biashara (uuzaaji wa jumla, msambazaji, mzalishaji au muuzaji mdogo) kwa taarifa za aina moja kutoka kwa msajiliwa kutokana na mapungufu katika mfumo wa taarifa wa mbolea. Hali ya utoaji wa leseni zaidi ya moja za aina moja kwa mtu mmoja inatia shaka juu ya usahihi wa takwimu, taarifa, na maamuzi yaliyofanywa kuititia taarifa kutoka katika mfumo huo.

Vilevile, nilibaini wafanyabiashara wa mbolea ya ruzuku katika mikoa ya Mbeya, Songea, Njombe na mji wa Makambako hawakufuata kanuni za utunzaji wa mbolea kweye maghala na stoo, hali inayoathiri ubora wa mbolea na viuatilifu. Mambo mengine yaliyokiukwa katika mpango wa mbolea ya ruzuku yanajumuisha kuweka mbolea kwenye maghala ambayo hayana hewa ya kutosha, mbolea za aina tofauti kuwekwa pamoja badala ya kuzitenganisha. Uuzaji wa mbolea ambayo haijasajiliwa, Kuifanya mbolea ya majani kama dawa ya kuulia wadudu na uuzaaji wa mbolea katika ujazo usiokubalika kinyume cha sheria ambayo inataka mbolea ya ruzuku iuzwe katika ujazo wa kilogramu 50 tu. Pia, nilibaini kuwa, wakaguzi 20 wa mbolea kati ya 37 katika kanda ya kaskazini hawakuwa na vigezo inavyotakiwa kwa wao kufanya kazi ya ukaguzi wa mbolea kwa kuwa hawakufanyiwa mafunzo wala majina yao kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama inavyotakiwa na Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009. Hivyo inahujumu jitihada za Serikali katika kuhakikisha ubora na usalama katika sekta ya mbolea na kuhatarisha usalama wa jamii na uzalishaji katika sekta ya kilimo.

Pia, katika ziara niliyofanya mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, nilibaini wafanyabiashara wa mbolea 30 kati ya 233 niliowatembelea walikuwa wakifanya biashara bila ya kuwa na leseni, hali inayotia shaka kuhusu kuwapo kwa uwezekano wa kuhujumu ubora wa mbolea.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Wizara ya Kilimo kuhakikisha mapungufu yaliyobainishwa yanarekebishwa kwa ajili ya kuendeleza mpango wa mbolea ya ruzuku na kuwanufaisha wakulima.**

#### 18.4.3 Kasoro katika usajili wa wakulima kwenye mpango wa mbolea ya ruzuku

Mpango wa mbolea wa msimu wa 2022/23 uliipa majukumu Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa kushirikiana na sekretariati za mikoa na Serikali za mitaa kuwasajili wakulima watakaonufaika na mpango wa mbolea ya ruzuku kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini orodha ya wakulima 4,628 kati ya 3,389,951 ilikuwa na majina ambayo hayakutambuliwa, mashamba yaliandikishwa bila kuhakiki ukubwa ultiotajwa, wakulima walisajiliwa kwa kutumia namba badala ya majina yao, wauzaji wa mbolea walijisajili kama wakulima na huku ukubwa mashamba yao haukuwa halisi kwa lengo la kupata kiwango kikubwa cha mbolea ya ruzuku ili waiuze.

Majina yasiyo halisi na ukubwa wa mashamba usio halisi unaweza kusababisha mianya katika kudhibiti na kuhakikisha hakuna matumizi mabaya ya mbolea ya ruzuku wala hasara ya kifedha kwa Serikali. Taarifa za wakulima na takwimu zisizo sahihi zinaathiri usahihi katika mipango ya mahitaji na utumiaji wa mbolea, utumiaji wa namba badala ya jina la mkulima kunazuia ufuatiliaji na kuchukua hatua za kisheria inapobainika kufanyaika kwa ubadhilifu ama udanganyifu.

Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, Sekretariati za Mikoa, na Serikali za Mitaa, kuweka na kutekeleza mbini zenye ufanisi katika kusimamia na kudhibiti taarifa za mpango wa mbolea ya ruzuku, kuzuia ubadhilifu wa mbolea ya ruzuku, na kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu watakaobainika kufanya ubadhilifu.

#### 18.5 Hatua zisizotosheleza kudhibiti upungufu wa sukari

Matumizi ya sukari hayaepukiki kwa watumiaji wote wa majumbani na viwandani, mahitaji ambayo kwa kiwango kikubwa yanaathiriwa na usambazaji wa sukari kwenye soko. Serikali kupitia Bodi ya Sukari Tanzania ina wajibu wa kusimamia uzalishaji, uuzaaji na uingizwaji na usambazaji wa sukari nichini. Kila mwaka nchi imekuwa ikikabiliwa na hali ya upungufu wa sukari na kuongezeka kwa bei za sukari. Hali hii imekuwa ikijirudia bila kuwa na juhudzi zinazoenda sambamba katika kudhibiti hali hiyo.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa hatua zinazochukuliwa na Bodi ya Sukari ili kudhibiti upungufu wa sukari nchini hazitoshelezi. Kasi ya hatua zinazochukuliwa ili kuongeza uzalishaji wa sukari wa ndani kwa kuongeza uwekezaji wa ndani ya nchi, bado ni ndogo.

Pia, nilibaini kuwa, njia mbadala na za haraka za kudhibiti upungufu wa sukari ni kuagiza sukari kutoka nje kwa wakati. Hata hivyo, hazitekelezwi kikamilifu. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2022/23 kiwango cha sukari kilichoingizwa kutoka nje ni kidogo licha ya kuwa kiasi kilichoidhinishwa cha kuagiza sukari kilikuwa kikubwa kwa ajili ya sukari ya majumbani na viwandani (**Jedwali 43**).

Nina mashaka juu ya sababu za uwepo wa upungufu huu hali ya kuwa Serikali ilitoa vibali vya kuagiza sukari nyingi zaidi kwa lengo la kudhibiti hali hii.

**Jedwali Na. 43: Mwenendo wa sukari ndani ya nchi**

Maelezo	2022/23		
	Lengo (MT)	Halisia (MT)	Upungufu (MT)
Sukari majumbani			
Uzalishaji wa ndani	490,000	460,000	29,951
Vibali vya kuagiza nje	30,000	6,801	23,199
Sukari viwandani			
Vibali kuagiza nje	249,880	196,270	53,610

**Chanzo: Taarifa ya bodi ya wakurugenzi**

Kutokuwa na udhibiti wa kutosha wa upatikanaji wa sukari sokoni kunasababisha ongezeko kubwa la bei za sukari kusikotarajiwambazo wananchi wengi hawazimudu. Pia, kunasababisha ongezeko la bei za bidhaa za viwandani ambazo zinategemea sukari wakati wa uzalishaji, hivyo kuongeza mzigoto wa bei kwa watumiaji wa bidhaa hizo, ambao wengi ni wananchi wa kawaida.

**Ninapendekeza Bodi ya Sukari kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa upungufu wa sukari kwa kuhakikisha kiwango cha sukari kilichokubaliwa kuagizwa kutoka nje kinaagizwa kwa wakati na kwa ukamilifu; kuitia na kuhakiki utekelezaji wa vibali vya uagizaji wa sukari vilivyotolea na kuchukua hatua stahiki kwa waagizaji ambao hawakutimiza majukumu yao; na kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango mikakati ya muda mrefu ya uzalishaji wa sukari ya kutosha ndani ya nchi.**

### **18.6 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) haina mifumo ya kielektroniki na wataalamu wa kusimamia na kudhibiti gharama za uzalishaji na uendeshaji**

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ni taasisi ya uzalishaji yenye michakato migumu kama vile ya ununuvi wa mali ghafi (kama vile ngano, mahindi, alizeti, mpunga na mazao mengine), kuchakata mali ghafi kuwa bidhaa zinazotakiwa, kufungasha, kusambaza na kuuza bidhaa zilizozalishwa au kuuza mali ghafi kama bidhaa. Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inamiliki viwanda vya kusindika Iringa, Arusha, Mwanza na Dodoma. Pia, Bodi ina vihenge katika mikoa ya Arusha na Iringa na maghala maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuhifadhi nafaka ghafi na bidhaa zilizokwisha zalistwa au kusindikwa.

Kutokana na aina ya kazi na miyamala, Bodi haiwezi kuepuka kuwa na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia gharama mbalimbali kwa ufanisi na kwa ukamilifu ili kuwezesha maamuzi sahihi juu ya sera za usimamizi wa gharama, usimamizi wa bei za kuuzia bidhaa na uamuzi juu ya mikakati na mbinu za masoko ili kuwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kupata faida na kuepuka ama kupunguza hasara.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko haina mifumo ya uendeshaji wa kazi zake za kitaasisi, na pia, haina mifumo wala wahasibu wataalamu kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa gharama za uzalishaji na uendeshaji. Gharama za uzalishaji na uendeshaji zinahesabiwa kwa mikono kwa kutumia “excel” na zinafanywa na wahasibu ambao siyo wabobezi kwenye kufuatilia, kusimamia na kuchakata gharama.

Nina mashaka kuwa Bodi iko katika hatari ya kupata hasara kutokana na hatari ya kupanga bei za kuuzia zisizo sahihi kunakosababishwa na kutochakata kwa usahihi na kwa ukamilifu gharama za uzalishaji wa bidhaa au kuwepo kwa mianya ya udanganyifu

**Ninapendekeza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; (a) Kuajiri wahasibu wataalamu wa kusimamia na kuchakata gharama; na (b) kuweka mifumo ya kielektroniki katika uendeshaji wa kazi zake ikiwa ni pamoja na kuwa na mfumo wa ufuatiliaji na uchakataji wa gharama ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa gharama na kufanya maamuzi sahihi ya kibiashara.**

### 18.7 Kutokuwa na udhibiti wa bei za kununulia malighafi za Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inanunua malighafi kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kulisha viwanda vyake vya kuzalishia bidhaa za nafaka. Mali ghafi zinazonunuliwa ni mahindi, mpunga, mbegu za alizeti, mtama na mazao mengine kulingana na maamuzi ya menejimenti. Malighafi hizi zinanunuliwa aidha kuititia vyama vya ushirika (AMCOS) au kuititia watumishi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Kanuni ya 17 (1-2) ya Kanuni za Nafaka na Mazao Mengine ya mwaka 2011, na kifungu cha 1.3 (1-5) cha Muongozo wa Huduma za Biashara zinaelekeza kuwa katika kupanga bei, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iwe inawasiliana na wadau mbalimbali, na kamati ya kupanga bei ipange bei na kuipeleke kwa mkurugenzi mkuu wa Bodi ili aidhinishi kabla ya kuanza kutumika katika kanda zake zote.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Bodi ilinunua mazao kwa bei kubwa kuliko bei zilizokuwa zinatumika kununulia mazao kwenye maeneo ambayo Bodi ilinunua mazao. Hali hii inasababisha Bodi kutumia gharama kubwa kuliko inavyostahili katika ununuzi wa mali ghafi, hivyo kupelekea kupata hasara na kutopata faida, ama kupata faida kidogo kuliko ilivyostahili. Kwa mfano, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilitumia jumla ya shilingi milioni 8,140.32 kununua tani 8,523.109 za mahindi kutoka kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati, ambapo kwa bei ya chini iliyokuwa inatumika Bodi ingetumia shilingi milioni 7,112.44 na kwa bei ya juu Bodi ingetumia shilingi 7,301.21. Kwa kutotumia bei ya chini ya soko, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imepata hasara ya shilingi milioni 1,027.88 na kwa kutotumia bei ya juu imepata hasara ya shilingi milioni 839.11 katika ununuzi wa tani 8,523.109 za mahindi kutoka kanda hizo. Hii inaashiria kuwa Bodi inapata hasara kubwa wakati wa kununua malighafi.

Vilevile, wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Bodi haikuwa na nyaraka zozote za kumbukumbu za mchakato wa kupanga bei zilizotumika kununulia mazao kutoka maeneo mbalimbali. Hii inaashiria kutokuwepo kwa mchakato wa uwazi na uwajibikaji katika kupanga bei za kununulia mazao kunakoweza kutoa mianya ya udanganyifu kwenye bei za kununulia mazao hasa kwa watumishi wasio waadilifu. Hivyo, sikuweza kuthibitisha sababu, uhalali na ushindani wa bei zilizotumiwa na Bodi kununua malighafi.

Kutokuwa na udhibiti wa bei za kununulia malighafi kunasababisha gharama kubwa zisizo za lazima ambazo zinaweza kusababishwa na bei kubwa zisizo halisia kwa lengo la udanganyifu na kujinufaisha kwa watu wasio waadilifu. Hivyo inaweza kuisababishia Bodi hasara kubwa kwa kuwa bei ya kuuzia sokoni inaweza kushindwa kurudisha gharama za uzalishaji na kuifanya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kutokuwa na bei shindani za kuuzia bidhaa zake.

**Ninapendekeza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iweke mifumo imara ya kudhibiti bei ya kununulia mali ghafi sambamba na kuzingatia miongozo iliyowekwa katika kupanga bei za kununulia mazao.**

#### **18.8 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kufanya kazi chini ya uwezo wake wa kuzalisha, kusindika na kuhifadhi bidhaa**

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) inaendelea kuzalisha kwa kiwango cha chini kwa miaka nane mfululizo ikilinganishwa na uwezo wa viwanda vyake ambavyo kwa mwaka 2021/22 vilikuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya mita za ujazo 126,900 ikatumia asilimia 12 wakati mwaka huu 2022/23 vilikuwa na uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 98,100 ikatumia asilimia 19.27 tu, kwa mwaka (Jedwali Na. 44)

Kwa upande mwingine, kama nilivyoripoti mwaka uliopita 2021/22, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilitumia asilimia 71 tu ya uwezo wake wa kuhifadhi kwenye maghala yake. Wakati wa ukaguzi wa mwaka 2022/23, nilibaini ufanisi umepungua ambapo Bodi ilitumia asilimia 43.10 ya uwezo wake wa kuhifadhi amba ni MT 106,600 (Jedwali Na. 45).

Mambo yanayosababisha Bodi kujiendesha chini ya uwezo wa viwanda na maghala yake ni pamoja na mtaji mdogo uliowekezwa katika biashara, ufanisi mdogo katika kutumia uwezo wa viwanda na maghala, baadhi ya malighafi au nafaka kuwa chache, na kutokuwa na mipango thabiti ya kibiashara. Pia, kuna viashiria kuwa taasisi hii inaendeshwa kwa mtizamo wa kutoa huduma za kiserikali badala ya mtazamo wa kibiashara, na kukosa watumishi wa kutosha wenye mitizamo ya kibiashara.

Kutotumika kwa uwezo wa viwanda na maghala kwa ukamilifu kunainyima fursa Bodi ya kukua na kuchocheara kuongezeka kwa mapato na kunufaika na faida za uzalishaji kwa kiwango kikubwa

Jedwali Na. 44: Mwenendo wa uwezo wa kuzalisha kwa viwanda vya CPB

Mwaka wa Fedha	Uwezo wa kiwanda kuzalisha (MTs)	Uzalishaji halisi (MTs)	Uwezo wa kiwanda uliotumika (%)	Uwezo wa kiwanda ambao haukutumiwa (%)
2022/23	98,100	18,905	19.27	80.73
2021/22	126,900	14,623.93	12	88
2019/20	65,700	6,833.34	10	90
2018/19	16,200	3,820.96	24	76
2017/18	16,200	385.50	2	98
2016/17	16,200	2,040.28	13	87
2015/16	16,200	1,082.80	7	93

Chanzo: Taarifa za utekelezaji za mwaka wa fedha 2022/23

Jedwali Na. 45: Mwenendo wa CPB kutumia uweza wa maghala yake kuhifadhi bidhaa

Mahali ghalalilipo	Uwezo wa ghalaluhifadhi (MT)	Malengo na matumizi halisi ya uwezo wa maghala kuhifadhi					
		2022/23			2021/22		
		Lengo	Matumizi halisi	%	Lengo	Matumizi	%
<b>Arusha</b>							
Vihenge	28,100	28,100	12,841.5	33.70	28,100	3,805	13.5
Ghala	10,000	10,000	0		10,000	4,033	40.3
<b>Iringa</b>							
Vihenge	13,500	13,500	14,505.3	82.89	13,500	25,954	192.5
Ghala	4,000	4,000	2		4,000	4,000	100
<b>Mwanza</b>							
Ghala	20,000	20,000	4,015.36	20.10	20,000	20,000	100
<b>Dodoma</b>							
Ghala	30,000	30,000	14,489.40	48.30	30,000	16,608	55.4
<b>Kiteto</b>							
Ghala	1,000	1000	421.10	42.11	1,000	1000	100.0
<b>Jumla</b>	<b>106,600</b>	<b>106,600</b>	<b>46,273</b>	<b>43.10</b>	<b>106,600</b>	<b>75,400</b>	<b>71</b>

Chanzo: Taarifa za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23

Ninarejea pendekezo nilolitoa katika taarifa yangu ya mwaka uliopita kuwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa kushirikiana na Serikali kuwekeza mtaji mkubwa zaidi, kutengeneza na kutekeleza mikakati na mbinu za kibashara zenye ufanisi, na kuajiri watu wenyewe mtizamo na uzoefu katika biashara ili

kuiwezesha Bodi kujientesha kwa kutumia uwezo wake wote wa viwanda na maghala ya kuhifadhi bidhaa.



# SURA YA KUMI NA TISA

## UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA

### 19.0 Utangulizi

Sura hii inahusu ufanisi wa uziduaji ambao unajumuisha shughuli zote za uchimbaji wa malighafi (madini, gesi na mafuta) kutoka ardhini hadi kwa watumiaji.

Nilipitia utendaji wa mashirika ya umma yanayohusika na uziduaji katika sekta ya uziduaji wa madini, mafuta na gesi. Mashirika hayo ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli (PURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kwa upande wa madini nilikagua Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), na Kampuni ya STAMIGOLD na kubaini mapungufu mbalimbali.

Ukaguzi wangu ulibaini ucheleweshaji wa muda mrefu wa kutokuanza kwa shughuli chini ya leseni za utafutaji, Kushindwa kwa wenye leseni kuwasilisha ripoti za utafiti kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini, na kuchelewa katika kufanya utafiti wa msingi kwa uwezo wa ndani wa wananchi katika kutoa huduma katika sekta ya Mafuta na Gesi.

### 19.1 Ukaguzi wa uendeshaji wa shughuli za madini katika tasnia ya uziduaji

Ukaguzi wangu wa shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini katika sekta ya uziduaji katika mashirika ya umma ulibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuboresha utendaji:

#### 19.1.1 Ucheleweshaji wa muda mrefu wa kutokuanza kwa shughuli chini ya leseni za utafutaji wa madini na STAMIGOLD

Nilibaini kuwa kampuni ya STAMIGOLD ilipewa leseni nne za utafutaji madini kwa mwaka 2022. Hata hivyo, hakuna leseni yoyote kati ya hizo

iliyoanza shughuli za utafutaji ndani ya mwaka mmoja baada ya kutolewa kinyume na Kifungu cha 36(1)(a) cha Sheria ya uchimbaji madini ya mwaka 2010 (na kurekebishwa mwaka 2019), kinachoagiza wamiliki wa leseni za utafutaji madini kuanzisha shughuli hiyo ndani ya miezi mitatu baada ya leseni kutolewa. Ucheleweshaji wa shughuli ya utafutaji wa madini unatokana na ufinyu wa bajeti ya kugharamia shughuli pamoja na mikakati duni ya kusimamia shughuli za utafutaji au utafiti.

Taarifa nilizopata kutoka kampuni ya STAMIGOLD zinaeleza kuwa hifadhi ya dhahabu ndani ya sehemu ya leseni maalum ya uchimbaji wa madini kwa kampuni ya STAMIGOLD (SML 157/2003) inakadiriwa kuwa na takribani tani 2,303,148 za madini yenye dhahabu ambayo ni sawa na jumla ya wakia 72,875 za dhahabu ambapo uzalishwaji wake hautarajiwu kuendelea zaidi ya Agosti 2027. Hivyo basi, ni vyema shughuli za utafutaji kwa mujibu wa leseni zilizotajwa hapo juu zianzishwe bila kuchelewa zaidi ili kuongeza muda wa utendaji kazi na uendeshaji wa mgodi.

Kuna hatari ya kutopata faida inayotarajiwa kwani kampuni ya STAMIGOLD inaweza kupoteza haki ya leseni za utafutaji madini ambazo shughuli za utafutaji madini bado hazijaanza. Hii ni kwa sababu leseni hizo hazitarejeshwa tena kwa kampuni ya STAMIGOLD bali zitarejeshwa Serikalini kama inavyotakiwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

**Ninapendekeza kampuni ya STAMIGOLD ishirikiane na Wizara ya Madini kutafuta fedha kwa ajili ya utafutaji madini bila kuchelewa zaidi.**

#### **19.1.2 Ukosefu wa mipaka ya kudumu inayozunguka eneo la leseni ya uchimbaji madini huko Buhembwa**

Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya Good-Field International DMCC ziliingia Makubaliano ya ubia tarehe 29 Oktoba 2021 ambayo yalieleza majukumu ya kila mshirika wa ubia. STAMICO pamoja na mambo mengine ilitakiwa, kuhakikisha usalama wa eneo, na kushiriki katika usimamizi kuitia Bodi. Pia, lilipaswa kusafisha eneo hilo na kutoa huduma za kuchimba kwa kuzingatia viwango vya ushindani. Kampuni ya GoodField ilijitolea kushiriki katika usimamizi, ikitoa pesa kwa ajili ya mtaji na gharama za uendeshaji, kwa kuzingatia vifungu Na. 9 na 10 vya makubaliano ya ushirika wa pamoja.

Nilibaini kuwa watu wasioidhinishwa walivamia eneo la leseni ya madini ya Buhemba na kujihusisha na shughuli zisizoidhinishwa. Uvamizi huu unafanyika kutokana na ukosefu wa utaratibu na hatua za kiusalama na wamiliki wa leseni (STAMICO). Sikupata ushahidi wowote kuwa Shirika la Madini la Taifa lilikuwa linachukua hatua yoyote kuzuia uvamizi huo licha ya mamlaka yaliyotolewa chini ya kifungu cha 6.3 (d) cha mkataba wa ubia na kifungu cha 52(b) cha Sheria ya Sura 123 Madini kinachomtaka mwenye leseni ya uchimbaji kuweka mipaka na kutunza maeneo ya uchimbaji ipasavyo.

Ninapendekeza kuwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); (a) kuzingatia Mkataba wa Ubia uliosainiwa kwa kuhakikisha kuwa kuna mipaka thabiti inayozunguka eneo lenye leseni ya uchimbaji madini; na (b) kuchukua hatua sahihi za kuondoa wavamizi ndani ya eneo lenye Leseni ya Madini na kusitisha shughuli zote zinazofanywa ili kuhakikisha eneo linakuwa wazi bila vizuizi vyovyote.

#### **19.1.3 Kuchelewa kuanza kwa shughuli za uchimbaji madini katika mgodi wa Kiwira na kusababisha hasara ya shilingi milioni 257.33 zilizotumika katika ukarabati**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hakuwa shughuli zozote za uzalishaji zilizokuwa zikifanyika katika uchimbaji wa makaa ya mawe Kiwira tangu mwaka 2014 wakati umiliki ulipohamishiwa kikamilifu kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Hii ni kinyume na kifungu cha 47 (a) cha Sheria ya Madini (Sura ya 123 iliyorekebishwa mwaka 2019) kinachotaka Leseni maalumu za Madini kuanza kufanya kazi ndani ya miezi 18 kuanzia tarehe ya kutolewa. STAMICO ilipewa leseni maalumu Na. 233/2005 ya mwaka 2014. Katika mwaka 2021/22, shilingi milioni 257.33 zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa mgodi wa chini ya ardhi lakini hakuna fedha zilizotengwa katika mwaka 2022/23 kwa mradi huo ambao unaonesha dhamira duni ya kuwekeza katika mradi huo.

Kucheleweshwa kwa uzalishwaji kulihusishwa na ukosefu wa fedha zilizohitajika ili kukamilisha mchakato wa ukarabati unaohitajika, na ucheleweshwaji wa ununuzi wa vifaa vya kuimarissha kuta za mgodi.

Kuchelewa kuanza kwa shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe katika Migodi ya Makaa ya Mawe ya Kiwira kunasababisha kukosa fursa za mapato kwa Shirika la Madini la Taifa na uwezekano wa hasara ya shilingi milioni 257.33 zilizotumika mwaka 2021/22 kwa ajili ya ukarabati wa mgodi wa chini ya ardhi.

Ninapendekeza STAMICO itenge bajeti inayotosheleza kabla ya kuanzishwa kwa mradi na kutekeleza mradi huo bila kucheleva ili kuepusha ongezeko la gharama.

#### **19.1.4 Ukosefu wa mpango Kamili na utoaji huduma za kitaalamu kwa wachimbaji wadogo wa madini nchi nzima**

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2019, mchimbaji mdogo huelezewa kama mtu binafsi au taasisi zenyenye leseni ya msingi ya uchimbaji madini, na hutumia mashine ndogo au teknolojia ya mtaji wa awali kwa uwekezaji ambao hauzidi dola za Marekani milioni 5 au sawa na shilingi ya Tanzania zenyenye thamani hiyo.

Kifungu cha 27A (2)(k) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2019, kinaipa mamlaka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) kutoa huduma za kijiolojia ili kusaidia wachimbaji wadogo na wakubwa. Hata hivyo, baada ya ukaguzi wetu wa mipango ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini inayohusiana na kutimiza wajibu huu, tulibaini kutokuwapo kwa mpango kamili wa kutoa utaalamu kwa wachimbaji wadogo nchi nzima. Nilibaini mipango ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini inaandaliwa kwa kuzingatia mwaka wa fedha, bila kuweka vigezo maalumu vyatya ulinganishi na kujiridhisha kama lengo la kuwafikia wachimbaji wadogo linafanyika kwa usahihi.

Aidha, licha ya mpango mkakati ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini ukitaka utekelezaji wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini katika mikoa minne ifikapo tarehe 30 Juni 2023, nilibaini kuwa utaalamu ultolewa katika mikoa miwili tu Lindi na Morogoro. Kutoa utaalamu hafifu kunaibua mashaka kama msaada unaotolewa na taasisi hiyo kwa wachimbaji wadogo nchi nzima unatosha, na kunaonesha haja ya kuwa na mpango kamili, wafanyakazi wa ziada, na fedha zaidi ili kushughulikia pengo hili kwa ufanisi. Hali hii, inakwamisha maendeleo ya shughuli ndogo za uchimbaji madini na kupunguza mchango wao kwa pato la taifa.

**Ninapendekeza Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini;** (a) itengeneze mpango wa kina wa utoaji wa utaalamu kwa wachimbaji wadogo kote nchini; (b) ifanye tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa vikundi lengwa vyatya wachimbaji madini na kuandaa mipango ambayo inaweza kutekelezwa kila mwaka kwa malengo yaliyobainishwa wazi; na (c) iwasiliane na mamlaka inayohusika ili kuwezesha

upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mafunzo.

#### **19.1.5 Kutokuwapo kwa uchambuzi na uthibitisho wa taarifa na ripoti za utafiti za awali zilizowasilishwa na wamiliki wa haki za madini**

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwapo kwa mapungufu katika Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini wakati wa kutekeleza jukumu lake katika kuchambua na kuthibitisha taarifa za utafutaji wa madini. Upungufu uliibuka hasa kwa sababu Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini haichanganui na kuthibitisha taarifa za utafutaji kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 8 ya Kanuni za Madini (Benki ya Taifa ya Rasilimali za Madini) ya 2021 ambayo inamtaka Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini au mtu ye yeyote aliyeidhinishwa kuthibitisha taarifa ya madini, kanzidata na ripoti au taarifa zilizowasilishwa kabla ya kuzihifadhi.

Kutokuwapo kwa uchambuzi na uthibitisho wa taarifa kunatokana na ukosefu wa fedha ambazo zingewezesha upatikanaji wa programu ya tathmini ya uthibitisho wa taarifa. Ukosefu wa programu huzuia uwezo wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini wa kusimamia taarifa iliyopokelewa kutoka kwa wamiliki wa haki za madini.

Ni maoni yangu kuwa, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini hupokea aina mbalimbali za taarifa za utafutaji wa madini, ikiwamo tafiti za kijiofizikia, taarifa za uchimbaji, na matokeo ya majoribio, kukosekana kwa uchambuzi wa taarifa na uthibitisho huongeza hatari kubwa kuhusiana na taarifa za uchimbaji na kuwa na uwezekano wa kuwa na taarifa isyo sahihi. Aidha, kwa kuwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini hutoa taarifa kuhusiana na jiolojia na rasilimali za madini za Tanzania, na kwa ujumla husaidia wananchi kutafuta habari kuhusu masuala ya kijiolojia, kutokuwapo kwa uthibitisho huhatarisha upotoshaji wa taarifa kwa umma kwa ujumla.

**Ninapendekeza Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini itenye fedha katika bajeti yake ya uendeshaji kwa ajili ya ununuzi wa programu itakayohakikisha uthibitishwaji wa taarifa kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 8 ya Madini (National Mineral Resources Data Bank) ya mwaka 2021.**

### 19.1.6 Kushindwa kwa wenye leseni kuwasilisha ripoti za utafiti kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini

Nilipitia rejista ya taarifa za Kijiolojia na kubaini kuwa, ni wamiliki 14 pekee waliowasilisha takwimu za madini angalau mara moja katika mwaka 2022/23 kwa ajili ya Leseni 28 za Madini na Leseni Maalumu za Madini sawa na asilimia 12 kati ya jumla ya leseni 244 zilizotolewa na Tume ya Madini, hadi tarehe 30 Juni 2023. Hii ni kinyume na Kifungu cha 27 F (3) cha Sheria ya Madini, Sura 123. Hali hii inatokana na ukosefu wa taratibu za utekelezaji au uelewa mionganoni mwa wamiliki wa leseni kuhusu mahitaji ya kisheria inayotaka wamiliki wa leseni kuwasilisha ripoti za uchunguzi kwa taasisi ya jiolojia na utafiti wa madini.

Kwa maoni yangu kutofuata kanuni kunazuia ukusanyaji wa kina wa takwimu za madini, jambo linaloweza kuathiri maamuzi ya sera, utafiti na uwazi katika sekta ya madini.

**Ninapendekeza Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini iimarishe mbinu za utekelezaji, na iongeze kampeni za uhamasishaji kuhusu wajibu wa kisheria, na kuzingatia kuanzisha adhabu au motisha ili kuhakikisha wenye leseni wanawasilisha data kwa wakati unaofaa kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini .**

### 19.2 Ukaguzi wa uendeshaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia

Ukaguzi wangu wa sekta ya uziduaji katika mashirika ya umma kuhusiana na shughuli za petroli nilibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji uangalizi wa Serikali:

#### 19.2.1 Ucheleweshaji wa kuanza na kukamilika kwa miradi ya usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani shilingi bilioni 17.23

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa miradi mitatu iliyoundwa kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia kwenda sehemu mbalimbali kwa matumizi ya majumbani ilichelewa kukamilika kinyume na mpango (**Jedwali Na. 46**). Kwa mujibu wa mpango mkakati wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) 2018/19 - 2022/23, miradi hiyo ilipaswa kukamilika kufikia tarehe 30 Juni 2023, hata hivyo miradi hiyo ilikuwa katika hatua za awali.

Utekelezaji ulicheleweshwa kutokana na kutotolewa kwa fedha za kutosha kutoka kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuchelewa kuidhinishwa kwa vibali kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), mchakato wa ununuizi usio na ufanisi, na kuchelewesha malipo ya awali kwa makandarasi. Ucheleweshaji huu unaweza kusababisha ongezeko kubwa la gharama, na kuzuia umma kufaidika na chanzo cha nishati ya gharama nafuu, cha kuaminika na rafiki kwa mazingira na matumizi ya nyumbani.

**Jedwali Na. 46: Kuchelewa kuanza na Kukamilika kwa Mradi**

Na.	Mradi wa gesi asilia	Hali ya Mradi	mwaka wa kimkakati wa kukamilika (Sh. Bilioni)	(Sh. Bilioni)
1	Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mnazi mmoja na Mkuranga Ucheleweshwaji	Ucheleweshwa ji wa kuanza kwa ununuizi	2018/19 - 2022/23	13.27
2	Mradi wa usambazaji gesi asilia Trunkline kando ya Barabara ya Bagamoyo	Kuchelewa kukamilika, asimilia 29 tu imekamilika	2018/19 - 2022/23	3.26
3	Kuunganishwa kwa gesi asilia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es salaam na Mlimani City Dar es Salaam	Ucheleweshaji wa utekelezaji-Katika hatua ya ununuizi	2018/19 - 2022/23	0.7
<b>Jumla</b>				<b>17.23</b>

*Chanzo: Taarifa za utekelezaji wa miradi 2022/23*

Ninapendekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania; (a) lihakikishe vibali vya ujenzi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji vinapatikana kwa wakati na kuharakisha taratibu za ununuizi mahitaji kwa ajili ya miradi ya gesi; na (b) lishirikiane na Wakala wa Nishati Vijijini kuhakikisha fedha za mradi wa gesi zinapatikana kwa wakati.

### 19.2.2 Kutokuwapo kwa hifadhi ya Taifa ya Petroli

Wakati wa ukaguzi wa shughuli za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania , nilibaini kuwa, Tanzania kama nchi, haina Hifadhi ya Taifa ya Petroli ya kimkakati kwa ajili ya uhifadhi wa kimkakati wa mafuta ya petroli kama inavyotakiwa chini ya Kanuni za Taifa za Hifadhi ya Petroli za mwaka 2014. Kulingana na kanuni iliyotajwa uhifadhi wa mafuta utahusisha upatikanaji na usimamizi wa vifaa vya kuhifadhi kwa ajili ya kuendesha operesheni hii kwa urahisi. Kazi hizi zilipaswa kutekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ambalo linawajibika

kufunga, kudhibiti, kufuatilia na kusimamia uendeshaji wa Hifadhi ya Taifa ya Petroli.

Hii inasababishwa na ukosefu wa mkakati wa utekelezaji uliofanuliwa vizuri kwa uundaji na utunzaji wa hifadhi ya kitaifa ya mafuta ya petroli. Ukosefu wa Hifadhi ya Taifa ya Petroli ya Mkakati unaiweka nchi katika hatari ya kuwa na uhaba wa nishati wakati wa shida.

**Ninapendekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli, kwa kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali, zikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli Wakala wa Ununuvi wa Petroli, Mamlaka ya Bandari, Wizara ya Nishati, litengeneze mkakati wa utekelezaji wenye muundo mzuri, na wa kina unaobainisha mpango wa hatua kwa hatua wa kupata, kusimamia na kutunza Hifadhi ya Taifa ya Petroli. Mkakati huu unapaswa kueleza kwa kina majukumu, kalenda ya matukio, ugawaji wa rasilimali, na usimamizi wa vihatarishi.**

#### **19.2.3 Kuchelewa katika kufanya utafiti wa msingi kwa uwezo wa watoa huduma wa ndani (Local contents) katika kuhudumia sekta ya mafuta na gesi**

Lengo mojawapo la maudhui ya utoaji huduma kwa utaalamu wa ndani chini ya Kanuni za dhana ya ushirikishwaji wazawa wa ndani (Local content) ya mwaka 2017, Kanuni ya 4 (2); (a) inahitaji pamoja na mambo mengine ni kuandaa takwimu za msingi na taarifa ili kutambua uwezo wa sasa wa Tanzania kuajiriwa na makampuni ya ndani katika kutoa huduma; na (b) kufanya tathmini ya mahitaji ya uwezo unaohitajika na kuzalisha wataalamu wa Kitanzania katika sekta ya mafuta na gesi. Utafiti unalenga kubaini uwezo wa ndani wa wauzaji katika utoaji wa bidhaa na huduma zinazojumuisha huduma za kisheria, kifedha na kihandisi, Utafiti zaidi utatambua uwezo wa elimu kwa Watanzania katika sekta ya gesi. Mfano wa watoa huduma katika sekta ya gesi ni pamoja na, ulinzi, chakula, uhandisi na kadhalika.

Kulingana na andiko la awali kwa ajili ya kuandaa hadidu za rejea lilioandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), PURA ilipaswa kufanya utafiti wa msingi wa uwezo wa soko la watoa huduma wa ndani na ushindani ambapo utafiti ultakiwa kuwa umemalizika ifikapo tarehe 30 Juni 2023. Hata hivyo, utafiti huo haukufanyika kwa sababu hadidu za rejea za utafiti hazikuhitimishwa kwa ufanisi kutokana na ukosefu wa fedha.

Utafiti huo, ungewezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli na nchi kwa ujumla kupata uelewa kamili wa kukuza uwezo wa sekta ya watoa huduma wa ndani; hivyo kuwezesha kuwa na ufahamu muhimu ambao ungesaidia Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli kuunda mikakati bora ili kuendelea kutoa mchango katika ukuzaji wa watoa huduma wa ndani katika sekta ya gesi.

Kushindwa kufanya utafiti kunaichelewesha nchi na kuharibu mikakati na mipango juu ya ushiriki wa wataalamu wa ndani kwenye miradi ijayo katika sekta ya uziduaji ukiwamo mradi wa Gesi Asilia (LNG). Aidha, kunaweza kuchelewesha kuimarisha ushiriki wa ndani, uvumbuzi, na ushindani kwa shughuli zinazoendelea chini ya sekta ya petroli kama vile mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki.

Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli (PURA); (a) itenge bajeti ya kutosha na itoe kipaumbele kukamilishwa kwa utafiti wa uwezo wa watoa huduma wa ndani katika sekta ya gesi; na (b) ishirikishe wadau wa sekta husika katika mchakato wa utafiti ili kuimarisha ushirikiano na kuhakikisha ukusanyaji wa taarifa wa kina.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na bajeti kwa mwaka 2022/23

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
1.	Kampuni ya Ndege Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
2.	Kituo cha Uwekezaji APC	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
3.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
4.	Chuo Kikuu Ardhi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
5.	Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu Ardhi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
6.	Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu Ardhi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
7.	Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
8.	Chuo cha Ufundji Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
9.	Kampuni ya Uzalishaji na Ushauri Elekezi ya Chuo cha Ufundji Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
10.	Kitengo cha Uzalishaji na Ushauri Elekezi cha Chuo cha Ufundji Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
12.	Benki ya Azania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
13.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
14.	Benki Kuu ya Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
15.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
16.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
17.	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
18.	Bodi ya Korosho Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
19.	Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Korosho	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
20.	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
21.	Chuo cha Diplomasia	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
22.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Yenye shaka	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
23.	Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
24.	Chuo cha Elimu ya Biashara	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
25.	Bodi ya Usajili wa Makandarasi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
26.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
27.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
28.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
29.	Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
30.	Kampuni ya Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
31.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
32.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
33.	Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
34.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
35.	Bodi ya Bima ya Amana	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
36.	Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
37.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
38.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
39.	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
40.	Bodi ya Usajili wa Wahandisi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
41.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
42.	Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
43.	Mfuko wa Faida	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
44.	Tume ya Ushindani	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
45.	Baraza la Ushindani	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
46.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
47.	Kampuni ya Gesi Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
48.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
49.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
50.	Kampuni ya Nyumba na Mafao	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
51.	Chuo cha Uhaisibu Arusha	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
52.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
53.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
54.	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
55.	Chuo cha Ustawi wa Jamii	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
56.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
57.	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
58.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
59.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
60.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
61.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
62.	Kituo cha Elimu Kibaha	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
63.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
64.	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
65.	Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
66.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
67.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
68.	Mamlaka ya Udhibili wa Usafiri wa Nchi Kavu	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
69.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
70.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
71.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
72.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
73.	Kampuni ya Huduma za Meli	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
74.	Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
75.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
76.	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
77.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
78.	Kampuni ya MCB	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
79.	Bohari Kuu ya Dawa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
80.	Kampuni ya Mkulazi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
81.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
82.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
83.	Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
84.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
85.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
86.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
87.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
88.	Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
89.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	Yenye shaka	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
90.	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
91.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
92.	Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
93.	Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
94.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
95.	Kampuni ya Majengo ya Biashara ya Jiji la Mwanza	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
96.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
97.	Chuo Kikuu Mzumbe	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
98.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
99.	Baraza la Sanaa Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
100.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
101.	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
102.	Baraza la Taifa la Ujenzi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
103.	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
104.	Shirika la Taifa la Maendeleo	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
105.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
106.	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
107.	Baraza la Mitihani la Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
108.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
109.	Shirika la Nyumba la Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
110.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
111.	Chuo cha Usafirishaji cha Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
112.	Shirika la Bima la Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
113.	Baraza la Kiswahili la Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
114.	Makumbusho ya Taifa la Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
115.	Kampuni ya Ranchi za Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
116.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
117.	Baraza la Michezo Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
118.	Chuo cha Sukari cha Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
119.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
120.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
121.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
122.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
123.	Taasisi ya Saratani ya Ocean Road	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
124.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
125.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
126.	Kampuni ya Uwekezaji ya PPF na DCC	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
127.	Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
128.	Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
129.	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
130.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
131.	Mfuko wa Reli	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
132.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
133.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
134.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
135.	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
136.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
137.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
138.	Mfuko wa Maendeleo ya Michezo	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
139.	Kampuni ya STAMIGOLD	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
140.	Shirika la Madini la Taifa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
141.	Bodi ya Sukari Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
142.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
143.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
144.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
145.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
146.	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
147.	Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
148.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaoilojia Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
149.	Shirika la Utangazaji Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
150.	Shirika la Viwango Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
151.	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
152.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
153.	Bodi ya Kahawa Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
154.	Benki ya Biashara Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
155.	Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
156.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
157.	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
158.	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
159.	Bodi ya Pamba Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
160.	Bodi ya Maziwa Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
161.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
162.	Shirika la Umeme Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
163.	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
164.	Kampuni ya Mbolea Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
165.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
166.	Taasisi ya Utafiti wa Uvvi Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
167.	Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
168.	Tasisi ya Utafiti Wa Misitu Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
169.	Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
170.	Taasisi ya Elimu Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
171.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
172.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
173.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
174.	Bodi ya Nyama Tanzania	Yenye shaka	Limekidhi	Limekidhi
175.	Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
176.	Soko la Ubadilishanaji Bidhaa Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
177.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
178.	Hifadhi za Taifa Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
179.	Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
180.	Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
181.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
182.	Shirika la Posta Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
183.	Bodi ya Pareto Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
184.	Shirika la Reli Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
185.	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
186.	Bodi ya Mkonge Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
187.	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
188.	Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania	Yenye shaka	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
189.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
190.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
191.	Bodi ya Utalii Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
192.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
193.	Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
194.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
195.	Bodi ya Rufani za Kodi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
196.	Baraza la Rufani za Kodi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
197.	Mfuko wa Mafunzo ya Usafiri wa Anga	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
198.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
199.	Bodi ya Chai Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
200.	Benki ya TIB Maendeleo	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
201.	Benki ya TIB Rasilimali	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
202.	Kampuni ya TTCL Pesa	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
203.	Mfuko wa wadhamini wa Kampuni ya TTCL Pesa	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
204.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi na baadhi ya mapungufu
205.	Kampuni ya Ubungo Plaza	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
206.	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
207.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
208.	Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
209.	Chuo Kikuu cha Dodoma	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
210.	Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
211.	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi	Inayoridhisha	Limekidhi na baadhi ya mapungufu	Limekidhi
212.	Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Gharani	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
213.	Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi
214.	Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja katika Milki	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi

Na	Jina shirika/Taasisi	Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake	Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti
215.	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi	Inayoridhisha	Limekidhi	Limekidhi

#### Kiambatisho Na. II: Taasisi zilizopata hasara au nakisi kwa miaka miwili

Na.	Jina la Taasisi	2022/23 (Sh. Milioni)	2021/22 (Sh. Milioni)
<b>Mashirika ya kibiashara</b>			
1.	Shirika la Reli Tanzania	(100,704.74)	(190,013.51)
2.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	(76,564.00)	(7,840.00)
3.	Kampuni ya Ndege ya Tanzania	(56,640.69)	(35,238.36)
4.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	(41,568.55)	(517.97)
5.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania	(6,103.53)	(3,855.71)
6.	Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro	(4,236.20)	(4,931.14)
7.	Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania	(1,239.19)	(791.68)
8.	Kituo cha Uwekezaji APC	(1,200.30)	(1,946.02)
9.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	(894.00)	(19,229.00)
10.	Soko la Bidhaa Tanzania	(722.57)	(509.24)
11.	Kampuni ya Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam	(233.30)	(2.28)
<b>Mashirika yasiyo ya kibiashara</b>			
12.	Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya	(156,770.72)	(205,952.79)
13.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam	(12,559.36)	(15,324.80)
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	(3,190.28)	(56.36)
15.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli	(2,230.62)	(355.95)
16.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	(1,696.82)	(5,517.66)
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	(1,522.552)	(425.79)
18.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	(1,296.21)	(1,224.09)
19.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	(1,281.04)	(677.32)
20.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega	(1,122.17)	(284.82)
21.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea	(626.48)	(633.46)
22.	Baraza la Taifa la Ujenzi	(330.76)	(305.43)
23.	Bodi ya Mkonge Tanzania	(255.72)	(202.93)
24.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	(195.46)	(731.06)
25.	Bodi ya Pamba Tanzania	(192.62)	(384.69)
26.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	(182.34)	(424.83)
27.	Tasisi ya Utafiti Wa Misitu Tanzania	(160.61)	(193.50)
28.	Mfuko wa Dhamana ya Kuendeleza Sekta ya Korosho	(146.40)	(497.74)
29.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	(106.25)	(59.09)
30.	Baraza la Rufani za Kodi	(50.40)	(52.24)
31.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu	(49.89)	(103.40)
32.	Bodi ya Maziwa Tanzania	(10.62)	(51.79)
33.	Bodi ya Pareto Tanzania	(8.73)	(8.87)
34.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	(8.85)	(23.75)

Chanzo: *Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2022/23*

#### Kiambatisho Na. III: Mashirika yaliyopata faida 2020/21 na hasara/nakisi 2022/23

Na.	Jina la Taasisi	2022/23 (Sh. Milioni)	2021/22 (Sh. Milioni)
<b>Mashirika ya Biashara</b>			
1.	Kampuni ya Ubungo Plaza	(8,831.84)	423.80
2.	Kampuni ya Gesi Tanzania	(4,588.00)	277.00
3.	Shirika La Posta Tanzania	(1,343.79)	30,699.40
4.	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO)	(785.16)	129.55
5.	Kampuni ya TTCL Pesa	(352.74)	55.14
6.	Kampuni ya Nyumba na Mafao	(59.82)	627.69

Na.	Jina la Taasisi	2022/23 (Sh. Milioni)	2021/22 (Sh. Milioni)
7.	Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	(7.21)	81.66
<b>Mashirika yasiyo ya kibiashara</b>			
8.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	(19,109.10)	13,869.62
9.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	(6,310.62)	5,953.73
10.	Bodi ya Utalii Tanzania	(6,027.74)	7,232.69
11.	Hifadhi za Taifa Tanzania	(5,794.47)	21,121.43
12.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga	(3,744.36)	332.48
13.	Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	(1,530.52)	1,550.90
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	(1,280.03)	68,935.46
15.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti Wa Dawa (NIMR)	(1,008.84)	6,500.24
16.	Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia	(733.08)	770.08
17.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	(725.15)	1,273.47
18.	Kituo cha Komputa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	(416.18)	63.88
19.	Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania	(131.10)	597.35
20.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	(103.17)	374.77
21.	Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia	(88.43)	7,721.71
22.	Bodi ya Rufani za Kodi	(49.13)	123.73
23.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	(28.18)	22.48
24.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu	(4.35)	1,656.19

#### Kiambatisho Na. IV: Taasisi zenyе uwiano wa ukwasi chini ya moja

Na.	Jina la Taasisi	Jumla ya Mali za Muda Mfupi (Sh. Milioni)	Jumla ya Madeni ya Muda Mfupi (Sh.Milioni)	Uwiano
<b>Mashirika ya kibiashara</b>				
1.	Kampuni ya Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam	1,144.71	1,420.04	0.81
2.	Kampuni ya Gesi Tanzania	20,331.00	25,707.00	0.79
3.	Kampuni ya Uwekezaji ya PPF na DCC	674.02	883.32	0.76
4.	Kampuni ya STAMIGOLD	36,671.37	57,465.49	0.64
5.	Kampuni ya Mbolea Tanzania	8,022.52	15,796.25	0.51
6.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	639,150.52	1,329,688.23	0.48
7.	Shirika la Posta Tanzania	37,225.03	78,721.10	0.47
8.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	189,423	409,176.00	0.46
9.	Shirika la Umeme Tanzania	907,119.00	2,418,523	0.38
10.	Kampuni ya Ndege ya Tanzania	155,670.28	461,897.09	0.34
11.	Kampuni ya Huduma ya Meli	4,923.43	16,908.61	0.29
12.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania	2,162.23	9,889.37	0.22
13.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	711.50	3,903.94	0.18
<b>Mashirika yasiyo ya Kibiashara</b>				
14.	Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia	17,527.83	17,918.63	0.98
15.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	2,332.31	2,384.26	0.98
16.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	1,245.99	1,294.44	0.96
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea	1,624.11	1,741.60	0.93
18.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga	873.84	951.64	0.92
19.	Baraza la Kiswahili la Taifa	72.33	80.55	0.90
20.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	783.85	869.97	0.90
21.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	4,949.62	5,585.68	0.89
22.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	147,436.77	168,274.87	0.88
23.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	352.65	401.41	0.88
24.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	6,320.02	7,248.72	0.87
25.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga	7,753.30	9,036.77	0.86
26.	Shirika la Utangazaji Tanzania	10,177.12	12,249.84	0.83
27.	Hospital ya Taifa Muhimbili	66,428.36	81,399.69	0.82
28.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	6,437.68	8,038.50	0.8

Na.	Jina la Taasisi	Jumla ya Mali za Muda Mfupi (Sh. Milioni)	Jumla ya Madeni ya Muda (Sh.Milioni)	Uwiano
29.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi	1,853.52	2,346.09	0.79
30.	Kampuni ya Ranchi za Taifa	11,323.89	14,822.51	0.76
31.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	63.43	82.97	0.76
32.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma	2,271.61	3,070.68	0.74
33.	Bodi ya Pamba Tanzania	3,412.57	4,904.18	0.70
34.	Bodi ya Utalii Tanzania	1,716.34	2,602.37	0.66
35.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	2,248.76	3,417.19	0.66
36.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi	1,739.44	2,665.81	0.65
37.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	780.24	1,224.16	0.64
38.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	8,898.05	14,370.01	0.62
39.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	1,302.49	2,158.91	0.60
40.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	13,350.27	22,549.72	0.59
41.	Baraza la Rufani za Kodi	40.13	68.87	0.58
42.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	1,753.46	3,169.24	0.55
43.	Hifadhi za Taifa Tanzania	18,589.02	37,805.79	0.49
44.	Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila	10,532.11	22,460.02	0.47
45.	Tasisi ya Utafiti Wa Misitu Tanzania	908.52	1,913.02	0.47
46.	Bodi ya Mkonge Tanzania	1,755.65	3,842.83	0.46
47.	Makumbusho ya Taifa la Tanzania	254.24	561.72	0.45
48.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati	6,435.67	14,658.55	0.44
49.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega	1,049.18	2,471.20	0.42
50.	Balaza la Sanaa Tanzania	194.69	510.82	0.38
51.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	1,340.60	3,574.59	0.38
52.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania	94.93	256.43	0.37
53.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	12,497.97	37,102.70	0.34
54.	Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania	1,341.40	4,030.93	0.33
55.	Kituo cha Komputa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	457.36	1,487.12	0.31
56.	Bodi ya Maziwa Tanzania	61.19	259.38	0.24
57.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu	61.32	261.24	0.23
58.	Baraza la Ushindani	28.63	195.19	0.15
59.	Bodi ya Rufani za Kodi	8.26	182.19	0.05
60.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	2.19	74.31	0.03
61.	Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje	2,188.23	99,843.93	0.02
62.	Bodi ya Pareto Tanzania	19.09	2,019.75	0.01
63.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania	2,076.83	262,533.49	0.01

#### Kiambatisho Na. V: Taasisi za umma zenyenye madeni zaidi ya mtaji

Na.	Jina la Taasisi	Jumla la madeni (Sh.milioni)	Mtaji (Sh. Milioni)	Uwiano (Asilimia)
Taasisi za kibiashara				
1.	Shirika la Reli Tanzania	11,532,469.87	141,053.14	8176
2.	Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu Ardhi	3,283.96	227.25	1445
3.	Kampuni ya MCB	2,565.77	622.42	412
4.	Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing	5,919.02	1,516.40	390
5.	Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)	15,586,904.00	5,962,862.00	261
6.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	82,433.38	33,630.55	245
7.	Kituo cha Uwekezaji APC	20,877.94	8,555.36	244
8.	Shirika la mawasiliano Tanzania	409,195.00	181,951.00	225

9.	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	2,138.09	1,223.13	175
10.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	33,250.00	19,659.00	169
11.	Kampuni ya Mbolea Tanzania	21,200.54	13,417.66	158
12.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	2,290,044.07	1,465,210.56	156
<b>Taasisi zisizo za kibiashara</b>				
13.	Taasisi ya Utafiti wa Uvvi Tanzania	23,146.09	1,701.09	1361
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	484,485.92	109,685.81	442
15.	Bodi ya Rufani za Kodi	182.19	44.67	408
16.	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	111,822.08	29,402.89	380
17.	Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma	194,406.09	55,929.70	348
18.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	49,129.33	15,498.27	317
19.	Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia	17,918.63	7,505.03	239
20.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano	134.45	67.24	200
21.	Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje	99,843.93	50,412.20	198
22.	Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Gharani	970.46	506.08	192
23.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	401.41	258.05	156
24.	Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	2,776.81	1,791.83	155
25.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	36,027.69	30,126.25	120
26.	Bohari Kuu ya Dawa	475,856.12	398,316.68	119
27.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	65,555.64	56,582.41	116
28.	Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Uzalishaji Chuo cha Ufundu Arusha - Kikuletwa	886.11	785.82	113

#### Kiambatisho Na. VI:Mashirika yenye madeni ya Muda mrefu wanayodai

Na.	Jina la Taasisi ya Umma	Shilingi (Milioni)
1.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	808,105.73
2.	Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania	475,158.56
3.	Shirika la Umeme Tanzania	435,437.50
4.	Bohari Kuu ya Dawa	366,322.49
5.	Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya	208,316.60
6.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	107,412.00
7.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	92,835.45
8.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania	57,153.71
9.	Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania	35,208.66
10.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	33,744.45
11.	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi	30,827.90
12.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	28,608.98
13.	Shirika la Nyumba la Taifa	24,894.78
14.	Shirika la Bima la Taifa	24,522.87
15.	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote	23,265.55
16.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam	18,979.38
17.	Chuo Kikuu cha Dodoma	16,408.02
18.	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira	16,338.81
19.	Bodi ya Usajili wa Makandarasi	15,733.00
20.	Kampuni ya Ranchi za Taifa	15,643.01
21.	Kampuni ya Ndege Tanzania	13,429.21
22.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga	9,654.00
23.	Shirika la Madini la Taifa	8,304.93
24.	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	7,184.62
25.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu	5,050.68
26.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	4,956.41
27.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	3,352.93
28.	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini	3,120.24
29.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	2,537.15
30.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli	2,517.78

31.	Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi	2,103.74
32.	Chuo cha Usafirishaji cha Taifa	1,649.80
33.	Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania	1,642.41
34.	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	1,570.30
35.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	1,527.63
36.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	1,395.01
37.	Tume ya Ushindani	1,222.47
38.	Chuo cha Ufundji Arusha	1,101.69
39.	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	956.84
40.	Bodi ya Sukari Tanzania	939.61
41.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	868.27
42.	Mfuko wa Dhamana ya Kuendeleza Sekta ya Korosho	741.6
43.	Taasisi ya Elimu Tanzania	739.51
44.	Chuo cha Ustawi wa Jamii	729.38
45.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	578.61
46.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	544.42
47.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	522.13
48.	Chuo Kikuu Ardhi	406.1
49.	Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka	395.03
50.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	382.79
51.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea	353.15
52.	Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila	299.84
53.	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	239.34
54.	Makumbusho ya Taifa la Tanzania	192.88
55.	Bodi ya Utalii Tanzania	184.75
56.	Chuo Kikuu Mzumbe	126.31
57.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	121.33
58.	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	105.51
59.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	98.47
60.	Bodi ya Bima ya Amana	43.16
61.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	41.1
62.	Bodi ya Nyama Tanzania	10.7
63.	Baraza la Kiswahili la Taifa	7.4
64.	Bodi ya Maziwa Tanzania	6.23
65.	Chuo cha Sukari cha Taifa	4.77
66.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	1.94
Jumla		2,916,879.62

Chanzo: Taarifa za madeni za mashirika ya Umma

#### Kiambatisho Na. VII: Mashirika ya umma yenye madeni wanayodaiwa

Na.	Jina la Shirika	Kiasi (Sh. Milioni)
1.	Shirika la Reli Tanzania	1,074,717.69
2.	Shirika la Umeme Tanzania	677,851.52
3.	Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya	335,859.60
4.	Shirika la Mawasiliano Tanzania	319,892.00
5.	Bohari Kuu ya Dawa	197,432.07
6.	Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania	152,725.00
7.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	78,361.74
8.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	69,944.48
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam	66,211.04
10.	Kampuni ya STAMIGOLD	40,847.34
11.	Hifadhi za Taifa Tanzania	37,805.79
12.	Shirika la Bima la Taifa	33,287.93
13.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	30,927.00

Na.	Jina la Shirika	Kiasi (Sh. Milioni)
14.	Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania	25,380.76
15.	Shirika la Nyumba la Taifa	25,773.81
16.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi	24,544.84
17.	Kampuni ya Ndege Tanzania	24,132.68
18.	Shirika la Madini la Taifa	19,962.76
19.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	18,736.00
20.	Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila	17,066.94
21.	Bodi ya Korosho Tanzania	15,800.64
22.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	14,305.00
23.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma	12,407.87
24.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	10,519.37
25.	Shirika la Utangazaji Tanzania	9,281.00
26.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga	8,536.83
27.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	7,984.05
28.	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	7,829.42
29.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	7,248.72
30.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga	6,973.00
31.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	6,842.54
32.	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo	6,711.78
33.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	5,839.77
34.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam	5,699.36
35.	Chuo Kikuu cha Dodoma	5,481.22
36.	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania	5,111.06
37.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	4,454.29
38.	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	4,427.00
39.	Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania	4,246.99
40.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania	4,116.42
41.	Chuo Kikuu Mzumbe	3,975.88
42.	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini	3,616.27
43.	Baraza la Mitihani la Tanzania	3,486.50
44.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu	3,361.00
45.	Shirika la Viwango Tanzania	3,267.15
46.	Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania	3,094.00
47.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	2,626.54
48.	Chuo cha Uhasisbu Arusha	2,580.68
49.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara	2,484.63
50.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	2,362.20
51.	Bodi ya Mkonge Tanzania	2,351.70
52.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	2,343.61
53.	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania	1,997.71
54.	Bodi ya Pareto Tanzania	1,906.11
55.	Bodi ya Utalii Tanzania	1,659.00
56.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa	1,302.85
57.	Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja katika Milki	1,293.17
58.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania	1,252.33
59.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	1,239.03
60.	Chuo cha Diplomasia	1,237.88
61.	Bodi ya Sukari Tanzania	1,056.31
62.	Kampuni ya Gesi Tanzania	1,048.00
63.	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira	1,022.00
64.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama	963.46

Na.	Jina la Shirika	Kiasi (Sh. Milioni)
65.	Shirika la Taifa la Maendeleo	952.55
66.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea	950.00
67.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	925.21
68.	Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania	923.00
69.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	828.45
70.	Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania	800.15
71.	Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	756.20
72.	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	746.07
73.	Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	715.59
74.	Kampuni ya Mkulazi	662.26
75.	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji	627.77
76.	Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania	563.52
77.	Kituo cha Elimu Kibaha	527.55
78.	Baraza la Sanaa Tanzania	510.80
79.	Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia	456.15
80.	Tume ya Ushindani	426.33
81.	Mfuko wa Mafunzo ya Usafiri wa Anga	395.00
82.	Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka	376.46
83.	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	367.93
84.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	306.48
85.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	287.21
86.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania	256.00
87.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	233.02
88.	Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania	214.50
89.	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	209.97
90.	Bodi ya Wataalamu wa Ununuza na Ugavi Tanzania	187.18
91.	Baraza la Ushindani	177.60
92.	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana	172.00
93.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi	145.03
94.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi	139.89
95.	Kituo cha Uwekezaji APC	139.15
96.	Kampuni ya TTCL Pesa	136.52
97.	Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania	120.66
98.	Soko la Ubadilishanaji Bidhaa Tanzania	105.00
99.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	102.31
Jumla		3,492,248.84

#### Kiambatisho Na. VIII: Fedha za bajeti zilizotolewa kulinganisha na fedha zilizoidhinishwa

Na.	Jina la Taasisi	Bajeti	Kiasi	Nakisi	Asilimi
		iliyoidhinishwa	Kilichotolewa	bajeti ya	aya nakisi
Shilingi milioni					
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo	130.00	-	130	100
2.	Chuo Kikuu cha Dodoma -(Ujenzi wa bweni la wanafunzi)	500.00	-	500	100
3.	Shirika la Mawasiliano Tanzania (Serikali na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote)	86,051.26	2,631.51	83,419.75	97
4.	Hospitali ya Taifa Muhimbili	60,712.93	8,826.77	51,886.15	85
5.	Balaza la Sanaa Tanzania	905.45	171.55	733.90	81
6.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma	30,470.00	6,421.00	24,049.00	79
7.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara	20,947.29	4,965.82	15,981.47	76
8.	Taasisi ya Elimu Tanzania	107,206.84	30,650.28	76,556.56	71
9.	Chuo Kikuu Ardhi	39,491.27	13,769.52	25,722	65

Na.	Jina la Taasisi	Bajeti iliyoidhinishwa	Kiasi Kilichotolewa	Nakisi ya bajeti	Asilimi aya nakisi
<b>Shilingi milioni</b>					
10.	Bodi ya Maziwa Tanzania	2,928.04	1,067.55	1,860.49	64
11.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	1,551.84	600.00	951.84	61
12.	Soko la Bidhaa Tanzania	2,606.88	1,038.33	1,568.55	60
13.	Bodi ya Utalii Tanzania	13,446.39	5,747.70	7,698.69	57
14.	Ofisi ya Taifa ya Takwimu	949,213.37	430,136.25	519,077.12	55
15.	Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje	5,990.52	2,920.35	3,070.17	51
16.	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania	1,806.35	982.48	823.86	46
17.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	28,311.43	16,122.61	12,188.82	43
18.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	35,244.16	20,251.83	14,992	43
19.	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	102,812.15	59,641.66	43,170.49	42
20.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	892.59	550.00	343	38
21.	Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania	9,052.49	5,595.81	3,456.68	38
22.	Shirika la Utangazaji Tanzania	37,431.98	23,183.67	14,248.31	38
23.	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini	4,100.68	2,605.24	1,495.44	36
24.	Taasisi ya Saratani ya Ocean Road	29,601.04	18,894.06	10,707	36
25.	Bodi ya Kahawa Tanzania	2,757.07	1,811.44	945.63	34
26.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu	756.99	499.62	257.37	34
27.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	2,135.86	1,449.47	686.39	32
28.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	1,800.00	1,230.48	569.52	32
29.	Kituo cha Elimu Kibaha	11,175.12	7,753.17	3,421.95	31
30.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	3,904.84	2,777.87	1,126.97	29
31.	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	22,915.03	16,481.20	6,433.83	28
32.	Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia	185.70	137.73	47.97	26
33.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi	5,615.16	4,186.61	1,428.55	25
34.	Tume ya Ushindani	3,882.75	2,945.33	937.42	24
35.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania	4,459.66	3,413.08	1,047	23
36.	Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa	15,678.50	12,204.09	3,474.41	22
37.	Bohari Kuu ya Dawa	200,000.00	157,600.00	42,400	21
38.	Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi	16,065.42	12,955.49	3,109.93	19
39.	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania	3,321.80	2,721.25	600.55	18
40.	Ofisi ya Hakimiliki Tanzania	2,039.35	1,690.48	348.87	17
41.	Chuo cha Diplomasia	4,720.35	4,002.23	718	15
42.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro	120,053.50	102,707.25	17,346.25	14
43.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika	5,915.35	5,067.46	847.89	14
44.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma	2,981.74	2,572.71	409.03	14
45.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	2,216.90	1,917.30	299.60	14
46.	Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka	6,404.60	5,509.98	894.62	14
47.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti Wa Dawa	12,418.69	10,803.77	1,614.92	13
48.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	42,091.26	36,855.39	5,236	12
49.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	8,497.60	7,480.13	1,017.47	12
50.	Chuo cha Uhaisibu Arusha	16,831.14	14,894.62	1,956	12
<b>Jumla</b>		<b>2,090,229.33</b>	<b>1,078,442.14</b>	<b>1,011,807.43</b>	

*Chanzo: Taarifa za utekelezaji wa bajeti na taarifa za fedha*

**Kiambatisho Na. IX: Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani**

Na. .	Jina la Taasisi	Bajeti iliyoidhinish wa	Kiasi Kilichokusan ywa	Makusanyo Pungufu	Asilimia ya nakisi ya bajeti
				Shilingi milioni	
1.	Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari	60	7.14	52.86	88
2.	Tasisi ya Utafiti Wa Misitu Tanzania	1,002.75	156.51	846.24	84
3.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	1,533.39	442.8	1,090.59	71
4.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe	1,153	338	815.3	71
5.	Bodi ya Utalii Tanzania	439.89	133.79	306.1	70
6.	Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania	448	145.59	302.41	68
7.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	125,825.89	44,837.04	80,988.85	64
8.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibailolojia Tanzania	1,763.67	746.76	1,016.91	58
9.	Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba	96,094.77	42,244.22	53,850.55	56
10.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania	3,852.57	1,712.24	2,140.33	56
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako	1,348.27	664.72	683.55	51
12.	Bodi ya Korosho Tanzania	6,096.70	3,022.62	3,074.08	50
13.	Kampuni ya TTCL Pesa	1,955.32	976.53	978.79	50
14.	Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro	6,777.09	3,431.14	3,345.95	49
15.	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijiini	2,131.63	1,106.42	1,025.21	48
16.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi	558.45	305.18	253.27	45
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi	2,066.44	1,132.14	934.3	45
18.	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania	2,633.58	1,470.53	1,163.05	44
19.	Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka	8,175.73	4,724.93	3,450.80	42
20.	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira	28,042.56	16,837.47	11,205.09	40
21.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega	3,060.96	1,937.76	1,123.20	37
22.	Baraza la Taifa la Ujenzi	1,804.97	1,129.99	674.98	36
23.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara	723.58	463.7	259.88	36
24.	Chuo cha Elimu ya Biashara	32,734.20	21,193.15	11,541.05	35
25.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	3,045.20	2,002.51	1,042.69	34
26.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	5,845.58	3,846.55	1,999.03	34
27.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika	2,360.00	1,555.12	804.88	34
28.	Kampuni ya Huduma ya Meli	9,293.59	6,159.47	3,134.12	34
29.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo	159.92	106.31	53.61	34
30.	Shirika la Utangazaji Tanzania	15,809.17	10,517.18	5,291.99	33
31.	Bodi ya Pamba Tanzania	4,595.47	3,065.07	1,530.40	33
32.	Chuo Kikuu Ardhi	13,151.39	8,820.92	4,330.47	33
33.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	2,901.07	1,985.06	916.01	32
34.	Soko la Bidhaa Tanzania	250	172.56	77.44	31
35.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	8,525.10	5,975.51	2,549.59	30
36.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara	6,712.08	4,726.43	1,985.65	30
37.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma	4,718.66	3,343.04	1,375.62	29
38.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	14,546.71	10,441.78	4,104.93	28
39.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	1,744.39	1,264.52	479.87	28
40.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	12,056.95	8,748.69	3,308.26	27
41.	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma	2,249.94	1,634.15	615.79	27
42.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi Wa Mazingira Bukoba	5,525.32	4,035.21	1,490.11	27
43.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	9,191.16	6,743.94	2,447.22	27
44.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	35,011.89	25,709.97	9,301.92	27
45.	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	188.96	138.96	50	26
46.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	11,437.19	8,564.40	2,872.79	25
47.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro	18,152.76	14,041.49	4,111.27	23
48.	Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania	14,500.00	11,226.95	3,273.05	23
49.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu	136.6	107.34	29.26	21
50.	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	6,361.74	5,008.65	1,353.09	21

Na. .	Jina la Taasisi	Bajeti iliyoidhinish wa	Kiasi Kilichokusan ywa	Makusanyo Pungufu	Asilimia ya nakisi ya bajeti
		Shilingi milioni			
51.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma	32,121.91	25,307.56	6,814.35	21
52.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi- Nachingwea	4,396.67	3,465.72	930.95	21
53.	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	78,510.99	62,542.82	15,968.17	20
54.	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	21,311	17,048	4262.84	20
55.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe	1,600.00	1,297.87	302.13	19
56.	Kituo cha Elimu Kibaha	1,706.95	1,399.25	307.7	18
57.	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi	9,262.49	7,609.22	1,653.27	18
58.	Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania	1,975.00	1,640.02	334.98	17
59.	Baraza la Kiswahili la Taifa	416.75	347.26	69.49	17
60.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya	16,442.97	13,870.67	2,572.30	16
61.	Bodi ya Sukari Tanzania	2,051.85	1,757.18	294.67	14
62.	Chuo cha Diplomasia	3,601.21	3,098.70	502.51	14
63.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine	37,263.46	32,084.24	5,179.22	14
64.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili	35,064.17	30,664.45	4,399.72	13
65.	Kituo cha Uwekezaji APC	4,976.24	4,468.28	507.96	10
66.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti Wa Dawa	9,636.68	8,682.11	954.57	10
<b>Jumla</b>		<b>799,092.59</b>	<b>514,385.5</b>	<b>284,707.23</b>	

*Chanzo: Taarifa za utekelezaji wa bajeti na taarifa za fedha*

#### Kiambatisho Na. X: Mashirika ya umma yenyeye mapungufu katika dhamana za zabuni

Mashirika yenyeye Mikataba isiyo na dhamana			
Na.	Jina la Shirika	Idadi ya mikataba	Kiasi
<b>Mikata yenyeye kiasi kwa (Sh. Milioni)</b>			
1	Bohari Kuu ya Dawa	5	8,073.44
2	Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme	8	7,978.88
3	Kampuni ya Ranchi za Taifa	3	2,890.39
4	Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete	8	2,883.97
5	Shirika la Nyumba la Taifa	1	2,337.50
6	Hospitali ya Taifa Muhimbili	5	1,513.13
7	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	5	1,498.34
8	Shirika la Umeme Tanzania	2	1,275.00
9	Benki ya Biashara Tanzania	3	759.13
10	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga	7	587.07
11	Chuo Kikuu cha Dodoma	8	451.16
12	Chuo cha Diplomasia	6	391.24
13	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	3	246.79
14	Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila	2	227.53
<b>Jumla</b>		<b>66</b>	<b>31,113.57</b>
<b>Mashirika yalizosaini mikataba kabla ya kuwasilishwa kwa dhamana</b>			
1	Chuo Kikuu cha Dodoma	12	2,387.06
2	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	7	1,428.11
3	Shirika la PostaTanzania	3	1,258.21
4	Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila	3	993.82
5	Benki ya Biashara Tanzania	3	616.50

<b>6</b>	Shirika la Reli Tanzania	<b>2</b>	<b>447.89</b>
<b>7</b>	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	<b>1</b>	<b>29.8</b>
<b>Jumla</b>		<b>31</b>	<b>7,161.39</b>
<b>Mikataba yenye Kiasi kwa dola za Marekeni ("milioni")</b>			
<b>1</b>	Shirika la Reli Tanzania	<b>1</b>	<b>3.34</b>
<b>2</b>	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	<b>1</b>	<b>0.17</b>
<b>Jumla</b>		<b>2</b>	<b>3.51</b>
<b>Mikataba yenye kiasi kwa Euro "milioni"</b>			
<b>1</b>	Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro	<b>1</b>	<b>0.67</b>
<b>Jumla</b>		<b>1</b>	<b>0.67</b>

**Chanzo:** faili za Ununuizi

#### Kiambatisho Na. XI: Taasisi zilizochelewa kupokea bidhaa na huduma

Na.	Jina la Taasisi	Idadi ya Mikataba	Kiasi cha Mkataba (Sh. Milioni)	Muda uliochelewa (Siku)
<b>1.</b>	Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania	<b>1</b>	<b>5,587.69</b>	<b>30</b>
<b>2.</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga	<b>7</b>	<b>3,158.53</b>	<b>60 hadi 240</b>
<b>3.</b>	Shirika la Mawasiliano Tanzania	<b>2</b>	<b>1,662.48</b>	<b>65 hadi 142</b>
<b>4.</b>	Benki ya Biashara Tanzania	<b>5</b>	<b>1,529.06</b>	<b>40 hadi 180</b>
<b>5.</b>	Chuo Kikuu Mzumbe	<b>8</b>	<b>454.29</b>	<b>30 hadi 152</b>
<b>6.</b>	Shirika la Utangazaji Tanzania	<b>3</b>	<b>388.20</b>	<b>61 hadi 71</b>
<b>7.</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako	<b>1</b>	<b>277.24</b>	<b>600</b>
<b>8.</b>	Chuo cha Uhasibu Arusha	<b>3</b>	<b>219.95</b>	<b>34 hadi 79</b>
<b>9.</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza	<b>1</b>	<b>206.41</b>	<b>192 hadi 330</b>
<b>10.</b>	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	<b>2</b>	<b>197.16</b>	<b>45 hadi 120</b>
<b>11.</b>	Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi	<b>24</b>	<b>184.85</b>	<b>32 hadi 252</b>
<b>12.</b>	Chuo Kikuu cha Dodoma	<b>1</b>	<b>165.28</b>	<b>287</b>
<b>13.</b>	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	<b>4</b>	<b>152.07</b>	<b>32 hadi 136</b>
<b>14.</b>	Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira	<b>2</b>	<b>118.73</b>	<b>193 hadi 409</b>
<b>15.</b>	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	<b>3</b>	<b>116.97</b>	<b>52 hadi 107</b>
<b>16.</b>	Kampuni ya MCB	<b>3</b>	<b>114.57</b>	<b>47 hadi 224</b>
<b>17.</b>	Chuo cha Elimu ya Biashara	<b>1</b>	<b>100.2</b>	<b>30</b>
<b>18.</b>	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	<b>1</b>	<b>98.17</b>	<b>52</b>
<b>19.</b>	Shirika la Viwango Tanzania	<b>1</b>	<b>36.41</b>	<b>60</b>
<b>20.</b>	Chuo Kikuu Ardhi	<b>1</b>	<b>25.19</b>	<b>170</b>
<b>21.</b>	Chuo cha Ufundji Arusha	<b>1</b>	<b>22.85</b>	<b>1140</b>
<b>22.</b>	Bodi ya Rufani za Kodi	<b>1</b>	<b>21.58</b>	<b>40</b>
<b>Jumla</b>		<b>76</b>	<b>14,837.88</b>	

**Chanzo:** faili za ununuizi

#### Kiambatisho Na. XII: Mashirika ambayo hayakutumia Mfumo wa kutunza Taarifa na Usimamizi wa Rasilimali Watu

S/n	Jina La Taasisi/Shirika
<b>1</b>	Shirika la Ndege Tanzania
<b>2</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha
<b>3</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati
<b>4</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi
<b>5</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Bukoba
<b>6</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam
<b>7</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma
<b>8</b>	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
<b>9</b>	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
<b>10</b>	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Geita

S/n	Jina La Taasisi/Shirika
11	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa
12	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga
13	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama
14	Shirika la Masoko ya Kariakoo
15	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma
16	Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji wa Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro
17	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe
18	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela
19	Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini
20	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi
21	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi - Nachingwea
22	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya
23	Bohari ya Dawa
24	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro
25	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi
26	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda
27	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara
28	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma
29	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza
30	Shirika la Taifa la Maendeleo
31	Shirika la Nyumba la Taifa
32	Kampuni ya Ranchi za Taifa Limited
33	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii
34	Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro
35	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe
36	Mfuko wa SELF
37	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga
38	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida
39	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea
40	Bodi ya Sukari Tanzania
41	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga
42	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora
43	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga
44	Benki ya Biashara Tanzania
45	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
46	Shirika la Umeme Tanzania
47	Kampuni ya Mbolea Tanzania
48	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
49	Shirika la Posta Tanzania
50	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania
51	Shirika la Mawasiliano Tanzania
52	Benki ya Maendeleo TIB
53	Kampuni ya Ubungo Plaza
54	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote
55	Kampuni ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (UTT - AMIS)
56	Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

#### Kiambatisho Na. XIII: Mashirika ya umma yenye nyenzo za kufanya kazi zisizoridhisha

Na.	Jina La Taasisi/Shirika	Mapungufu niliyobaini
1.	Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari	Hakuna muundo wa shirika unao akisi majukumu ya shirika Hakuna mpango mkuu wa usimamizi wa Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari Dar es Salaam pamoja na Mnazi Bay, Ruvuma; Kutokuwepo kwa katiba ya Ukaguzi wa Ndani na Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani.
2.	Hifadhi za Taifa Tanzania	Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Hifadhi uliopitwa na wakati

3.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu	Hakuna taratibu za uendeshaji ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake
4.	Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Kutokuwepo kwa miongozo ya uendeshaji wa zahanati ya chuo
5.	Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania	Hakuna Mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Bima kama inavyoainishwa kwenye mpango mkakati wa mamlaka kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi 2023/24."
6.	Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania	Kukosekana kwa kanuni zilizoidhinishwa za kuendesha Shirika ikiwamo Kanuni za Usafirishaji Tanzania za Mwaka 2022, Sheria wa Usafirishaji wa Mabaharia ya Mwaka 2022, sera ya Kudhibiti Udanganyifu, Sera ya Usimamizi wa vihatarishi nya Kodi ya Kampuni, pamoja na Mfumo wa Kudhibiti Udanganyifu.
7.	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam	Sera zilizopitwa na wakati, zikiwamo sera ya uhakiki wa Ubora, mfumo wa usimamizi wa vihatarishi pamoja na rejista ya vihatarishi,
8.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita	Hakuna mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na udanganyifu unaojumuisha sera ya usimamizi wa vihatarishi, mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi, mpango wa tathmini ya vihatarishi na sera ya udanganyifu na utaratibu wa kutoa taarifa za siri.
9.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga	Hakuna mifumo ya Usimamizi wa vihatarishi na Udanganyifu katika Mamlaka pamoja na mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani.
10.	Baraza la Michezo Tanzania	Hakuna rejista ya hatari, Mipango ya Hatua ya Usimamizi wa vihatarishi pamoja na tathmini ya Hatari.
11.	Chuo cha Sukari cha Taifa	Hakuna mfumo wa usimamizi wa vihatarishi.
12.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	Hakuna sera ya kudhibiti udanganyifu.
13.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga	Hakuna sera ya kudhibiti udanganyifu.
14.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora	Kutokuwepo kwa (i) Mipango, Ufutiliaji na Tathmini ya Sera, (ii) Sera ya Usimamizi wa vihatarishi, (iii) Sera ya Afya na Mazingira (SHE), (iv) Sera wa wajibu wa Jamii (CSR), na pamoja na Sera ya Masoko na Masuala ya mamlaka.
15.	Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania	Ukosefu wa sera ya usimamizi wa vihatarishi iliyoidhinishwa, hakuna sera ya kuzuia udanganyifu iliyoidhinishwa
16.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi	Hakuna Mkataba wa Ukaguzi wa Ndani
17.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma	Hakuna Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani
18.	Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Kukosekana kwa kanuni za kifedha
19.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	Kanuni za Fedha na Wafanyakazi zilizopitwa na wakati
20.	Kampuni ya Gesi Tanzania	Kukosekana kwa mpango wa motisha, kanuni za wafanyakazi, na kanuni za Fedha, na bajeti inayojitegemea na mpango mkakati wa kampuni
21.	Chuo cha Uhaisbu Arusha	Kuwepo kwa kanuni za Fedha Zilizopitwa na Wakati
22.	Kiwanda cha Kutengeneneza dawa cha Keko	Kutokuwepo kwa miongozo ya rasilimali watu
23.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi	Hakuna mwongozo wa uhaisbu na kanuni za zamani za kifedha
24.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	Mwongozo wa uhaisbu uliopitwa na wakati

25.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida	Miongozo iliyopitwa na wakati ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Fedha 2014, Mwongozo wa Rasilimali Watu 2014, Mkataba wa Ukaguzi wa Ndani 2014, vilevile, hakuna mpango mkakati na bajeti inayojitegemea ya mamlaka
26.	Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL	Hakuna mpango wa motisha, kanuni za kifedha na kanuni za wafanyakazi.
27.	Shirika la Viwango Tanzania	Kanuni za kifedha zilizopitwa na wakati
28.	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania	Kanuni za kifedha zilizopitwa na wakati
29.	Taasisi ya Elimu Tanzania	Hakuna Sera ya Rasilimali Watu, Kanuni za Wafanyakazi na Mwongozo wa Uhasibu
30.	Bodi ya Nyama Tanzania	Mwongozo wa uhasibu uliopitwa na wakati, pamoja na Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani
31.	Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania	Kukosekana kwa Sera za Fedha na Taratibu za mamlaka ambapo kwa sasa mamlaka inatumia miongozo iliyoandalishi kwa ajili ya kutumiwa na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Tanzania (TPRI).
32.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu	Kanuni za Fedha zilizopitwa na wakati.
33.	Bodi ya Kahawa Tanzania	Kukosekana kwa Sera ya Mikopo ya Wafanyakazi
34.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha	Kukosekana kwa mwongozo wa Uhifadhi uliopitwa na wakati, na Mwongozo wa Ununuzi uliopitwa na wakati
35.	Bodi ya Usajili wa Makandarasi	Kutokuwepo kwa Mwongozo na Sera ya Utafiti
36.	Bodi ya Korosho Tanzania	Hakuna mpango wa mapitio ya utekelezaji wa mpango mkakati unaofanyika kwa mwaka
37.	Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila	Kukosekana kwa viashiria muhimu vya Utendaji pamoja na kukosekana kwa mpango mkakati wa Hospitali
38.	Bodi ya Bima ya Amana	Kuwa na Muundo wa Maendelo ya Watumishi uliopitwa na wakati
39.	Kampuni ya Mkulazi	Kuwa na Muundo wa Maendelo ya Watumishi uliopitwa na wakati
40.	Shirika la nyuma la Taifa	Kuwa na Muundo wa Maendelo ya Watumishi uliopitwa na wakati

*Chanzo: Uchambuzi wa ripoti za utendaji*

#### Kiambatisho Na. XIV: Kodi ambazo hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Na.	Jina la Taasisi	Kodi ya Mapato	kodi ya ongezeko la Thamani	kodi ya zuio	kodi ya mapato yatokanayo na ajira	kodi ya ujuzi na maendeleo	kodi ya mapato	Jumla
Shilingi milioni								
1.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam			1,223	17,899	7,896		27,018
2.	Shirika la Posta Tanzania	1,698	2,600					4,298
3.	Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini		23	133	435			591
4.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga			256		52	256	564
5.	Kampuni ya Huduma ya Meli				312			312
6.	Kampuni ya STAMIGOLD			256				256
7.	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam				131	27		158
8.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania		82					82
9.	Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji				78			78

10.	Chuo Kikuu cha Dodoma			22				22
11.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma					20		20
12.	Shirika la Masoko ya Kariakoo					18		18
13.	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda					12		12
14.	Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viwatilifu Tanzania			10				10
15.	Baraza la Ushindani			4				4
16.	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania			4				4
Jumla		1698	2,705	1908	18,855	8,025	256	33,447

Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za kodi

**RIPOTI KUU YA MWAKA YA  
UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi  
4 Barabara ya Ukaguzi,  
S.L.P 950,  
Tambukareli, 41104 Dodoma.

 +255 (026) 2161200  
 [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)  
 [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

